2 JUNI, 2025

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 2 Juni, 2025

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika. Kanuni ya 39(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inampatia mamlaka Spika kutoa taarifa yoyote katika kikao chochote kadiri atakavyoona inafaa. Hivyo, leo katika Kikao cha Thelathini na Saba cha Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili, ninaomba kuwapatia Taarifa kuhusu Tuzo Maalum ya Heshima iliyotolewa na Bunge kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mara ya kwanza katika historia yake, liliandaa tuzo iliyojulikana kama Tuzo Maalum kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tukio hili la kipekee la Bunge kutoa tuzo lilifanyika siku ya Jumamosi, tarehe 31 Mei, 2025.

Waheshimiwa Wabunge, siku ile nilieleza kwa kirefu kwenye maneno yangu ya utangulizi, kabla ya kukabidhi tuzo, sababu ya Bunge hili la Kumi na Mbili kuamua kumpatia Mheshimiwa Rais tuzo hii. Hapa nieleze kwa kifupi tu kwamba, Bunge lilifikia uamuzi huo baada ya sisi Wabunge na wawakilishi wa wananchi kutambua na kuyapatia heshima mambo makubwa aliyoyafanya katika kipindi chake cha uongozi wa miaka minne.

Mambo aliyoyafanya, kwa uchache, ni kusimamia vyema Falsafa ya *4R*, kusimamia na kuimarisha Muungano wetu, kuimarisha mahusiano ya Kimataifa na kupeleka maendeleo katika kila sekta, ikiwemo sekta za elimu, afya, nishati, maji, uchukuzi na kadhalika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nirudie tena kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kukubali wito wetu na kuja mwenyewe kupokea tuzo tuliyomwandalia. Aidha, tunamshukuru kwa maneno yake ya hekima, busara na kutia moyo aliyoyatoa siku ile kuonesha kuguswa na jambo tulilolifanya, ambalo limeonesha Bunge lipo pamoja na yeye, kama Rais, na pia Serikali yake kwa ujumla katika kuwaletea wananchi wetu maendeleo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, natumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa kuhudhuria tukio hili kwa wingi na kuonesha hamasa kubwa mbele ya mgeni rasmi, ambaye alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu. Aidha, naipongeza kwa dhati Sekretarieti ya Bunge ikiongozwa na Katibu wetu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard, kwa maandalizi na uratibu mzuri wa tukio zima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati ninahitimisha siku ile, nilieleza tukio hili litaingia Bungeni. Kwa vile lilifanyika nje ya Ukumbi wa Bunge, ili sasa liwe sehemu ya Taarifa Rasmi ya Bunge kwa kumbukumbu ya vizazi vya sasa na vijavyo, hivyo, kwa taarifa hii, Tuzo hii Maalum ya

Heshima kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeingia Rasmi katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Baada ya kusema hayo Mwenyekiti atakuja kunipokea.

Hapa, Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA AFYA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Namwita sasa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, aulize swali lake. Hayupo ndani ya Bunge, kwa niaba yake, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 470

Wenyeviti wa Vijiji Kuanza Kulipwa Posho, Msalala

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. IDDI K. IDDI aliuliza: -

Je, lini Serikali itaielekeza Halmashauri ya Msalala kuanza kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Festo Dugange.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ina jumla ya vijiji 92 ambavyo vyote vina Wenyeviti wa Vijiji. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Halmashauri ya Msalala ilitenga shilingi milioni 5.5, kwa ajili ya posho za Wenyeviti wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, halmashauri ilitenga shilingi milioni 11.04. Hadi Mei, 2025, shilingi milioni 10.1 zimelipwa na kiasi cha shilingi 920,000 kitalipwa kufikia Juni, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 11.04, kwa ajili ya kuendelea kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji katika Halmashauri ya Msalala, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Naibu Waziri. Sasa kwa kuwa, fedha zilizotengwa ni nyingi ukilinganisha na ambazo zimetolewa, nini kauli ya Serikali?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Christina Mnzava kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia ustawi wa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa. Nimhakikishie tu kwamba, kwanza Serikali hii inajali sana na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa, ndiyo maana katika halmashauri zote 184 Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kulipa posho za kila mwezi za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Msalala ilitenga shilingi milioni 11.04 na imelipa shilingi milioni 10.1 kwa maana ya kwamba, ifikapo tarehe 30 mwezi huu wa Juni, fedha hii yote itakuwa imeshalipwa na wale Waheshimiwa Wenyeviti watakuwa wamepata fedha zao zote. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kulipa posho hizo kwa Wenyeviti wa Vijiji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Madiwani wanafanya kazi kubwa sana

kwenye Kata na Majimbo yetu, Serikali, inaonaje sasa iweke bayana ni kiasi gani cha posho ambayo inaenda kuongezwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba, Waheshimiwa Madiwani na Wahehsimiwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa wanafanya kazi kubwa sana za uongozi katika maeneo yao. Serikali hii inatambua kazi nzuri inayofanywa na viongozi hao, ndiyo maana, kwanza kwa upande wa Waheshimiwa Madiwani, ilichukua jukumu la kulipa posho kwa Waheshimiwa Madiwani katika halmashauri zetu zote na inalipa kila mwezi kiwango ambacho kimewekwa kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa, halmashauri husika hutenga fedha kila mwaka kulingana na uwezo wa halmashauri husika. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kwanza kumhakikishia, Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tutaendelea kuona uwezekano, kwa kadiri ya uwezo wa Serikali, namna ambavyo halmashauri zitaboresha posho za Wenyeviti wa Vijiji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Namwita sasa Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

(Hapa kipaza sauti hakikuwaka)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bushiri, hamia kwenye kisemeo kingine. *(Makofi)*

Na. 471

Ujenzi wa Wodi Hospitali ya Wilaya, Same

MHE. ZUENA A. BUSHIRI aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Wodi za Wanaume na Wanawake katika Hospitali ya Wilaya ya Same?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Same, Novemba, 2022. Hadi mwezi Aprili, 2025 Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 3.4, ambapo shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika ujenzi wa majengo ya hospitali ya halmashauri hiyo na shilingi milioni 800 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Aidha, majengo matano kati ya nane, ujenzi umekamilika na yameanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imetenga shilingi milioni 800, kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wanaume, wanawake, watoto na ujenzi wa njia za kutembea wagonjwa *(Walkways)* katika Hospitali ya Wilaya ya Same, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bushiri, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza naipongeza kwa hatua ambayo imefikia katika ujenzi wa hospitali hiyo, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali hiyo, wodi ya akinamama na watoto imeanza kufanya kazi, lakini kuna changamoto ya wauguzi kutokuwa na nyumba za kuishi katika

maeneo hayo. Je, ni mpango gani wa Serikali, wa haraka, wa kujenga nyumba za watumishi? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri kwa namna ambavyo amekuwa akiwasemea kwa dhati wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namhakikishia tu kwamba, hoja yake mwanzo ilikuwa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri katika Wilaya ya Same. Tayari Serikali sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshajenga. Imepeleka zaidi ya shilingi 3,400,000,000.00 na mwaka wa fedha ujao 2025/2026 tumetenga shilingi milioni 800, kwa ajili ya kujenga wodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa hivi vituo vya huduma na kupeleka vifaatiba na watumishi, Serikali imeweka mpango kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi. Kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Hospitali ya Halmashauri ya Same ni moja ya hospitali ambazo zimetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba za utumishi katika mwaka wa fedha ujao 2025/2026.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Bupe.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kituo cha Afya cha Kata ta Kilando hakina jengo la *mortuary*. Ni lini Serikali itajenga jengo hilo kwa Kata ya Kilando? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti,

Mpango wa Serikali ni kujenga majengo yote muhimu katika vituo vya afya, yakiwepo majengo ya kuhifadhia maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Kituo cha Afya cha Kilando, Serikali inatambua kuna baadhi ya majengo ambayo yanahitajika, likiwemo jengo hilo la kuhifadhia maiti, na tayari tumeweka mpango mkakati wa ukamilishaji wa majengo katika zahanati na vituo vyote ambavyo vina majengo pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaweka kipaumbele katika Kituo cha Afya cha Kilando, ili tuweze kujenga jengo hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Amar Hussein.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kukamilisha kutujengea Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale. Pale kuna thamani nyingi, majengo yapo na wagonjwa wapo wengi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea uzio kwa ajili ya kulinda mali zilizopo pamoja na wagonjwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga hospitali za Halmashauri, ikiwepo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, kama alivyosema Mheshimiwa Amar, lakini nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge tumepanga na tumeweka vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha kwanza kilikuwa ni kuhakikisha majengo ya huduma yanakamilika, kupeleka vifaatiba na watumishi. Kwa kuwa tumekamilisha hilo, tutakwenda kipaumbele cha

pili, kuangalia namna ya kuboresha usalama katika maeneo hayo, ikiwemo kujenga *fence,* uzio, katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii, kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale pamoja na Serikali Kuu tutaendelea kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uzio katika hospitali hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Dorothy Kilave.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo mmeweza kutujengea Kituo cha Afya, Kata ya Kilakala na vifaa vyote vimeingia. Je, sasa Serikali ni lini itaanza kile Kituo cha Afya cha Kata ya Sandali, ndani ya Jimbo la Temeke?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Ndiyo maana hivi leo ninapoongea, Mheshimiwa Rais, ndani ya mwezi huu mmoja, ametoa shilingi bilioni 30 kwa ajili ya majimbo 120 katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge waliainisha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Kwa hiyo, hii ni dhamira ya dhati ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunatambua katika Jimbo la Temeke yapo maeneo ambayo, Serikali tayari imejenga vituo vya afya, lakini bado kuna kata za kimkakati. Nakuhakikishia tu kwamba, tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha pia, katika kata hiyo tunapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Ahsante.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Minza Mjika.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Meatu ina hospitali ambayo ni kubwa, ina wodi moja ya wanaume na moja ya wanawake, lakini zile wodi hazitoshi, wagonjwa wanalala wawili wawili. Je, ni lini Serikali itaongeza wodi nyingine katika Hospitali hiyo ya Wilaya ya Meatu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ni moja ya hospitali kongwe. Tayari Serikali imepeleka fedha, kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa hospitali hiyo. Kazi imefanyika kwa ufanisi mkubwa na wananchi wanaendelea kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali inatambua kwamba, pamoja na fedha zilizopelekwa bado kuna baadhi ya miundombinu inayopungua. Ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Minza kwamba, tunaendelea kupeleka fedha kwa awamu, kwa ajili ya kukamilisha miundombinu mingine ambayo imebaki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Namuita sasa, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka aulize swali lake.

Na. 472

Hitaji la Vifaatiba na Wataalam, Wilaya ya Chunya

MHE. MASACHE N. KASAKA aliuliza: -

Je, lini Selikali itapeleka Vifaatiba na Wataalam katika Zahanati za Wilaya ya Chunya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa vibali vya ajira kila mwaka, ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 jumla ya watumishi wa kada ya afya 34,720 wameajiriwa na kupangiwa vituo kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imepokea jumla ya watumishi 151 wa kada ya afya na watumishi 46 wamepangiwa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 44 ngazi ya vituo vya afya na watumishi 61 katika zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha upatikanaji wa vifaatiba; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepeleka shilingi milioni 400 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, ambapo shilingi milioni 100 zimetumika kununua vifaatiba, ngazi ya zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba ambapo shilingi milioni 50 zitatumika kununua vifaatiba, ngazi ya zahanati, katika Halmashauri ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepeleka shilingi milioni 400 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ambapo shilingi milioni 100 zimetumika kununua vifaatiba ngazi ya zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba ambapo shilingi milioni 50 zitatumika kununua vifaatiba ngazi ya zahanati katika Halmashauri ya Chunya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kuajiri na kutuletea wataalam pamoja na vifaatiba, lakini naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kasi kubwa ya ujenzi wa zahanati pamoja na vituo vya afya, uhitaji wa vifaatiba bado ni mkubwa sana. Je, ni upi mpango wa Serikali wa haraka kwa Wilaya yetu ya Chunya kuweza kutuletea vifaatiba kwa kuwa tayari vituo vya afya vya Sangambi, Mafyeko na Matwiga vimeshakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Pamoja na kutuletea madaktari pamoja na watumishi wa ngazi mbalimbali ndani ya Wilaya ya Chunya, bado tuna upungufu wa watumishi wasiopungua 719. Je, Serikali ina mkakati upi wa haraka itakayotuletea sisi wananchi wa Wilaya ya Chunya, ili kupunguza upungufu huo wa watumishi wa sekta ya afya?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka hii miwili ya fedha, Serikali imetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 100 na kuzipeleka kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Moja ya halmashauri ambazo zimepata fedha hizo ni pamoja na Jimbo la Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Kasaka kwamba fedha za vifaatiba zinaendelea kutolewa. Katika huu mwaka wa fedha Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 63.7 kwa ajili ya vifaatiba katika halmashauri zote 184 ikiwemo halmashauri ya Chunya. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutaendelea kupeleka fedha kwenye vituo vya afya ambavyo amevitaja ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili la uhitaji wa watumishi na nyumba za watumishi, Serikali pia imeweka mpango

kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga nyumba za watumishi pamoja na kuhakikisha kwamba watumishi wanaendelea kuajiriwa. Ndiyo maana watumishi waliojiriwa katika kipindi cha miaka minne ni zaidi ya 34,720. Zoezi hili ni endelevu, na Serikali itaendelea kuweka kibali cha ajira na kuendelea kuajiri watumishi katika halmashauri zetu.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kumaliza zahanati yetu katika Kata ya Misha ambayo inaitwa Igambilo lakini zahanati ile bado ina upungufu mkubwa wa vifaatiba. Je, ni lini Serikali itatupelekea vifaatiba katika zahanati ile?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mwakasaka kwamba tayari Serikali imeshapeleka fedha katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa ajili ya kununua vifaatiba kwenye zahanati zote mpya ambazo zimekamilika ikiwemo Zahanati ya Misha. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kufanya haraka iwezekanavyo kuhakikisha kwamba vifaatiba ambavyo vimepelekwa katika halmashauri yake vinapelekwa pia katika Zahanati ya Misha ili ianze kutoa huduma ambazo zinatarajiwa kwa wananchi.

MWENYEKITI: Nilikuona Dkt. Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba niiulize Serikali, je, ni lini watapeleka *X-Ray* kwenye Kituo cha Afya pale Kahe Magharibi ambacho kinahudumia wananchi zaidi ya 60,000 kutoka kwenye Kata za Njia Panda, Kirua-Vunjo Kusini, Kahe Magharibi yenyewe pamoja na Kahe Mashariki?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Ntahi Magharibi katika Jimbo la Vunjo ni moja ya vituo ambavyo vimewekwa kwenye awamu ya pili ambavyo tutanunua *digital X-Ray* 350 kwa ajili ya kupeleka kwenye hivyo vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua uhitaji wa *X-Ray* katika kituo hicho cha afya, na tayari imeshaweka mpango wa ununuzi wa *X-Ray* hizo katika mwaka wa fedha ujao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Nimwite sasa Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu aulize swali lake.

Na. 473

Daraja Linalounganisha Kijiji cha Mwanduti na Ibambo

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Daraja linalounganisha Kijiji cha Mwanduti na Ibambo katika Kata ya Mwongozo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha usanifu wa awali wa daraja linalounganisha Kijiji cha Mwanduti na Ibambo. Aidha, usanifu wa kina umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa lengo la kubaini gharama halisi za ujenzi, mahitaji ya kiufundi na maandalizi ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya usanifu wa kina kukamilika, Serikali itatafuta fedha za ujenzi wa daraja hilo ili kutatua changamoto ya mawasiliano katika Vijiji vya Mwanduti na Ibambo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rehema Migilla.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo yanaonesha kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa ujenzi wa hili daraja kutokana na kwamba wananchi wangu wengi walishakufa na bado wanatembea umbali mrefu kufuata shughuli zao; na kwa sababu daraja hili kuna mto katikati na barabara ya kutoka Mwanduti mpaka Ibambo hakuna; je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuipandisha hadhi barabara hiyo ya kutoka Mwanduti mpaka Ibambo ili iweze kuhudumiwa na *TARURA?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Wananchi wa Kijiji cha Ng'wande na Mwanduti wamefanya jitihada kubwa sana za kuchonga barabara wao wenyewe kwa nguvu zao, lakini barabara hiyo haina viwango na inahitaji umuhimu wa kuwekewa madaraja na makalavati. Je, Serikali inawaunga vipi mkono wananchi wangu hawa kwa kuwapelekea madaraja na makalavati, ili barabara hiyo iweze kupitika katika vipindi vyote vya mwaka?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Utaratibu wa kuziingiza barabara zetu kwenye mtandao wa *TARURA,* kwa maana ya kuzisajili, ni kwa halmashauri husika kuanza kwa kufanya maombi maalum Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia kwa Katibu Tawala Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi tutafanya utaratibu wa kupandisha hadhi na kuzisajili barabara hizo katika mtandao wa *TARURA*. Kwa hiyo, ninaomba kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Migilla kwamba Serikali

inathamini umuhimu wa miundombinu kuwa salama na bora kwa shughuli za kiuchumi na za kijamiii kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia halmashauri hiyo tuanze utaratibu wa kuomba kupandisha hadhi na kuisajili barabara hiyo ya kutoka Mwanduti kwenda Ibambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kaliua kuleta maombi hayo kwa kufuata utaratibu kwa kushirikiana na Meneja wa *TARURA,* ili Serikali ianze hatua ya kutathmini, kuona vigezo na pia kupandisha hadhi wakati tunajiandaa kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, tunafahamu kwamba yapo maeneo ambayo wananchi wanajitolea nguvu zao. Nitumie nafasi hii kawapongeza wananchi wa kijiji hicho. Niwahakikishie kwamba, mara baada ya barabara hiyo kusajiliwa, Serikali itaiweka kwenye Bajeti ya *TARURA,* ili iweze kulimwa na kujengewa makalavati na madaraja, wananchi waweze kusafiri kwa usalama zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Tumaini Magessa.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itatenga fedha ili kujenga daraja linalounganisha kati ya Kitongoji cha Nyakasoma, Kijiji cha Isima Jimboni Busanda kwenda Kijiji cha Chibumba Jimboni Chato? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba daraja la eneo la Nyakasoma kwenda Chibunda ni daraja muhimu, ni kubwa na Serikali inatambua umuhimu wa kujenga daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali imeanza kufanya usanifu wa ujenzi wa daraja hilo; na tumeshamwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Geita na Wilaya ya Geita kuleta taarifa ya usanifu wa kina na kuleta makadirio ya ujenzi wa daraja hilo ili Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Chaya.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Halmashauri ya Manyoni kuna Madaraja ya Kapiti na Magasai ambayo yamekuwa kikwazo kikubwa sana cha wananchi kusafiri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananusuru wananchi hawa kwa kujenga madaraja hayo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini na kuainisha maeneo yote korofi katika halmashauri na majimbo yote likiwemo Jimbo la Manyoni katika Daraja hilo la Kapiti na Makasai. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja hayo kwa awamu ili kuhakikisha kwamba wananchi wanasafiri na kupita kwa usalama zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa ninaomba maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Yahya Mhata.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili kujenga daraja linalounganisha Kata ya Malatani na Kata ya Nanyumbu kwenye Kijiji cha Chitoha ambalo limekuwa kero sana kwa wananchi hao?

MWENYEKITI: Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Halmashauri ya Nanyumbu pamoja na Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Mtwara kutuletea taarifa rasmi ya usanifu na mahitaji ya fedha katika ujenzi wa daraja hilo muhimu, ili Serikali ione namna ya kutafuta fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Felista Njau.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Kata ya Mbokomu daraja limefunikwa na kifusi baada ya maafa kutokea Mbokomu kwenda Kidia, pia barabara hii haipitiki kabisa tangu maafa haya yametokea, je, Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha mundombinu hii ili kuruhusu wananchi waweze kufanya shughuli zao za maendeleo?

MWENYEKITI: Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapa katikati tulipata baraka ya mvua nyingi, lakini ilikuja na changamoto kwa kuharibu miundombinu, likiwemo daraja hili la Mbokomu – Kidia katika Mkoa wa kilimanjario Jimbo la Vunjo (Moshi Vijijini). Ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza Serikali imeshatoa maelekezo kwa mameneja wote wa *TARURA* kote nchini kufanya tathmini ya barabara zilizoharibiwa na mafuriko na kutuwasilishia Ofisi ya Rais, TAMISEMI *(TARURA)* kwa ajili ya kufanya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeanza kutoa fedha kwa awamu katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa madaraja hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italifikia daraja hilo, tutafanyia

matengenezo pamoja na barabara ili kuhakikisha kuwa tunalirejesha kwenye hali nzuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jumanne Mtaturu.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraja ya Ujaile pamoja na Kimbwi yalizolewa na mvua wakati wa mvua kubwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuyajenga madaraja haya, likiwemo Daraja la Ujaile ambalo tayari *IMF* walishatoa fedha ili kumpata mkandarasi kumaliza tatizo hilo?

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Serikali imekwishatoa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo la Ujaile. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu za kuanza ujenzi zipo mwishoni, na tunatarajia wakati wowote kazi ya ujenzi itaanza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Barabara inayotoka Liwale kwenda kwenye Kata ya Mpigamiti ina daraja la Ngorongopa ambalo ni chakavu sana. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha kujenga Daraja hilo la Ngorongopa pamoja na ukarabati wa barabara hiyo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa daraja lile la Ngorokomu na kwamba Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa na nimhakikishie kwamba sisi kama Serikali tayari tumeliwekea mpango madhubuti kabisa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati maeneo mbalimbali ya barabara hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Priscus Tarimo.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Moshi Mjini ipo katika Mradi wa *TACTIC Tyre Two*. Barabara inayoanzia Kata ya Ng'ambo – Miembeni – Msaranga – Njoro inalo Daraja la Otieno ambalo tunategemea litengenezwe na mradi huu. Je, ni nini kinachokwamisha kusainiwa kwa mkandarasi kwa ajili ya barabara hizi?

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mpango wa kukarabati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali kupitia Mpango wa *TACTIC,* na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni moja ya halmashauri zilizokuwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna kinachokwamisha kusaini mkataba. Tupo kwenye hatua za kawaida za manunuzi na wakati wowote mkataba utasainiwa na barabara hiyo pamoja na daraja hilo vitajengwa kupitia Mpango wa *TACTIC*.

MWENYEKITI: Tumalizie na Mheshimiwa Ussi Pondeza.

MHE. USSI S. PONDEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa ninataka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Daraja la Ibukilo kwenda Kata ya Sengo ambalo lipo Wilayani Maswa limeahidiwa na *TARURA* litajengwa. Je, ni lini ujenzi wake utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa daraja hilo na imeendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kujenga madaraja yote ya kimkakati katika maeneo

ambayo yameharibiwa na mvua, na daraja hilo katika Halmashauri ya Maswa litajengwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee swali la mwisho kwa Wizara hii. Nimwite sasa Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali aweze kuuliza swali lake.

Na. 474

Ujenzi wa Majengo ya Utawala Shule za Manonga

MHE. SEIF K. S. GULAMALI aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa majengo ya utawala katika Shule za Sekondari za Choma, Ziba na Mwisi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) aliuliza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa shule kuwa na miundombinu yote muhimu ikiwa ni pamoja na majengo ya utawala. Aidha, kwa sasa Serikali imejikita katika ujenzi wa madarasa, vyoo, mabweni na nyumba za walimu katika shule za sekondari ili kuendana na ongezeko la wanafunzi katika ngazi zote za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa shilingi milioni 777.71 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili na matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Choma, mabweni mawili, madarasa manne na matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Ziba na ukamilishaji wa bwalo moja katika Shule ya Sekondari Mwisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za sekondari, ikiwa ni pamoja na majengo ya utawala. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Serikali kwa fedha nyingi ambazo imezileta katika hizo shule, na kwa kutambua zile shule ambazo nimezitaja hapo, kwa maana ya Mwisi, Choma na Ziba kuwa ni shule za Kidato cha Tano na Sita; na kwa wingi wa wanafunzi ambao wanakwenda pale kwenye hizo shule walimu wanakosa sehemu ya jengo la utawala. Je, ni lini tatapata fedha kwa ajili ya shule hizo tatu za kimkakati za *form five* na *form six?*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Shule hizi za Sekondari Choma, Ziba na Mwisi ni shule za kidato cha tano na sita; na Serikali iliweka vipaumbele; kwanza, kuhakikisha kwamba miundombinu ya wanafunzi kusomea na kuishi katika shule hizo inakamilishwa ikiwemo mabweni, madarasa, vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shughuli hizi zimeshatekelezwa, sasa kipaumbele cha pili ni kujenga majengo ya utawala. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Gulamali kwamba Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo ya utawala. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa Serikali ilitupa fedha shilingi milioni 585 kwa ajili ya kujenga shule ya ufundi katika Jimbo la Makambako, je, ni lini Serikali itatupa fedha kwa ajili ya kukamilisha shule ya ufundi katika Mji wa Makambako?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilishapeleka fedha katika Halmahsauri ya Mji wa Makambako shilingi milioni 585 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari za amali ama ufundi. Tunafahamu kwamba ile ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule hizo, na shule hizo zimejengwa katika majimbo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, awamu hiyo ya kwanza tayari shughuli za ujenzi zinaendelea. Serikali inaandaa mpango wa awamu ya pili kwa ajili ya kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu inayobaki. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa shughuli hiyo pia itatekelezwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia Theonest.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa ajili ya kujenga vyoo kwenye shule za msingi na sekondari vya kutumia maji, bila kuweka *specifications* wala kuweka gharama za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyoo vinajengwa vinapaswa kutumia maji na shule hazina maji. Je, Serikali ina mkakati gani, kwamba inavyopeleka vyoo vya maji iwe inaweka pia miundombinu ya maji ikiwepo Shule ya Msingi Kitwechenkura na Omuchekano ambao wana vyoo wanabaki kuviangalia tu kwa sababu hawana maji?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka kipaumbele kwamba katika taasisi zote za umma lazima huduma za kijamii kama maji, umeme, barabara na kadhalika iwe ni kipaumbele namba moja. Kwa hiyo, katika shule hizo ninaomba nitumie nafasi hii

kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kyerwa kuhakikishwa kwamba anawasiliana na *RUWASA* katika eneo husika ili waweze kupekeka maji mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maeneo yote kote nchini ujenzi wa vyoo vya maji unakwenda sambamba na ujenzi wa miundiombinu na maji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Grace Tendega.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Shule nyingi zilizopo katika Jimbo la Kalenga zina changamoto ya majengo ya utawala, hususan Shule ya Sekondari ya Muhwana ambayo ipo katika Kata ya Magulilwa, walimu wanakaa kwenye madarasa hawana majengo ya utawala wala samani za kutumia walimu hawa. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kujenga majengo ya utawala katika maeneo hayo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba zipo shule ambazo zina upungufu wa miundombinu yakiwemo majengo ya utawala, ikiwemo shule ya sekondari ambayo ipo katika Jimbo la Kalenga ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia Mpango wa *SEQUIP* na programu mbalimbali za Serikali, tayari imeainisha shule zote zenye upungufu wa majengo ya utawala. Katika mwaka ujao wa fedha tutaendelea na ujenzi wa majengo ya utawala na tutahakikisha shule hiyo tunaipatia kipaumbele.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako, kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge niwaombe turuke haya maswali ili tuweze kum-*accommodate* Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye hana Naibu hapa leo, na ana shughuli nyingine. Kwa hiyo, twende kwenye Swali Namba 480 na nimwite Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, aulize swali lake.

Na. 480

Mabadiliko ya Sera za Nchi Tajiri Kusaidia Kukuza Uchumi

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI aliuliza: -

Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na mabadiliko ya sera za baadhi ya nchi tajiri kulisaidia Taifa letu kukuza uchumi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA FEDHA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuongeza mapato ya ndani ili kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kutambua umuhimu wa mahitaji ya kibajeti ikiwemo ugharamiaji wa miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia njia mbadala ikiwemo ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Hii itasaidia kuipunguzia Serikali mzigo wa kukopa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupunguza utegemezi wa kibajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nianze kwa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni kwa kiasi gani Amri za Kimamlaka *(Executive Orders)* alizotoa Rais Trump wa Marekani kusitisha misaada katika nchi yetu imeathiri miradi iliyokuwa inaendelea hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunajua maendeleo ya nchi yetu yako mikononi mwetu sisi Watanzania na siyo vinginevyo, wala sio kwa wageni. Je, ni kwa kiasi gani nchi yetu imejipanga kutumia rasilimali zetu za asili ambazo zina utajiri mkubwa kukabiliana na mkwamo huu ambao unaendelea kujitokeza? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri aliyoyauliza, maswali ya kiprofesa kabisa hayo. Ameuliza *orders* zilizotolewa na nchi ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Serikali ya Tanzania haikuwa ina ushirikiano wa Kiserikali kwa Serikali kwenye masuala ya fedha za miradi ya maendeleo na Serikali ya Marekani. Fedha nyingi za miradi ya maendeleo kutoka Serikali ya Marekani zilikuwa zinatumia taasisi zake za Marekani, baina ya taasisi mbalimbali za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kwa upande wa kibajeti ya moja kwa moja hakukuwepo na athari hizo, na kwa upande wa taasisi zilizokuwa zinapokea fedha tayari Serikali ya Tanzania imeshafanya tathmini, siyo tu kwa tamko la Marekani, bali ni kwa mwenendo wote unaohusisha fedha zinazotoka kwa *development partners*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imepiga hatua nyingi za masuala ya aina hiyo, ikianza zamani sana ambapo kulikuwepo na fedha za misaada zinazokwenda kwenye bajeti, ambazo zilishaisha, na Serikali ina-*finance* miradi ya maendeleo kutumia fedha za ndani

kufidia pengo lile ambalo lilikuwa bajeti inapata fedha kutoka kwa nchi wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, sasa hivi Serikali baada ya kufanya tathmini kutokufuatana na jambo hili lililotokea siku hizi za hivi karibuni, Serikali tayari imepangilia upya matumizi yake kwa bajeti hii inayoendelea na kupata zaidi ya shilingi bilioni 220 ambazo zilikuwa zinahitajika, na hasa maeneo ambayo yalionekana kuathirika, kama maeneo ya afya ambayo tayari tulishapeleka zaidi ya shilingi bilioni 88 na zimeendelea na utekelezaji wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia tathmini hiyo, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa inapata fedha kutokana na ushirika huo pamoja na maeneo mengine, ili kuweza kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo pamoja na maisha ya Watanzania hayaathiriki kutokana na mabadiliko ya kisera ya mbia yeyote wa maendeleo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujipanga kutumia rasilimali zetu, Mheshimiwa umeleta swali zuri sana. Serikali inaendelea na mkakati wa kuweza kufanya miradi ya ndani, ile iliyo mikubwa inayotumia rasilimali za ndani kuweza kuanza kufanya kazi ili kuhakikisha tunaongeza mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya miradi hiyo kama ambavyo taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taarifa ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji wakati wa Bajeti za Kisekta ilibainisha kwamba Serikali imelipa fidia kwenye maeneo mengi ambayo ni ya kimkakati kiuwekezaji ili kuweza sasa kuanza kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali imepiga hatua kwenye majadiliano ya miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaweza ikaingizia mapato makubwa nchi yetu ili kuweza na yenyewe kuanza kutekelezeka. Pia, Serikali inajipanga kuanza uzalishaji zaidi wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa ndani ya nchi ili kuondokana na uagizaji wa bidhaa za aina hiyo ambazo Serikali ama nchi inaweza kuzalisha ndani ya nchi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na ninadhani pengine kwenye bajeti yako, jambo hili litajitokeza tena.

WAZIRI WA FEDHA: Ahsante.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tunakushukuru sana kwa majibu ya sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna baraka ya kuwa na wageni wengi sana leo. Kwa hiyo, tuwatangaze wageni waliopo ili waweze kutoa nafasi kwa wageni wengine.

Wageni ambao tunao ndani ya Ukumbi wa Bunge asubuhi hii, wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani. Hawa ni wapigakura wake kutoka Babati Vijijini Mkoa wa Manyara, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge, na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje Afrika Mashariki. Hawa ni *Diaspora* kutoka nchi mbalimbali. Karibuni Bungeni na tumekuwa nanyi toka juzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Paschal Katambi Patrobass, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Hawa ni wapigakura wake kutoka Shinyanga Mjini, ahsanteni. *(Makofi)*

Nina wageni 17 wa Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly, Mbunge wetu hapa ndani. Hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Sumbawanga Mjini wakiongozwa na Ndugu Anuari Mbwilo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sumbawanga Mjini. Karibuni sana, tunawakaribisha Bungeni na tunafanya kazi vizuri na Mbunge wenu hapa. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi. Hawa ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, huyu ni Ndugu Addelide Kiliba kutoka Jijini Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni mmoja, huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge mwenzetu. Huyu ni Ndugu Baraka Lazima, ni mdogo wake kutoka Mkoani Mtwara. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge; ni wapigakura wake kutoka Mbogwe Mkoa wa Geita. Wako pale, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge; hawa ni wadogo zake kutoka Tarime Mkoa wa Mara, Dodoma, na Jijini Dar es Salaam kwa pamoja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge; hawa ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Mohammed Maulid Ali, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge na Wakili; hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na marafiki zake kutoka Mkoani Mara. Karibuni sana ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza; hawa ni wapigakura wake kutoka Bukoba Vijijini Mkoani Kagera. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa *Engineer* Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge; hawa ni Makatibu Kata wa CCM kutoka Butundwe Mkoani Geita. Karibuni sana. Wako pale. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 27 wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge; hawa ni vijana wa Jumuiya kutoka Kanisa la Mennonite Tanzania wakiongozwa na Askofu Gabriel Magwega, Mlezi wa vijana. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 33 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge; hawa ni Wanakwaya wa KKKT Usharika wa Mlandege kutoka Mkoa wa Iringa. Wako pale, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 50 wa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge; hawa ni walimu wawili na wanafunzi 48 kutoka Shule ya Sekondari Nakwa, Babati Mkoa wa Manyara. Wako kule juu, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge; hawa ni wapigakura kutoka Buchosa Mkoa wa Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wageni watano wa Kampuni ya *China Railway Jianchang Engineering (CRJE) East Africa Limited* kutoka Jijini Dar es Salaam. *Welcome to the Parliament*, karibuni sana. Hawa wakandarasi wetu kila mahali wapo. *(Makofi)*

Tunao viongozi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* waliokuja Bungeni kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja wa Mfumo wa *NeST* wakiongozwa na Ndg. Denis Simba, Mkurugenzi Mkuu wa *PPRA*. Ninaona wako pale, wametawanyika tawanyika, lakini ninadhani tuna shughuli na ninyi leo. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 36 na Walimu watatu kutoka Shule ya Sekondari Kinyerezi Mpya kutoka Jijini Dar es Salaam. Wako pale, karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 93 na walimu saba kutoka *Saint Mary Rwakatare Memorial International School* ya Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana kwa mafunzo watoto wetu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 18 kutoka Chuo cha Biblia cha Jijini Dodoma. Wako pale juu, karibuni sana katika Ukumbi wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali, kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, nimwite sasa Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima aweze kuuliza swali lake. Simwoni, na sioni watu wanao-*volunteer*. Eeh, Mheshimiwa Shangazi. *(Makofi)*

Na. 475

Ilani za Uchaguzi Kuendana na Dira ya Taifa

MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha Ilani za Uchaguzi za Vyama vya Siasa zinaendana na Dira ya Taifa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo umeshirikisha wadau mbalimbali ikiwemo vyama vya siasa. Kwa mfano, mnamo tarehe 21 Agosti, 2024 Msajili wa Vyama vya Siasa aliandaa kikao cha vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu nchini, kwa lengo la kuwapa nafasi viongozi wa vyama hivyo kutoa maoni yao kuhusu Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hiki pamoja na mambo mengine, viongozi wa vyama vya siasa walitoa maoni na kukubaliana kuwa maudhui ya Ilani ya vyama vyao kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa

mwaka 2025 yaakisi maudhui ya Dira 2050. Hivyo, Serikali inaamini kuwa vyama vya siasa vitazingatia makubaliano yao na kutumia kikamilifu maudhui ya Rasimu ya Dira 2050 katika kuandaa Ilani ya vyama vyao vya siasa, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri kabisa ya Serikali, lakini nina jambo moja la nyongeza, aidha likawa swali ama ni ushauri. Kwa kuwa linazungumzwa kama ni hiari, lakini kama Dira ya Maendeleo ya Taifa inalihusu Taifa letu, kwa nini Serikali isiweke mkazo na msisitizo kwamba vyama vyote vinavyotengeneza Ilani ni lazima ziakisi Dira ya Maendeleo ya Taifa?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Dira ya Taifa Maendeleo rasimu yake italetwa hapa Bungeni kujadiliwa, na Bunge ndilo litakaloidhinisha, kwa hiyo, kama hayo ndiyo yatakuwa mapendekezo au matakwa ya Wabunge, ninadhani muda ukifika tutajadiliana na wakiweka hivyo tutaliweka. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu. Tutajadili hiyo Rasimu hapa, kwa hiyo utapata muda zaidi.

Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, nimwite sasa Mheshimiwa *Nagweja* Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba jina langu umeshindwa kulitamka baada ya wote kuwa Bungeni hapa kwa miaka 10, basi niombe swali langu namba 476 lipate majibu ya Serikali, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ninashukuru na samahani, kwa jina lako gumu kidogo.

Na. 476

Usafi wa Mazingira Maeneo ya Mjini

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha usafi wa mazingira kwenye makazi ya watu hasa mijini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba yake, Mheshimiwa Patrobass Katambi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha uhifadhi wa taka na usafi wa miji na majiji nchini, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa miongozo mahususi inayoelekeza mbinu za kupunguza uzalishaji wa taka. Miongozo hii ni pamoja na Mwongozo wa Kupunguza, Kutumia Tena na Rejeleza; Mwongozo wa Uwajibikaji wa Mzalishaji wa Taka Zitokanazo na Bidhaa Anazozizalisha; na Mwongozo wa Uwekezaji katika Sekta Ndogo ya Udhibiti wa Taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miongozo hii umeweza kupunguza baadhi ya taka hususan taka za plastiki zitokanazo na vinywaji vinavyohifadhiwa katika chupa za plastiki. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Mkakati wa Taifa wa Udhibiti wa Taka, ambapo mkakati huo utahusisha usimamizi wa taka katika mnyororo mzima wa uzalishaji na udhibiti wa taka kuanzia katika vyanzo vya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kuhimiza Sekta Binafsi kuendelea kuwajibika kwa taka zinazotokana na bidhaa zinazozalishwa pamoja na kuchangamkia fursa ya udhibiti wa taka kwa kuwa taka ni mali na ni malighafi katika uzalishaji wa bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wananchi wote kujenga tabia ya usafi wa mazingira yao na kuhakikisha kuwa kila mmoja wetu anawajibika kwa taka anazozizalisha, ili kuifanya Tanzania kuwa safi na salama na kuiepusha jamii na magonjwa ya milipuko yanayoweza kutokea, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa magari mengi yanayozoa taka ni mabovu, na yakipita barabarani yanamwaga taka chafu zinazonuka, na kwa kuwa tunajua Mawaziri wengi mnaenda nchi za nje na mnaona wenzetu wanavyozoa taka, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba magari haya yanakuwa mazuri na yanabeba taka zile kwa ustadi mzuri, badala ya kwenda kuzimwaga njiani kwenye kila barabara inayopita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa ubora wa miji siyo kuzoa taka tu, tunajua kwamba mitaro yetu mingi imetengenezwa, lakini imejaa taka, barabara zetu zimejaa taka, vibanda vingi vimetengenezwa ovyo ovyo kila mahali ukipita unakuta huyu anauza hapa mchanga, huyu anauza chakula, huyu anauza vitu ambavyo haviendani kabisa na matakwa ya mipango miji; na kwa kuwa tumeona Serikali yetu ina Wizara tatu ambazo zote zinahusiana na mazingira, kwa mfano, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi, Wizara ya TAMISEMI ambayo ni halmashauri, na Wizara hii ya Makamu wa Rais, ...

MWENYEKITI: Ninaomba uulize swali.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Je, Serikali haioni ni wakati mwafaka kuangalia tuwe na taasisi moja ambayo itaangalia jinsi ya kuboresha miji yetu iwe mizuri na ya kisasa, ambapo hata watalii wakija wanaona kweli nchi ya Tanzania ni nzuri? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kaboyoka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ninakubaliana naye kwamba kuna wakati mwingine yapo magari ambayo yanaonekana ni mabovu yanayohusiana na takataka; lakini nieleze tu Bunge lako Tukufu kwamba tunazo sheria mahususi za utaratibu wa usimamizi wa masuala ya mazingira na usafi wa mazingira pamoja na afya. Kwenye halmashauri zetu, tunayo Sheria ya Mamlaka za Miji na Majiji ya Sura Namba 288.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria hii inaruhusu kutungwa kwa sheria ndogo kwenye kila halmashauri nchini, kuweza kuhakikisha kwamba wanakuwa na sheria ndogo za masuala ya afya na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika sheria hii inaelekeza kwamba, kupitia halmashauri, Mkurugenzi wa Jiji au Mji atakuwa na haki au anao wajibu wa kutengeneza vikundi ambavyo vitakuwa ni vikundi mahususi kwa ajili ya ukusanyaji wa taka. Pia, anapewa *power* za kisheria za kuweza kuingia mikataba na watu wanaoweza kufanya kazi (kandarasi) za kusafisha majiji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati mwingine kumekuwa na udhaifu katika namna ya kuingia mikataba ile au wale wanaopewa kazi hiyo wanajikuta hawana vifaa vya kutosha au utoshelevu kulingana na mikataba inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhamasisha sasa mamlaka zetu za Serikali za Mitaa huko chini kuendelea kusimamia vizuri, kwa sababu tunazo na sheria ndogo hizi zinazohusu hifadhi ya usafi na mazingira, zinaeleza ndani ya hiyo sheria, inaeleza namna gani ambavyo masuala ya utoaji wa huduma za chakula, usafi uweje na kunakuwa na mkaguzi ambaye anapewa idhini na Mkurugenzi kufanya kaguzi. Hata wale wahudumu wale wanaotoa huduma wanahitaji hata kupimwa kila baada ya miezi sita afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo upo wajibu kwa upande wa wananchi kufanya usafi kila kipindi kulingana na sheria hizi ndogo. Kuna siku maalum ambazo zimetengwa kulingana na halmashauri husika. Kwa hiyo, mkazi, mmiliki wa biashara au mmiliki wa nyumba au eneo la wazi, anao wajibu wa kuhakikisha anafanya usafi kwenye mitaro, mifereji lakini pia maeneo yote yanayozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi ndogo katika kila halmashauri zinatoa pia adhabu ya faini au kifungo cha miezi sita... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu yako ni marefu sana. Nadhani ameelewa. Ni usimamizi zaidi...

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria tunazo, tunachohitaji ni usimamizi zaidi ili kuweza kuhakikisha kwamba tunachukua hatua na kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa salama. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula.

MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika maeneo mengi ya miji hasa kwa wananchi wanaokaa karibu na mito na mifereji, wamekuwa wakitupa mara kwa mara taka

katika mifereji ile na kusababisha kuziba kwa maeneo mengi na kuleta mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, magugumaji pia yametambaa katika maeneo ya ziwa kiasi kwamba yanakwenda kufifisha mazalia ya Samaki. Nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba magugumaji yote yanatoka, na pia watu hawa wanaotupa takataka katika mifereji wanadhibitiwa?

MWENYEKITI: Swali ni moja, kuhakikisha magugumaji yanatoka. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la utupaji taka ovyo ni rai yangu nitoe, lakini pia ni kwa mujibu wa sheria. Ni marufuku kwa mwananchi yeyote kutupa taka tofauti na maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya ukusanyaji taka. Kwenye maeneo hayo ndiyo inapopaswa kwenda kutupa taka. Kwa mfano, sheria inahamasisha hata kwenye familia zetu na maeneo ya biashara, maeneo ya viwanda kuwa na sehemu maalum na vyombo maalum kwa ajili ya utupaji wa taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kosa kisheria na kuna adhabu hapa ya faini au kifungo kwa yeyote ambaye atafanya tofauti na hivyo na nihamasishe sheria itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magugumaji. Ofisi ya Makamu wa Rais inazo programu tayari za ukuhakikisha kwamba kwenye maeneo yote ya Bahari, na pia ziwa, mito na maeneo yote ambayo yamekuwa na huo uoto wa magugumaji, kuna jitihada na programu ambazo zimekuwa zikifanyika mahususi kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba yanatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii imeshafanyika Babati, Mwanza, pia kazi hiyo inaendelea chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ahsante.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hivi unavyoniona, masikio yangu sasa hivi hayako vizuri kutokana na pikipiki zinazoweka sauti kali sana pamoja na magari. Kuna siku nimepatwa na hilo tatizo. Nini mpango wa Serikali kudhibiti hatua hii ya uharibifu wa sauti katika maeneo yetu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo hili ni kweli, yapo magari na pikipiki ambazo wanazihuisha au kuharibu ile *muffler* ili itoe sauti ambayo ni kinyume na sauti ambayo imetengenezwa au muungurumo tofauti. Hili ni kosa kwa sababu kwanza ni *noise pollution* na kwa mujibu wa sheria, hili linaweza kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana kwa sababu tunafanya kazi kwa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, waweze kutusaidia kwa sababu vyombo hivi vya moto vina utaratibu wake na sheria ipo, waweze kuchukua hatua. Hasa kwa vijana walio wengi sasa hivi, imeendelea kuwa *fashion* kwenye kuharibu mazingira, lakini pia kuleta hali ya kukosa utulivu hasa kwa wale walio na magonjwa ya mshtuko kama ugonjwa wa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa pamoja tushirikiane nao kuweza kuhakikisha tunatatua tatizo hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Nimwite Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, aulize swali lake.

Na. 477

Tozo Daraja la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na la Tanzanite Jijini Dar es Salaam

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza: -

Je, kwa nini watumiaji wa Daraja la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wanalipia kila wanapopita huku watumiaji wa Daraja la *Tanzanite* hawalipi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumiaji wa Daraja la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wanalipia kila wanapopita kwa sababu daraja hili limejengwa kwa utaratibu wa ubia *(Public Private Partnership - PPP)* ambapo mwekezaji hurudisha fedha zake alizowekeza pamoja na faida kutokana na tozo kwa watumiaji. Kwa upande wa Daraja la Tanzanite watumiaji hawalipi kwa sababu daraja hilo limejengwa kwa utaratibu wa kawaida kama uliotumika kujenga madaraja mengine nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Daraja la Tanzanite linahudumia ukanda wa Kinondoni, watu wenye uwezo mkubwa kipesa. Wakati huo huo Daraja la Kigamboni linahudumia watu kawaida. Serikali haioni kwamba kuwatoza hao wenye kipato cha chini na kuwaacha wenye kipato kikubwa inaleta mkakanganyiko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa Serikali ina majukumu makubwa na mahitaji makubwa sana ya kipesa kwa ajili ya kujenga miundombinu hasa vijijini. Je, haioni ni busara kutoza kwenye lile

Daraja la *Tanzanite* ukizingatia wanaopita wengi wana uwezo, tukatumia hizo pesa kulipa mkopo na wakati huo kujenga barabara ambazo tuna mahitaji makubwa hasa kwenye Jimbo langu la Muleba Kusini? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Kasekenya.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ilivyojibu jibu lake la msingi, hapa katika nchi yetu ya Tanzania, madaraja yote tumekuwa tukijenga kwa utaratibu wa kwamba yatatumika bure na ndivyo umekuwa utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi nimesema, Daraja la Kigamboni lilijengwa kwa ubia; ambapo Serikali ilijenga pamoja na wenzetu wa *NSSF* ambao waliwekeza fedha na ndiyo maana kukishakuwa na ubia maana yake kuna tozo ama kuna malipo ambayo yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu Daraja la Tanzanite pamoja na madaraja mengine, kumekuwa na maoni mbalimbali ikiwepo hata Kamati ya Miundombinu ambayo imekuwa inashauri kwamba yale madaraja makubwa ambayo Serikali imetumia fedha nyingi, pengine ifikie wakati wa sasa watumiaji kuanza kuyalipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Serikali imeendelea kupokea maoni na Bunge hili, pengine itafika mahali litatengeneza utaratibu ama litatoa mapendekezo ama maoni kwamba ni madaraja yapi ambayo sasa yaanze kulipiwa na Serikali itaendelea kukusanya maoni, kuona kama suala hilo lini lianze kutumika kutokana na maoni ya wananchi ili tuendelee kujenga madaraja mengine kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

MWENYEKITI: Tunaendelea. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, nimwite sasa Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, aulieze swali lake.

Na. 478

Hitaji la Mnara Eneo la Mbawala Chini Kata ya Naliendele – Mtwara

MHE. HASSAN S. MTENGA aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga mnara katika Eneo la Mbawala Chini, Kata ya Naliendele, Manispaa ya Mtwara Mikindani? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Maryprisca.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Naliendele ipo Minara ya Mawasiliano ya simu iliyojengwa na watoa huduma ambao ni Kampuni ya Airtel, Vodacom na Honora. Minara hii inatoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kuhusu kujengwa kwa mnara katika kata tajwa, inaashiria kuwa bado kuna changamoto ya upatikanaji wa mawasiliano ya simu. Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itafanya tathmini kwenye kata tajwa ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano ya simu, na endapo ikibainika kuwepo kwa tatizo la mawasiliano katika kata husika, itaingizwa katika zabuni ya miradi itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtenga, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa nafasi. Pia naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na ninamshukuru Naibu Waziri kwa kweli kazi anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Serikali imejenga minara maeneo tajwa, lakini eneo la Naliendele ya Chini, tukizungumza maeneo ya Naulongo, na kuelekea mpaka kwenye hospitali ya kanda pale hakuna mawasiliano. Je, ni lini Serikali itakuja kutujengea minara hiyo ili hospitali ya kanda na maeneo mengine niliyoyazungumza tupate mawasiliano? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nipokee shukrani za Mheshimiwa Mbunge, na pia nikushukuru kwa kunipongeza mimi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, nikuhakikishie mwaka ujao wa fedha (2025/2026) tutahakikisha Maeneo ya Naliendele ya Chini yanaweza kujengewa minara, mawasiliano yawe ya uhakika. Vilevile, kwenye hospitali ya kanda, wito wetu ni kuhakikisha maeneo yote yanayotoa huduma za umma kama hospitali na shule yanapata mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, nitoe pongezi kwa Serikali kutujengea mnara mzuri sana pale Mwakashindye. Nina swali la nyongeza. Lini Serikali itajenga mnara katika Kijiji cha Mbeya, Kata ya Igulungu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Maige kwa ufuatiliaji, na juzi tu tulikuwa pamoja jimboni kwake kwenye ziara ya

kuhakikisha mawasiliano yanapatikana maeneo yote. Kijiji cha Mbeya kipo kwenye utaratibu, mwaka ujao wa fedha (2025/2026) na chenyewe tutakifikia kuhakikisha mawasiliano yanakaa vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

(Hapa kulikuwa na tatizo la kipaza sauti)

MWENYEKITI: Naona kuna shida ya visemeo huko. Wakati unatafuta kisemeo, hebu twende kwa Mheshimiwa Eng. Hhayuma.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwezesha hii mitandao ya simu iwe inaingiliana, badala ya sasa hivi mtu kwa wilaya kubwa kama ya Hanang ili uwe na uhakika wa kupata mawasiliano kila sehemu lazima uwe na simu zaidi ya nne? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mkakati unafanya kazi. Tumeshawaelekeza watoa huduma kama mwenzake ameshajenga mnara pale, basi waweze kutumia ule mnara kwa umoja wao. Vilevile tayari tunao mkakati wa kuona kwamba unatumia *line* moja kwa watoa huduma wote, pia michakato inaendelea. Lengo ni kuhakikisha mtu anatumia simu moja kumpunguzia mizigo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ntara, upo tayari?

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Naongea kwa sauti.

MWENYEKITI: Aah, tunataka *Hansard* iweze ku-*record*. Kama haupo tayari, basi tunaendelea. Kuna visemeo vinafanya kazi pale, naomba usogee kwa haraka. *(Makofi)*

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyote vinafanya kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omari Kigua naomba uendelee wakati Mheshimiwa Dkt. Ntara anajiandaa.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

MWENYEKITI: Uko tayari? Basi endelea Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba, ni lini mtarekebisha mawasiliano kutoka Njombe mpaka Songea? Maana yake pale katikati tukifika tu Njombe, ndiyo hatuwezi kuwasiliana kabisa na ndugu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kwa ufuatiliaji wa mawasiliano ya uhakika eneo la Njombe – Songea, naomba niwe nimepokea. Wataalam watakwenda kulifanyika tathmini na kuhakikisha linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omari Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka kujua kwamba ni lini Serikali itatujengea mnara kwenye Kijiji cha Masileye kwenye Kata ya Pagwi? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Omari Kigua; lengo la Serikali ni kuhakikisha vijiji vyote tunavifikia na kupata

mawasiliano ya uhakika. Kwa hiyo, Kijiji hiki alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, Masileye na chenyewe tutahakikisha mwaka ujao wa fedha (2025/2026) kinakuja kufanyiwa tathmini na kuhakikisha mawasiliano ya uhakika yanawafikia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kandege, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba mtandao wa mawasiliano ya simu yanapatikana *along the way SGR* yote kuanzia Dodoma mpaka Dar es Salaam? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Kandege kwa ufuatiliaji wa mawasiliano ya uhakika. Katika barabara nzima ya *SGR* tayari wataalam wamefanya tathmini, na kazi inaendelea kuhakikisha barabara nzima toka tunavyotokea Dodoma mpaka Dar es Salaam watu waweze kupatikana bila kukatika mahali popote. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako. Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nimwite sasa Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu aulize swali lake.

Na. 479

Hitaji la Magereza Wilaya ya Kishapu

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Kishapu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Sillo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kishapu iliyopo Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa wilaya 50 nchini ambazo hazina Magereza. Aidha, mchakato wa maandalizi ya ujenzi wa Gereza la Wilaya Kishapu umekamilika sambamba na upatikanaji wa eneo la ekari 200 na zoezi la kuwalipa fidia wananchi wanaopisha eneo la ujenzi wa gereza limekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Gereza hilo utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia mpango mahsusi wa ujenzi wa magereza mapya kwenye wilaya zisizokuwa na magereza nchini, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Butondo, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali iliweka katika mpango wa bajeti kutekeleza ujenzi wa Magereza hii ya Wilaya ya Kishapu lakini kwa bahati mbaya mpaka hatua hii ya mwisho utekelezaji wake haujatekelezwa. Je, Serikali iko tayari kuwahakikishia wananchi wa Kishapu kwamba Magereza hii itaenda kujengwa katika mwaka wa fedha unaokuja (2025/2026)? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna changamoto kubwa ya usafiri na hasa kwa wale mahabusu ambao wanakuwa na mashauri katika Mahakama iliyopo katika Wilaya ya Kishapu na inawabidi wasafirishwe kwenda Manispaa ya Shinyanga kuliko na Magereza ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba inawapatia Mahakama ya Wilaya ya Kishapu na magereza kuhakikisha kwamba wanapata usafiri ambao utasaidia mahabusu hukudhuria mashauri kwa wakati bila usumbufu wa aina yoyote? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake katika ujenzi wa gereza katika eneo la Kishapu. Ni kweli, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Gereza la Kishapu lilikuwa limewekwa kwenye mpango, lakini halikutengewa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kishapu kwamba kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ndiyo tunatenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa magereza hapo Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gari, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshaagiza magari 11, kwa takribani shilingi bilioni 2.5. Basi Wizara ya Kishapu pia tutaiweka kwenye mpango ili wapate gari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu kwenda kusikiliza mashauri yao katika Halmashauri ya Shinyanga, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimewaona mliosimama, lakini ninaomba maswali kwa kifupi. Moja kwa moja tuanze na Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna magereza ambayo yapo kwa ajili ya wafungwa kwa maana ya uzalishaji wa kilimo na mifugo takribani saba nchini yaliyojengwa enzi ya miaka ya 1970 ni ya matope, lakini sasa hivi yana wafungwa wachache, Askari Magereza wengi, hivyo hayana tija katika uzalishaji. Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kupunguza magereza haya yabaki walau mawili ili yaweze kuzalisha kwa tija? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther ametoa ushauri na sisi kama Serikali tunaupokea ushauri huo kwenda kuufanyia kazi tuone namna ya kuboresha eneo hilo, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pauline Gekul.

(Hapa kulikuwa na tatizo la kipaza sauti)

MWENYEKITI: Ninaomba wanaouliza maswali upande wa huku wawe wameshajaribu visemeo kama vinafanya kazi, tuendelee na Mheshimiwa Fiyao.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Magereza nyingi nchini zina hali mbaya sana na ni chakavu. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha mnakarabati Magereza haya ili yawe katika hali nzuri au kujenga Magereza mpya nzuri na za kisasa ambazo zinaendana na wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuzikarabati Magereza zote, ndiyo maana hata mwaka wa fedha huu wa 2025/2026 tumetenga shilingi bilioni 6.27 kwa ajili ya kufanyia ukarabati Gereza la Keko, Segerea, pamoja na Lilungu lililoko Mkoa wa Mtwara, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pauline.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Gereza la Mji wa Babati ni gereza linalotumika na Mkoa mzima wa Manyara; na wafungwa na mahabusu wamekuwa ni wengi, nafasi hazitoshi kabisa. Je, nini mkakati wa Serikali kujenga Gereza la Mji wa Babati ambalo ni la Mkoa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Gereza la Babati ni dogo na kama alivyosema lina msongamano mkubwa, lakini tutaliweka kwenye mpango wa Gereza la Mkoa wa Manyara ili tuhakikishe tunajenga gereza kubwa

linalotosheleza mahabusu pamoja na wafungwa katika eneo hilo, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selemani Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Kilimo la Kalilankulukulu ni gereza la muda mrefu, lina uchakavu wa hali ya juu na halina nyumba za watumishi. Je, ni lini Serikali itaenda kupeleka fedha za ukarabati wa gereza na kujenga nyumba za watumishi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Serikali ina mpango wa kukarabati hayo Magereza, lakini hatuwezi kukarabati kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, kila mwaka tunatenga bajeti kwa mwaka. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pia gereza lake ambalo amelitaja, tutaliweka kwenye mpango ili kutengewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa uhakika, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asenga, umelisikia jibu hapa. Swali ni hilo hilo? Haya, kwa kifupi.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Lini Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kutembelea Gereza letu zuri la Kiberege kujionea miradi yetu mizuri na kuunga mkono miradi ya gereza? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge ili tupange namna ya kwenda kuona kazi kubwa inayofanyika katika gereza hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, nimwite Mheshimiwa Stella Ikupa Alex Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Mheshimiwa Stella.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba...

MWENYEKITI: Makamu Mwenyekiti, kisemeo kinafanya kazi?

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kinafanya kazi.

MWENYEKITI: Endelea kwa niaba ya Mheshimiwa Stella.

Na. 481

Lugha ya Alama kuwa Lugha Rasmi ya Mawasiliano

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. STELLA I. ALEX aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuifanya lugha ya alama kuwa lugha rasmi ya mawasiliano?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua lugha ya alama kama mojawapo ya lugha rasmi za mawasiliano miongoni mwa wenzetu wenye changamoto ya usikivu hafifu. Aidha, Kanuni za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) za mwaka 2019, Kifungu cha 34 (1 - 3) na 35 (1 - 3) vinaeleza namna bora ya usimamizi na uendeshaji wa ukalimani wa lugha ya alama ikiwa ni pamoja na kuunda kanzidata ya wakalimani wa lugha hiyo na kuratibu utumiaji wao katika shughuli mbalimbali za kiserikali na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kusaidia ukuaji na weledi katika taaluma hii kwa kuwapatia mafunzo ya msasa yatakayowasaidia kuwa wakalimani bora na wanaoweza kutumiwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kupitia Kanuni hizo, tayari kanzidata ya wakalimani wa lugha hiyo imeanza kuundwa ambapo zaidi ya wakalimani 300 wamejisajili na hatua inayofuata ni kuwapa mafunzo na kubainisha wale wanaokidhi vigezo. Vilevile, muundo wa utumishi wa kada hii tayari umeandaliwa. Hatua nyingine zilizopangwa na Serikali ni pamoja na kuwawezesha wale watakaokidhi vigezo kujifunza pia alama za Kimataifa ili waweze kutumiwa ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nitumie tu fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa jitihada ambazo inaendelea kuchukua kwa ajili ya kutoa elimu kwa watu wenye uhitaji maalumu. Tunaiomba Serikali iendelee kutoa elimu hii kwa jamii nzima siyo kwa ajili ya wenye uhitaji pekee yake, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa nimwite Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki aweze kuuliza swali lake.

Na. 482

Wanyamapori Waharibifu Singida Mashariki

MHE. MIRAJI J. MTATURU aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tembo ambao wanasumbua na kuharibu mashamba ya wananchi wa Singida Mashariki?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti tembo wanaovamia na kuharibu mashamba ya wananchi wa Singida Mashariki, Serikali kupitia *TAWA* inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuweka vikosi viwili vyenye Askari 24 wakiwemo Wahifadhi 13 na Askari Wanyamapori wa Vijiji 11 na kutoa magari matatu. Vilevile, kuimarisha matumizi ya ndegenyuki kwa kuwafukuza tembo kutoka kwenye maeneo ya wananchi na kuwarejesha hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, kati ya mwezi Novemba, 2024 na Mei, 2025 kikosi maalum cha Askari wa Hifadhi 18 na *VGS* Sita, kikitumia ndege nyuki mbili na mabomu baridi kiliweka kambi katika Jimbo la Singida Mashariki, Wilayani Ikungi na kufanikiwa kudhibiti makundi 23 ya tembo kwa kuwarudisha ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo. Mathalani, kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025, elimu hiyo imetolewa kwa wananchi 517 na Askari 110 wa Jeshi la Akiba katika Kata za Mkiwa, Igombwe, Iglansonia, Mang'onyi, Issuna, Ntuntu na Ikungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kutumia teknolojia ikiwemo ndegenyuki na kufunga visukuma mawimbi ili kufuatilia mienendo ya tembo na kuwadhibiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ambayo wametupatia. Ninaomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kupitia Wizara, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kufukuza tembo wale ambao walikuwa wasumbufu wakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata usiku wa kuamkia tarehe moja ya mwezi wa Sita, kulitokea tena kundi ambalo lilienda kufukuzwa na vijana hawa wa *TAWA*. Ninaipongeza sana Serikali, ambapo Mheshimiwa Mzee Augustino Joseph nyumbani kwake pale waliharibu sana mazao. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kama alivyosema hapa, nini mkakati wa Serikali wa kudumu ili kuondokana na tatizo la tembo ambao wanaharibu sana uchumi wa wananchi katika haya maeneo yetu ambayo nimeyataja katika Vijiji vya Mkiwa, Issuna, Mang'onyi, pamoja na Ntuntu. Hali ni mbaya sana kwa sababu kila siku makundi haya yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Toka mwaka 2021 mpaka tunavyoongea ni miaka takribani mitano, matukio au wananchi zaidi ya 400 wameharibiwa vitu vyao pamoja na mali zao na mashamba ikiwemo na wengine kupoteza maisha. Ni nini hatua ya Serikali kuwalipa kifuta machozi wananchi hawa ambao kwa kweli wengi wao bado wanalia mpaka leo, ukizingatia wiki iliyopita nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Naibu Waziri akaniambia wanafanya tathmini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tathmini hiyo imeisha? Kama imekamilika, ni nini hatua ya Serikali kuwalipa wananchi hawa ili kuwafuta machozi kwa kuondokewa na ndugu zao na mali zao ambazo mpaka leo hawajalipwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali inajidhatiti kukabiliana na changamoto hii ambayo kwa kweli imesambaa katika maeneo

yetu nchi nzima. Tunapambana na aina ya mnyama ambaye uwezo wake wa kiakili na maarifa ni mkubwa sana. Kwa hiyo, huwa anabadilikabadilika ili kuweza kukwepa ile mikakati ambayo tunaiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachofanya kila siku inavyokwenda, tunabuni mbinu mpya na kubadilisha mifumo ya kukabiliana na wanyama hawa ili kuondokana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, tumeweka mkakati pale ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza Askari karibu na makazi ya watu. Vilevile tunao mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi ili wajue tabia za wanyama hawa na jinsi ya kujilinda nao. Tatu, tumesema tunakwenda na mkakati wa kutumia teknolojia sasa, ndegenyuki, kufunga mikanda ili kudhibiti mienendo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ambalo elimu yetu tunaielekeza kwa wananchi ni kwamba, ni ukweli usiopingika kwamba kama Taifa idadi ya wananchi imeongezeka, maeneo ambayo zamani yalikuwa ni maeneo mahsusi kwa ajili ya wanyama hawa, shughuli za kibinadamu zimeongezeka kwenye maeneo yale, na migogoro hii imeongezeka. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inachukua jitihada zote uhakikisha kwamba tunawanusuru wananchi na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lake la pili, ni kweli nimpongeze, tulikuwa na kikao naye wiki mbili zilizopita ofisini. Tulimwahidi kwamba, tunakamilisha tathmini ya wale waliopata madhara, na tathmini ile imekamilika. Tunajua sasa tunahitajika kulipa zaidi ya shilingi milioni 104 kwenye Jimbo lake, kwa hiyo, ninamwomba awe na subira. Tayari tumeshaomba kibali kutoka Wizara ya Fedha, na mara tu baada ya fedha hizi kupatikana tutawalipa wahusika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninayo *list* ya watu wengi wanaotaka kuuliza maswali hapa, lakini kama ni swali la uvamizi wa tembo, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu *very comprehensively* hapa mikakati mbalimbali, kwa hiyo ninaomba wale watakaouliza maswali

wawe ni watu ambao watauliza maswali tofauti kwa sababu hamtapata majibu zaidi ya hayo niliyoyasikia hapo. Tuanze na Mheshimiwa Catherine Magige.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Hivi karibuni kumekuwa na viashiria vya udhalilishaji dhidi ya kabila la jamii ya Wahadzabe, kwa watoto wadogo na hata watu wazima wanaoishi porini. Wamekuwa wakirekodiwa kwa kudhalilishwa. Kwa mfano tu, unakuta anapewa soda hawezi kuifungua, anaitoboa wanawarekodi, au wanakaa kwenye kiti cha gari cha dereva wanataka wakae wawili. Je, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lina utajiri wa makabila zaidi ya 120. Kwa wingi huu wa makabila tuna utajiri wa mila, tamaduni, desturi, lakini na maarifa ya asili ambayo kama Taifa tuna wajibu wa kuyalinda kwa wivu mkubwa, na Serikali inajielekeza kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa viashiria vyovyote ambavyo vinafanywa na baadhi ya wananchi wenzetu, kutweza utu wa Mtanzania havikubaliki kisheria. Sheria zetu ziko wazi, tunakwenda zaidi pale ambapo sasa mitandao inatumika kusambaza maudhui yanayotweza utu wa Mtanzania, sheria zetu ziko wazi, ni makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kukemea vikali wale wote ambao wanasambaza, wanatengeneza maudhui ya kutweza utu wa Mtanzania. Serikali haitasita kuchukua hatua kali kwa wale wote watakaobainika kufanya vitendo hivi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Naona mmepungua, afadhali. Mheshimiwa Sylvia Sigula.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na mikakati mizuri ya Serikali, bado kilio kikubwa cha wananchi wa Kabwe na Kirando ni uharibifu wa mazao kutokana na tembo. Tunavyoongea sasa hivi, uharibifu unaendelea. Ninataka kujua kauli ya Serikali ya haraka ya kuhakikisha uharibifu huu unaoendelea sasa hivi unakomeshwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kwenye maswali ya msingi, jambo hili ni jambo kubwa, ni jambo ambalo Serikali inapambana nalo kuhakikisha tunawahakikishia wananchi kwanza, usalama wa maisha yao, vilevile wa mali zao. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya kipindi hiki cha maswali, nikutane naye anieleze eneo hilo ni nini hasa kinatokea ili timu zetu zilizopo uwandani ziweze kuchukua hatua kwa haraka. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Kata ya Oldeani Wilayani Karatu, kumekuwa na matukio, na kila mwezi ni lazima tusikie vifo vya wananchi kutokana na nyati kutoka katika Hifadhi ya Ngorongoro kuingia kwenye maeneo ya watu na kujeruhi. Mwezi uliopita watu wawili wamefariki, na haya matukio tunayasikia kila siku, inafika mahali wananchi wamechoka. Nini kauli ya Serikali kudhibiti wanyama hawa wasiingie ili wananchi waishi kwa usalama? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba tunalichukulia kwa uzito mkubwa jambo hili, na tunalishukuru Bunge lako Tukufu liliridhia kwamba, katika eneo lile sasa tuweze kwenda kuweka uzio wa umeme kwa ajili ya kuwanusuru wananchi. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge

kwamba, tutafanya kila linalowezekana kulinda uhai wa wananchi na mali zao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Jimbo langu la Itigi, Halmashauri ya Itigi, Vijiji vya Gurungu, Sanjaranda, Njirii, Kamenyanga, vina changamoto kubwa ya tembo kwa muda mrefu. Zamani Askari wa Wanyamapori, tembo wakishaingia makundi makubwa mara mbili, mara tatu, mara nne na sasa ni miaka mitano karibu, walikuwa wanapiga tembo mmoja, wale tembo wanarudi kwenye Hifadhi ya Muhesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali sasa iko tayari kutoa kibali angalau tembo mmoja akapigwa ili wale warudi katika hifadhi na wananchi wapate angalau nyama, maana kwa muda mrefu wameliwa mazao yao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi, mnyama tembo ni mwenye maarifa mengi. Inawezekana mbinu iliyokuwa ikitumika miaka ya nyuma ya kuwawinda leo hii isiwe ni jibu. Ninaomba atupatie fursa hii, tutatuma timu yetu iende ikaangalie nini hasa kinaendelea kwenye eneo lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi katika eneo hili la Itigi, Manyoni mpaka kule Singida, eneo hili kiasili ni ushoroba wa hifadhi ya kutoka kule Ruaha kwenda kwenye mapori ya akiba ya Rungwa, Kigosi, Muhesi. Haya yalikuwa ni maeneo ambayo tembo walikuwa wanazagaa. Katika miaka ya karibuni shughuli za kibinadamu zimeongezeka kwenye eneo hili, na hiki ndicho chanzo kikubwa kinacholeta mgogoro huu. Tunaendelea kutoa elimu, tunaomba tusaidiane ili tulitatue jambo hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, nimwite Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 483

Ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Kituo Kikuu cha *SGR* Dodoma hadi Uwanja wa Ndege Msalato

MHE. FATMA H. TOUFIQ aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga reli ya kisasa kutoka Kituo Kikuu cha *SGR* Dodoma hadi Uwanja wa Ndege Msalato?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa katika Jiji la Dodoma *(Dodoma Commuter Train)*. Ujenzi wa Reli hiyo unalenga kuimarisha usafiri katika Jiji la Dodoma kwa kuunganisha Jiji na viunga vyake ikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali ipo katika hatua za utafutaji wa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Kwa kuwa Serikali imeanza utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli hii, je, haioni upo umuhimu wa kupata wabia ili kuharakisha ujenzi wa reli hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Ah, *okay,* kuna swali la pili.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa *Magufuli City* ni eneo ambalo Wizara mbalimbali za Serikali pamoja na Idara za Serikali zipo kule na ufikaji wake nao umekuwa ni wa kusuasua, je, Serikali haioni kwamba miongoni mwa vipaumbele vya maeneo ya viunga vya Dodoma kujengewa reli kama hii ni pamoja na *Magufuli City*? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq kwa jinsi anavyofuatilia kwa ukaribu mapinduzi ya reli nchini na kipekee reli ya maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza maswali mawili; la kwanza ni umuhimu wa kupata wabia. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na wabia wa Sekta Binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya reli na miundombinu mingine, mwaka 2023 ilifanya maboresho ya Sheria Na. 10 ya 2017 ambapo sasa tumeruhusu wawekezaji binafsi au wabia kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa reli yetu. Hivi ninavyozungumza, tumekwishaanza taratibu kwa ajili ya kupata wabia kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo katika Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hiyo pia kuendelea kutangaza kwa yeyote mwenye mbia yeyote ambaye anapenda kushiriki katika maeneo haya mawili, nafasi na fursa ipo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, amezungumzia kwenye upande wa *Magufuli City*. Sote ni mashahidi kwamba huu ni mji mzuri na mkubwa ambao Serikali imetenga fedha nyingi kuuendeleza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *Magufuli City* ni sehemu ya mradi wa *Commuter train* wa hapa Dodoma, hivyo basi, tumeshakamilisha usanifu, na sasa tunatafuta fedha. Tutakapopata fedha, hatua itakayofuata ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpe habari njema Mama yangu Mheshimiwa Toufiq, anakumbuka juzi tarehe 30 mwezi wa Tano hapa

Dodoma, CCM ilizindua Ilani yake ya Miaka Mitano ijayo. Ukienda katika ukurasa wa 25 mpaka 31 imeainisha kwa kina miradi itakayokwenda kutekelezwa. Katika miradi hiyo ukisoma ukurasa wa 29, mradi huu umetaja kwa kina wa kujenga reli ya kisasa katika Miji ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tumwombee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aweze kuendelea kuongoza nchi yetu kwa kipindi cha pili kwa maana ya kwamba atakapochaguliwa itadhihirisha na kumaanisha tunakwenda kutekeleza miradi hii miwili ambayo nimeshaielezea hapo awali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako ya maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Kiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara Mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali Na. 482 Wizara ya Maliasili na Utalii, alieleza mkakati wa Serikali wa namna ambavyo wanazuia tembo. Hata hivyo, ninaomba mwongozo wako kwa sababu tarehe 31, tembo wametoka Hifadhi ya Serengeti wakavuka Kata ya Kemambo, Matongo, Kibasuka, Kyole, Manga wakaenda mpaka Nyagise.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza kuna mama amechomwa na pembe ya ndovu, yupo Hospitali Kwangwa na hana huduma ambayo anasaidiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa ikitokea kesi kama hizi, mwongozo wako unisaidie huyu mama anapataje msaada kabla ya kuweza kupoteza maisha yake kwa sababu wana huduma ambayo ni ya gharama na familia yake haina uwezo wa kuchangia gharama hizo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali na tumekuwa na Mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Waitara kuhusiana na swali la tembo ambaye ameleta madhara na anaomba Mwongozo wa Kiti.

Ninaomba hili nilirudishe kwenye maongezi; yaani kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ameongea hapa kwa kirefu, amewataka baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakutane mara tu baada ya kikao hiki ili waweze kuongea. Nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri na yeye amwingize Mheshimiwa Waitara ili waweze kuliongea jambo hilo na kulipatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Spika anaingia kuendelea na Kikao.

Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuanze na tangazo la wageni. Kwanza tutaanza na wageni wangu ambao wamekaa Jukwaa la Spika, kisha tutaendelea na wengine.

Ninao wageni 16, kwanza yupo Ndugu Raphael Mollel ambaye ni Katibu wa Vijana Wilaya ya Mbeya Mjini; yupo Ndugu Lilian Mwakitosi, Kamati ya Utekelezaji UWT Mbeya Mjini; Ndugu Miriam Kikasi, Kamati Tendaji UWT Mkoa wa Mbeya; Ndugu Magreth Kalonga, Kiongozi wa Saneti Mkoa wa Mbeya; Ndugu Juliana Kibasa, Mjumbe wa Halmashauri Kuu UWT Wilaya ya Mbeya Mjini; Mheshimiwa Mariam Kabuje Diwani Viti Maalum; Mheshimiwa Attu Msai, Diwani Viti Maalum; Ndugu Tumaini Mwakasege, Mjumbe wa Baraza UWT Taifa kutoka Mkoa wa Mbeya na Ndugu Neema Mwangwala Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja MBEYAUWSA. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Nancy Evance, Mkurugenzi Mtendaji SOLABON Tanzania; Ndugu Jackline Ngalula, Daktari wa Hospitali ya Kanda ya Mbeya; Ndugu Herieth Ntukula Meneja MBEYAUWSA Kanda ya Uyole; na Ndugu Doroth Kasubi, Daktari Hospital ya Kanda. *(Makofi)*

Haya, wapo pia Ndugu Ester Gawile, Ndugu Monalisa Mabuku, na Ndugu Anna Yasin; karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliokaa Jukwaa la Spika, na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. Kwanza tutaanza na Dkt. Seif Shekalaghe ambaye ni Katibu Mkuu; Dkt. Magereza Mzee, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Zanzibar; Ndugu Ismail Rumatila, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Grace Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali na Prof. Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmeanza kupiga makofi kabla sijamaliza utambulisho wake, lakini sasa mmeyapiga kabla kwa hiyo, ni sawa pia yamepokelewa, lakini huyu ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, ahsante sana. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa makofi hayo, nitumie fursa hii kukupongeza sana Prof. Janabi kwa nafasi hiyo ambayo umeipata na tunakutakia kila la heri katika utendaji wako na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakupa ushirikiano ule unaostahili katika kazi yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana viongozi wote wa nchi hii ambao wameshiriki kwa namna moja au nyingine kuhakikisha ushindi huu unakuja Tanzania. *(Makofi)*

Kwanza, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wameshiriki katika jambo hili. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Elibariki Kingu kwa ushiriki wako wa moja kwa moja kwenye kampeni. Pia, Mheshimiwa Neema Lugangira na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kweli mlishiriki, wengine mnapiga simu huku na kule; tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Pia, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Afya Mheshimiwa Jenista Joakim

Mhagama, umefanya kazi nzuri sana, tunakushukuru kwa kampeni nzuri wewe na Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuwa hapa ameshikilia kiti wakati wewe unafanya hiyo kazi huko Kimataifa, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Pia umeshirikiana na viongozi wengine wengi, wewe ukiwa unaongoza timu hiyo. Tunakushukuru kwa sababu kama usingeshirikiana nao vizuri, kampeni zingekuwa ngumu. Kwa hiyo, tunakushukuru. *(Makofi)*

Kwa viongozi wale ambao hawapo hapa Bungeni wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, tunawashukuru sana kwa namna walivyofanya kazi hii kwa ukubwa kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tulisema jambo hili kabla ya leo, lakini pia na Jumamosi tulisema nitumie pia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Mheshimiwa Rais wetu kwa namna ambavyo anajitoa sana kuhakikisha wananchi wa nchi hii, wale ambao wanaweza kuonyesha uwezo huko nje, basi anakwenda nao moja kwa moja. *(Makofi)*

Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anajitoa kwenye kuhakikisha wananchi wake wanaonyesha vipaji huko nje. Kama nilivyosema, kwa kweli tupo wengi, lakini Mheshimiwa Rais mchango wake ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Dkt. Ntuli Kapologwe ambaye ni Mkurugenzi Mkuu (nadhani hapa ni Kitengo cha Afya, hapa ameandikwa Jumuiya ya Afya). Sasa huyu ni wa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini, yaani huyu ndio Mkurugenzi wao. Haya, amesimama, aah, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kwa sababu na yeye ndio amekuja hapa leo tutumie fursa hii kumpongeza kwa nafasi hii kubwa ambayo ameipata. Naye tena ni sehemu ya wale ambao tunasema Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kuhakikisha mahusiano kidiplomasia yanakaa vizuri, basi tunaona na nafasi nyingine hii hapa

ambayo kijana wetu kutoka Tanzania anaongoza upande wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Kwa hiyo, tukisema Watanzania tusijidharau, ni kwamba tupo vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni Dkt. Marina Njelekela, Mwenyekiti wa Bodi Taasisi ya Mifupa *(MOI)*; Ndugu Erick Shitindi, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA)*; Ndugu Rosemary Silaa ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi Bohari Kuu ya Madawa *(MSD)*; Ndugu Christopher Kadio, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; Ndugu Veronica Kishera, Makamu Mwenyekiti wa Bodi Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF);* na Ndugu Esther Kitoka, Mwenyekiti wa Bodi Hospitali ya *Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT)*, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa Abel Makubi, Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Benjamini Mkapa, Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili *(MOI),* Dkt. Irene Isaka, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mhagama ni Dkt. Magdalena Lyimo, Mke wa Hayati Dkt. Faustine Ndugulile aliyekuwa Mteule wa nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika; karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Joakim Mhagama, mtoto wa Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wengine kutoka Mkoa wa Ruvuma, wageni wa Mheshimiwa Waziri ambapo ni Ndugu Oddo Mwisho, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Osmunda Issa, Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Ruvuma; Ndugu John Haule, Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Happiness Ngwando, Mjumbe wa Baraza la UWT Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Elizabeth Gumbo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Songea; Ndugu Mennas Komba, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Songea; Ndugu Thomas Masolwa, Mwenyekiti wa

CCM Wilaya ya Songea; Ndugu Juma Nambaila, Katibu wa CCM Wilaya ya Songea; Ndugu Modesta Luonga, Katibu Mwenezi wa CCM Songea; na Ndugu Mtela Mwampamba, Katibu Tawala Wilaya ya Songea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine waliopo hapa Bungeni, wageni 181 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ambao ni Mheshimiwa Hashim Komba, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Maafisa Tarafa Mkoa wa Geita; Watendaji wa Kata Halmashauri ya Manispaa ya Geita; Watendaji wa Kata Halmashauri ya Bukombe; Watendaji wa Kata Halmashauri ya Chato; Watendaji wa Kata Halmashauri ya Nyang'hwale; na Watendaji wa Kata Halmashauri ya Mbogwe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wageni hawa wamesimama kwa makundi makundi, sasa wasimame wote kwa pamoja. Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 102 wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ambao ni wanafunzi 90 na walimu 12 wa Shule ya Sekondari Image Vosa kutoka Ilula Mkoani Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jacqueline Andrea Kainja ambao ni watumishi wa Shirika la EANNASO linalojihusisha na utekelezaji wa afua za afya kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanachama 36 wa Shirika lisilo la Kiserikali la *Federation of VICOBA Implementers* in Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam linalojihusisha na uhamasishaji wa vikundi vya kifedha na kijamii vinavyotumia mfumo wa *VICOBA*. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa ujumbe hapa kwamba yupo pia Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Wilman Kapenjama, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio majina ya wageni waliopo Bungeni hapa asubuhi hii, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Waziri wa Afya, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aje awasilishe hoja ya Wizara yake.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, leo hii baada ya kupokea Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ambayo imepitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara ya Afya, naomba, kwa mujibu wa Vifungu Namba 118 hadi 123 vya Kanuni za kudumu za Bunge kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025 na Kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu yote katika kitabu nilichowasilisha iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu. Hotuba hii inaonesha kishindo, kimbunga cha nguvu, cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake ya Awamu ya Sita, katika kujali ustawi wa afya za wananchi wa Tanzania. Imejumuisha mambo makubwa yaliyojitokeza kutokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia, inaonesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 na vipaumbele na maombi ya fedha kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee naomba kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa imani yake kwangu na kuniteua kusimamia Wizara ya Afya. Nasema, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa rasilimali na kuimarisha kwa viwango vya juu vya Diplomasia ya Kimataifa katika eneo la Afya pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hakika Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni jemedari na kiongozi mbobezi wa aina ya kipekee na mwenye uwezo mkubwa anayefanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya Afya. Mapinduzi hayo makubwa yamewezesha mazingira ya sekta ya afya kuendelea kujizatiti na kutimiza kauli ya Mtu ni Afya, Afya ni Mtaji na Afya ni Usalama na Ustawi wa Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuaminiwa na Chama cha Mapinduzi na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais kwa kipindi kijacho cha miaka mitano katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuchaguliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika sekta ya afya. Napenda pia, kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kuratibu huduma zinazoendelea kwenye Sekta ya Afya. Napenda pia, kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia Sekta ya Afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati unaowezesha kuimarisha huduma bora za afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa pamoja na majukumu ya Urais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza Bunge letu. Pia, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kwa kuiongoza vyema Kamati yake. Hakika Mwenyekiti wetu wa Kamati ni kiongozi mchapakazi na mwenye upeo wa juu kusimamia Sekta ya Afya katika nchi yetu. Napenda kumshukuru yeye na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na maelekezo wanayotoa katika kuboresha utendaji wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, hakika utendaji wa Wizara umetegemea sana ushauri wao. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia katika kunipa ushauri wa kuendesha sekta na huduma za afya kwa Watanzania. Wizara itazingatia ushauri wao. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nampongeza pia, Mheshimiwa Steven Masatu Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Tanzania Bara. Vilevile nachukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, pacha wangu katika sekta ya afya. Nawashukuru pia, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao wameweza kunipatia katika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati ya moyo wangu kwa Daktari mbobezi, Mheshimiwa Godwin Oloyce Mollel, Mbunge na Naibu Waziri wa Afya, kwa mchango wake muhimu katika Sekta ya Afya na kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kunisaidia kusimamia sekta hii, lakini hasa kwa uchapaji kazi wake. Ninawaomba wananchi wa Siha, waendelee kumwamini Mheshimiwa Dkt. Mollel katika kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe, Katibu Mkuu; Ndugu Ismail Hassan Rumatila, Naibu Katibu Mkuu; pamoja na Dkt. Grace Elias Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali; kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Ninawashukuru pia, kwa ushirikiano wanaonipatia.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Menejimenti yangu ya Wizara ya Afya na Watumishi wote wa Sekta ya Afya kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, moyo wa kizalendo na imani thabiti kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Prof. Tumaini Nagu kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, katika upande wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuimarisha mizania ya ukuaji wa mahusiano ya kidiplomasia katika sekta ya afya Kimataifa. Jambo hili limewezesha nchi yetu kutambulika, kukubalika na

kuaminiwa na Mataifa mengine na kupewa fursa adhimu za Uongozi wa Sekta ya Afya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Sekta ya Afya, naomba niungane nawe kumpongeza Profesa Mohammed Yakub Janabi kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kihistoria na kishindo kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika. Nafasi hii tumeshinda kwa mara ya pili baada ya Mkurugenzi Mteule Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile kufariki dunia, na hivyo, nafasi hii kuwa wazi. Aidha, napenda kumpongeza Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe kwa kuchaguliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya Nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Mhehimiwa Spika, nafasi hii tumeipata kwa mara nyingine baada ya Dkt. Winnie Mpanju, ambaye alishika nafasi hii katika kipindi cha nyuma, inaweza kuwa takribani miaka kumi iliyopita. Ushindi wao umeleta heshima kwa Bara la Afrika, kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuishukuru Kamati ya Kampeni iliyowezesha wagombea wetu kushinda kwa kishindo. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampeni pamoja na Kamati nzima, kama ulivyosema, wakiwemo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya kazi usiku na mchana bila kuchoka na kwa weledi mkubwa. Napenda kutambua michango ya Wizara zilizochangia katika ushindi huu zikiongozwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nasema kwa niaba ya Sekta ya Afya, asanteni sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza pia, Dkt. John Christian Rwegasha kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Tiba katika Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Nampongeza pia, Prof. Kaushik Ramaiya kwa kutunukiwa tuzo ya Pravasi Bharatiya Samman ya Rais wa India.

Mheshimiwa Spika, kipekee naishukuru sana familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa, sala, pamoja na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, natumia fursa hii, mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwashukuru kwa moyo wa dhati wananchi wote wa Jimbo langu pendwa sana kwangu la Peramiho kwa namna ambavyo wanamwamini Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wanavyoniamini na kunipa ushirikiano wa kiwango cha juu katika kipindi chote ninachowatumikia, kama Mbunge wao.

Mhehimiwa Spika, mara zote ninajikuta mwenye nguvu, mnyenyekevu, nikiwa na ari kubwa ya kuwatumikia pasipo kuchoka. Ninawathibitishia kwamba, bado nguvu yangu ni ile ile ya kushirikiana nao katika kuendeleza kazi tuliyoianza kwa pamoja ya kuleta maendeleo. Mahaba yangu kwao na Jimbo zima la Peramiho hayana kipimo; moyo wangu, akili zangu, muda wote ni kuhusu namna ya kuendelea kuwatumikia wananchi hawa wa Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtoto wao mnyenyekevu sana, ninawaahidi kuwa, baada ya shughuli hii nitarudi kuungana nao kwa mara nyingine ili tuendelee kuungana mkono, kama tunavyofanya katika vipindi vyote vilivyopita katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko, napenda kutoa pole kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki, na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu wafuatao; mzee wetu Cleopa David Msuya, Prof. Philemon Sarungi, kaka yetu Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile na Jaji Frederick Werema. Viongozi hawa walitoa mchango mkubwa kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho, jana tumepokea taarifa za msiba wa mzee wetu mwasisi wa Chama cha Mapinduzi na mpigania uhuru, Mzee Songambele, ambaye atazikwa leo. Ninatoa pole kwa wananchi wote wa Mkoa wa Ruvuma kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho. Natoa pole pia kwa Watumishi wa Sekta ya Afya na Watanzania wote

ambao wamepoteza maisha katika kipindi hiki. Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo yangu ya utangulizi, naomba sasa kutambua mafanikio makubwa. Kama nilivyosema mwanzo, ya kishindo cha kimbunga, ya uwekezaji yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi chini ya Uongozi makini wa mbobezi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tangu alipoingia madarakani, Mheshimiwa Rais wetu na Serikali yake ameokoa vifo vya wajawazito na watoto kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Amejenga vituo vya kutolea huduma za upasuaji wa dharura kutoka 388 mpaka vituo 577, hongera sana Mheshimiwa Rais wetu.

(ii) Ameongeza vyumba maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wenye changamoto na hasa upungufu wa uzito kutoka vyumba 80 mpaka vyumba 362 nchi nzima ya Tanzania.

(iii) Mheshimiwa Rais wetu ameimarisha huduma za mkoba kupitia Madaktari Bingwa wa Samia. Madaktari hao pia, leo wako hapa ndani na wanaanza huduma za mkoba katika Mkoa huu wa Dodoma, na huduma hizo zimewafikia Watanzania 154,015 ikiwemo wanawake katika halmashauri zote nchini na kujenga uwezo kwa watumishi 9,434.

(iv) Mheshimiwa Rais na Serikali yake ameokoa maisha ya akina mama wakati wa uzazi, wanawake 135,526, kupitia mfumo wa rufaa wa dharura wa *M-MAMA* aliouasisi yeye mwenyewe, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umeenea nchi nzima, Bara na Visiwani. Mfumo huu sasa umeanza kukopiwa *(copy)* na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, ujumbe wa Waziri wa Afya na Wizara kwa wananchi ni kwamba, maono haya ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uzazi salama yamewezesha

kupunguza vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000. Mafanikio hayo yamesababisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutunukiwa tuzo ya Kimataifa ijulikanayo kwa jina la *Goalkeeper Award*. Ninaomba kwa uzito wa pekee nieleze ni kwa namna gani tuzo hii ina uzito wa namna yake katika nchi yetu ya Tanzania:-

(i) Mheshimiwa Rais amekuwa Rais wa kwanza Barani Afrika kutunukiwa tuzo hiyo tunampongeza sana;

(ii) Amekuwa pia Rais wa kwanza mwanamke kutunukiwa tuzo hii, tunampongeza sana;

(iii) Mheshimiwa Rais amekuwa pia ni Rais wa kwanza kutunukiwa tuzo hiyo ndani ya nchi yake, tuzo hii haijawahi kutunukiwa kwa kiongozi yoyote ndani ya nchi yake;

(iv) Mheshimiwa Rais amekuwa pia ni Rais wa kwanza Duniani kutunukiwa tuzo ambayo inahusiana na uokoaji wa vifo vya wanawake wakati wa uzazi, hongera sana Mheshimiwa Rais wetu;

(v) Mheshimiwa Rais amekuwa pia ni Rais wa kwanza kupokea tuzo ya namna hiyo na kuikabidhi kwa watumishi wa Sekta ya Afya ambao walichangia kuokoa vifo vya akinamama na watoto wakati wa uzazi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais, mafanikio mengine ni mpango wake aliuoubuni. Mpango jumuishi na shirikishi wa wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii. Wahudumu hawa jukumu lao kubwa limekuwa ni kuelimisha kutambua mazingira hatarishi ya kiafya mapema na kuwezesha jamii na Serikali kuchukua hatua za udhibiti mapema.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe wito kwa wananchi na viongozi wengine wote kuwapa ushirikiano wahudumu hawa wanapokuwa kwenye majukumu yao maana ni kiungo muhimu katika

kuifikia afya bora kwa wote. Mpaka sasa jumla ya wahudumu 12,832 wamechaguliwa, kati yao 3,706 wamehitimu mafunzo na 4,309 wanaendelea na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, wahudumu hawa wamefanya kazi nzuri sana hata wakati wa mapambano na *Marburg*. Naomba tuwapigie makofi na tuwashukuru wahudumu hao, lengo ni kufikia wahudumu ngazi ya jamii 137,294 ifikapo 2029 katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Rais wetu amelifanyia kazi ya kutosha ni kuongeza miundombinu yenye ubora ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote nchini. Hospitali za rufaa za Mikoa ya Geita, Njombe, Songwe, Simuyu, Katavi na Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kwangwa, zimekwisha kukamilika kwa awamu iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, jengo la huduma za tiba-mionzi kwa matibabu ya wagonjwa wa saratani, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini, *KCMC*, limekamilika. Naomba nitoe taarifa kuwa Bunge lako Tukufu, tarehe 24 Juni, 2025, Hospitali ya Rufaa ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini, *KCMC* itaanza kutoa tiba mionzi kwa wagonjwa wa saratani katika kanda hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanikiwa kujenga Jengo la Damu Salama katika Hospitali ya Mkoa wa Kigoma, Maweni, na maabara yenye uwezo wa usalama wa kibaiolojia, daraja la tatu, imekamilika katika Hospitali ya Kibong'oto. Serikali imeweza kufanikisha nchi yetu kuwa ni kati ya nchi tano katika Bara la Afrika zenye hadhi ya kuwa na Maabara za Rufaa za Kimataifa, tunamshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais ameasisi ujenzi wa vichomea taka vya kisasa vinavyotumia umeme katika mikoa yote, ikiwemo kichomea taka maalum kabisa na cha namna yake kilichojengwa hapa Dodoma, chenye uwezo wa kuteketeza taka tani moja kwa saa mbili tu.

Mheshimiwa Spika, vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka 10,153 mpaka 12,843. Vitanda vya wagonjwa mahututi vimeongezeka kutoka 258 mpaka 1,362, hongera sana Rais wetu; vitanda vya kulaza wagonjwa wa kawaida vimeongezeka kutoka 86,131 hadi 153,683; hiyo nguvu ya *Tsunami,* Serikali yetu imetekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa haya niliyosema ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wastani wa 80% ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilomita tano za maeneo yao wanayoishi, lengo ni kufikia 95% ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine makubwa yamepatikana katika huduma za uchunguzi. *MRI* zimeongezeka kutoka saba hadi kufikia 13 na zinapatikana katika hospitali zote za kanda, hospitali maalum na Hospitali ya Taifa. *CT-Scan* zimeongezeka kutoka 12 mpaka 45 na zinapatikana katika Hospitali zote za Rufaa za Serikali na za binafsi. *Ultra-sound* zimeongezeka kutoka 476 mpaka 970 na zimesambazwa mpaka kwenye ngazi ya vituo vya afya nchini.

Mheshimiwa Spika, *Angel suit* zimetoka nne mpaka tano. *Fluoroscopic Machine* zimetoka tisa mpaka 13, *Digital X-Ray* zimetoka 147 mpaka 491. *Cath lab* zimetoka moja hadi nne na sasa Serikali hii ya Daktari bingwa, Samia Suluhu Hassan, imeweza kusimika mtambo wenye thamani ya shilingi bilioni 18.5 maarufu kwa jina la *pet CT- Scan,* ili kuweza kufanya kazi ya uchunguzi na ufuatiliaji wa matibabu ya wagonjwa wa saratani.

Mheshimiwa Spika, heshima ya mtambo huu imeongeza sifa ya Tanzania kuwa na vifaatiba. Tanzania sasa ni miongoni mwa nchi mbili tu kati ya nchi nane zilizopo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki zenye mashine hii ya kufuatilia matibabu ya kansa. Vilevile ni miongoni mwa nchi tatu tu kati ya nchi zote za Jumuiya ya *SADC* zenye mashine hii, na ni miongoni mwa nchi tisa kati ya nchi zote katika Bara la Afrika ambazo zimeweza kununua mtambo huu wa *Pet CT-Scan* kwa matibabu hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme kwamba kuongezeka kwa vifaatiba hivi Wizara ya Afya inatoa ujumbe kwa Watanzania kwamba Rais wetu amepunguza rufaa za ndani na nje ya nchi kwa wananchi wa Tanzania. Pia, amewezesha kusogeza huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu na kusaidia matibabu yenye ubora na yanayotumia teknolojia ya kisasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanikiwa pia kuimarisha huduma za uokoaji wakati wa dharura kwa kupunguza vifo vya wananchi wa Tanzania kutoka 40% mpaka 50%; na kazi hiyo imefanyika kwa sababu ya ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za dharura kutoka saba mpaka 125 ambayo yamekwenda mpaka kwenye hospitali za wilaya. Magari ya kubebea wagonjwa yametoka 540 mpaka 1,267 ili kuweza kutoa huduma za uokoaji wa dharura.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watumishi wa afya imeongezeka kutoka 48,633 hadi kufikia 177,711. Ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu. Kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na kanuni zake zitawawesha sasa wananchi wote wa Tanzania kufaidi huduma hizo za afya na miundombinu iliyowekezwa na Serikali yao na kufikia lengo la *Universal Health Coverage*. Kuimarika kwa makusanyo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutoka shilingi bilioni 560.8 mwaka 2024 hadi shilingi bilioni 619.8 kumeongeza uhimilivu na uhai wa mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza wataalamu bingwa na wataalamu bobezi kupitia Mfuko wa Mheshimiwa Rais wa *Health Super Specialisation Scholarship Programme* kutoka watumishi bingwa na wabobezi 2,188 mpaka watumishi 4,967. Lengo la kufanya haya kutoka kwa Mheshimiwa Rais ni kupata wataalamu wa afya wenye ubingwa na ubobezi ndani ya nchi watakaokuza uwezo wa ujuzi kwa wataalamu wa ndani, kupunguza rufaa za nje na rufaa za ndani ya nchi, kupunguza gharama za matibabu na kupunguza utegemezi wa wataalamu wa nje katika kutoa huduma katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa watu wasio na uwezo. Tumeweza

kutumia shilingi bilioni 11 ambazo zimetolewa na wananchi takribani 1,022 wamenufaika na huduma hizo. Huduma hizo ni pamoja na upandikizaji wa figo, usikivu, uroto, upoasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo na maeneo mengine. Kazi hii ya Rais imewezesha Watanzania wengi kufikiwa na uwekezaji wa huduma hizi bobezi ambazo zimewezeshwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililotekelezwa vizuri ni hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu na zenye kipaumbele 388. Tumetoka 58% hadi kufikia 87%. Vilevile, viwanda vya kuzalisha dawa na vifaatiba vimeongezeka kutoka 23 mpaka 92. Ongezeko hilo la viwanda limepunguza uingizaji wa dawa na vifaatiba nchini kutoka nje kwa 20%.

Mheshimiwa Spika, tumeweza pia kuweka rekodi ya ununuzi wa bidhaa za afya nchini, ambapo jumla ya shilingi bilioni 183.2 zimetolewa, sawa na 91.6%; zimekuwa zikitolewa katika kila mwaka. Aidha, Serikali yetu imeendelea kuimarisha *MSD* kwa kuipatia mtaji. Hadi sasa mtaji huo umefika jumla ya shilingi bilioni 150, ikiwa ni mara ya kwanza kwa Serikali kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa dawa za kuua viluilui vinavyosababisha ugonjwa wa Malaria. Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa jumla ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ununuzi wa dawa ambapo tayari lita 833,333.3 zimeanza kusambazwa katika halmashauri zote nchini. Nitoe wito kwa viongozi wote kutekeleza zoezi la unyunyiziaji wa dawa hiyo ili kuua vimelea vyote vya mbu wa Malaria.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kuifanya mamlaka ya dawa na vifaatiba nchini kuendelea kuwa kinara katika ngazi ya tatu *(maturity level 3)* kwa viwango vya Shirika la Afya Duniani. Serikali imekamilisha na kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika tiba utalii nchini, ambapo wagonjwa kutoka nje ya nchi wameongezeka kutoka 5,000.7 hadi kufikia wagonjwa 12,180.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeongeza pia vituo vya *management* ya dharura za afya kutoka sita hadi 20; na Serikali pia imeimarisha uwezo wa nchi katika uchunguzi wa kimaabara wa magonjwa mbalimbali na hasa magonjwa ya mlipuko kwa kununua maabara jongezi mbili ambazo zimeshaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeimarisha usalama wa afya mipakani kwa kusimika mashine 16 za kisasa za uchunguzi wa jotomwili. Serikali imefanikisha pia kujenga maghala tisa ya kuhifadhia chanjo pamoja na ununuzi wa magari 96 na pikipiki 300 kwa ajili ya kusambaza chanjo katika maeneo ambayo hayafikiki kiurahisi vijijini.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma hizo za chanjo umeweza kutoka 81% kufika 97%. Ni zaidi ya kiwango kilichowekwa na Shirika la Afya Duniani cha 90%. Tunamshukuru Makamu wa Rais alikuja mwezi wa 12 ili kushuhudia kazi hiyo nzuri ambayo imefanywa na Serikali yetu kwa kugawa vitendea kazi hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeokoa maisha ya Watanzania dhidi ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele kwa kufanya upasuaji wa mabusha kwa watu 11,228 na kufanya upasuaji mdogo wa usawazishaji wa vikope kwa watu 13,779.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeboresha hali ya lishe nchini kwa kuongeza mashine 230 za kunyunyiza virutubishi *(Dosifiers)* kwenye vyakula hadi kufikia mashine 1,402.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo ambayo mengine yanajionesha katika kitabu changu ya utekelezaji wa ilani katika hali ya kimbunga, ninaomba sasa nitoe maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025 na mpango wa makadirio ya mapato na matumizi pamoja na maombi ya fedha katika kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2025/2026. Maeneo hayo yako ukurasa wa 29 mpaka ukurasa wa 206 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara na taasisi zilizoko chini yake zilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 756.9 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 70.8 ni kutoka Makao Makuu ya Wizara; shilingi bilioni 134.2 ni kutoka hospitali za rufaa za mikoa na shilingi bilioni 57.9 ni kutoka Hospitali ya Taifa, hospitali maalum na hospitali za rufaa za kanda pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025, Wizara na taasisi zilizo chini yake zimekusanya jumla ya shilingi bilioni 603.7, sawa na 80% ya lengo na kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 756.9. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 52.4, sawa na 74% ya makadirio kimekusanywa kutoka makao makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni 117.9, sawa na 88% kimekusanywa kutoka hospitali za rufaa za mikoa na kiasi cha shilingi bilioni 433.4, sawa na 79% kimekusanywa kutoka katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kutumia jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 1.312 ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 632.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo mshahara ni shilingi bilioni 484.9 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 147.3. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 679.6 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 416.3 na fedha za nje ni shilingi bilioni 263.3.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 1.2 kimepokelewa, sawa na 94% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 472.7, sawa na 75% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi bilioni 375.2 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 97.5. Aidha, kiasi cha shilingi 759.2 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 501.1, sawa na fedha za nje ambazo ni shilingi bilioni 258, sawa na 98%.

Mheshimiwa Spika, ninaomba uridhie nipitie katika maeneo ya utekelezaji kwa ufupi kwa sababu mengi yanaakisi utekelezaji wa ilani ambao nimekwishausema. Jumla ya wajawazito 2,127,548 waliwezeshwa kuhudhuria kliniki angalau mara moja kati ya wajawazito 2,077,689 waliotarajiwa. Aidha, katika kuimarisha huduma wakati wa kujifungua jumla ya wajawazito milioni 1.6, sawa na 87.4% walijifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya baada ya kujifungua ambapo tunajivunia kwamba watoto wachanga milioni 1.5 sawa na 88.9% walipatiwa huduma ndani ya siku tatu za mwanzo baada ya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali imeendelea kusimamia utakalezaji wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007 na tamko namba 5.3.4 (c) linaloelekeza kuhusu kutolewa kwa huduma bila malipo kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Pamoja na uwepo wa changamoto Wizara imeendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, ujumbe wangu na ujumbe wa Wizara ni kwamba, kwanza tunawapongeza wanawake wote waliojitokeza kwenda kwenye vituo vyetu vya afya katika kipindi cha uzito na wakati wa kujifungua. Hata hivyo, tunawahimiza wakina mama kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya pale wakati wa ujauzito.

Mheshimiwa Spika, niwaombe wananchi wote, na hasa Waheshimiwa Wabunge wanaume, kuwa vinara kwa kuwasindikiza wenza wao kupata huduma wakati wa mahudhurio ya kliniki na wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya vizuri pia katika udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza. Jumla ya wagonjwa wa saratani 11,801 walibainika na kuanza matibabu katika vituo vyetu vya huduma za afya vile ambavyo ni taasisi na Hospitali yetu ya Taifa. Aidha, jumla ya wagonjwa wa kisukari 646,474 walipatiwa matibabu na wagonjwa wa shinikizo la damu milioni 1,394,632 waliweza pia kupatiwa matibabu.

Mheshimiwa Spika, hapa tunajivunia katika kipindi hiki kwa kuwa vifo vitokanavyo na ugonjwa wa shinikizo la damu vimepungua kutoka 502 hadi 439, sawa na 12%. Hii ni kutokana na uwekezaji mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Serikali imeendelea kuimarisha afua za udhibiti katika ngazi zote, ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi taribani watu milioni 20 walipatiwa elimu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo. Taarifa zote ziko kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za tiba, Wizara imeendelea kujenga vituo vipya vya kutolea huduma za afya, na sasa katika kipindi hiki cha mwaka mmoja vituo 580 katika ngazi zote vimeongezeka; na nimesema kule kwenye utekelezaji wa ilani kuna hatua nzuri tuliyofikia, ya vituo 12,846. Jumla ya wananchi 39,386,226 walipatiwa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba takwimu za utoaji wa huduma za afya zinaonesha kwamba 81% ya wananchi wamefanikiwa kupata huduma katika ngazi ya afya ya msingi; na hapa inaonekana Serikali yetu imejidhatiti katika kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya katika ngazi ya msingi na kuboresha huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali yetu imeendelea kutoa msamaha ili kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata matibabu katika ngazi zote, na hasa matibabu ya kibingwa na kibobezi. Msamaha wenye thamani ya shilingi bilioni 34.7 umetolewa kwa wananchi 268,244 wasio na uwezo. Magonjwa ambayo yametolewa msamaha ni pamoja na uchujaji wa damu, huduma za mionzi, wagonjwa wa saratani, vipimo vya maabara, huduma za *radiology,* upasuaji, gharama za kumwona daktari na huduma za wagonjwa mahututi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeimarisha pia huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambazo zimefanyika katika hospitali zote

za kanda na hospitali maalum na Hospitali yetu ya Taifa kwa lengo la kusogeza huduma hizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine Tanzania imeendelea kuweka historia katika huduma hizo za kibobezi ambapo imeweza kupandikiza figo wagonjwa 21, vifaa vya usikivu wagonjwa 16, uroto wagonjwa saba, meno wagonjwa 64, mimba kwa wanawake nane, upasuaji wa kupunguza uzito wagonjwa 13, nyonga na magoti wagonjwa 320, moyo bila kufungua kifua wagonjwa 3,103, moyo kwa kufungua kifua wagonjwa 1,086, ubongo wagonjwa 89, tiba mionzi wagonjwa 152,287, tiba ya kinga wagonjwa 44, saratani ya mlango wa kizazi wagonjwa 527,606, saratani ya matiti wagonjwa 546,993, kuweka puto tumboni wagonjwa 153, kuchuja damu wagonjwa 1,095 na tiba radiolojia wagonjwa 264.

Mheshimiwa Spika, huduma mpya za ubingwa na bobezi zilizoanzishwa katika kipindi hiki katika hospitali za umma ni pamoja na upandikizaji wa mimba, upasuaji na uchunguzi wa kichwa na ubongo bila kufungua fuvu, upasuaji wa mgongo kwa kufungua eneo dogo, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo kupitia tundu la pua.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma angalau nane za msingi za ubingwa katika hospitali za rufaa za mikoa 15 zinapatikana ikilinganishwa na mikoa nane katika mwaka wa 2024; na huduma hizo nimeshazisema pale mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ni wito wangu, pamoja na huduma hizo, Serikali imeweza kuhudumia jumla ya wagonjwa 99,885 ambao walihudumiwa na kambi za madaktari bingwa wa Dkt. Samia, kama nilivyosema tuko nao hapa ndani. Katika kipindi hiki ni mikoa saba tu ilipata fursa ya huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, wito wangu ni kuwasisitiza wananchi na viongozi walioko katika maeneo husika, kwamba pale tunapotangaza huduma za madaktari bingwa wa Dkt. Samia wawahamasishe wananchi kujitokeza kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuboresha tiba utalii, katika kipindi hiki jumla ya wagonjwa 4,337 wametibiwa hapa nchini kutoka Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Msumbiji, Congo DRC, Sudan, Uganda, Zimbabwe, Ethiopia, Somalia, Kenye, Egypt, na Mauritius; na wote hao walikuja kwa ajili ya huduma ya magonjwa ya moyo, mifupa, mifumo ya fahamu, figo na saratani.

Mheshimiwa Spika, hii inadhihirisha kuwa Serikali yetu imeshajenga ubobezi wa kutosha unaoweza kuvutia na Mataifa mengine kuja kutibiwa hapa nchini. Wizara kupitia hospitali na taasisi zake walikwenda pia nje ya nchi na kutoa huduma mkoba kwa wagonjwa 2,770 katika nchi ya Malawi, Visiwa vya Comoro, Burundi na pia kutangaza huduma za kibingwa zinazotolewa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali na Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na kuhakikisha kwamba huduma za kupunguza na kuzuia maambukizi mapya ya magonjwa kama Kifua Kikuu, Malaria, VVU na UKIMWI, homa ya ini na magonjwa ya ngono vinaendelea kushushwa. Tunashukuru kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maambukizi ya magonjwa haya yameendelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia magonjwa ya mlipuko na huduma za mpakani, Serikali imeendelea kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwepo kipindupindu, *Marburg* na *Mpox*. Aidha, tarehe 13 Machi, Serikali ilitangaza kwisha kwa mlipuko wa ugonjwa wa *Marburg* ndani ya siku 54 tu na kuvunja rekodi ya mapambano ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwahakikishiwa wananchi wa Tanzania kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya imejipanga kuzuia na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, huduma za chanjo zimeendelea kufanya vizuri. Jumla ya watoto zaidi ya 2,995,314, sawa na 96% ya watoto

wote walipatiwa chanjo. Mafanikio hayo yamekidhi viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani kufikia 90% na kutufanya tuwe tumezidi viwango hivyo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yametokana na ushirikiano wa Serikali na wadau na kama nilivyosema mwanzo, na ujenzi wa maghala na miundombinu ya kusambaza chanjo nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo ambalo tunajivunia katika kazi hiyo ya chanjo kwa kazi kubwa ya Serikali, Serikali yetu imeweza kupunguza gharama za uendeshaji wa huduma za chanjo kutoka shilingi bilioni 18 mpaka kufikia shilingi bilioni 1.8**.** Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kuweza kusaidia ku-*save* fedha hiyo nyingi kwa matumizi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, huduma za lishe nazo zimeimarika, watoto milioni 9.4 wamepata matone ya *vitamin A* sawa na 99.8%. Vilevile, wananchi wameweza kufikiwa na kuelimishwa kutumia vyakula vinavyoongeza virutubishi nchini na nimeshasema mashine ambazo tumezisambaza.

Mheshimiwa Spika, shughuli za afya, mazingira na usafi na hasa kampeni yetu ya 'Fanya kweli usibaki nyuma: mtu ni afya' imefanya vizuri kwa kuongeza kaya zenye vyoo bora kutoka milioni 8.2 mpaka kufika milioni 8.5, sawa na 74.4%.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa dawa, vifaatiba na vitendanishi. Serikali imeamua kuweka mifumo katika kusimamia uagizaji, utunzaji na matumizi ya vifaatiba kuanzia ngazi ya Bohari ya Dawa *(MSD)* mpaka kwenye vituo vya kutolea huduma. Sambamba na hilo, Serikali imeamua kuweka alama ya utambuzi ya *Government of Tanzania (GOT)* kwenye bidhaa zote za afya ambazo zinasambazwa na Serikali ili kudhibiti matumizi mabaya ya vifaa hivyo katika mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeongeza maabara 883 na kufanya kuwa na maabara 11,665. Tunashukuru sekta binafsi nayo imeweza

kuchangia kuweka maabara za kiuchunguzi 4,282. Sisi kama Serikali tunasema sekta binafsi ni washirika katika shughuli za maendeleo ya afya na siyo washindani na tutafanya nao kazi bega kwa bega.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya chupa za damu salama 418,609 kwa ajili ya huduma nchini. Huduma za ukunga Serikali kupitia Wizara imeweza kuwawezesha watumishi 12,000 kuweza kutoa huduma za staha zenye kuzingatia utu, heshima, mawasiliano, mila na desturi zetu. Aidha, madawati 400 tumeyafungua ili kusikiliza na kupokea changamoto na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rasilimali katika sekta ya afya, nimeshasema na tukiangalia ukurasa wa 151 tumetoa maelezo zaidi. Wizara pia, imeendelea kutoa ufadhili wa *Samia Health Super-Specialization Program* na tumefanya vizuri. Ninaomba turejee ukurasa wa 153 kwa sababu nilishatoa maelezo hapo awali.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora na ufanisi wa utoaji huduma na kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa na muda wa kupata huduma. Wizara imesimika Mfumo wa Afya wa *Electronic Health Management Information System* katika hospitali zote za rufaa mikoa 28 na hata hivyo tunataka sasa twende mpaka kwenye hospitali zote za kanda ili kufanya udhibiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la tathmini, tumeendelea kufanya vizuri, ninaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie ukurasa wa 157 wa kitabu changu kwa sababu tumefanikiwa kuunda timu ya wataalam 126 wa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugharamiaji wa huduma za afya tumeendelea kufanya vizuri katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Shilingi trilioni 2.54 kutoka Wizara zote za kisekta zinazotekeleza afua za afya ziliweza kupatikana ukilinganisha na shilingi trilioni 2.66 ambazo zilitengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hapo pia kiasi cha shilingi bilioni 183.2 sawa na 91.6% kimetolewa kwa ajili ya ununuzi, ugomboaji, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaatiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na athari zinazotokana na mabadiliko ya sera za Kimataifa katika kufadhili sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri imefanya tathmini ya namna ya kukabiliana na changamoto ya athari hizo kwa kutenga kiasi cha fedha bilioni 202 kwa ajili ya kutumika katika kipindi cha mwezi Machi - Juni. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 141.9 kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa Dawa za *ARV*, bidhaa za Kifua Kikuu na Malaria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kwa mwaka huu wa fedha kutoka shilingi bilioni 200, 2024/2025 hadi shilingi bilioni 300 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ongezeko hilo litawezesha ununuzi wa dawa za *ARV* pamoja na dawa nyingine.

Mheshimiwa Spika, hapa ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejipanga kweli kweli kuhakikisha dawa hizo muhimu zinaendelea kupatikana kwa wananchi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kama kawaida bila kuwa na mabadiliko yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo; miradi ifuatayo ya ujenzi imefikia zaidi ya 80%. Jengo la Huduma ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu; Jengo la Wagonjwa wa Nje katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi na Mtwara; na Hospitali ya Mkoa wa Mara awamu ya nne. Jengo lingine la Huduma ya Uzazi Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi; Jengo la Kutolea Huduma za Wagonjwa wa Nje awamu ya pili katika Hospitali ya Rufaa ya Ruvuma; na Jengo la Saratani katika Hospitali ya Benjamini Mkapa, nalo limefikia 60% na kuelekea 80%.

Mheshimiwa Spika, miradi mipya ya ujenzi inayofanyiwa usanifu kwa ajili ya kuanza utekelezaji ni pamoja na uhuishaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali yetu ya Taifa kongwe. Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Magharibi Kigoma; ujenzi na majengo na ukarabati wa miundombinu ya kutolea mafunzo katika vyuo vya kati 13; na ujenzi wa Jengo la Watoto Wachanga katika Hospitali ya Mkoa wa Pwani

Tumbi, Ruvuma, Tabora, Kiteto, Geita, Simiyu, Dodoma, Singida na Manyara.

Mheshimiwa Spika, pia ujenzi wa Jengo la Uzazi wa Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera, Tanga, Morogoro, na Katavi; ujenzi wa *OPD* katika Hospitali ya *Mount Meru* Mkoani Arusha; ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti na kichomea taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga; ujenzi wa majengo ya damu salama katika Hospitali za Mikoa ya Mara, Shinyanga, Ruvuma, Singida, Songwe, Chato na Katavi; ujenzi wa ghala la kuhifadhia dawa Chato; ujenzi wa usimikaji wa mitambo ya hewa katika hospitali zote za rufaa katika nchi yetu ya Tanzania; ujenzi na usimikaji wa vifaa katika wodi za watoto wachanga kwenye Hospitali za Rufaa za Tumbi, Songwe, Tabora, Geita, Simiyu, Dodoma, Singida, Manyara; na ujenzi wa *maternity complex* katika Hospitali ya Rufaa ya Kagera.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tutaendelea na ujenzi wa hospitali maalum katika Mkoa wa Kagera na Hospitali ya Tiba Shufaa katika Mkoa wa Tabora Nzega, maelezo zaidi yako ukurasa wa 161 mpaka 162 pamoja na viambatisho. Utekelezaji wa majukumu ya taasisi umeoneshwa ukurasa wa 163 mpaka 191. Utekelezaji wa majukumu ya bodi za usajili umeelezwa ukurasa wa 191 mpaka 206.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kwa heshima na taadhima niweze kusema kwa ufupi vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2025/2026, ambapo kiasi cha shilingi 161,8191,235,000 kimekadiriwa kutumiwa katika vipaumbele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipaumbe cha kwanza ni kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya mlipuko na magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele. Hapa, tutaendeleza usimamizi wa magonjwa hayo katika mikoa 20 tutakamilisha uanzishwaji wa programu ya Taifa ya lishe na kuendelea na shughuli nyingine kama zinavyojionesha kwenye kitabu changu. Katika eneo hilo pia tutanunua boti tano za *ambulance* na vipima joto

tembezi 28. Tutaendelea na ile *program* ya wahudumu wa afya ya jamii katika mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni kuimarisha upatikanaji wa ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia zahanati hadi Taifa. Hapo tutaimarisha mifumo ya TEHAMA na kuanza kutumia Akili Mnemba *(Artificial Intelligence)* katika huduma za tiba nchini.

Mheshimiwa Spika, tutashughulika pia na suala zima la mikataba ya huduma bora kwa wateja, wananchi waweze kupata huduma bora katika nchi yetu ya Tanzania kwa miundombinu iliyowekwa. Tutaanzisha taasisi ya afya ya jamii, tutaimarisha Hospitali ya Benjamini Mkapa kufikia kuwa Hospitali ya Taifa na kuanzisha kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya magonjwa ya damu katika Hospitali ya Benjamini Mkapa. Tutaanzisha pia, Kituo cha Umahiri cha Figo katika Hospitali ya Benjamini Mkapa.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine tutafanya kuzipa hadhi za kitaasisi, Hospitali ya Mirembe, Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya. Tutashughulika pia na tafiti za kushughulika na usugu wa vimelea vya dawa.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuimarisha mifumo ya ugharamiaji na hasa utekelezaji wa Sera ya Bima ya Afya kwa wote na kusimamia pia bajeti ya fedha kukidhi mahitaji ya nchi. Tunaendelea kufanya tafiti kwa kutumia Taasisi ya *NIMR* na taasisi nyingine; na tutaendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi na hasa kuendeleza ununuzi wa vifaatiba kwenye wodi za watoto na kununua dawa na hasa dawa ya *surfactant* ambayo inatumika kuokoa maisha ya watoto wanaozaliwa chini ya uzito.

Mheshimiwa Spika, tutaimarisha uendelezaji wa wataalamu wa sekta ya afya kwa kukosemesha wabobezi kwa kwa seti na vilevile, tutasimamia mafunzo ya afya kwa kutumia TEHAMA. Tutaimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuanzisha kituo cha uzalishaji wa viungo tiba. Vilevile, tutaendelea kusimamia

afua za tiba asili na tiba mbadala kwa kuendeleza tafiti na kufanya mambo mengine ambayo yameainishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, tutaimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyoambukizwa na hapa Serikali imejipanga kufufua kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical* cha Arusha ili kiweze kuzalisha *ARV;* lakini tutaanzisha viwanda vingine vya chanjo na viwanda vingine vya *ARV* kwa kushirikiana na wawekezaji na pia Chanjo za *Hepatitis*.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho tutaimarisha huduma ya afya ya akili na utengamao na hususan kwa watoto, wazee, na Watanzania kwa ujumla kwa kufanya yale ambayo yameainishwa kwenye eneo langu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa namna ya pekee nitoe shukrani kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi na hapa nitawataja wachache: Mavere Ali, Irene Charles Isaka, Bwana Adam Mitangu, Profe. Said Shebe, Fidelice Mbaruku Mafumiko.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninaomba niwapongeze Wakurugenzi wa Hospitali za Taifa, Kanda na Maalum: Prof. Mohamed Yakub Janabi, Dkt. Mpoki, Daktari Peter Kisenge, Dkt. Diwani Bakari Msemo, Dkt. Leonard Maduhu Subi, Dkt. Paul Sarea Lawala na madaktari wengine ambao ni Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa na Hospitali za Kanda.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia watendaji kuanzia ngazi ya Taifa mpaka kwenye zahanati zetu, Waganga Wafawidhi na wale wote ambao wameendelea kutusaidia. Katika kutekeleza majukumu yangu katika Wizara tumeendelea kushirikiana na nchi rafiki na mashirika ya Kimataifa katika sekta mbalimbali, lakini ambayo yameweza kujumuisha nguvu zao kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, nitumie wasaa huu kuzishukuru nchi za Canada, Denmark, Uingereza, Ireland, Uswisi, Korea Kusini, na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia,

UNFPA na *UNICEF* kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa pamoja *(Health Basket Fund)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninazishukuru nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, Uturuki, Marekani, Ujerumani, Ufaransa, China, Cuba, India, Italia, Japan, Misri, Sweeden na nyingine kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, ninayashukuru mashirika yote ambayo ni ya Kimataifa yanayochangia katika Wizara ya Afya. Nishukuru taasisi za ndani ya nchi na hapa orodha ya taasisi hizo zote iko kwenye kitabu changu. Kipekee niwashukuru sana ndugu zetu wa 'Ubaya Ubwela' chini ya *Mo Foundation* lakini na 'Wananchi' kupitia *GSM,* benki na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, mwisho sasa ninaomba nilete maombi ya fedha kwa mwaka 2025/2026. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi 819,977,862,602.14.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi 74,207,303,307.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara; shilingi 153,792,696,693.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa; na shilingi 591,977,862,602.14 zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kawaida. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 626,433,136,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 39% ya bajeti iliyotengwa, ambapo kiasi cha shilingi 475,414,119,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake; na kiasi cha shilingi 151,015,017,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya maendeleo. Wizara imepanga kutumia shilingi 961,758,099,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 61% ya bajeti iliyotengwa. Kati ya hizo, fedha za

ndani ni shilingi 564,458,609,000.00 na fedha za nje ni shilingi 427,299,490,000.00.

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zote zinazoombwa kuhidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake Fungu 52 ni shilingi 1,618,191,235,000.00 ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele nilivyovisema.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kuwa na utekelezaji mwingine wa Kimbunga cha *Tsunami* katika sekta ya afya kwa mwaka ujao wa fedha. Hotuba hii inapatikana pia katika Tofuti ya Wizara ya Afya *www.moh.go.tz*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kwa heshima kubwa niweze kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA I:
UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, leo hii baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ambayo imepitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Afya, naomba kwa mujibu wa **Vifungu namba 118 hadi 123 vya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la mwaka 2023**, kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/25 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/26.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee naomba kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Imani yake kwangu na kuniteua kusimamia Wizara ya Afya.

Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa rasilimali na kuimarisha kwa viwango vya juu vya Diplomasia ya Kimataifa katika eneo la Afya pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora kwa wananchi. Hakika Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **ni jemedari na kiongozi mbobezi** wa aina ya kipekee anayefanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya afya. Uwekezaji alioufanya unajidhihirisha kupitia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne cha uongozi wake kwani unagusa maisha ya kila siku ya wananchi kutokana na ukweli kwamba **Mtu ni Afya, Afya ni Mtaji na Afya ni Usalama na Ustawi wa Nchi**.

3. Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Rais** kwa kuaminiwa na Chama cha Mapinduzi na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa mgombea wa nafasi ya urais kwa kipindi kijacho cha miaka mitano (5) katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025. Pia, nampongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kwa kuteuliwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kupendekezwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuwa mstari wa mbele kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha huduma za afya nchini. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuratibu huduma zinazotolewa na Sekta ya Afya nchini. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko**

(Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia Sekta ya Afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati unaowezesha kuimarisha huduma bora za afya nchini.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa unaodhihirika katika kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu licha ya majukumu uliyonayo ya Urais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Aidha, nampongeza **Naibu Spika**, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu**, kwa kuendelea kukusaidia vyema katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uadilifu mkubwa. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

6. Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa **Elibariki Emmanuel Kingu (Mb)** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kuiongoza vyema Kamati. Hakika Mwenyekiti wetu wa Kamati ni kiongozi mchapakazi na mwenye upeo wa juu katika kusimamia Sekta ya Afya. Napenda kumshukuru yeye na wajumbe wa Kamati kwa ushauri na maelekezo wanayotoa katika kuboresha utendaji wa Wizara. Aidha, **ninawashukuru Waheshimiwa wabunge wote** kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya kwa Watanzania. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge kwamba, Wizara itazingatia ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku kwa wananchi. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati **kwa Katibu wa Bunge na watumishi wa Bunge** kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia. Niwahakikishie kuwa viongozi na watumishi wa Sekta ya Afya nchini tutaendelea kutekeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utoaji huduma za afya.

7. Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa **Steven Masatu Wasira** kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa

Chama cha Mapinduzi Tanzania Bara. Vilevile nichukue fursa hii kumshkuru sana Waziri wa nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa mawaziri wenzangu na **Mwanasheria Mkuu wa Serikali** kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuboresha usimamizi wa utoaji huduma bora za afya nchini.

8. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa **Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel** (Mb), Naibu Waziri wa Afya, kwa mchango wake muhimu katika Sekta ya afya na kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kunisaidia kusimamia Sekta hii na kwa uchapaji kazi wake huo ninawaomba wananchi wa Siha kuendelea kumuamini. Vilevile, nawapongeza **Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe**, Katibu Mkuu, **Ndugu Ismail Hassan Rumatila**, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na **Dkt. Grace Elias Magembe**, Mganga Mkuu wa Serikali kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo na ninawashukuru kwa ushirikiano wao wa dhati kwangu. Kipekee niishukuru **Menejimenti ya Wizara ya Afya na watumishi wote wa Sekta ya Afya** kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, moyo wa kizalendo na imani thabiti kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza **Prof. Tumaini J. Nagu** kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI.

9. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kuimarisha mizania ya ukuaji wa mahusiano ya kidiplomasia ya afya, jambo lililowezesha nchi yetu **kutambulika, kukubalika na kuaminiwa** na mataifa mengine na kupewa nafasi adhimu za uongozi wa Sekta ya Afya kimataifa. Napenda kumpongeza **Prof. Mohammed Yakub Janabi** kuchaguliwa kwa ushindi wa kihistoria na kishindo kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Nafasi hii tumeshinda kwa mara ya pili baada ya Mkurugenzi Mteule **Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** kufariki dunia. Aidha, napenda kumpongeza Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe kwa kuchaguliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Nafasi hii tumeipata kwa mara nyingine baada ya **Dkt.**

Winnie Mpanju ambaye alishika kipindi cha nyuma. Ushindi wao umeleta heshima kwa Bara la Afrika na kwa watanzania kwa ujumla.

10. Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu napenda kuishukuru Kamati ya Kampeni iliyowezesha wagombea wetu kushinda kwa kishindo. Kipekee namshukuru **Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampeni** pamoja na kamati nzima kwa kufanya kazi usiku na mchana bila kuchoka na kwa weledi mkubwa. Aidha, napenda kutambua michango ya Wizara zote zikiongozwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hivyo, kwa niaba ya Sekta ya Afya nasema asanteni sana.

11. Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza **Dkt. John Christian Rwegasha** kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Tiba katika Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Aidha, nampongeza **Prof. Kaushik Ramaiya** kwa kutunukiwa tuzo ya **Pravasi Bharatiya Samman** ya Rais wa India inayotambua mchango wake kwa jamii katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

12. Mheshimiwa Spika, kipekee naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa, sala na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwashukuru kwa moyo wa dhati **wananchi wote wa jimbo langu pendwa la Peramiho** kwa namna mnavyoniamini na kunipa ushirikiano wa kiwango cha juu katika kipindi chote ninachowatumikia kama Mbunge wenu. Mara zote ninajikuta mwenye nguvu na ari kubwa ya kuwatumikia pasipo kuchoka na ninawathibitishia kwamba bado nina nia, nguvu na ari ya kuendelea kushirikiana nanyi katika kuendeleza kazi tuliyoianza kwa pamoja ya kuleta maendeleo. Mahaba yangu kwa wananchi wa jimbo la Peramiho hayana kipimo, moyo na akili zangu muda wote ni kuhusu namna ya kuendelea kuwatumikia. Mimi mtoto wenu ninawaahidi kuwa baada ya shughuli hii nitarudi kuungana nanyi na ninaamini kuwa mtaendelea kuniunga mkono kama mlivyofanya katika vipindi vilivyopita.

13. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko napenda kutoa pole kwako wewe Binafsi na Bunge lako Tukufu, wanafamilia wote, ndugu, jamaa, marafiki, na wananchi wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu; **Cleopa David Msuya** aliyewahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; **Profesa Philemon Sarungi,** aliyewahi kuwa Waziri katika Wizara mbalimbali, **Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika na **Jaji Frederick Werema** aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

14. Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuwapoteza watumishi wenzao katika kipindi hiki na watanzania wote, waliopoteza ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali ikiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

SEHEMU YA II:
MAMBO MAKUBWAYALIYOTEKELEZWA NA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA AFYA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2025

15. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo yangu ya utangulizi, naomba sasa kutambua mafanikio makubwa ya kiuwekezaji yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 20202025 chini ya Uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu alipoingia madarakani.

Kuimarika kwa Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

16. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya ambayo tayari inatumika na imegharimu Shilingi Bilioni 13.2. Kukamilisha ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto (Maternity Blocks) kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe

ambazo zimegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 71.1. Kuongezeka kwa idadi ya vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni kutoka vituo 388 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 577 Machi, 2025 ikiwa ni ongezeko la vituo 178. Kuongezeka kwa wodi/vyumba maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wanaozaliwa na uzito pungufu (NCU), kutoka 80 mwaka 2021 hadi kufikia 362 Machi, 2025. Huduma hizi zinapatikana katika Hospitali 318 za Halmashauri, Hospitali za Rufaa za Mikoa 28, Hospitali za Rufaa za Kanda sita (6), Hospitali ya Taifa na 108 Hospitali za Mashirika ya Dini na Binafsi. Kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za Afya ya Uzazi na Mtoto ambao umeongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88 Machi 2025.

17. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuongezeka kwa idadi ya vifaa tiba vya afya ya uzazi, mama na mtoto vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 10.8 katika vituo vya kutolea huduma za afya. Vifaa hivyo ni pamoja na "BP Machine" 50,000 zenye thamani ya Shilingi Billioni 3.01; mashine za CPAP 130 zenye thamani ya Shilingi Milioni 213; vifaa vya CPAC vyenye thamani ya Shilingi milioni 276; vifaa vya NICU 120 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.2; mashine 140 (Thermalcoagulator) za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.1.

18. Mheshimiwa Spika, kupitia kampeni za Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia kwa awamu ya kwanza na ya pili jumla ya wagonjwa 154,015 kutoka katika Halmashauri 184 nchini waliweza kupata huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za Afya ya uzazi na ukunga, Watoto wachanga, upasuaji magonjwa ya ndani, kinywa na meno, usingizi na ganzi. Aidha, kupitia kampeni hiyo jumla ya watumishi wa afya wapatao 9,434 walijengewa uwezo katika kutoa huduma za dharura za uzazi mama na mtoto. Huduma hizo katika awamu zote mbili zimegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 3.8

19. Mheshimiwa Spika, Maono ya Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uwekezaji katika miundombinu ya upasuaji kwa wajawazito, dawa za uzazi salama, uwepo wa mfumo wa rufaa wa dharura kwa wajawazito (M-MAMA),

kuimarika kwa uwajibikaji wa watendaji katika ngazi zote za utoaji huduma na ushirikishwaji wa vyama vya kitaaluma umefanikisha kupunguza vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi kutoka 556 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000.

Mafanikio hayo yamesababisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunukiwa tuzo ya kimataifa ijulikanayo kwa jina la Goalkeeper Award, iliyotolewa na Taasisi ya Gates ya Marekani, tarehe 4 Februari, 2025. **Tuzo hii hutolewa kwa Viongozi waliofanikiwa kutekeleza kwa mafanikio Malengo ya Maendeleo Endelevu;**

- Mheshimiwa Rais amekuwa Rais wa kwanza Barani Afrika kutunukiwa tuzo hii
- Amekuwa Rais wa kwanza mwanamke kutunukiwa tuzo hii
- Amekuwa ni Rais wa kwanza kutunukiwa tuzo hii nchini kwake
- Amekuwa ni Rais wa kwanza Duniani kutunukiwa tuzo ya kuokoa vifo vya wanawake wakati wa uzazi
- Amekuwa ni Rais wa kwanza kupokea tuzo hiyo na kuikabidhi kwa watumishi wa Sekta ya Afya waliochangia kuokoa vifo vya akinamama na watoto.

20. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa **Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii** kwa lengo la kuwafikia wananchi katika ngazi ya kaya, jumla ya wahudumu 12,832 wamechaguliwa na kati yao 3,706 wamehitimu mafunzo na 4,309 wanaendelea na mafunzo katika vyuo 45 nchini. Lengo ni kufikia wahudumu ngazi ya jamii 137,294 ifikapo 2029.

"Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii ni macho yetu, masikio yetu, na mikono yetu katika kaya, vijiji na mitaa. Wanaelimisha, wanatambua mazingira hatarishi ya kiafya mapema na kuwezesha jamii na Serikali kuchukua hatua za udhibiti mapema. Wahudumu hao si tu watoa huduma, bali ni viongozi wa mabadiliko ya afya katika jamii zao. Hivyo wananchi wawapokee na kuwapa ushirikiano wanapokuwa kwenye majukumu yao maana ni kiungo muhimu katika kufikia afya bora kwa wote". **Kuimarika kwa Miundombinu ya kutolea Huduma za Afya**

21. Mheshimiwa Spika, vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 na kufikia vituo 12,846 Machi, 2025 sawa na ongezeko la vituo 4,297 vilivyojengwa katika kipindi cha Awamu ya Sita. Aidha, kuna ongezeko la majengo mapya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa-Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe na Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini Mtwara na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato pamoja Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Ligula (Mtwara), Sekou Toure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Sumbawanga (Rukwa), Kitete (Tabora), Ukerewe (Mwanza) pamoja na ujenzi wa hospitali mpya katika mikoa mipya mitano (Katavi, Njombe, Geita, Simiyu na Songwe) na kuhamisha Hospitali tano (5) kutoka majengo yake ya zamani kwa kujenga Hospitali mpya katika maeneo mapya, Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi. Maboresho hayo na ujenzi vimegharimu jumla ya Shilingi Trilioni 1.03. Vilevile, kumefanyika ukarabati wa majengo ya zamani katika Hospitali Kongwe 50 za Halmashauri, ukamilishaji wa maboma ya Zahanati 980, ujenzi wa Vituo vya Afya 390, ujenzi wa kituo cha kutibu magonjwa ya milipuko Kisopwa mkoani Pwani, ujenzi wa mitambo 21 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na Wagonjwa wa dharura na ujenzi wa nyumba za Watumishi wa afya 270.

22. Mheshimiwa Spika, idadi ya **vitanda vya wagonjwa** katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeongezeka kutoka vitanda 86,131 mwaka 2021 hadi vitanda 153,683 Machi, 2025. Ongezeko la vitanda vya wagonjwa limesaidia kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za afya hususan huduma za afya ya mama na mtoto. Aidha, idadi ya vitanda katika vituo vya umma kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) imeongezeka kutoka vitanda 258 vya mwaka 2021 hadi kufikia vitanda 1,362 Machi 2025. Ongezeko hili limejumuisha vitanda vya wodi za watoto wachanga wagonjwa (NCU).

Ongezeko la vitanda vya wagonjwa mahututi (ICU) katika Hospitali za umma linalenga kuboresha huduma na kupunguza vifo vinavyotokea ndani ya hospitali ambavyo vinaweza kuzuilika.

Kuimarika kwa upatikanaji na uimarishaji wa Huduma za Uchunguzi

23. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi kwa wagonjwa, Serikali imenunua na kusimika vifaa tiba vya uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 228.1 ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi katika ngazi ya Afya ya Msingi ambapo Mwaka 2021 hadi Machi 2025 MRI zimeongezeka kutoka saba (7) hadi kufikia 13, CT Scan 12 hadi 45, Mini Angio Suite tano (5), kipimo cha uchunguzi na tiba ya magonjwa ya mfumo wa chakula na mfumo wa uzazi (Fluoroscopy) 13, Digital X-ray 147 hadi 491, Ultrasound 476 hadi 970, huduma ya kutibu matatizo ya moyo ya dharura (CATHLAB) moja (1) hadi nne (4) na matibabu ya hali ya juu ya magonjwa ya saratani (PET CT SCAN) haikuwepo sasa ipo moja (1) nchini yenye thamani ya Shilingi Bilioni 18.5. Aidha, kuongezeka kwa vifaa, vifaa tiba vya uchunguzi kumepunguza rufaa za ndani na nje ya nchi, kumewezesha kusogeza huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu na kusaidia kutoa matibabu sahihi zaidi na kwa wakati sahihi.

Kuimarika kwa Magonjwa ya Milipuko na Huduma za dharura

24. Mheshimiwa Spika, kwa miaka ya hivi karibuni nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na milipuko ya magonjwa mbalimbali ikiwemo UVIKO-19, Kipindupindu, Homa ya Mgunda, Kimeta, Surua, Marburg pamoja na ongezeko la magonjwa ya mafua makali ya influenza na virusi vingine. Vilevile nchi yetu imekuwa katika hatari ya kupata magonjwa mengine kutokana na uwepo wa milipuko ya magonjwa hayo katika nchi jirani ikiwa ni pamoja na Polio, Ebola na Homa ya Manjano katika nchi za jirani. Hivi Karibuni, mnamo mwezi Machi 2025, nchi yetu ilithibitisha uwepo wa ugonjwa wa Mpox ambao kwa kipindi cha miaka miwili (2) tangu ulipoathiri nchi za Ulaya, Amerika na nchi nyingine za Afrika, Serikali imekuwa ikipambana kuuzuia usiingie nchini.

25. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya utayari kwa nchi kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Ebola uliotokea kwa nyakati tofauti katika mwaka 2022, 2024 na 2025 katika nchi jirani ya Uganda, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo, hivyo kuimarisha uchunguzi wa wasafiri na udhibiti wa ugonjwa kuingia nchini kupitia mipaka na mikoa iliyoko katika hatari zaidi mfano mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Mara, Geita, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya na Songwe. Hatari hiyo ni kutokana na mwingiliano katika shughuli za kiuchumi na kijamii na nchi hizo. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ilichukua hatua za kuzuia kuingia kwa maambukizi nchini na kuimarisha hali ya utayari katika Mikoa yote. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna taarifa za uwepo wa mgonjwa aliyethibitika kuwa na ugonjwa wa Ebola nchini.

26. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na matishio ya magonjwa haya ya milipuko Serikali imeendelea kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama dhidi ya magonjwa hayo kwa kuweka miundombinu imara katika maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege, bandari na stendi za mabasi. Aidha, Serikali imeongeza vituo vya menejimenti ya matukio ya dharura za afya ya jamii (Public Health Emergency Operations Centers - PHEOC) mikoani kutoka vituo sita (6) mwaka 2021 hadi kufikia vituo 20 Machi, 2025. Vilevile, Serikali imeimarisha miundombinu na kununua vifaa vya kisasa vya TEHAMA na samani vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.02 kwa ajili ya vituo hivyo katika Mikoa 20 hadi kufikia Machi 2025. Vituo hivi vinawezesha kupokea na kuchakata taarifa za matukio na milipuko ya magonjwa kutoka katika mifumo mingine ya ufuatiliaji wa magonjwa ili kuchukua hatua na kuratibu afua za udhibiti kwa haraka.

27. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa uchunguzi wa maabara nchini ikiwemo maboresho ya miundombinu na vifaa vya kisasa kwa kujenga maabara ya kisasa ya Usalama wa Kibailojia Daraja la 3 katika hospitali ya Kibong'oto. Maabara hii ni mojawapo ya maabara tano (5) Afrika zenye hadhi ya kuwa maabara za rufaa za kimataifa. Aidha, maboresho yamefanyika katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii ikiwemo ununuzi wa Maabara jongezi mbili (2) za uchunguzi wa maabara, zinazoweza

kutumika eneo lolote nchini ambako mlipuko utatokea. Maabara hizi ziliwezesha nchi yetu kupima na kugundua virusi hatari vinavyosababisha ugonjwa wa Marburg bila kusafirisha sampuli nje ya nchi. Vilevile, Serikali imeimarisha uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko katika mipaka ya nchi kavu, majini na viwanja vya ndege kwa kuweka mashine za kisasa za uchunguzi wa jotomwili (thermoscanners) 16 kwa ajili ya kuchunguza wasafiri wote wanaoingia au kutoka nchini kwa mujibu wa kanuni za afya za kimataifa.

28. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya magonjwa hatari ya kuambukiza kwa kuanzisha hospitali ambayo itakuwa ni kituo cha umahiri cha kuwatenga na kutibu magonjwa ya kuambukiza ikiwemo Marburg, Ebola na magonjwa mengine ya mlipuko katika mkoa wa Kagera. Eneo limepatikana katika mji wa Bukoba, upembuzi yakinifu umekamilika na Serikali imesaini makubaliano ya kuanza ujenzi wa hospitali hiyo na Serikali ya watu wa Falme za Kiarabu (UAE) ili ujenzi huo uanze mapema mwaka huu.

29. Mheshimiwa Spika, kufuatia uwekezaji katika miundombinu na kuzijejengea uwezo timu za wataalam , Tanzania iliweza kukabiliana kwa mafanikio makubwa dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19 kwa mwaka 2021 hadi 2023. Vilevile, nchi yetu ilikumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa Marburg kwa mara ya kwanza mwaka 2023 Mkoani Kagera ambapo tuliweza kukabiliana nao ndani ya siku 69 na kuudhibiti. Mnamo Januari 2025 ulitokea mlipuko wa pili wa ugonjwa wa Marburg ambao uliweza kudhibitiwa na kutokomezwa ndani ya siku 54 ikilinganishwa na siku 69 za mlipuko wa kwanza.

30. Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa kinara kwa kushiriki kufanya tathmini za kimataifa za kupima uwezo wa kukabiliana na dharura za afya zenye athari kimataifa, ambapo Februari 2016 Tanzania ilikuwa ya kwanza duniani kufanya *Joint External Evaluation (JEE),* ambapo wataalam wa sekta mbalimbali ndani na nje ya nchi hufanya tathmini ya uwezo wa nchi wa kuzuia, kugundua na kukabiliana na dharura za afya ya jamii ikiwemo magonjwa ya

mlipuko. Nchi yetu imefanya tathmini ya pili mwaka 2023 na kuonesha kuimarika zaidi kwa uwezo wa ndani wa nchi katika kujikinga, uchunguzi wa kimaabara na kukabiliana na magonjwa ya afya ya jamii. Hatua hii inawezesha nchi kufanya vizuri katika utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) na agenda ya usalama wa afya kimataifa (Global Health Security Agenda) inayotutaka kuimarisha uwezo wa kubaini mapema, kupima, kuthibitisha na kutoa taarifa na namna nchi inavyokabiliana na dharura hizi na kudhibiti zisisambae katika nchi zingine bila kuathiri biashara na usafirishaji wa bidhaa na watu.

31. Mheshimiwa Spika, mnamo Novemba, 2024 Tanzania ilifanya tathmini nyingine ya hiari ya kimataifa iliyoanzishwa na Shirika la Afya Duniani inayoitwa *Universal Health and Preparedness Review*. Taarifa ya tathmini hiyo ilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanya nchi yetu kuwa ya tano (5) katika Afrika na ya nane (8) duniani kujifanyia tathmini ya uwezo wa kukabiliana na dharura za afya na kuhakikisha ngazi ya juu ya Serikali na jamii yote inashirikishwa na kutambua kuwa suala la mapambano dhidi ya milipuko ya magonjwa ni la sekta zote na la kila mtu chini ya afya moja yaani afya ya wanyama na mifugo, afya ya vyakula, afya ya mazingira na afya ya binadamu.

32. Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Sekta zingine, inaendelea kutekeleza na afua za udhibiti wa mlipuko wa Mpox kwa kutoa elimu kwa umma, ufuatiliaji wa wahisiwa na wagonjwa katika jamii na kuimarisha matibabu kwa wagonjwa wanaothibitika kuwa na maambukizi ya Mpox. Hadi kufikia Machi, 2025 wagonjwa waliokuwa wakifika katika vituo vya kutolea huduma za afya wameendelea kupatiwa matibabu na afya zao kuimarika na kuruhusiwa. Wizara inaendelea kuwahimiza wananchi kuendelea kushiriki kikamilifu kudhibiti na kuzuia usambaaji wa ugonjwa huu kwa kuchukua hatua za kinga hususani kuepuka kujamiiana na mpenzi au mwenza mpya usiyejua hali yake ya kiafya, kuepuka kumhudumia au kugusa majimaji ya mwili ya mtu mwenye dalili za ugonjwa bila kinga, kuweka vitakasa mikono katika maeneo ya mikusanyiko ikiwemo Masoko, Shule, Kumbi za Starehe, Nyumba za

ibada, majumbani na maeneo mengine ya shughuli za kila siku. Afua hii itapunguza uwezekano wa kusambaa kwa maambukizi ya Mpox na magonjwa mengine ya kuhara na kutapika.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo maalum kuhusu magonjwa ya mlipuko, huduma za wagonjwa mahututi, na tahadhari za kuzuia maambukizi kwa mikoa yote iliyopo kwenye hatari ya magonjwa hayo. Kwa kuwa Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON mwaka 2027, Wizara imeongeza idadi ya madaktari bingwa 48 wa magonjwa ya dharura kwa kuwagharamia masomo katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili. Hatua hii inalenga kupunguza uhaba wa wataalam wa huduma za dharura na kuboresha utoaji wa huduma wakati wa mashindano hayo muhimu. Aidha, madaktari 20 wa dharura kutoka Muhimbili, Amana, Temeke, Kigamboni, Tumbi, na Arusha wamepatiwa mafunzo maalum nchini Uturuki mwaka 2024, yanayolenga kuimarisha huduma za dharura nchini.

Kuongezeka kwa Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

34. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalam 48,633 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 na hivyo kufanya idadi ya watumishi katika Sekta ya Afya kufikia 177,711 mwezi Machi, 2025. Aidha, watumishi 8,146 waliajiriwa kwa mikataba kutumia vyanzo vya ndani vya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya.

35. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa wataalam bingwa na bingwa bobezi kwa ajili ya utoaji wa huduma za uubingwa na ubingwa bobezi kwa kuanzisha **Samia Health Super Specialization Scholarship Program** ambapo hadi sasa, jumla ya wataalam 2,779 wamepata mafunzo mbalimbali ya uubingwa na ubingwa bobezi kazini na hivyo kuongeza idadi ya wataalam wa mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi kutoka 768 mwaka 2021 hadi 1,420 Machi, 2025.

Jitihada hizo zimesaidia kupata wataalam wa afya kwenye fani za kibingwa na bobezi watakaotumika kujenga uwezo wa wataalam wetu wa afya katika vyuo vya mafunzo ya afya nchini pamoja na kupunguza rufaa za matibabu kwa wagonjwa nje ya nchi. Vilevile, jitihada hizo zitaimarisha tiba utalii nchini. Kuimarika na Kuongezeka kwa Hali ya Upatikanaji wa Bidhaa za Afya

36. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025 hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu za kipaumbele 382 ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeimarika kutoka asilimia 58 mpaka asilimia 87 sawa na ongezeko la asilimia 29. Katika kipindi hicho, Zahanati asilimia 69 hadi kufikia asilimia 78, Vituo vya Afya asilimia 68 hadi kufikia asilimia 76, Hospitali za Wilaya asilimia 72 hadi kufikia asilimia 81, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 83 hadi kufikia asilimia 97, Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa asilimia 58 hadi kufikia asilimia 99.

37. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025, Jumla ya Shilingi Bilioni 529.2 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Pia, katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kumewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 10 vya dawa na vifaa tiba ambavyo ni viwanda vya kuzalisha maji tiba viwili (2), viwanda vya kuzalisha vitendanishi vya maabara vitatu (3), viwanda vya kuzalisha dawa za vidonge na maji viwili (2) na viwanda vya kuzalisha vifaa tiba vitatu (3).

38. Mheshimiwa Spika, **kuimarika kwa uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini** ambapo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 10 vya dawa na vifaa tiba. Viwanda hivi vitawezesha uwepo endelevu wa maji tiba, vitendanishi vya maabara, dawa za vidonge na maji hususan dawa za ARV ambapo Serikali kupitia MSD imeanzisha utaratibu wa kufufua na kukiwezesha kiwanda cha Tanzania Pharmacetical Industry (TPI) kilichopo Arusha kuanza kuzalisha ARV.

39. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuimarisha kiwanda cha **Viuadudu Kibaha** kwa kutoa jumla ya Shilingi Bilioni 7 kwa ajili ya kuendeleza kiwanda hicho hususan katika eneo la uimarishaji wa matumizi ya teknolojia. Fedha hizo, zimewezesha ununuzi wa lita 583,333.3 ambazo zinaendelea kusambazwa katika Halmashauri zote nchini.

40. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vifaa tiba nchini ambapo **Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba nchini (TMDA) imeendelea kuwa kinara** kwa kushikilia cheti cha utambuzi wa umahiri katika mifumo ya udhibiti ubora wa dawa kwa vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ngazi ya tatu (Maturity Level 3). Hii ikimaanisha kuwa, wananchi wameendelea kupata bidhaa za afya kwa ubora unaokubalika kimataifa.

Kuimarika kwa Huduma za Ubingwa na Ubingwa Bobezi

41. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospital Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda, na Hospitali za Rufaa za Mikoa ili kuhakikisha huduma hizi zinapatikana ndani ya nchi. Huduma za ubingwa bobezi zilizotolewa ni pamoja na upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa Watoto, Upandikizaji wa figo, Kuwekewa Puto tumboni, Upasuaji wa Moyo bila kufungua kifua, Upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua, Upasuaji ubongo, Upasuaji wa uti wa mgongo, Upandikizaji wa nyonga bandia, Tiba ya saratani ya mlango wa kizazi, Tiba ya saratani ya matiti, Tiba ya saratani ya umio, Tiba ya saratani ya Ngozi, Tiba ya saratani ya tezi dume, Upasuaji wa goti bandia, *Kurekebisha mishipa ya damu ya kwenye ubongo*, Upasuaji wa Ubongo kwa njia ya Matundu, Upasuaji wa Vichwa Vikubwa na Mgongo wazi, Upasuaji wa Kiuno, Upasuaji wa Magoti kwa njia ya Matundu na Radiolojia Tiba .

Uwekezaji katika huduma za ubingwa na ubingwa bobezi umewezesha watanzania wengi kupata huduma hizi ndani ya nchi

kwa gharama nafuu ambapo hapo awali walikuwa wakizifuata huduma hizo nje ya nchi.

Kuimarika kwa Tiba Utalii

42. Mheshimiwa Spika, kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika kuboresha huduma za ubigwa na ubingwa bobezi nchini, uwekezaji huo umevutia wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025 idadi ya wagonjwa kutoka nje ya nchi waliokuja kutibiwa nchini imeongezeka kutoka wagonjwa 5,705 mwaka 2021 hadi kufikia wagonjwa 12,180 Machi, 2025. Wagonjwa hao ni kutoka katika nchi za **Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Msumbiji, Congo DRC, Sudan, Uganda, Zimbabwe, Ethipia, Somalia, Kenya, Egypt, na Mauritius.** Aidha Wagonjwa hao walihudumiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Hospitali ya Aga khan na Hospitali ya Saifee.

Kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote

43. Mheshimiwa Spika, **kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na Bunge lako tukufu Novemba,** 2023 kutahakikisha watanzania wote wanapata huduma bora za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya bila kikwazo cha fedha kipindi watakapougua**.**

44. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za chanjo nchini ambapo usimamizi wa mfumo wa utoaji huduma za chanjo umeimarika na **kiwango cha utoaji wa chanjo za kawaida kimepanda kutoka asilimia 81 hadi kufikia asilimia 97**. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imejenga maghala tisa (9) ya kuhifadhia chanjo pamoja na kununua magari 96 kwa ajili ya kutoa huduma za chanjo nchini.

45. Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma kwa magonjwa yasiyopewa kipaumbela umeendelea kuimarika kwa **kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais katika azimio la Kigali ambapo takriban**

watu milioni 34.4 wameweza kukingwa na magonjwa hayo. Mafanikio hayo yamepunguza idadi ya watu wanaohitaji kinga kwa asilimia 76. Aidha, jumla ya watu 11,228 walipata huduma ya upasuaji wa mabusha na watu 13,779 walipata huduma ya upasuaji mdogo wa kusawazisha vikope ili kuwakinga na upofu utokanao na maambukizi ya trakoma na hivyo kufanya Tanzania kuwa kinara katika kutokomeza magonjwa hayo ndani na nje ya Afrika.

46. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za Lishe nchini jumla ya mashine 230 za kunyunyizia virutubishi (dosifiers) kwenye vyakula zimefungwa katika Mikoa 26 nchini na hivyo kufanya jumla ya mashine zote zilizofungwa kufikia 1,402 katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025. Kufungwa kwa mashine hizo kutaimarisha maendeleo ya ukuaji wa afya ya watoto na hivyo kuboresha afya zao na kuwakinga na maradhi mbalimbali yanayoweza kuzuilika.

SEHEMU YA III: MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025

47. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa (2021/22–2025/26), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya - HSSP V (2021/22 – 2025/26), Mpango Mkakati wa muda wa kati wa Wizara wa mwaka (2021/22 – 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs - 2030) pamoja na makubaliano ya Kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

48. Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala za Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa;

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Taifa;
iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;
iv. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga;
v. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;
vi. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini;
vii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;
viii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko;
ix. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu; na
x. Kusimamia Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya.

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA

49. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Fungu 52 hukusanya mapato kutokana na huduma zitolewazo katika Hospitali na Taasisi zilizo chini yake ikiwemo uchangiaji wa huduma mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 756,866,060,248.00 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 70,828,500,189.69 ni kutoka Makao Makuu ya Wizara (ikiwemo Bodi, Mabaraza ya Kitaaluma, Elimu ya Afya kwa Umma na Afya Mipakani), Shilingi 134,171,499,810.31 kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na Shilingi 551,866,060,248.00 ni kutoka Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum, Hospitali ya Taifa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

51. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekusanya jumla ya kiasi cha Shilingi **603,699,104,749.50** sawa na **asilimia 80** ya lengo la kukusanya maduhuli ya Shilingi **756,866,060,248.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **52,396,314,305.99** sawa na **asilimia 74** ya makadirio kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, kiasi cha Shilingi **117,897,942,665.16** sawa na asilimia **88** kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha Shilingi **433,404,847,778.35** sawa asilimia **79** kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara. ***Kiambatisho Na. 1 kinaonesha makusanyo ya maduhuli hayo.***

52. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu kutumia jumla ya kiasi cha **Shilingi 1,311,837,466,000.00** ili kutekeleza majukumu yake.
Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 632,267,220,000.00** ni kwa ajili ya **Matumizi ya kawaida** ambapo Mishahara ni **Shilingi 484,935,496,000.00** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 147,331,724,000.00**. Aidha, jumla ya **Shilingi 679,570,246,000.00** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo** ambapo Fedha za Ndani ni **Shilingi 416,258,609,000.00** na Fedha za Nje ni **Shilingi 263,311,637,000.00**.

53. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya kiasi cha **Shilingi 1,231,841,808,986.02** kimepokelewa sawa na **asilimia 94** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 472,676,230,409.77** sawa na **asilimia 75** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 375,215,222,929.79** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 97,461,007,479.98**. Aidha, kiasi cha **Shilingi 759,165,578,576.25** sawa na asilimia 112 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo Fedha za Ndani ni **Shilingi 501,120,174,316.25** sawa na asilimia 120 na Fedha za Nje ni **Shilingi 258,045,404,260.00** sawa na asilimia 98.

SEHEMU YA IV: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25.

Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

54. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na kuongeza na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuongeza watumishi wa Sekta ya Afya. Maboresho hayo ni pamoja na kuimarisha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto ambapo katika kipindi cha miaka mitano, vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

55. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa, ambapo ifikapo mwaka 2030, lengo ni **kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 104 ya sasa hadi 70** kwa vizazi hai 100,000, vifo vya watoto wachanga kutoka 24 hadi 12 kwa vizazi hai 1,000, na vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 43 hadi 25 kwa vizazi hai 1,000. Kwa kasi iliyopo sasa ni dhahiri kwamba Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi chache zitakazoweza kufikia malengo hayo kwa wakati.

56. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika **kuboresha miundombinu** ya kutolea huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto. Uboreshaji huo wa miundombinu umewezesha huduma za dharura za uzazi kuendelea kuimarika kwa kiwango kikubwa. Baadhi ya miundombinu iliyokamilishwa au kuboreshwa katika kipindi hiki ni pamoja na kuboresha vituo vya afya ili viweze kuwa na uwezo wa kufanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni (Comprehensive Emergency Management of Obstetric and Newborn Care - CEmONC), ambapo hadi kufikia Machi 2025 **vituo vinavyotoa huduma za CEmONC vimefikia 577 kutoka vituo 525** kipindi kama hicho mwaka 2024.

57. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya **wajawazito 2,127,548 walihudhuria kliniki** angalau mara moja kati ya wajawazito **2,077,689** waliotarajiwa. Ongezeko hilo la matumizi ya huduma za kliniki wakati wa ujauzito limetokana na utoaji wa elimu, uwepo wa vituo vya kutolea huduma za afya karibu na wananchi, pamoja na utekelezaji wa mwongozo wa huduma muhimu wakati wa ujauzito.

58. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo vya Umoja wa Mataifa, Wizara imeendelea kuimarisha **huduma wakati wa kujifungua** na kuhamasisha wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wajawazito 1,928,708 walijifungua na kati yao**, wajawazito 1,686,476 sawa na asilimia 87.4 walijifungulia kwenye vituo** vya kutolea huduma. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wajawazito 1,586,953 sawa na asilimia 94.6 walihudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi, ikilinganishwa na wajawazito 1,543,856 sawa na asilimia 93.7 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

59. Mheshimiwa Spika, asilimia 60 ya vifo vitokanavyo na uzazi hutokea baada ya kujifungua, hususan siku tatu za mwanzo, vinavyosababishwa na kupoteza damu nyingi baada ya kujifungua, kifafa cha mimba na maambukizi ya bakteria. Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya baada ya kujifungua**. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **jumla ya akina mama 1,525,672 sawa na asilimia 89.4 ya waliojifungua walipatiwa huduma ndani ya siku tatu za mwanzo** baada ya kujifungua. Sambamba na hilo, jumla ya watoto wachanga 1,517,219 sawa na asilimia 88.9 ya watoto waliozaliwa hai walipata huduma ndani ya siku tatu baada ya kuzaliwa.

'Nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwahimiza kinamama kuendelea kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya wakati wa ujauzito ili changamoto zao ziweze kugunduliwa na kushughulikiwa mapema. Naomba nitumie fursa hii pia kuwaomba waheshimiwa wabunge wanaume kuwa vinara (champions) wa kuwasindikiza wenza wao kupata huduma wakati wa mahudhurio ya kliniki, wakati wa

kujifungua na baada ya kujifungua. Naomba kuwasihi waheshimiwa wabunge wanaume kuwa mfano bora wa matumizi ya huduma hii'.

60. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha **upatikanaji wa bidhaa za uzazi salama** ikiwemo; Sindano ya *Magnesium Sulphate* kwa ajili ya kifafa cha mimba dozi 335,668 sawa na asilimia 91 ya lengo, dawa ya sindano ya *Oxytocin* dozi 3,468,001 sawa na asilimia 95 ya lengo, kwa ajili ya kukinga na kuzuia kupoteza damu wakati na baada ya kujifungua, dozi 150,583,100 za *Fefol* sawa na asilimia 93 ya lengo, kwa ajili ya kuhakikisha mjamzito ana damu ya kutosha, *Misoprostol* vidonge 349,385 sawa na asilimia 92 ya lengo na dozi 1,963 za *Anti D* sawa na asilimia 86 ya lengo, kwa ajili ya kuzuia kuharibika mimba.

61. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **Wizara imeanza ujenzi wa NCUs 121**, **hivyo kufikisha jumla ya NCUs 362 ikilinganishwa na 241 zilizokuwepo kwa kipindi kama hiki mwaka 2024**. Kati ya NCUs 362 zilizopo, 318 zipo kwenye ngazi ya Hospitali na 44 zipo katika ngazi ya Vituo vya Afya vinavyofanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni - CEmONC. Aidha, kati ya NCUs 318 zipo kwenye ngazi ya hospitali; 175 ni hospitali ngazi ya Halmashauri, 28 Hospitali za Rufaa za Mikoa, sita (6) Hospitali yza Rufaa za Kanda, moja (1) Hospitali ya Taifa na 108 Hospitali za Mashirika ya Dini na Binafsi.

62. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za Afya kwa watoto wachanga wagonjwa na wale waliozaliwa kabla ya wakati**. Wizara imenunua na kusambaza mashine za kumsaidia mtoto mchanga kupumua aina ya "Continuous Positive Airway Pressure, CPAP" 130, ambazo zilisambazwa kwenye hospitali za halmashauri 100 zenye Wodi Maalum ya watoto wachanga yaani "Neonatal Care Unit, NCUs". Pia, Wizara kupitia Bohari ya Dawa ilinunua dawa ya kusaidia watoto wachanga kupumua, aina ya "Surfactant" dose 550, ambazo zilisambazwa kwenye kanda zote za Bohari ya Dawa nchini.

"***Nitoe rai kwa viongozi ngazi ya Vituo vya kutolea huduma za Afya, Halmashauri na Mikoa kuhakikisha NCUs zote zilizoanzishwa zina vifaa na zifanye kazi; Hospitali na Vituo vya Afya ambavyo bado havijaanzisha NCUs zianzishe na kila Zahanati na wodi za kujifungulia ziwe na "stabilization corner".***

63. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha huduma kwa watoto chini ya miaka mitano, Wizara imenunua dawa aina ya *Amoxilin* kidonge myeyuko kwa ajili ya kutibu homa ya mapafu (Nimonia) Vidonge 43,763,700 sawa na asilimia 86 ya lengo. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara imenunua dawa ya kutibu kuharisha aina ya Zinki na ORS zilizofungashwa pamoja, pakiti 967,425 sawa na asilimia 89 ya lengo. Upatikanaji wa bidhaa hizi umeimarika hadi kufikia asilimia 90 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2024.

"Tiba dhidi ya Nimonia na Kuharisha kwa watoto ni muhimu katika kuimarisha ubora wa huduma za watoto chini ya miaka mitano, nawasisitiza Viongozi ngazi ya vituo vya kutolea huduma, Halmashauri na Mkoa kuhakikisha, dawa hizi zinapatikana muda wote".

64. Mheshimiwa Spika, katika kipindi Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeimarisha **upatikanaji wa vitabu vya kliniki ya mtoto na mama (kadi za kliniki)**, kwa kuchapisha na kusambaza nakala 2,350,000 kwa ajili ya kliniki za wajawazito na Watoto, ikilinganishwa na nakala 1,200,000 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Vitabu hivyo vinalenga kuwasaidia wazazi na watoa huduma kufuatilia afya na maendeleo ya ujauzito na maendeleo ya watoto.

'Napenda kuwakumbusha watoa huduma za Afya katika Halmashauri na Mikoa, kuwa "Vitabu vya Kliniki ya Mama na Mtoto haviuzwi na wahakikishe vinapatikana muda wote bila malipo kwa wajawazito na watoto'.

65. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea **kuboresha huduma rafiki ya Afya ya uzazi kwa vijana, wenye umri kati ya miaka 10 hadi 24**

kwa kuzingatia mwongozo wa Ajenda ya Kitaifa ya kuwekeza katika afya na Maendeleo ya vijana (NAIA-AHW) yenye nguzo kuu sita;

(i) Kupunguza maambukizi ya VVU kwa vijana,
(ii) Kupunguza mimba katika umri mdogo,
(iii) Kupunguza madhara ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto,
(iv) Kuimarisha afya lishe kwa vijana,
(v) Kuhakikisha vijana wa kike na kiume wanabaki shuleni na kumaliza masomo yao; na
(vi) Kuwajengea ujuzi vijana ili waweze kujiajiri au kuajiriwa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, elimu kwa vijana zaidi ya 450 katika Mikoa ya Njombe, Ruvuma, Iringa, Manyara, Dodoma, Morogoro, Pwani na Tabora imetolewa, na idadi ya vituo vya kutoa huduma rafiki ya Afya ya uzazi kwa vijana vimeongezeka hadi kufikia 1,561 ikilinganishwa na 1,111 kipindi kama hiki mwaka 2024.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma **kwa manusura wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto (GBV & VAC)**. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya manusura wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto (GBV & VAC) 183,824 walipatiwa huduma. Kati ya manusura hao, 58,784 sawa na asilimia 32 walifanyiwa ukatili wa kimwili, 17,896 sawa na asilimia 10 ukatili wa kingono, na 6,673 sawa na asilimia 4 walikuwa ni manusura wa ukatili dhidi ya watoto. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, idadi ya vituo jumuishi vya kutoa huduma kwa manusura wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto "One-Stop Centre", imeongezeka na kufikia vituo 31 kutoka vituo 27 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

"Natoa wito kwa jamii kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, na inapotokea manusura wafikishwe kwenye vituo vya kutolea huduma haraka kwa ajili ya uchunguzi na matibabu"

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za uzazi wa mpango,** ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi

2025 **jumla ya wateja 5,930,037** walipatiwa huduma za uzazi wa mpango. Kati ya hao wateja wapya walikuwa 3,951,648 sawa asilimia 67 ya wateja wote. Aidha, Wateja 1,430,955 sawa na asilimia 24 walipata huduma hizo kupitia huduma mkoba. Vilevile, wanawake 711,626 walipatiwa huduma za uzazi wa mpango mara baada ya kujifungua. Wizara imeendelea kuhamasisha wanaume kutumia njia za uzazi wa Mpango ikiwemo ya kufunga uzazi (Vasectomy) ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wanaume 305 walitumia njia hiyo.

68. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea **kununua na kusambaza dawa mbalimbali kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango**. Bidhaa zilizonunuliwa na kusambazwa ni pamoja *Depo provera* dozi 3,874,810 sawa na asilimia 92 ya lengo, Vidonge vya uzazi wa mpango 3,610,038 sawa na asilimia 99 ya lengo, Vipandikizi aina ya *Implanon NXT* 297,721 sawa na asilimia 65 ya lengo, Vipandikizi aina ya *Jadelle* 277,942 sawa na asilimia 87 ya lengo na Vitanzi aina ya *Copper T* 62,470 sawa na asilimia 82 ya lengo.

69. Mheshimiwa Spika*,* Wizara, katika kuimarisha **huduma ya saratani ya mlango wa kizazi** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wanawake 527,606 walifanyiwa uchunguzi** wa awali. Kati ya hao, 20,528 walionesha mabadiliko ya mlango wa kizazi ambapo 15,614 walikuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na 4,914 walionesha dalili za saratani. Aidha, wateja 546,993 walifanyiwa uchunguzi wa matiti na kati ya hao 4,692 walikutwa na dalili za awali za Saratani ya Matiti na kupewa huduma stahiki.

70. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha **uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi,** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeanzisha utaratibu wa kutumia kipimo cha *HPV DNA testing*, katika Mikoa 14 ya; Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Tanga, Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Tabora, Kagera, Shinyanga, Arusha, Simiyu na Mwanza. Aidha, katika kipidi hicho, Wizara imenunua jumla ya mashine 70 za tiba joto (Thermocoagulators)kwa ajili ya kutibu

mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi. Mashine hizo zimesambazwa katika vituo 70 vya kutolea huduma za afya nchini.

"***Natoa wito kwa wanawake kwenda katika vituo vya kutolea huduma za Afya kwa ajili ya uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi na matiti, kwani aina hizo za saratani zinatibika iwapo zitagundulika mapema***".

71. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **watoa huduma 12,330** wamepatiwa mafunzo elekezi kazini kuhusu stadi mbalimbali ikiwemo namna ya kutibu matatizo yatokanayo na uzazi na matatizo ya watoto wachanga (EmONC) katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, ikilinganishwa na watoa huduma 6,000 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa programu ya **Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia** katika Hospitali za Halmashauri zote 184 nchini na utekelezaji wa mafunzo elekezi kazini kwa kutumia mfumo wa "***Hub and Spoke*".**

72. Mheshimiwa Spika*,* napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 tamko la 5.3.4 (c) linaloeleza kuhusu kutolewa kwa huduma bila malipo kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili ikiwemo mahitaji makubwa ya dawa ikilinganishwa na bajeti inayoidhinishwa na bunge.

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza

73. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari, magonjwa ya moyo na shinikizo la juu la damu, saratani, magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji, matatizo ya afya ya akili, selimundu, magonjwa ya macho na magonjwa ya figo. Afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza zinajumuisha afua za mazoezi dhidi ya tabia bwete; udhibiti wa matumizi ya tumbaku; udhibiti wa matumizi ya pombe

kupita kiasi; pamoja na afua za lishe ikiwemo udhibiti wa matumizi makubwa ya chumvi, sukari na mafuta. Afua nyingine ni pamoja na kuimarisha huduma za afya ya akili, afya ya macho pamoja na huduma za elimu na uhamasishaji wa utambuzi wa viashiria hatarishi vya magonjwa hayo pamoja na matibabu yanayojumuisha huduma za utengamao na huduma shufaa.

74. Mheshimiwa Spika, takwimu za utafiti na ufuatiliaji wa viashiria hatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza uliofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) mwaka 2024, zinaonesha kuwa **ugonjwa wa kisukari katika jamii umepungua kwa asilimia 6.2 kutoka asilimia 9.1 mwaka 2012 hadi asilimia 2.9 mwaka 2023** na tatizo la **shinikizo la juu la damu limepungua kutoka asilimia 26 mwaka 2012 hadi asilimia 22 mwaka 2023**. Hali hii inaweza kuwa imechangiwa na kupungua kwa matumizi ya pombe kutoka asilimia 29.3 mwaka 2012 hadi asilimia 20 mwaka 2023 na matumizi ya tumbaku kutoka asilimia 14.1 mwaka 2012 hadi asilimia 10 mwaka 2023. Aidha, takwimu zinaonesha ongezeko la hali ya ufanyaji mazoezi, hata hivyo kumekuwa na ongezeko la hali ya unene na unene uliokithiri kutoka asilimia 26.0 mwaka 2012 hadi asilimia 30.8 mwaka 2023. Vilevile, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) idadi ya wagonjwa wapya wa saratani imeongezeka kutoka visa vipya 40,464 na vifo vitokanavyo na saratani 26,945 mwaka 2020 na kufikia visa vipya 44,931 na vifo 29,743 mwaka 2022 mtawalia.

75. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la magonjwa yasiyoambukiza, Serikali imeimarisha afua za udhibiti katika ngazi zote ikijumuisha udhibiti katika ngazi ya jamii, mashuleni na mahali pa kazi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **takribani watu milioni 20 walipatiwa elimu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo** kupitia njia mbalimbali ikiwemo usambazaji wa nakala ngumu 15,050 za kitabu cha mtindo bora wa maisha, kuelimisha kuhusu ugonjwa wa kisukari, udhibiti wa pombe na tumbaku pamoja na nakala laini za ujumbe mfupi na kurusha video fupi zaidi ya 10,000 kupitia mitandao ya kijamii.

76. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha tunaifikia jamii na kujenga mazingira wezeshi ya kuelimisha jamii na kuhamasisha utekelezaji wa afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kila mwaka, Wizara huazimisha wiki ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ambayo hutekelezwa katika mikoa na halmashauri zote nchini. Katika maadhimisho ya mwezi Novemba, 2024 takribani watu **5,634,348** walipata elimu kuhusu magonjwa hayo na afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza. Aidha, watu 412,816 walifanyiwa uchunguzi na kupatiwa huduma ambapo kati yao **watu 11,557 walibainika kuwa na shinikizo la juu la damu na watu 13,796 walibainika kuwa na tatizo la kisukari**. Zoezi la upimaji na uibuaji wa wagonjwa wakati wa maadhimisho, kambi Maalum na huduma mkoba limekuwa na mchango mkubwa katika kuibua wagonjwa wakiwa katika hatua za awali na limesaidia kujenga uelewa katika jamii.

77. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Chama cha Olimpiki Duniani (IOC) na Shirika la Afya Duniani (WHO) ilitoa mafunzo na kuwajengea uwezo watu 10,780 wakiwemo wasimamizi wa rasilimaliwatu, waratibu wa mipango kutoka Wizara zote, watumishi wa afya, walimu kutoka shule za sekondari na msingi kuhusu ya udhibiti wa Magonjwa hayo kwa lengo la kuimarisha uratibu na usimamizi wa afua hizo mahala pa kazi.

78. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mapitio ya mwongozo jumuishi wa matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza ili kuruhusu utoaji wa huduma sambamba na huduma nyingine zinazotolewa katika miradi misonge ikiwemo huduma kwa wagonjwa ya VVU, kifua kikuu, magonjwa ya ngono, na Homa ya Ini kwa kujumuisha magonjwa yasiyoambukiza na afya ya akili. Wizara ilifanya tathmini na kuandaa mpango kazi wa utekelezaji (Action Plan for National Scale-Up of Integrated HIV and NCD Services and Mental Health (2025-2027). Utekelezaji wa mpango kazi umeanza katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kagera na Kigoma ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya WAVIU 317,335 walifanyiwa uchunguzi na kati

yao WAVIU 13,777 walibainika kuwa na shinikizo la juu la damu na kuanzishiwa matibabu.

79. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wagonjwa wa Kisukari na Shinikizo la Damu na Selimundu, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI imewajengea uwezo watoa huduma 427 kutoka katika Vituo vya kutolea huduma za Afya kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi ngazi ya afya ya Msingi pamoja na kwenye kambi za wakimbizi.

80. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa **vipimo na dawa za kukabiliana na ugonjwa wa kisukari na magonjwa mengine yasiyoambukiza**. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara ilisambaza mashine 710 na vitendanishi 355,000 vya uchunguzi wa kisukari katika vituo vya afya vya umma 710 nchi nzima kwa ajili ya uchunguzi na ufuatiliaji wa huduma za kisukari. Aidha, Wizara imesambaza dawa za kisukari ikiwemo *Metformin* vidonge milioni 4.5 na *insulin vichupa* 395,000 kwa watoto na vijana wanaoishi na ugonjwa wa kisukari. Mafanikio haya yamewezesha watu wengi zaidi kuzifikia huduma karibu na maeneo yao.

81. Mheshimiwa Spika, uwekezaji mkubwa katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza umechangia kuongezeka kwa wagonjwa wanaoibuliwa mapema kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kwenye jamii na hivyo **kupunguza vifo** vitokanavyo na magonjwa hayo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, idadi ya vifo vilivyotokana na shinikizo la damu vinavyoripotiwa katika mfumo wa takwimu za afya nchini (DHIS-2) vimepungua kutoka vifo 502 hadi vifo 439 sawa na punguzo la asilimia 12 la vifo vitokanavyo ugonjwa huo kipindi kama hicho mwaka 2024.

82. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2025 jumla ya vituo 73 vimesajiliwa kutoa huduma ya kuchuja damu katika mikoa yote nchini kupitia hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za rufaa za kanda, Hospitali Maalum, hospitali ya Taifa na hospitali binafsi. **Uwepo wa**

huduma za kuchuja damu karibu na wananchi kumeokoa maisha na kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa wenye uhitaji. Aidha, Serikali kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kuwekeza kwenye huduma za figo nchini kwa kuongeza mashine 137 za kuchuja damu katika hospitali 15 za umma na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vinavyotumika katika huduma za kuchuja damu kwa bei nafuu. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za upandikizaji figo ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya wagonjwa 155 walipatiwa huduma ya upandikizaji figo.

83. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wagonjwa wa Saratani 11,801 wapya walibainika** na kuanza matibabu katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali ya KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Ili kuimarisha utoaji wa huduma, Serikali inafanya upanuzi wa huduma za matibabu na uchunguzi wa Saratani kwa kuongeza majengo na mashine za tiba mionzi kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road, Bugando, KCMC, Hospitali ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa.

84. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi tano duniani zinazoongoza kwa idadi kubwa ya ugonjwa wa Selimundu ambapo **asilimia 15 ya watanzania wanaishi na vinasaba vya ugonjwa huo**. Katika kudhibiti ugonjwa huu, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha kampeni Maalum ya elimu ya ugonjwa wa Selimundu na kampeni ya **vunja mduara** ambayo inalenga vijana kutambua hali zao ya vinasaba. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **vijana 10,601 kutoka katika Mikoa ya Mwanza, Morogoro, Pwani, Mara, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Tabora walipatiwa elimu na fursa ya kupima vinasaba vya ugonjwa wa Selimundu**. Aidha, Wizara pia ilitoa elimu ya ugonjwa adimu wa Himofilia kwa wazazi, walezi na wagonjwa 1,690 katika Mikoa ya Morogoro, Manyara, Tanga na Arusha.

85. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na upimaji wa ugonjwa wa Selimundu kwa watoto wachanga ambapo katika kipindi cha

Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **watoto wachanga 3,171 walipimwa vinasaba vya ugonjwa wa Selimundu** ili kubaini ugonjwa katika hatua za awali. Aidha, hadi sasa jumla ya Wagonjwa 34,220 wa Selimundu wanaendelea kupatiwa matibabu ambapo zaidi ya asilimia 60 ya wagonjwa hawa wanapata matibabu kwa kutumia dawa ya *Hydroxyurea* na wagonjwa 11 wa Selimundu walipandikizwa uloto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Kupanuka kwa huduma za Hemofilia na Selimundu kutapunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano vinavyotokana na magonjwa haya.

86. Mheshimiwa Spika, kufuatia uwekezaji mkubwa wa Serikali katika kuboresha huduma za macho nchini ikiwemo uwekezaji kwenye rasilimali watu, miundombinu pamoja na mifumo ya ukusanyaji wa taarifa; **jumla ya watu 745,668 walifanyiwa uchunguzi wa macho** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ambapo watu 21,723 walifanyiwa upasuaji wa macho. Katika kipindi hicho, magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje wa macho ni pamoja na Mzio (Asilimia 40.1), Mtoto wa Jicho (Asilimia 15) na Shinikizo la juu la macho (Asilimia 11.4). Vilevile, asilimia **43.8 ya mahudhurio ya wagonjwa wa macho yalisababishwa na upeo mdogo wa macho** kuona unaorekebishika kwa miwani, ambapo jumla ya watu 45,058 walipatiwa huduma ya miwani tiba, sawa na asilimia 66.3 ya waliokutwa na uhitaji wa miwani.

87. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imejengea uwezo walimu na wanafunzi 250 kuhusu matatizo ya afya ya akili na elimu ya kukinga na kuzuia kujiua. Aidha, zaidi ya vijana 100,000 walijengewa uwezo kupitia elimu na midahalo iliyotolewa kwenye mitandao ya kijamii. Vilevile, katika kipindi hicho, watumishi 350 kutoka taasisi za umma walipatiwa elimu ya afya ya akili mahali pa kazi.

88. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na **uboreshaji wa Huduma za Kinywa na Meno na** katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025, imefanya ununuzi na kusambaza mashine 13 za CT- Scan Maalum za kinywa na meno zenye thamani ya Shilingi 3,599,900,000.00 zilizopelekwa katika Hospitali za Rufaa za Kanda za

Chato na Kusini - Mtwara pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Dodoma, Iringa, Manyara, Sekou Toure-Mwanza, Songea, Bombo, Singida, Mawenzi, Temeke, Bukoba na Hospitali ya Jeshi Lugalo. Mpaka sasa ni asilimia 66.7 ya Hospitali za Rufaa za Mikoa na asilimia 33.3 ya Hospitali za Rufaa za Kanda zenye Mashine hii. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya mashine Maalum za x-ray ya kinywa zipatazo 57 zenye thamani ya Shilingi 4,354,800,000.00 zimewasili Bohari ya Dawa (MSD) ambapo tayari Hospitali za Halmashauri 20 (sawa na asilimia 10.9) zimeshapokea mashine hiyo. Hospitali hizo ni Hospitali ya Manispaa ya Morogoro, Hospitali za Halmashauri ya Wilaya Morogoro, Mvomero, Kilosa, Ulanga, Chalinze-Msoga, Mbarali, Igunga, Tanganyika, Kilwa, Sikonge, Urambo, Muheza, Kasulu, Rombo, Bukoba, Mkomaindo-Masasi, Hospitali ya Uhuru-Chamwino na Hospitali ya Mbagala-Temeke na Kituo cha Afya Kaloleni-Arusha. Serikali pia imesambaza mashine za X-ray maalum za meno 48 kwenye Hospitali za Wilaya 6 na vituo vya afya 38. Mpaka sasa asilimia 100 ya hospitali za Rufaa za Kanda, Mikoa na Taifa, asilimia 80 ya Hospitali za Halmashauri na asilimia 30 ya Vituo vya Afya zina X-ray maalum za meno. Vilevile, Wizara imeendelea kusambaza *Dental Chairs* 114 kwenye Hospitali za Halmashauri 25 na vituo Vya Vfya 85.

89. Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa 571,566 walipatiwa matibabu ya kinywa na meno nchini, kati yao wagonjwa 385,633 sawa na asilimia 67.4 walikuwa na tatizo la kuoza kwa meno, wagonjwa 54,155 sawa na asilimia 9.4 walikuwa na tatizo la magonjwa ya fizi na wengine walikuwa na matatizo mengine ya kinywa na meno. Kati ya wagonjwa wenye tatizo la kuoza meno, 159,300 sawa na asilimia 41.3 walipewa matibabu ya kuziba meno. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la Watanzania wanaoziba meno kutoka asilimia 35.6 mwaka 2024 hadi asilimia 41.3 mwaka 2025 ambapo ongezeko hili limechangiwa na uwekezaji mkubwa wa eneo la kinywa na meno unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Nasisitiza kuwa dawa ya jino siyo kung'oa, jino linatibika na kupona kabisa.

90. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma za utengamao kwa watu wenye ulemavu na wenye mahitaji

Maalum wakiwemo watoto na wazee. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wagonjwa 237,174 walipatiwa huduma.** Aidha, katika kipindi hiki huduma zifuatazo zilitolewa; Fiziotherapia wateja 196,766, tiba kazi (Occupational Therapy) wateja 34,029, Matamshi na Lugha (Speech and Language Therapy) wateja 1,685, Vifaa Tiba Saidizi (Assistive Devices) wateja 2,019 na Viungo tiba na vifaa tiba saidizi (Prosthesis and Orthosis) wateja 5,028.

91. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **hospitali za Rufaa za Mikoa saba (7) zimeweza kutoa seti tatu (3) kati ya nne (4) ya huduma za utengamao** ambazo ni *Fiziotherapia, Occupational Therapy* na *Prosthesis and Orthosis*. Hospitali hizo ni Hospitali za Rufaa za Mikoa Dodoma, Tumbi, Iringa, Songea, Maweni, Katavi na Simiyu. Aidha, Wizara inaendelea kujenga uwezo kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa zilizobaki.

92. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, **imeanzisha klabu 32 za afya za wazee (Healthy Ageing Club)** katika Mikoa ya Ruvuma (9), Mbeya (8), Tanga (7) na Dodoma (8) kwenye ngazi za Kata. Lengo la klabu hizi za afya za wazee ni kuhamasisha wazee kufanya mazoezi ya pamoja, kujifurahisha na kupinga tabia bwete ili kujilinda na magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya uzeeni.

93. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya hospitali nane (8) zilifanya upimaji wa usikivu kwa watoto wachanga ili kubaini tatizo la ulemavu wa kusikia. Hospitali hizo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda Benjamin Mkapa, Bugando na Mbeya pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Dodoma, Tumbi, Bombo na Mtakatifu Francis Ifakara. Katika kipindi hiki, jumla ya watoto wachanga 3,163 walipimwa usikivu mara baada ya kuzaliwa na kati yao, 232 walionekana kuhitaji uchunguzi zaidi.

Huduma za Tiba

94. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za afya zinazotolewa na watoa huduma wenye weledi na ujuzi, pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya vituo vilivyopo, Wizara imeendelea kujenga vituo vipya ili kuleta huduma karibu na wananchi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka hadi kufikia 12,846 kutoka vituo 12,266 vilivyokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la vituo 580. Kati ya vituo hivyo 12,846, Vituo vya umma vilikuwa 7,627 na binafsi ni 5,219. **(Kielelezo Na1. Kinaonesha Idadi na Mgawanyo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya nchini)**



Kielelezo Na. 1. Idadi na Mgawanyo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya nchini.

95. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Wizara **imeendelea kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya kwa wananchi** katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vitanda vimeongezeka kutoka 145,374 hadi kufikia vitanda 153,683. Hivyo kufanya uwaino wa vitanda 2.1 kwa kila watu 1,000

ukilinganisha na Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaoelekeza kuwa na uwiano wa vitanda 2.5 kwa kila watu 1,000. Aidha, kati ya vitanda 153,683 vitanda 49,285 vipo katika ngazi ya Hospitali, vitanda 30,937 vipo katika Vituo vya Afya, vitanda 71,102 vipo katika Zahanati na vitanda 2,359 vinapatikana katika kliniki na vituo vinginevyo nchini, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1** hapa chini.

Jedwali Na. 1. Mchanganuo wa Idadi ya Vitanda.

	Vivyohitajika	**Vilivyopo wodini**	**Vitanda vya kujifungulia**	**Vitanda vya uchunguzi**	**Jumla ya Vitanda**
Hospital	58,802	43,664	1,709	3,912	49,285
Vituo vya Afya	35,119	24,051	2,851	4,035	30,937
Zahanati	73,711	36,906	15,156	19,040	71,102
Kliniki	2,030	1,211	112	1,036	2,359
Jumla	**169,662**	**105,832**	**19,828**	**28,023**	**153,683**

96. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi ambapo, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya mahudhurio 39,386,226 ya wananchi** walipata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini ikilinganishwa na wateja 38,031,200 waliopata huduma kipindi kama hiki mwaka 2024. Kati yao, asilimia 8.2 walipata huduma katika ngazi ya Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda, asilimia 11 ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, asilimia 15.9 Hospitali za Wilaya, asilimia 20.8 vituo vya afya na asilimia 37.5 katika ngazi ya Zahanati, asilimia 4 ngazi ya Kliniki, asilimia 0.10 *Maternity and Nursing Home* na asilimia 2.4 ni vituo vinginevyo. Takwimu za utoaji wa huduma za afya zinaonesha kwamba **wananchi asilimia 81 wanapata huduma katika ngazi ya afya ya msingi**, hali hiyo inaonesha juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali katika uwekezaji na uimarishaji wa huduma katika ngazi ya afya ya msingi na kuleta huduma karibu na wananchi **(Jedwali Na. 2)**.

Jedwali Na. 2. Idadi ya Wagonjwa Katika Vituo vya Huduma za Afya, Julai 2024 hadi Machi 2025.

AINA YA KITUO CHA HUDUMA	WAGONJWA WA NJE (OPD)	WAGONJWA WA KULAZWA (IPD)	JUMLA	ASILIMIA
Taifa, Maalum na Kanda	2,753,942	487,412	3,241,354	8.2%
Rufaa ngazi ya Mkoa	3,974,663	363,423	4,338,086	11.0%
Rufaa ngazi ya Wilaya	5,728,111	515,158	6,243,269	15.9%
Vituo vya Afya	7,747,809	454,788	8,202,597	20.8%
Zahanati	14,763,996	10,451	14,774,447	37.5%
Kliniki	1,590,716	101	1,590,817	4.0%
Nyinginezo	940,058	20,343	960,401	2.4%
Vituo vya Kujifungulia	35,255		35,255	0.1%
	37,534,550	**1,851,676**	**39,386,226**	

97. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje (OPD) wenye umri chini ya miaka mitano** yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (Asilimia 37.6), Malaria (Asilimia 9.2) na Kuhara pasipo upotevu wa maji (Asilimia 9.1). Katika umri wa miaka mitano na zaidi magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (Asilimia 17.3) na maambukizi katika njia ya mkojo (Asilimia 15.4). **(Jedwali Na. 3)**

Jedwali Na. 3. Mchanganuo wa Idadi ya Mahudhurio ya nje (OPD) kwa magonjwa yote katika ngazi za zote Huduma za Afya.

Wagonjwa wa nje wenye umri zaidi ya miaka mitano			**Wagonjwa wa nje wenye umri chini ya miaka mitano**		
Aina ya ugonjwa	**Idadi**	**Asilimia**	**Aina ya ugonjwa**	**Idadi**	**Asilimia**
Maambukizi katika Mfumo wa Hewa	3,640,510	17.3	Maambukizi katika Mfumo wa Hewa	4,521,142	37.6
Maambukizi katika Njia ya mkojo	3,247,002	15.4	Malaria (BS +ve, Clinical, mRDT +ve)	1,103,491	9.2
Other Diagnosis	1,705,269	8.1	Kuhara pasipo upotevu wa maji	1,089,108	9.1
Shinikizo la juu la Damu	1,366,693	6.5	Maambukizi katika Njia ya mkojo	816,782	6.8
Malaria (BS+ve, Clinical, mRDT +ve)	1,247,270	5.9	*Other Diagnosis*	769,669	6.4
Peptic Ulcers	870,143	4.1	*Other Non-Infectious GIT Diseases*	505,666	4.2
Other Non-Infectious GIT Diseases	727,340	3.5	Kichomi kisicho Kikali -	398,394	3.3

			NonSevere		
Kisukari	617,999	2.9	Kuhara na upotevu wa maji	306,644	2.6
Rheumatoid and Joint Diseases	475,324	2.3	Magonjwa ya ngozi - *Fungal*	261,731	2.2
Magonjwa ya ngozi - *Fungal*	366,455	1.7	Minyoo ya tumbo	231,350	1.9

98. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa waliolazwa (IPD) wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni Magonjwa ya mfumo wa hewa (asilimia 51.6) na magonjwa ya mfumo wa mkojo (asilimia 9.3). Aidha, magonjwa yaliyoongoza kwa wenye umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni magonjwa ya mfumo wa hewa (asilimia 21.1) na magonjwa ya mfumo wa mkojo (asilimia 18.9) kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4**.

Jedwali Na. 4. Magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa kulazwa chini ya umri wa miaka mitano na umri zaidi ya miaka mitano.

Wagonjwa wa kulazwa wenye umri zaidi ya Miaka Mitano			**Wagonjwa ya kulazwa wenye umri chini ya Miaka Mitano**		
Aina ya Ugonjwa	**Idadi**	**%**	**Aina ya Ugonjwa**	**Idadi**	**%**
Magonjwa ya mfumo wa hewa	3,640,510	21.1	Magonjwa ya mfumo wa hewa	521,142	51.61
Magonjwa ya mfumo wa mkojo	3,247,002	18.9	Magonjwa ya mfumo wa mkojo	816,782	9.32
Other Diagnosis	1,705,269	9.9	*Other Diagnosis*	769,669	8.79

Shinikizo la juu la damu	1,366,693	7.9	Magonjwa ya Ngozi- Non-Fungal	410,569	4.69
Vidonda tumbo	870,143	5.1	Kichomi kisicho kikali	398,394	4.55
Kisukari	617,999	3.6	Magonjwa ya ngozi - *Fungal*	261,731	2.99
Rheumatoid and Joint Diseases	475,324	2.8	Kichomi kikali	186,159	2.12
Magonjwa ya ngozi - *Fungal*	366,455	2.1	Magonjwa ya Ngozi- *Non-Infectious*	165,254	1.89
Upungufu wa damu	324,115	1.9	Upungufu wa damu	153,145	1.75
Wagonjwa wa kulazwa wenye umri zaidi ya Miaka Mitano			**Wagonjwa ya kulazwa wenye umri chini ya Miaka Mitano**		
Aina ya Ugonjwa	**Idadi**	**%**	**Aina ya Ugonjwa**	**Idadi**	**%**
Magonjwa akina Mama	303,125	1.8	*Acute Ear Infection*	115,023	1.31

UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU YA UBINGWA NA UBINGWA BOBEZI

99. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali **za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa** kwa lengo la kusogeza huduma hizi kwa wananchi na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata huduma nchini kwa wakati na kwa gharama nafuu bila kuhitajika kuzifuata nje ya nchi. Aidha, uwekezaji huu unatoa fursa kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi kupata huduma na kukuza dhana ya tiba utalii.

100. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla wa wagonjwa 7,579,440** walipatiwa huduma katika hospitali hizo. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa **6,728,605** na wa ndani (IPD) walikuwa **850,835** Aidha, Wizara imeendelea kuhakikisha **wananchi wasio na uwezo wanapata huduma za afya kwa kupitia utaratibu wa misamaha** mbalimbali inayotolewa na Hospitali. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali za kitaifa, Hospitali maalum, Hospitali za rufaa za kanda na mikoa zimeweza kutoa huduma za afya kwa njia ya **msamaha zenye thamani ya Shilingi** 34,720,233,085.28 **kwa wagonjwa 268,244** waliopatiwa huduma hizo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa**.** Huduma zilizoongoza kutolewa misamaha ni huduma za uchujaji damu (Dialysis), huduma za mionzi kwa wagonjwa wa saratani, vipimo vya maabara, huduma za radioiojia, huduma za upasuaji, gharama za kumuona daktari, dawa na huduma za wagonjwa mahututi (ICU).

101. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali **za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa** kwa lengo la kusogeza huduma hizo kwa wananchi na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata huduma nchini kwa wakati na kwa gharama nafuu bila kulazimika kuzifuata nje ya nchi. Aidha, uwekezaji huu unatoa fursa kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi kupata huduma na kukuza dhana ya tiba utalii.

102. Mheshimiwa Spika, baadhi ya huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upandikizaji wa figo (Wagonjwa 21) , upandikizaji wa vifaa vya usikivu (Wagonjwa 16), upandikizaji wa uloto (Wagonjwa 7), upandikizaji wa meno (Wagonjwa 64), upasuaji wa kupunguza uzito (Wagonjwa 13), upasuaji wa nyonga na goti (Wagonjwa 320), tiba mionzi (Wagonjwa 152,287), tiba kinga (Wagonjwa 42), upandikizaji wa mimba (Wanawake 8), upasuaji wa Moyo bila kufungua kifua (Wagonjwa 3,103), Upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua (Wagonjwa 1,086), upasuaji wa ubongo (Wagonjwa 89), tiba ya saratani ya mlango wa

kizazi (Wagonjwa 527,606), tiba ya saratani ya matiti (546,993), kuwekewa Puto tumboni (Wagonjwa 153), kuchuja damu (Wagonjwa 1,095) na radiolojia tiba (Wagonjwa 264).

103. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **huduma mpya** za ubingwa bobezi zilizoanzishwa katika hospitali za umma ni pamoja na upandikizaji wa mimba, upasuaji na uchunguzi wa kichwa na ubongo bila kufungua fuvu, upasuaji wa mgongo kwa kufungua eneo dogo, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo kupitia tundu la pua na upandikizaji meno.

104. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha **upatikanaji wa huduma angalau nane (8) za msingi za ubingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa**. Huduma hizo zinahusisha akina mama na uzazi, watoto, upasuaji, upasuaji wa mifupa, tiba ya ndani, dawa za usingizi na ganzi, radiolojia na dharura. Aidha, idadi ya madaktari bingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa imeongezeka kutoka 321 Machi 2024 hadi kufikia 431 Machi 2025 sawa na ongezeko la asilimia 25. Hadi kufikia Machi 2025, Hospitali 15 sawa na asilimia 54 zimefikisha lengo la kutoa huduma za fani nane (8) za kibingwa ikilinganishwa na Hospitali nane (8) katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

105. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **Hospitali za Rufaa za Mikoa zimeendelea kuimarisha huduma za ubingwa kwa kuanzisha huduma mpya za ubingwa** katika fani za magonjwa ya macho, mfumo wa mkojo, afya ya akili, masikio, pua na koo, kuchuja damu (dialysis), magonjwa ya ngozi, saratani na magonjwa ya mfumo wa chakula ambapo wagonjwa 10,898 walihudumiwa na kati ya hao, 944 walipata huduma ya kuchuja damu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 13. Huduma hizi zimeanzishwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Kagera, Geita, Iringa, Katavi, Mtwara, Manyara, Kigoma, Kilimanjaro, Morogoro, Arusha, Njombe, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Lindi, Songwe na Pwani.

106. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia kampeni ya **Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia** zaidi ya Madaktari 250 kutoka katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali ya Taifa na Hospitali

Maalum wa fani za kibingwa zaidi ya 14 walishiriki kutoa huduma katika kambi za madaktari bingwa na ubingwa bobezi nchini. Lengo kuu la kampeni hii ni kufikisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi, kupunguza gharama za huduma za kibingwa na kujenga uwezo wa wataalam wa afya katika utoaji wa huduma za ubingwa na bobezi zenye ubora. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa 99,888 walihudumiwa kupitia kambi za madaktari bingwa wa Dkt. Samia zilizofanyika katika Halmashauri na katika Hospitali za Rufaa za Mikoa sita (6) ya Iringa, Rukwa, Mara, Njombe, Dar es Salaam na Kilimanjaro. Kati ya wagonjwa hao, 5,998 walipatiwa huduma za upasuaji, 3,563 walipata rufaa kutoka ngazi ya msingi kwenda Hospitali za Rufaa za Mikoa na 258 walipatiwa rufaa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa kwenda kupata matibabu zaidi katika Hospitali za Kanda na Taifa.

107. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **wataalam 4,638** wa kada mbalimbali waliopo katika vituo vya ngazi ya msingi wamepatiwa mafunzo elekezi na kujengewa uwezo katika kutoa huduma za ubingwa wakati wa kambi za madaktari bingwa wa Dkt. Samia. Maeneo mahususi waliyojengewa uwezo ni pamoja na huduma za magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, magonjwa ya watoto, upasuaji, huduma za dawa ya usingizi na ganzi na huduma za afya ya kinywa na meno.

'Naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi ili kufaidika na huduma hizi kipindi wataalam hawa wanapofika kwenye maeneo yetu'.

108. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha **tiba utalii** nchini, Serikali imeimarisha huduma za ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda nchini. Uimarishaji huu umewezesha wananchi kupata huduma na kuvutia wagonjwa kutoka nchi za nje hususan nchi za ukanda wa Afrika. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya wagonjwa 4,337 waliweza kupata huduma za ubingwa bobezi nchini katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa - MOI, Taasisi ya Saratani -Ocean Road, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Saifee na Aga Khan. Wagonjwa hawa

walitoka katika nchi za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Msumbiji, Congo DRC, Sudan, Uganda, Zimbabwe, Ethiopia, Somalia, Kenya, Egypt, na Mauritius. Huduma zilizotolewa kwa wagonjwa hao ni pamoja na huduma za moyo, mifupa, mifumo ya fahamu, figo na Saratani.

109. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kupitia Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani -Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta binafsi walikwenda nje ya nchi na kutoa **huduma Mkoba** (**outreach services**) kwa wagonjwa katika nchi za Malawi, Visiwa vya Comoro na Burundi pia kutangaza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinazopatikana nchini. Jumla ya **wagonjwa 2,770** walihudumiwa katika kambi hizo. Utoaji wa huduma hizi ni mkakati maalum wa kutangaza huduma za tiba utalii na kuimarisha diplomasia ya afya ya nchi Kimataifa.

Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) – Upanga

110. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imetoa huduma kwa **wagonjwa 579,973** kati ya wagonjwa hao wagonjwa waliolazwa ni 254,881 na wagonjwa wa nje ni 325,092 ikilinganishwa na wagonjwa 354,926 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 63.4. Aidha, hospitali ilitoa **msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama** ambapo imetoa msamaha wenye thamani ya Shilingi 10,640,269,858 kwa wagonjwa 42,714 ikilinganishwa na msamaha wa Shilingi 10,653,345,520 kwa wagonjwa 46,307 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji wa damu (Dialysis), Wagonjwa mahututi (ICU), vipimo vya CT Scan na MRI pamoja na dawa.

111. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kuimarisha huduma za ubingwa bobezi kwa **kuanzisha huduma mpya** ya kupandikiza mimba (IVF) ili kusaidia wanawake wenye changamoto ya kushika mimba kwa njia ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya wanawake

nane (8) walipatiwa huduma hizo, hivyo kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hizi katika hospitali za umma sambamba na kupunguza gharama za huduma hiyo.

112. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zimeendelea kutolewa ambapo upandikizaji wa figo kwa wagonjwa tisa (9) ulifanyika na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 90 tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwaka 2017. Vilevile, upandikizaji wa vifaa vya usikivu ulifanyika kwa wagonjwa 16, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 88 tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwaka 2017.

113. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kufanya marekebisho kwenye majengo mbalimbali ikiwemo; majengo ya kutoa huduma na ofisi za utawala kwa gharama ya kiasi cha Shilingi 1,656,000,000 pamoja na kununua mashine za kisasa za usingizi kwa gharama ya Shilingi 650,000,000. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa maboresho ya Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kushirikiana na Serikali ya Korea ambapo upembuzi yakinifu wa kufanya maboresho ya miundombinu ya Hospitali umekamilika.

114. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Taasisi ya Afya Ifakara, *National Institute of Health* (NIH - Marekani) na *The Gates Foundation* (Marekani) katika tafiti mbalimbali za kimatibabu. Kupitia tafiti hizo, Hospitali imetoa machapisho 382 ya masuala ya afya katika majarida mbalimbali.

115. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **Tiba Utalii** iliendelea kushika kasi ambapo wagonjwa 844 toka nchi mbalimbali (Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mauritius na Zambia) walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 567 katika kipindi kama hiki mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 49.

Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila

116. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali imetoa huduma kwa **wagonjwa 158,528,** kati ya wagonjwa hao, waliolazwa walikuwa 9,564 na wagonjwa wa nje ni 148,964 ikilinganishwa na wagonjwa 147,071 waliohudumiwa kwa kipindi kama hiki mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Aidha, Hospitali imeanzisha huduma mpya moja (1) ya ubingwa na ubingwa bobezi ya upandikizaji meno ambapo wagonjwa 64 walipatiwa huduma za upandikizaji wa meno bandia. Katika kipindi hicho hospitali ilitoa msamaha kwa wagonjwa 6,955 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 3,338,583,678.94. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji wa damu (Dialysis), Huduma za dharura (Emergency), ICU, vipimo vya *CT Scan, X-ray* na huduma za kulazwa.

117. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, huduma za **ubingwa bobezi zilizoendelea** kutolewa na Hospitali ni pamoja na huduma za kupunguza uzito kwa kupunguza ukubwa wa mfuko wa chakula kwa wagonjwa 13, huduma ya upasuaji rekebishi (Cosmetic Surgeries) ambapo wagonjwa 46 walifanyiwa upasuaji huo, huduma ya upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 117, Upandikizaji wa mfupa (Bone grafting) kwa wagonjwa 5 na huduma za upandikizaji meno (Dental Implant) kwa wagonjwa 64. Vilevile, wagonjwa 12 walipatiwa huduma ya upandikizaji wa figo na wagonjwa 153 walipatiwa huduma ya kuwekewa Puto Tumboni kwa ajili ya kupunguza uzito wa mwili.

118. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi wa magonjwa** mbalimbali ambapo **vipimo 28,819** vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo, MRI vipimo 3,093, CT scan vipimo 2,146, X-Ray vipimo 11,412, Ultrasound vipimo 11,504, Panorama vipimo 565 na Mammography vipimo 99. Jumla ya **vipimo vya maabara 288,288** vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa na upatikanaji wa bidhaa tiba ni asilimia 94.

119. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mloganzila imeendelea **kuratibu mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wataalam 86 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali. Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba** (Outreach Services), ambapo kliniki za mkoba sita (6) zilifanyika na jumla ya wagonjwa 754 walipatiwa huduma za kibingwa, kati ya wagonjwa hao wagonjwa 43 walipatiwa huduma za upasuaji.

120. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Tiba Utalii**, katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025, wagonjwa 81 kutoka nchi za Comoro, Uganda, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Kenya walipatiwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Huduma walizopatiwa ni pamoja na upandikizaji wa nyonga na magoti bandia, huduma za kupunguza uzito kwa kuwekewa puto pamoja na huduma za uchunguzi kwa vipimo vya maabara na radiolojia.

Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

121. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imetoa **huduma kwa wagonjwa 222,803** kati ya wagonjwa hao, waliolazwa ni 12,070 na wagonjwa wa nje ni 210,733. Taasisi imeweza kufanya huduma ya kuchunguza mishipa ya miguu kwa wagonjwa 86 na kuzibua mishipa ya miguu kwa wagonjwa 28. Huduma nyingine za **ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea** kutolewa ni uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 1,305, kufunga vifaa visaidizi vya moyo kwa wagonjwa 115, kuzibua mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 244, kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo kwa wagonjwa 46, kuziba matundu ya moyo kwa Watoto wagonjwa 64 na kuchunguza matatizo ya moyo kwa Watoto wagonjwa 80.

122. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Hospitali ilitoa **msamaha** kwa wagonjwa 710 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 825,762,214 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 1,146,206,145 kwa wagonjwa 1,167 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni

pamoja na vipimo vya maabara, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo na malazi kwa upande wa wagonjwa mahututi.

123. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Taasisi **imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi** za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu kwa wagonjwa 455 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 8,249 tangu kuanza kwa huduma hiyo mwaka 2015. Gharama ya kufanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu ni wastani wa Shilingi 15,450,000 kwa mgonjwa mmoja ndani ya nchi ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 50,800,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Vilevile, Taasisi imefanikiwa kufanya upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa 2,632 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 36,022 tangu huduma hizo zilipoanza kutolewa. Gharama ya kufanya upasuaji huo katika Taasisi ni wastani wa Shilingi 6,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 20,000,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi.

124. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa ya moyo ambapo vipimo vya ECHO vilikuwa 23,023, *Holter* vilikuwa 2,710, *Stress ECG* vilikuwa 2,523, *Dobutamine* vilikuwa 132, *Stress ECHO* vilikuwa 35 na *Sparkle Traching ECHO* vilikuwa 732, *Transosophageal ECHO* vilikuwa 38, *X-Ray* vilikuwa 21,972 *Ultra Sound* vilikuwa 23,750, *ECG* vilikuwa 18,105, *Ultra Functional Test* vilikuwa 72 na *ABP* vilikuwa 1,528. Aidha, jumla ya **vipimo vya maabara** 405,258 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 248,409 kipindi kama hiki mwaka 2024.

125. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wataalam 62 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi katika masuala ya moyo ndani na nje ya nchi. Taasisi imetumia jumla ya kiasi cha Shilingi 222,885,033 kutoka katika mapato yake ya ndani kuwalipia watumishi hao.

126. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ***Dkt. Samia Cardiac Outreach Program,*** Taasisi imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 10,975 walifikiwa na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma tangu taasisi imeanza kutoa huduma za mkoba mwaka 2015 kufikia 46,788. Jumla ya wagonjwa 7,782 walipatiwa vipimo vya *ECHO* na *ECG* kupitia huduma hizo za mkoba na wagonjwa wapya 2,612 sawa na asilimia 33.5 waligundulika kuwa na magonjwa ya moyo.

127. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ilihudumia **jumla ya wagonjwa 518** kutoka nchi za Msumbiji, Comoro, Malawi, Zambia, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. Aidha, Taasisi imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo Norway, China, India, Poland na Marekani. Vilevile, kutokana na kuimarika kwa huduma za ubingwa za upasuaji wa moyo, Taasisi imezijengea uwezo nchi za Malawi, Rwanda na Zambia ili ziweze kutoa huduma hizo.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

128. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025 imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 168,483** ambapo wagonjwa waliolazwa ni 7,318 na wagonjwa wa nje ni 161,165 ikilinganishwa na wagonjwa 180,080 waliopatiwa huduma kwa kipindi hicho mwaka 2024. Katika kutekeleza dhana ya ubunifu na upanuzi wa huduma, Taasisi imeendelea kuhudumia wananchi kwa kuanzisha **huduma mpya** tatu (3) za kibobezi ambazo ni:- uchunguzi wa ubongo bila kufungua fuvu, upasuaji wa nyonga na magoti wa marudio na huduma ya kutibu kiharusi. Uanzishwaji na uendelezaji wa huduma za matibabu ya kibingwa bobezi umefanikisha kupunguza rufaa za wagonjwa wa mifupa kwa asilimia 98 na ubongo kwa asilimia 97.

129. Mheshimiwa Spika, huduma zingine za **ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa** na Taasisi ni pamoja na upasuaji wa nyonga, upandikizaji wa goti bandia, upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi. Kupitia matibabu hayo yote ya huduma za ubingwa bobezi

jumla ya wagonjwa 5,552 walihudumiwa kwa mafanikio makubwa na kuwezesha Serikali kuokoa Shilingi Bilioni 141 ambazo zingetumika iwapo wagonjwa hao wangepewa rufaa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

130. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ilitoa **msamaha** kwa wagonjwa 3,321 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 2,733,711,031.88 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 2,702,038,334 kwa wagonjwa 4,318 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na upasuaji na vipandikizi, mionzi, kulazwa, vipimo vya maabara pamoja na dawa.

131. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutumia teknolojia ya kisasa kwenye utoaji wa huduma za afya, Taasisi imeanza kutoa huduma ya upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa kutumia akili unde (Artificial Intelligence). Katika hatua ya kwanza **jumla ya wagonjwa 12** wamefanyiwa upasuaji kwa kutumia teknolojia hiyo. Hatua ya pili ni kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwa kufanya upanuzi wa vyumba vya kufanyia upasuaji ikiwa ni pamoja na kusimika mifumo ya kisasa ya kufanya upasuaji kwa kutumia roboti (Robotic Surgeries).

132. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 42,889 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo, vipimo vya MRI vilikuwa 7,133, CT scan vipimo 4,025, X-Ray vipimo 30,343 na Ultrasound vipimo 1,388. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **vipimo vya maabara** 88,779 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

133. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mifupa Muhimbili MOI imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wataalam sita (6) wamepelekwa masomoni katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi za upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu ndani na nje ya nchi.

134. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Taasisi ilihudumia jumla ya **wagonjwa 203** kutoka nchi za Comoro, Msumbiji, Malawi, Zambia, Uganda, DRC na Rwanda. Aidha, Taasisi imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo China na Slovakia. Idadi hii imeongezeka kwa asilimia 68 ikilinganishwa na wagonjwa 121 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Hii inadhihirisha kuendelea kuimarika kwa ubingwa bobezi zinazotolewa na Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Aidha, pamoja na kuimarisha huduma za tiba utalii, Taasisi imeendelea kutoa **huduma mkoba** katika maeneo mbalimbali nchini ambapo jumla ya wagonjwa 8,050 walipatiwa huduma na kati ya hao 6,162 walipatiwa huduma za kliniki na 1,888 walifanyiwa upasuaji.

135. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa, Taasisi inaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne na ukarabati wa iliyokuwa Hospitali ya Tumaini kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa nje. Aidha, katika kupunguza gharama za uendeshaji na ununuzi wa mitungi ya Oksijeni, Taasisi imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuvuna hewa tiba ya oksijeni ambacho kwa sasa kinatumika.

Taasisi ya Saratani Ocean Road

136. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ya Saratani Ocean Road ilihudumia **jumla ya wagonjwa 26,959** kati ya hao, wagonjwa wa nje ni 25,488 na waliolazwa 1,471. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambazo zimetolewa katika kipindi hiki ni pamoja na uchunguzi wa maabara, uchunguzi wa radiolojia, tiba mionzi nje, tiba mionzi ndani, tiba kemia, tiba kinga na tiba nyuklia. Katika kipindi hicho, jumla ya wagonjwa 188 walitibiwa kwa tiba mionzi IMRT), wagonjwa 153 walitibiwa kwa tiba mionzi ya *3D Brachytherapy*, na wagonjwa 42 walitibiwa kwa tiba kinga.

137. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba mionzi (3D-CRT) ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya tiba mionzi 151,946 zimetolewa. Gharama ya matibabu haya ya kibobezi hapa nchini ni Shilingi 5,000,000 kwa mgonjwa mmoja

ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 12,000,000 kama mgonjwa akitibiwa nje ya nchi. Katika kuendelea kuimarisha ubora wa maisha kwa wagonjwa wa saratani, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba shufaa ikiwemo dawa ya *Oral Morphine* kwa ajili ya kupunguza maumivu kwa wagonjwa 2,809 ikilinganishwa na wagonjwa 2,704 kwa mwaka 2024.

138. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ilitoa **misamaha kwa wagonjwa 3,868** wasioweza kumudu gharama za matibabu, yenye thamani ya Shilingi 3,286,270,154 ikilinganishwa na misamaha ya Shilingi 28,254,601,599.99 kwa wagonjwa 15,475 kwa kipindi hiki cha mwaka 2024. Huduma za misamaha zimepungua kutokana na wagonjwa wengi kutumia kadi za bima ya afya na pia kuweka utaratibu madhubuti kupitia Ofisi ya Ustawi wa Jamii katika kuchangia huduma. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni tiba kemia, tiba mionzi, uchunguzi wa maabara, radiolojia na huduma za kulazwa.

139. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali zimeendelea kuimarika ambapo kwa upande wa radiolojia, vipimo 18,694 vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 8,574 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya vipimo hivyo, vipimo 7,128 ni vya X-Ray, 6,382 vya Ultrasound, 2,589 vya CT scan, 2,229 vya MRI na 366 vya mammograph. Kwa upande wa maabara jumla ya vipimo 171,930 vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 158,607 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, Taasisi imeendelea kushikilia ithibati ya kimataifa ya maabara kutoka Chombo cha Ithibati cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAS) iliyopatiwa tangu mwaka 2021. Hali ya upatikanaji wa dawa za saratani ni wastani wa asilimia 100.

140. Mheshimiwa Spika, Taasisi imekamilisha mradi wa PET/CT Scan na huduma zimeanza kutolewa, hadi sasa **jumla ya wagonjwa 231** wamefanyiwa uchunguzi kwa kutumia mashine hiyo. Aidha, mradi wa ujenzi wa Kituo cha Saratani Mbeya (ORCI Mbeya Cancer Centre) unaendelea ambapo kazi ya ujenzi wa ghorofa moja itakayokuwa na

vyumba vya matibabu ya saratani, tiba kemia, tiba za dawa za nyuklia na kliniki za matibabu sasa umefikia asilimia 5. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuhudumia wagonjwa kutoka mikoa 11 na nchi jirani. Vilevile, utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Jengo la huduma jumuishi za saratani (Multi-purpose Oncology Hospital Building) kwa kutumia mapato ya ndani unaendelea na umefikia asilimia 35.

141. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa kusubiri huduma, Taasisi inaendelea na taratibu za ununuzi na usimikaji wa mashine nne (4) za kisasa za uchunguzi na tiba mionzi ya saratani ambazo ni *Linear Accelerator* kwa gharama ya Shilingi Billioni 8.08, mashine nyingine mbili (2) za *Cobalt - 60* kwa gharama ya Shilingi Billioni 4.4 na *C-Arm* kwa kushirikiana na Tume ya Kimataifa ya Nguvu za Atomiki kwa gharama ya Shilingi milioni 450.

142. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kusomesha wataalam wa kozi za ubingwa na ubingwa bobezi za muda mfupi, wataalam tisa (9) na za muda mrefu wataalam 11. Kozi hizo ni pamoja na *Radiology*, *Clinical Oncology*, *Haematology and Blood Transfusion*, *Women Imaging*, *Urology, Surgery, Gyanecology Oncology,* Famasia na *Medical Physicist*.

143. Mheshimiwa Spika, Taasisi imehudumia jumla ya wateja 11,237 kupitia **huduma mkoba** katika mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Shinyanga, Tanga, Pwani, Simiyu, Dodoma na Zanzibar. Huduma zilizotolewa ni uchunguzi wa saratani ya matiti, mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana na tezi dume.

144. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii,** Taasisi imeendelea kuimarisha huduma ambapo kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Jumla ya wagonjwa 607 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikilinganishwa na wagonjwa 526 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Afrika ya Kusini, Malawi, Kenya, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Msumbiji, Sudani ya Kusini,

Zambia, Rwanda, Burundi na Uganda. Pia, Taasisi imehudumia raia wa kigeni waliotoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo Oman, Marekani, India, Pakistan na Bangladesh hali inayodhihirisha kuendelea kuaminiwa kwa Taasisi hii kwa wageni wanaotembelea au wanaoishi nchini.

145. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma kwa wagonjwa, **tafiti** mbalimbali za kimatibabu zimeendelea kufanyika ambapo kwa sasa Taasisi inafanya tafiti 15 kwa kushirikiana na Taasisi zingine ndani na nje ya nchi ikiwemo MUHAS, NIMR, *University of Zambia*, *University of California San Francisco* (UCSF) na *Lousiana State University* (LSU). Faida ya tafiti hizi ni kuongeza uelewa wa vyanzo vya magonjwa ya saratani, vihatarishi na matokeo ya matibabu ya saratani. Matokeo ya tafiti hizi yatakuwa na manufaa katika tiba ya saratani nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **machapisho ya kitafiti 22** yalifanyika katika majarida ya kimataifa.

146. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili iliendelea kutoa **mafunzo** kwa wanafunzi 170 katika fani za uchunguzi na Tiba ya Radiografia, Onkolojia na Uuguzi katika Onkolojia. Mafunzo hayo yameongeza idadi ya wataalam wa huduma za saratani nchini.

Hospitali ya Benjamin Mkapa

147. Mheshimiwa Spika, Hospitali imetoa huduma kwa **wagonjwa 209,080** kati ya hao, wagonjwa waliolazwa 10,158 na wagonjwa wa nje 198,922 ikilinganishwa na wagonjwa 191,528 katika kipindi kama hiki mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 9. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Taasisi ilitoa misamaha kwa wagonjwa 1,408 wasioweza kumudu gharama za matibabu, yenye thamani ya Shilingi 361,030,133 ikilinganishwa na Shilingi 279,943,046 kwa wagonjwa 1,463 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji damu, vipimo vya maabara, wagonjwa mahututi, huduma za upasuaji na dawa.

148. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ikiwemo; upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa saba (7), upandikizaji figo kwa wagonjwa kumi (10), uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 75, upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 125, Upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa wagonjwa 77 na upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum wa *Cathlab* kwa wagonjwa 472.

149. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za upandikizaji mimba, Hospitali ya Benjamin Mkapa inaendelea na maandalizi ya utoaji wa huduma hii, hadi sasa Wataalam watatu wanamalizia masomo yao ya kupata ujuzi zaidi kuhusu upandikizaji mimba katika vyuo vya nje ya nchi (India na Scotland). Aidha, ukarabati wa eneo maalum la kufanyia upandikizaji unaendelea na mpaka sasa utekelezaji umefikia asilimia 43.

150. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 65,777 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo MRI vilikuwa 3,956, *CT scan* vipimo 3,857, *X-Ray* vipimo 22,682, Fluoroscopy 1239, Mammography 181 na *Ultrasound* vipimo 33,862. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vipimo vya maabara 330,320 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa na hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 98.

151. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwezo wa Taasisi kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya hospitali ya Kanda na Taifa, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 55 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi.

152. Mheshimiwa Spika, Hospitali ilizipeleka huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa utaratibu wa **huduma mkoba** katika mikoa mbalimbali, ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa 5,440 walifikiwa. Kati ya hao 3,509 walipatiwa

huduma za Macho, 200 huduma za Mifupa na ajali, 223 huduma ya koo, masikio na pua, 149 huduma ya upasuaji wa mishipa ya fahamu na ubongo, 208 huduma za mfumo wa mkojo na uzazi kwa wanaume, 389 matibabu ya magonjwa ya ndani, 250 matibabu ya magonjwa ya moyo, 248 matibabu ya saratani, 166 matibabu ya meno na 98 walipatiwa matibabu ya figo.

153. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ya Benjamin Mkapa imefanya **tafiti** mbili (2) ambazo zipo katika mchakato wa kuchapishwa (publication). Aidha, Hospitali inatarajia kukamilisha tafiti nyingine nne katika maeneo ya magonjwa ya figo, damu, moyo na njia ya mkojo. Ukamilikaji wa tafiti hizo na matokeo yake utasaidia hospitali kufanya maamuzi ya uboreshaji wa huduma kwa wagonjwa.

Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe

154. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe imeendelea kutoa huduma za matibabu ya afya ya akili kwa wananchi wa kawaida na wagonjwa wa afya ya akili kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya huduma za uchunguzi na matibabu ya afya ya akili pamoja na utoaji wa huduma za matibabu kwa waraibu wa aina mbalimbali ikiwemo waathirika wa dawa za kulevya. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wagonjwa 75,409** walihudumiwa**,** kati yao 72,421 wagonjwa wa nje na 2,988 walilazwa. Aidha, wagonjwa 134,643 sawa na asilimia 89.1 ni wagonjwa wa Akili na wagonjwa 16,420 sawa na asilimia 10.9 ni wagonjwa wa kawaida.

155. Mheshimiwa Spika; Taasisi ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 4,606 wasioweza kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 651,233,855 ambapo Shilingi 52,593,355 ni gharama ya matibabu na Shilingi 598,640,599 ni gharama ya malazi, chakula na mavazi ikilinganishwa na Shilingi 626,921,346 kwa wagonjwa 964 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na matibabu, chakula, mavazi na malazi.

156. Mheshimiwa Spika; Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ikiwemo uchunguzi wa magonjwa ya akili kati ya hizo, kipimo cha umeme wa Ubongo EEG kilifanyika kwa wagonjwa 56, *ECHO* 270, *ECG* 276, X-Ray 2,625 na *Ultrasound* 2,344. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya **vipimo vya maabara** 35,252 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa na hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 96.4.

157. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwezo wa Hospitali kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya Taifa, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 15 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya **ajira za mkataba 79** zilitolewa na Hospitali ili kupunguza uhaba wa watumishi uliopo katika fani mbalimbali za utoaji huduma.

158. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali iliwafikia wananchi **125,606** kwa njia **huduma mkoba** uliolenga kutoa elimu ya afya ya akili, matibabu na msaada wa kisaikolojia kwenye mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma, Kigoma, Ruvuma na Singida. Jumla ya wananchi **524** walibainika kuwa na magonjwa na changamoto za Afya ya akili na walipatiwa huduma za matibabu.

159. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha North Carolina, Chuo Kikuu cha Miami, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Afya Sayansi Shirikishi Muhimbili, KCMC na KCMUCo inaendelea na tafiti kubwa nne (4), ambazo ni umuhimu wa elimu ya afya akili kwa wagonjwa na familia zinazohudumiwa wagonjwa wa afya ya akili, matumizi ya akili mnemba katika afya ya akili, mtazamo wa masuala ya afya akili kwa watumishi wa afya na watu wa tiba asili, na utafiti wa ugonjwa unaoathiri kumbukumbu kwa wazee (Dementia). Matokeo ya tafiti hizi yanatarajiwa kuchangia kuboresha utoaji wa huduma za afya ya akili nchini.

Hospitali ya Magonjwa Ambukizi - Kibong'oto

160. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto inatoa matibabu ya magonjwa ambukizi kama Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu pamoja *na* utaalam wa kimatibabu kwa mikoa na halmashauri kwa njia ya teknolojia ya masafa (MDRTB -ECHO). Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya wagonjwa 14,552 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 16,174 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Kati ya wagonjwa hao, wa nje 13,947 na waliolazwa 605. Aidha, kati ya wagonjwa 14,552 waliohudumiwa, wagonjwa 418 waligundulika kuwa na Kifua kikuu, kati yao 367 Kifua kikuu cha kawaida na 51 Kifua kikuu sugu. Wagonjwa 51 wa Kifua kikuu sugu walitokana na rufaa kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao hulazwa kwa muda wa wastani wa miezi 6 au zaidi wakipatiwa matibabu, chakula, chakula dawa kwa wenye utapiamlo mkali na mahitaji mengine muhimu ya kijamii. Vilevile, kupitia teknolojia ya masafa Hospitali ilihudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu 39 kutoka Mikoa mbalimbali nchini pasipo kulazimika kupatiwa rufaa.

161. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 1,468 wasioweza kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 21,892,630 ikilinganishwa na Shilingi 58,382,803 kwa wagonjwa 3,712 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zilizoongoza kutolewa misamaha ni dawa, huduma za maabara pamoja na huduma za uchunguzi kwa kutumia mionzi.

162. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vipimo 3,682 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo, vipimo 2,864 vya X-Ray, 784 vya Ultrasound na 34 vya CT Scan. Vilevile, vipimo vya maabara 17,763 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa. Aidha,hali ya upatikanaji wa dawa za Kifua Kikuu na kufubaza virusi vya UKIMWI ni asilimia 100 na asilimia 90 kwa aina nyingine za dawa.

163. Mheshimiwa Spika, Hospitali katika kuboresha huduma za afya imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) kwa ajili ya huduma za radiolojia ambapo usimikaji wa mashine ya CT Scan umekamilika na huduma kuanza kutolewa. Aidha, hospitali imekamilisha usimikaji wa kichomea taka cha kisasa, usimikaji wa mtambo na kuanza uzalishaji wa hewa tiba pamoja na upanuzi na ukarabati wa majengo ya utawala.

164. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwezo wa Hospitali kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya Taifa, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 44 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi wakiwemo wanaofadhiliwa na Samia *Health specialization scholarship program*

165. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto imeendelea kufanya **tafiti** mbalimbali kwa lengo la kuboresha tiba na ugunduzi. Tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa kupunguza muda wa matibabu ya kifua kikuu cha kawaida kutoka miezi sita (6) hadi minne (4) na utafiti wa kuboresha matibabu ya wagonjwa wa UKIMWI wenye maambukizi ya Kifua Kikuu ili kuona uwezekano wa kupunguza vifo katika kundi hili. Utafiti huu unafanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Mbarara nchini Uganda na Chuo Kikuu cha Virginia nchini Marekani.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando

166. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa Kanda Bugando hutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika Mikoa nane (8) ya Kanda ya Ziwa yenye jumla ya wakazi wapatao milioni 22. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 286,718**. Kati ya hao, waliolazwa 27,016 na wa nje ni 259,702 ikilinganishwa na wagonjwa 365,261 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 22,397 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 3,305,676,941 ikilinganishwa na Shilingi 3,619,939,055 kwa

wagonjwa 22,277 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na mionzi tiba, magonjwa ya afya ya akili, matibabu ya watoto wachanga, mama wajawazito, uchujaji wa damu na huduma kwa wazee wasiojiweza.

167. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa huduma za Upasuaji wa ubingwa bobezi kwenye maeneo ya kubadilisha nyonga na magoti, upasuaji wa kinywa na meno, upasuaji wa watoto wenye mdomo sungura (cleft lip/palate), upasuaji wa macho, upasuaji wa koo, pua na masikio, upasuaji wa kifua na moyo, upasuaji wa ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo, upasuaji wa mfumo wa mkojo, upasuaji sanifu, upasuaji Maalumu wa watoto, upasuaji wa matundu madogo na huduma ya viungo tiba (saidizi) na vifaa tiba saidizi (orthopedic – rosthetics and orthotics unit). Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wagonjwa 10,907 walifanyiwa upasuaji kati yao 10,626 walifanyiwa upasuaji mkubwa na 281 upasuaji mdogo. Aidha, katika kuendelea kutoa huduma za saratani, jumla ya wagonjwa 23,712 walihudumiwa na kati ya hao, wagonjwa 20,551 ni wa nje na 3,161 walilazwa.

168. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vipimo 57,406 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo 2,729 MRI, 7,136 CT-Scan, 22,602 X-Ray, 23,749 Ultrasound, 112 Mammography, 814 Fluoroscopy na Interventional radiology vipimo 264. Katika kipindi hiki, jumla ya **vipimo vya maabara** 713,196 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

169. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwezo wa Hospitali kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya Kanda, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 61 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi wakiwemo wanaofadhiliwa na Samia *Health Specialization Scholarship Program*. Pia, katika kipindi hicho Hospitali imepokea watumishi wapya 35 kutoka Serikali Kuu ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

170. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa kusubiri huduma, Hospitali inaendelea na taratibu za ununuzi wa Mashine Tiba ya Mionzi (Linear Accelerator) kwa ajili ya matibabu ya Saratani yenye thamani ya Shilingi 1,763,940,285 kwa ufadhili wa Serikali na mapato ya ndani. Mashine hii itasaidia kuongeza idadi ya wagonjwa watakaohudumiwa kwa siku kutoka 82 hadi 164. Aidha, Hospitali inaendelea na ununuzi wa mashine ya *C-Arm* kwa ajili ya *Interventional Radiology* yenye thamani ya Shilingi 407,000,000.

171. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma mkoba** kwa vituo 38 katika wilaya za Magu, Bariadi, Buchosa, Misungwi na Biharamulo. Katika zoezi hilo, **jumla ya wagonjwa 2,517** walipatiwa huduma na kati yao 328 walifanyiwa Upasuaji. Aidha, Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 85 kutoka nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali imefanya **tafiti** 182 katika maeneo mbalimbali ya afya. Tafiti hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika kutengeneza miongozo mbalimbali ya matibabu hapa nchini ikiwemo miongozo ya usugu wa Dawa za *Antibiotic*. Vilevile, Hospitali inaendelea na utafiti wa jani la mgomba katika kuwezesha matibabu ya vidonda vya kuungua na moto.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya

172. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa wananchi wa mikoa saba (7) ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 307,253** ikilinganishwa na wagonjwa 263,011 sawa na ongezeko la asilimia 17 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 36,433 na wagonjwa wa nje (OPD) ni 270,820. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 32,411 wasio na uwezo yenye thamani ya Shilingi 809,499,200

ikilinganishwa na Shilingi 603,730,000 kwa wagonjwa 17,700 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

173. Mheshimiwa Spika, Hospitali imetoa huduma katika fani za upasuaji wa moyo wagonjwa 226, ubongo na mishipa ya fahamu 11,122 na mfumo wa chakula na ini 7,302, mfumo wa upumuaji 6,359 pamoja na upasuaji wa watoto wachanga kwa wagonjwa 455. Aidha, **huduma nyingine za ubingwa bobezi** zilizoendelea kutolewa ni upasuaji, masikio, pua na koo, saratani, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya wanawake, uzazi na watoto, ajali na dharura (EMD), magonjwa ya ndani na ngozi. Kwa huduma za watoto Hospitali imetoa huduma za watoto wachanga wagonjwa 2,216 ikilingalishwa na Watoto wachanga 1,872 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Katika mwaka huu wa fedha huduma za wagonjwa mahututi zilitolewa kwa wagonjwa 1,131 ukilingalisha wagonjwa 904 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

174. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali na jumla ya vipimo 51,603 vya Radiolojia vilifanyika. Vipimo hivyo ni pamoja na; MRI vipimo 502, CT Scan 3,089, X-Ray 13,123, Fluoroscopy 11,234 na Ultrasound 23,655. Aidha, katika kipindi hiki jumla ya vipimo vya **maabara** 191,808 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa. Vilevile, kwa sasa hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 91.5.

175. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea **kuratibu mafunzo** kwa wataalam na katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla wataalam 58 wapo masomo katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya **ajira za mkataba 543** zilitolewa na Hospitali ili kupunguza upungufu wa watumishi.

176. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 177 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Wagonjwa waliohudumiwa ni kutoka nchi za Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Msumbiji.

Taasisi imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo China.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda – KCMC

177. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ilihudumia **jumla ya wagonjwa 187,731**. Kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni 173,193 na wagonjwa wa kulazwa ni 14,538 ikilinganishwa na wagonjwa 340,455 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Aidha, Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ikiwemo ubadilishaji wa nyonga wagonjwa 78 na upasuaji kwa njia ya tundu dogo kwenye mfumo wa chakula kwa wagonjwa 231. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 4,002 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 2,102,960,145 ikilinganishwa na Shilingi 19,189,800,400 kwa wagonjwa 6,084 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

178. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeedelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambazo ni; ugumba na endokrinolojia wagonjwa 1,716, upandikizaji wa kornea wagonjwa 110, upasuaji wa saratani wagonjwa 713, matibabu ya saratani wagonjwa 9,165, upasuaji wa njia ya mkojo wagonjwa 743, matibabu ya ngozi wagonjwa 11,236, na matibabu ya macho wagonjwa 28,337. Huduma zingine zilizotolewa ni matibabu ya njia ya mkojo na kibofu wagonjwa 7,505, upasuaji wa kinywa na uso wagonjwa 131, upandikizaji wa taya wagonjwa 42, viungo bandia wagonjwa 333, viungo saidizi 847, na upasuaji wa retina wagonjwa 509. Huduma hizi zimewezesha wananchi wa mikoa ya Kaskazini kuzipata kwa haraka, urahisi na kuondoa ulazimu wa kuzifuata mbali.

179. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** ambapo wagonjwa 1,664 walifanyiwa kipimo cha MRI, CT-Scan wagonjwa 4,004, ultrasound wagonjwa 13,276, X-Ray wagonjwa 23,138 na maabara ilifanya vipimo 199,807. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali ni asilimia 99 ukilinganisha asilimia 98.5 kwa 2024.

180. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendele kutoa mafunzo kwa watumishi na katika kipindi hiki, jumla ya wataalam 281 wapo masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa Watumishi, Hospitali imeajiri jumla ya watumishi 470 wa mikataba.

181. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kuimarisha huduma kwa kuendelea na upanuzi wa miundombinu kwa ujenzi wa vyumba 11 vya upasuaji ambavyo vimefikia asilimia 78, jengo la mionzi (bunker) uliofikia asilimia 95.5 ikifadhiliwa na Serikali kwa Shilingi Bilioni 4, mabweni ya wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wa saratani umefikia asilimia 88 na maabara ya umahiri uliofikia asilimia 80. Vilevile, Hospitali imendelea kuboresha huduma za mama na mtoto kwa kukarabati na kuboresha miundombinu ya wodi ya wazazi ambapo ukarabati huu umekamilika kwa asilimia 100. Ukamilishaji wa miradi hii itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa, kupunguza muda wa kupata huduma na uanzishaji wa huduma za mionzi tiba ya magonjwa ya saratani.

182. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, na jumla ya wagonjwa 4,618 walipatiwa huduma. Kati yao wagonjwa 2,788 walipatiwa huduma katika Siku ya maadhimisho ya Figo, Macho na Usikivu Duniani na Wagonjwa 1,830 walipatiwa huduma za saratani, VVU/UKIMWI na Ngozi.

183. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilipokea jumla ya wagonjwa 579 ikilinganishwa na wagonjwa 384 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024 kutoka katika nchi za Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Comoro. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Hospitali iliwapatia huduma za matibabu raia wa kigeni 51 kutoka nchi mbalimbali waliofika nchini kwa shughuli anuai ikiwemo utalii kutoka Marekani, Uingereza na Canada.

184. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya **tafiti 35** zimefanyika katika maeneo ya magonjwa ya kuambukiza, usimamizi wa matibabu ya dharura, uchunguzi wa

vinasaba vya magonjwa kama VVU na uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza kama Kisukari na shinikizo la damu. Tafiti hizo hufanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo *Duke University, London School of Hygine and Tropical Medicine, Radbound University* na *Philips University of Murburg*.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato

185. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato inahudumia Mikoa ya Kagera, Kigoma, Geita na Shinyanga na nchi ya jirani ya Burundi. Hospitali inatoa huduma za kibingwa katika fani za afya ya uzazi na magonjwa ya akinamama, upasuaji, radiolojia, dawa za ganzi na usingizi na magonjwa ya watoto. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 30,553**, wagonjwa wa nje 28,759 na wa kulazwa ni 1,794 ikilinganishwa na wagonjwa 40,370 katika kipindi kama hiki 2024. Wagonjwa waliopata huduma za kibingwa ni 29,737 kati yao 6,226 magonjwa ya afya ya uzazi, 9,409 magonjwa ya Watoto, 3,222 huduma ya upasuaji na 10,880 magonjwa ya ndani. Aidha, hospitali inashirikiana na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete ili kutoa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi za moyo kupitia kliniki ya kila mwezi ambapo jumla ya wagonjwa 3,521 wamenufaika na huduma hiyo.

186. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeanzisha huduma mpya nne (4) katika kipindi hiki ambazo ni kliniki ya ubingwa na ubingwa bobezi ya mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu iliyohudumia wagonjwa 2,598, ambao kati yao, mifupa ni 1,795, mishipa ya fahamu ni 795, na upasuaji mkubwa wa mifupa 36 na wagonjwa 12 upasuaji mkubwa wa ubongo. Huduma nyingine mpya zilizoanzishwa ni pamoja na kuanzisha huduma ya benki ya damu, upimaji wa wingi wa Virusi vya UKIMWI na Kliniki ya Selimundu.

187. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 586 yenye thamani ya Shilingi 121,201,313 ikilinganishwa na wagonjwa 314 yenye thamani ya Shilingi 94,679,090 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

188. Mheshimiwa Spika, huduma za uchunguzi wa magonjwa zimeendelea kutolewa na katika kipindi hiki vipimo 12,397 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya *MRI* vilikuwa 279, *CT Scan* 351, *XRay* 2,565, *Dental X-Ray* 133 na *Ultrasound* 2,635, *ECHO* 3,102 na *ECG* 3,342. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya vipimo vya maabara 40,745 vimefanyika kwa kutumia mashine za kisasa na hali ya upatikanaji wa dawa imefikia asilimia 97.

189. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kuratibu mafunzo kwa watumishi na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya madaktari 20 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Kati ya wataalam hao 20, watumishi saba (7) wanasomeshwa kutokana na mapato ya ndani. Sambamba na hili Hospitali kupitia mapato ya ndani imeajiri watumishi 30 wa mkataba.

190. Mheshimiwa Spika, huduma za mkoba zimeendelea kutolewa na katika kipindi hiki huduma hizo zimefanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Muleba ambapo wagonjwa 1,600 walipata huduma za kibingwa. Aidha, wagonjwa 695 walipatiwa huduma za afya ya uzazi, 327 huduma za watoto, 208 huduma za upasuaji na 370 huduma za magonjwa ya ndani. Vilevile, wagonjwa 21 walifanyiwa upasuaji, 13 upasuaji mdogo na 8 upasuaji mkubwa.

191. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii**, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 15 kutoka nchi za Uganda na Burundi. Aidha, katika kuboresha huduma za Hospitali kupitia tafiti, Hospitali imefanya tafiti sita (6) zinazohusu uboreshaji wa huduma. Tafiti hizo zipo katika hatua mbalimbali ambapo tafiti moja imeshachapishwa na nyingine zipo katika hatua mbalimbali za uchapishaji.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara

192. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara inahudumia wananchi wa mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma pamoja na wananchi wa nchi za nchi jirani kama Comoro, Msumbiji na Malawi. Wizara imeendelea kuiwezesha Hospitali kuwa na uwezo

zaidi wa kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambapo Hospitali imeendelea kuimarika na kuwa na uwezo wa kutoa huduma za kibingwa katika fani za Afya ya uzazi na magonjwa ya akina mama, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ndani, radiolojia na huduma ya ubobezi ya magonjwa ya moyo. Katika kipindi hiki hospitali imehudumia jumla ya wagonjwa 31,297. Kati yao, wagonjwa wa nje ni 29,239 na wa kulazwa ni 2,058 ikilinganishwa na wagonjwa 22,122 katika kipindi kama hiki mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 41.

193. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeanzisha kitengo maalum kwa ajili ya huduma za lishe, huduma hii itasaidia katika matibabu lishe kwa wagonjwa na hivyo kuboresha matokeo ya huduma za tiba. Aidha, Hospitali Inaendelea kukamilisha maandalizi ya huduma ya uchujaji damu (dialysis) baada ya mapokezi ya mashine tisa (9) na mafunzo ya watumishi kukamilika. Huduma hii itaongeza wigo wa huduma za kuchuja damu kutoka Hospitali moja ya umma kwa Kanda ya kusini na kufikia Hospitali mbili (2) zinazotoa huduma hizo.

194. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Hospitali ilitoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa 7,507 na kati yao; wagonjwa 492 walifanyiwa upasuaji, 1,517 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya moyo, 2,693 walipatiwa matibabu ya mifupa, 1376 walipatiwa huduma za dharura, 834 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya akinamama na uzazi na 595 walipatiwa huduma za magonjwa ya ndani. Pia, huduma za Mkoba kwa ajili ya matibabu ya mifupa na meno ziliendelea kutolewa ambapo wagonjwa 476 walipatiwa matibabu ya meno na wagonjwa 416 walipatiwa huduma ya matibabu ya mifupa.

195. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Hospitali ilitoa misamaha kwa wagonjwa 365 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 14,037,559 ikilinganishwa na Shilingi 14,091,153 kwa wagonjwa 241 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

196. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa kibingwa ambapo katika kipindi hiki, wagonjwa 152 walifanyiwa kipimo cha MRI, wagonjwa 410 walifanyiwa kipimo cha CTScan, wagonjwa 2,279 walifanyiwa kipimo cha ultrasound na wagonjwa 2,082 walifanyiwa kipimo cha Xray. Kwa upande wa **maabara** jumla ya vipimo 31,220 vilifanyika. Aidha, hali ya upatikanaji wa damu salama katika Hospitali ni asilimia 100 na upatikanaji wa dawa ni asilimia 95.

197. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Hospitali imeendelea kuratibu mafunzo kwa watumishi 21 ambao wapo masomoni kwa mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika fani mbalimbali. Vilevile, Hospitali imepokea watumishi 58 wa ajira mpya kutoka Serikali Kuu na pia imeajiri watumishi 53 kwa mapato ya fedha za ndani kwa mkataba ili kuongeza nguvu ya rasilimali kwa lengo la kuboresha huduma kwa wagonjwa.

198. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha diplomasia ya nchi kupitia **tiba utalii**, hospitali ilitoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 271 kutoka nchi za Comoro, Malawi na Msumbiji. Aidha, Hospitali imefanikiwa kuongeza vyumba sita (6) vya wodi ya watu maalum ambavyo vinaweza kutumika kwa wateja wanaohitaji huduma za kipekee kwa malipo ya ziada.

199. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kufanya tafiti tatu, ambazo zinahusu; (1) tathmini ya ufuasi wa matumizi ya dawa na viashiria vya dharura za shinikizo la damu, (2) uelewa wa watoa huduma kuhusu usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (UVIDA), na (3) uelewa wa vihatarishi vya maambukizi ya virusi vya Homa ya Ini B (HBV).

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mashariki – CCBRT

200. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi , na kipindi hiki wagonjwa 88,808 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 86,211 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Waliohudumiwa katika kipindi hiki, wagonjwa wa nje

ni 84,982 na wa kulazwa ni 3,826. Aidha, wagonjwa 9,557 walipata huduma na kati yao walikuwa na ulemavu wa macho, mdomo sungura, miguu kifundo, mtindio wa ubongo, ulemavu mwingine wa viungo na fistula kwa wanawake. Katika kipindi hiki, jumla ya wajawazito waliojifungua walikuwa 921.

201. Mheshimiwa Spika, Hospitali imetoa **huduma mpya nne (4)** ambazo ni upasuaji rekebishi wagonjwa (35), upasuaji kwa njia ya matundu madogo (14); kutoa uvimbe kwenye mayai ya uzazi wagonjwa (23), kufunga mirija ya uzazi kama njia ya uzazi wa mpango wagonjwa (9), upasuaji wa ndani ya kizazi kwa njia ya kamera wagonjwa (18) na huduma ya uchunguzi kwa njia ya matundu madogo wagonjwa (61), na kuweka lensi kwenye mboni 246. Hospitali pia imetoa huduma ya ziada ya Upasuaji wa makengeza kwa watoto 58.

202. Mheshimiwa Spika, Hospitali iliendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za upasuaji kwa wagonjwa 6,667 walinufaika. Kati yao, wagonjwa 5,289 walifanyiwa upasuaji wa macho, 322 fistula ya uzazi, 880 upasuaji wa mifupa, 90 upasuaji wa mdomo sungura, na 354 wenye miguu kifundo. Pia, hospitali ilitoa huduma za utengemao kwa wahitaji 3,100. Aidha, huduma zingine zilizotolewa ni pamoja na huduma ya kuchuja damu kwa wagonjwa 151 na kutoa viungo saidizi kwa wahitaji 663. Vilevile, katika kipindi hiki hospitali ilitoa misamaha kwa wagonjwa 6,150 yenye thamani ya Shilingi 3,248,719,944.46 ikilinganishwa na wagonjwa 4,552 waliogharimu Shilingi 6,695,986,236 kwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

203. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Hospitali imeimarisha huduma za **uchunguzi za maabara** ambapo vipimo 74,346 vilifanyika. Katika kipindi hicho, wagonjwa 268 walifanyiwa kipimo cha CT - Scan, 4,063 *ultra-sound*, 1,387 *Echocardiology* na 6,644 *X-Ray*. Sambamba na hilo, Hospitali imetoa ufadhili kwa mtaalam mmoja (1) aliyepo masomoni kwa kozi za ubingwa na ubingwa bobezi wa masuala ya obiti na upasuaji rekebishi wa jicho. ***Aidha,*** Hospitali imeendelea kutoa

huduma za mkoba kwa wagonjwa 10,433. Huduma hizo ni pamoja na utengemao kwa wateja 1615.

204. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya Tiba Utalii hospitali imehudumia wagonjwa 591 ikilinganishwa na wagonjwa 135 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma za matibabu zilizotolewa zilihusisha tiba ya macho, vifaa saidizi vya macho, mifupa na Fistula ya uzazi kwa wageni kutoka Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Eritrea, Ethiopia, Ghana, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Somalia na Sudan. Aidha, hospitali imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo Ireland ya Kaskazini, China, India, Indonesia na Iran.

Hospitali za Rufaa za Mikoa

205. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zimeendelea kuimarishwa ili kutoa huduma zenye hadhi ya ubingwa hususani katika fani nane za kipaumbele ambazo ni huduma za magonjwa ya ndani, magonjwa ya watoto, upasuaji, upasuaji wa mifupa, radiolojia, dawa za usingizi na ganzi, huduma za dharura na afya ya uzazi na magonjwa ya akina mama. Katika kipindi hiki Hospitali za Rufaa za Mikoa zimetoa huduma kwa wagonjwa 2,628,784 ambapo kati ya wagonjwa hao wa kulazwa ni 220,494 na wa nje ni 2,408,290 ikilinganishwa na wagonjwa 2,309,964 waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2024.

206. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali za Rufaa za Mikoa zilitoa misamaha kwa wagonjwa 134,145 yenye thamani ya Shilingi 2,630,043,203 ikilinganishwa na Shilingi 2,920,786,230 kwa wagonjwa 302,999 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

207. Mheshimiwa Spika, Hospitali za Rufaa za Mikoa zimetoa **huduma mkoba**, jumla ya wagonjwa 68,058 walihudumiwa na kati yao 5,121 walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 35,281 waliohudumiwa na 2,356 waliofanyiwa upasuaji kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma mkoba zilizotolewa zilikuwa za magonjwa ya

akinamama na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, macho, ngozi, utoaji wa dawa za usingizi na ganzi na radiolojia. Uanzishwaji wa huduma mpya na utoaji wa huduma mkoba uliwawezesha wananchi kupata huduma kwa haraka katika Mikoa yao, kupunguza gharama za matibabu na kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Kanda, Maalum na Taifa.

208. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, jumla ya vipimo 395,971 vilifanyika. Vipimo hivyo vimejumuisha CT scan 24,370, *Ultra Sound* 184,768 na *X-ray* 186,833. Aidha, jumla vya vipimo 1,920,148 vya maabara vilifanyika. Upatikanaji wa dawa kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa umeongezeka kutoka asilimia 94 mwaka 2024 na kufikia asilimia 96 mwaka 2025.

209. Mheshimiwa Spika, katika dhana ya kuendeleza **Tiba Utalii** nchini, Hospitali za Rufaa za Mikoa na hasa zilizopo pembezoni mwa mipaka ya nchi, zilihudumia wagonjwa 275 kutoka nchi jirani za Malawi, Ethiopia, Zambia, Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi, Kenya, Uganda na Msumbiji.

210. Mheshimiwa Spika, Hospitali zimeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kujenga majengo mapya, ukarabati wa majengo pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na mitambo. Baadhi ya vifaa tiba na mitambo iliyonunuliwa ni 3D-CBCT (CT- Scan Maalum za kinywa na meno), mashine za mionzi, meza za upasuaji, mashine za kutoa dawa za usingizi na ganzi, mashine za *ultra sound*, mitambo ya kisasa ya kuchomea taka, mashine za kufulia, mashine za huduma ya *endoscope*, mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni na magari ya wagonjwa na utawala.

211. Mheshimiwa Spika, idadi ya madaktari bingwa wanaopatikana Hospitali za Rufaa za Mikoa imeongezeka kufikia 402 hadi Machi 2025 ikilinganishwa na 328 kipindi kama hiki mwaka 2024. Hii imesababisha kuongezeka kwa hospitali zinazotoa huduma za kibingwa kwa fani 8 zinazohitajika kufikia 15 ukilinganisha na 8 za kipindi kama hicho

mwaka 2024. Hospitali zimeendelea kuratibu mafunzo ambapo katika kipindi hiki, watumishi 563 walikwenda masomoni katika fani mbalimbali, kati yao 146 sawa na asilimia 25 walifadhiliwa na hospitali kwa kutumia mapato ya ndani. Kwa upande wa tafiti, jumla ya tafiti 98 zimefanyika na tafiti hizo zimejikita katika maeneo ya magonjwa ya ndani, magonjwa ya mama na mtoto, maabara, magonjwa ya dharura na lishe.

Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Kuambukiza Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono

212. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuzuia maambukizi mapya na kutoa huduma za tiba kwa magonjwa ya VVU/UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini. Afua hizo ni pamoja na; kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU; kutoa huduma za ushauri nasaha; upimaji; matunzo na huduma za dawa kwa wenye maambukizi ya VVU/UKIMWI; huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; kuhamasisha wananchi kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kupima na kupata chanjo ya kujikinga na maambukizi ya Homa ya Ini; kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha wananchi, hususan wajawazito kupima maambukizi ya magonjwa ya ngono na kupata matibabu sahihi.

213. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025, takwimu zinaonesha kuwa jumla ya watu 1,530,227 walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi ikiwa ni sawa na asilimia 90 ya watu 1,700,000 wanaokadiriwa kuishi na VVU nchini (95 ya kwanza). Watu 1,500,212 kati ya waliopima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza VVU, sawa na asiilimia 98 (95 ya pili). Aidha, jumla ya vipimo 874,944 vya kujua wingi wa VVU (Viral Load) kwa wagonjwa walioanza kutumia dawa vilifanyika, ambapo vipimo vya wagonjwa 858,272 sawa na asilimia 98 vilionesha kuwa virusi vya UKIMWI vimefubazwa (95 ya tatu). **Jedwali Na. 5** linaonesha ufafanuzi huo.

Jedwali Na. 5. Mafanikio kuelekea kufikisha malengo ya 95-95-95.

Na.	Kiashiria	Machi 2024	Machi 2025	Hali ya 95-95-95
1	Wanaokadiriwa kuwa na maambukizi (People Living with HIV/AIDS - PLHIV)	1,700,000	1,700,000	95 ya kwanza
	Wanaotambua hali zao za Maambukizi	1,515,838	1,530,227	
	Asilimia ya wanaotambua hali zao (on care)	89	90	
2	Wenye maambukizi na wameanza dawa	1,493,532	1,500,212	95 ya pili
	Asilimia ya walioanza dawa (on ART)	98.5	98	
3	Idadi ya waliopimwa makali ya VVU (VL test)	974,405	874,944	95 ya tatu
	Idadi ya makali yaliyofubazwa	964,917	858,272	
	Asilimia ya waliofubazwa makali (VL<1000)	98	98	

214. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa **huduma kwa WAVIU** zinasogezwa karibu zaidi na jamii, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya nchini kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya vituo vinavyotoa huduma ya Tiba na Matunzo (CTC) vimefikia 7,994 sawa na asilimia 78 ya vituo 10,263 vinavyotoa huduma za afya nchini. Lengo ni kufikia zaidi ya asilimia 95 ya vituo vyote nchini vinavyotoa huduma za afya ifikapo mwaka 2030.

215. Mheshimiwa Spika, Serikali imevijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi ili viweze kufanya uchunguzi wa awali na kutoa rufaa kwa wanaobainika kuwa na Virusi vya **Ugonjwa wa Homa ya Ini**. Wagonjwa wanaopewa rufaa hupata huduma za tiba na matunzo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa. Aidha, Utafiti uliofanyika mwaka 2022/23 (THIS 2022/23) ulionesha kuwa ushamiri wa ugonjwa wa Virusi vya Homa ya Ini aina ya B nchini ni asilimia 3.5 na asilimia 0.2 aina ya C, ushamiri umepungua ikilinganishwa na utafiti kama huu uliofanyika mwaka 2016/17 ambapo ushamiri wa ugonjwa Virusi vya homa ya ini aina ya B ulikuwa asilimia 4.1 na asilimia 1.0 aina ya C. Katika tafiti hii matokeo yalionesha kuwa idadi kubwa ya walioathirika ni watumiaji na wajidunga wa dawa za kulevya. Wizara inatekeleza Mpango Mkakati jumuishi kwa ajili ya afua ya Homa ya Ini kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya nchini kote ili kuhakikisha huduma inawafikia wananchi kwa karibu zaidi.

216. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuhakikisha **upatikanaji wa dawa kinga kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa au kuambukiza VVU,** hadi kufikia Machi 2025 jumla ya wateja 47,307 walipatiwa huduma ya dawa kinga. Makundi lengwa ni wanaume na vijana wa kike na wakiume walio katika hatari zaidi ya maambukizi. Makundi hayo yanajumuisha wachimbaji madini, madereva wa masafa marefu, wavuvi, wajidunga, wanawake wanaoendesha maisha kwa kujihusisha na ngono na wateja wao, na vijana wa kike wasio na ajira wala kipato rasmi.

217. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mahususi hususan kwenye mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya ambayo ina kiwango cha juu cha maambukuzi ya VVU. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha afua ya tohara kwa wanaume, utoaji wa elimu ya kinga na matibabu na kufikisha huduma wezeshi za kiuchumi kwa vijana balehe kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

218. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha **mama wajawazito wanapimwa maambukizi ya VVU** wanapohudhuria kliniki na hata baada ya kujifungua. Lengo

likiwa ni kuhakikisha mtoto aliyeko tumboni anakingwa dhidi ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama. Huduma hizi zinaenda sambamba na kupima na kutibu maambukizi ya Kaswende na kukinga virusi vya Homa ya Ini aina 'B' kwa mama na mtoto. Aidha takwimu zinaonesha kwamba katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya **wajawazito 2,127,548 walihudhuria kliniki,** wajawazito **2,089,252** sawa na asilimia 98.2 walipimwa maambukizi ya VVU ikilinganishwa na asilimia 97.4 ya wajawazito waliopimwa VVU katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya waliopimwa asilimia 2.6 walikuwa na maambukizi ya VVU. Aidha, asilimia 94.6 ya wajawazito waliobainika kuwa na maambukizi walianzishiwa matibabu ili kumkinga mtoto aliye tumboni asipate maambukizi.

219. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 watoto waliozaliwa na kinamama wenye maambukizi ya VVU na kuwekwa katika uangalizi maalum kwa muda wa miezi 24 walikuwa 21,081 na kati yao watoto 235 sawa na asilimia 1.1 walibainika kuwa wameambukizwa VVU na hivyo kuwekwa katika mpango wa matibabu. Wizara inaendelea kuhakikisha kuwa watoto wote wanaozaliwa na mama wenye maambukizi wanazaliwa wakiwa hawana maambukizi na wanaishi hadi kufikia miezi 24 bila ya kuwa na maambukizi ya VVU kwa kutoa dawa za kuzuia maambukizi ya VVU, kutoa elimu ya unyonyeshaji sahihi na kufanya uchunguzi mapema.

220. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya kwa kuhakikisha vituo vinatoa **huduma bora za kliniki kwa kina mama wajawazito,** huduma hizo zikiwa ni pamoja kutoa elimu ya afya kuhusu viashiria vya hatari na lishe na kuwafanyia vipimo mbalimbali vya msingi ikiwemo vipimo vya uchunguzi wa VVU na magonjwa ya ngono pamoja na kaswende. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wajawazito **1,742,625** walifanyiwa kipimo cha kaswende ambapo wajawazito 7,787 sawa na asilimia 0.45 waligundulika kuwa na maambukizi ya kaswende na kupatiwa matibabu. Hii ni pungufu ya asilimia 0.19 ikilinganishwa na asilimia 0.64 ya wajawazito waliokutwa na maambukizi ya kaswende katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Jedwali Na. 6**).

Jedwali Na. 6. Ulinganifu wa Viashiria vya Huduma za Kuzuia Maambukizi ya VVU na Kaswende kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025.

Na.	Viashiria	Julai 2023-Machi 2024	Julai 2024-Machi 2025
1	Idadi ya wajawazito waliohudhuria Kliniki	1,973,955	**2,127,548**
2	Idadi wajawazito waliopima VVU kipimo cha kwanza	1,891,963	1,986,614
3	Asilimia ya waliopata uchauri na kupima VVU ANC	97.8	97.3
4	Idadi ya wajawazito waliokutwa na maambukizi ya VVU	53,454	55,363
5	Asilimia ya waliokutwa na maambukizi	2.8	2.7
6	Asilimia ya wajawazito walioanza Dawa kuzuia maambukizi kwa mtoto	95.8	89.7
7	Jumla ya watoto waliozaliwa	1,636,931	**1,708,556**
8	Watoto waliowekwa katika ufuatiliaji wa VVU kwa miezi 24	45,514	42,218
9	Watoto waliokutwa na VVU baada ya miezi 24	1,779	1,663
10	Asilimia waliokutwa na maambukizi ya VVU baada ya miezi 24	3.9	3.9
11	Wajawazito waliopima kaswende	1,772,993	1,742,625
12	Wajawazito waliogundulika na kaswende	11,419	7,787
13	Asilimia ya wajawazito waliokutwa na kaswende	0.64	0.45

Chanzo: DHIS2 2025

Mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma

221. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Kifua Kikuu kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma za uchunguzi, upimaji, na matibabu dhidi ya Kifua Kikuu. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani ya Mwaka 2024, imeonesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu (3) kati ya nchi zenye wagonjwa wengi wa Kifua Kikuu kukaribia lengo la kupunguza visa vipya vya Kifua Kikuu kwa asilimia 50 na kuwa kati ya nchi 13 zinazokaribia kufikia lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 75 ifikapo mwaka 2025. Nchi yetu imefanikiwa kupunguza visa vipya vya Kifua Kikuu kwa asilimia 40 na kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 68.

222. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imenunua na kusambaza mashine 75 za ***GeneXpert*** na ***Truenat*** 110 kwa ajili ya kuimarisha huduma za upimaji kwa kutumia teknolojia ya vinasaba. Mashine hizo zimesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya 165. Hii inafanya nchi kuwa na mashine za *GeneXpert* 417 na Truenat 157, na hivyo kufanya jumla ya mashine kufikia 573. Hii imeongeza uibuaji wa wagonjwa wenye vimelea vya Kifua Kikuu. Katika kipindi hicho, Wizara imefanikiwa kuibua jumla ya wagonjwa 56,002 wa Kifua Kikuu sawa na asilimia 76 ya lengo la kuibua visa 73,408. Aidha, wagonjwa 236 wa Kifua Kikuu sugu waliibuliwa sawa na asilimia 65 ya lengo la kuibua wagonjwa 362.

223. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa **huduma mkoba** na **kliniki tembezi** zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi kuambukizwa ugonjwa wa Kifua Kikuu. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla wananchi 14,827 walifikiwa, 6,810 walichunguzwa Kifua Kikuu, 3,079 walihisiwa kuwa na Kifua Kikuu, 1,500 walipimwa kwa kutumia mashine aina ya Gene-Xpert na wagonjwa 579 wa Kifua Kikuu wameibuliwa kupitia huduma za Mkoba za kliniki tembezi.

224. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya visa 1,067 vya Ukoma viliibuliwa nchini, ambapo mikoa

iliyoibua visa vingi zaidi ni pamoja na Morogoro, Lindi, Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na Unguja. Kiwango cha maambukizi kimeshuka kutoka wagonjwa 20 kwa kila watu 10,000 kwa mwaka 1979 hadi mgonjwa 1 kwa kila watu 10,000 kwa mwaka 2024. Hii ilichangiwa na uwepo wa mikakati ya kutoa elimu juu ya ugonjwa wa Ukoma na kushirikisha jamii katika uibuaji wa ugonjwa huu. Aidha, Visa vya ugonjwa wa Ukoma nchini vimepungua kutoka wagonjwa 35,400 mnamo mwaka 1979 hadi 1,346 kwa mwaka 2024 sawa na punguzo la asilimia 96.

225. Mheshimiwa Spika, Wizara imejipanga kuendelea kutoa elimu na hamasa kwa jamii kuhusu ugonjwa wa ukoma na pia inaendelea kujenga uwezo kwa watumishi wa afya ili waweze kuwa na uelewa wa ugonjwa huo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukabiliana na changamoto hii. Serikali inaendelea kutoa hamasa kwa mikoa, halmashauri na vituo viweze kuweka katika mipango yao afua za Ukoma zinazolenga kutokomeza ugonjwa huo.

Mapambano dhidi ya Malaria

226. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha **Mapambano dhidi ya Malaria**, Wizara imeendelea kuhakikisha Vipimo pamoja na dawa za kutibu malaria zinapatikana wakati wote katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Wizara ilinunua na kusambaza dozi 1,364,220 za dawa mseto ya malaria, vichupa 3,289,685 vya dawa ya sindano ya Artesunate na vitepe 9,644,925 vya vipimo vya MRDT. Mikakati hii imeimarisha hali ya upatikanaji wa dawa na vitendanishi vya malaria katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini na kufikia wastani wa asilimia 90. Upatikanaji wa vipimo na dawa za tiba ya malaria katika vituo vya kutolea huduma za Afya kwa wakati wote kunachangia kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria katika jamii, ambayo imesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wa malaria na kupungua kwa vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria. Mathalan, vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria vimepungua kwa asilimia 39 kutoka vifo 2,460 mwaka 2020 mpaka vifo 1503, mwaka 2024 vilivyoripotiwa kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mafanikio hayo yametokana na kutekeleza afua za kinga za matumizi ya vyandarua vyenye dawa, udhibiti wa mazalia ya mbu kwa kufanya usafi wa mazingira, matumizi ya tiba kinga na matumizi ya viuadudu vya kibaiolojia, kuwepo kwa huduma za upimaji na matibabu ya malaria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na uelimishaji wa jamii dhidi ya matumizi sahihi ya afua za kinga, vipimo na matibabu kwa wakati.

227. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza afua mbalimbali ambazo zimekuwa na lengo la kuhakikisha malaria inatokomea kabisa kufikia mwaka 2030. Mojawapo ya afua hizo ni pamoja na kugawa vyandarua vyenye dawa kupitia makundi Maalum kama wanafunzi wa shule za msingi, akinamama wajawazito na Watoto chini ya mwaka mmoja. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya vyandarua 6,220,340 vilisambazwa ambapo vyandarua 3,635,890 vilisambazwa kupitia njia ya kampeni (Targeted Mass Campaign) kwenye Halmashauri 12 za Mikoa ya Mwanza na Geita, vyandarua 2,469,375 vimesambazwa kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya kutolea huduma za afya na vyandarua 115,075 vilisambazwa kupitia wanafunzi wa shule za msingi kwenye Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Tabora ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na Halmashauri ya Mji wa Nzega. Halmashauri hizi zimechaguliwa miongoni mwa halmashauri 8 za Mkoa wa Tabora kwa kuonekana kuwa na kiwango kikubwa cha visa vya maambukizi ya malaria kwa mama wajawazito kwa taarifa za mwaka 2023.

228. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kuharakisha kutokomeza malaria ifikapo 2030, Wizara imeendelea kutekeleza afua ya kuangamiza viluilui wa mbu kwa kutumia viuadudu vinavyozalishwa na kiwanda cha ndani cha kuzalisha viuadudu vya kibaiolojia (Biolarvicides) cha *Tanzania Biotech Products Limited (TBPL)* kilichopo Kibaha Mkoani Pwani ambapo Wizara imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 10 kwa ajili ya kununua Lita 819,333 za viuadudu kutoka kiwandani humo. Aidha, hadi kufikia Machi 2025, tayari Serikali imetoa jumla ya Shilingi Bilioni 5.5 kwa ajili ya kununua Lita 458,333, na tayari lita 208,333 zimesambazwa kwenye halmashauri 57 zenye kiwango

cha juu cha maambukizi ya malaria kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili ya usambazaji itafuatia kwa kusambaza kwenye Halmashauri 127 zilizobaki na kuweza kufikia na kuzewezesha halmashauri zote 184 kutekeleza afua hiyo.

Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Afya Mipakani

229. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia, kuratibu na kutekeleza afua za ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, milipuko na huduma za afya mipakani. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara imeendelea **kukabiliana na milipuko ya magonjwa** ikiwemo Kipindupindu, Marburg na Mpox na magonjwa mengine ya milipuko.

230. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia, kuratibu na kutekeleza afua za ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, milipuko na huduma za afya mipakani. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, **Wizara imeendelea kukabiliana na milipuko ya magonjwa ikiwemo Kipindupindu, Marburg, Mpox** na magonjwa mengine. Aidha, Wizara imefuatilia mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa Kipindupindu ambapo jumla ya visa 6,940 vilitolewa taarifa kutoka Mikoa 24 nchini isipokuwa Kilimanjaro na Njombe. Hadi kufikia Machi 2025, ugonjwa huo ulikuwa umedhibitiwa katika Mikoa yote 26.

231. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya hewa yakiwemo UVIKO 19 na mafua makali yanayosababishwa na virusi vya Influenza kupitia vituo 27 vya ufuatiliaji (Sentinel Sites) vilivyopo nchini ambapo hadi kufikia Machi 2025 jumla ya sampuli 2,532 zilipimwa kati ya hizo 190 sawa na asilimia 7.5 zilithibitika kuwa na UVIKO 19. Aidha, sampuli 209 sawa na asilimia 8.3 zilithibitika kuwa na Virusi vya *Influenza*. Vilevile, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa Surua nchini katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Ruvuma, Kagera, Kigoma na Dodoma, ambapo jumla ya visa 63 vilitolewa taarifa na wagonjwa walipata matibabu na kupona.

232. Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 20 Januari 2025, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan alitangaza kuwepo kwa **mlipuko wa ugonjwa wa Marburg** uliotokea katika Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, baada ya wagonjwa wawili (2) kuthibitika kuwa na maambukizi ya vimelea vya ugonjwa huo. Kufuatia uwepo wa mlipuko huo, Wizara kupitia Kamati ya Kitaalamu ya Udhibiti wa Milipuko ya ngazi ya Taifa ikishirikiana na Uongozi wa Mkoa na Timu ya wataalam zilitekeleza afua za kukabiliana na udhibiti wa mlipuko huo na **hadi kufikia tarehe 13, Machi 2025 tulifanikiwa kuudhibiti na kutangaza kuisha kwa mlipuko ndani ya siku 54.** Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia tetesi za magonjwa ya milipuko nchini na kuhakikisha milipuko inadhibitiwa kikamilifu.

233. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **uboreshaji wa miundombinu** hususan katika eneo la dharura, uimarishaji umeendelea katika vituo vya Operesheni za Dharura na Majanga ngazi za Mikoa (Regional Public Health Emergency Operation Centers) na kufikisha Mikoa 20 kati ya 26 nchini. Vituo hivi vimeimarisha uwezo wa Mikoa kuratibu afua za udhibiti wa magonjwa na kuchakata taarifa za tetesi za matukio ya dharura. Taarifa hizi ni sehemu muhimu katika kupanga mikakati na kufanya maamuzi ya kudhibiti magonjwa hayo katika Mikoa husika.

Huduma za Afya Mipakani

234. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kudhibiti kuingia nchini kwa magonjwa hatari yanayoambukiza ambapo udhibiti huu unafanyika katika mipaka yote nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, **Wizara ilifanya uchunguzi wa awali (Screening) kwa wasafiri 1,175,710** walioingia nchini kutoka nchi zenye mlipuko au uwezekano wa kuwa na magonjwa ya mlipuko. Wasafiri wote hawakuthibitika kuwa na vimelea vya magonjwa ya mlipuko. Vilevile, kati ya wasafiri 389,653 waliotoka katika nchi zinazosadikiwa kuwa na ugonjwa wa homa ya manjano, **wasafiri 8,884** hawakuwa na uthibitisho wa kuchanjwa homa ya manjano, hivyo walipatiwa chanjo hiyo hapa nchini.

235. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti wa magonjwa mipakani, Wizara imejengea uwezo wataalam na kuwapa magari ya kubebea wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, viwanja vya ndege vya Songwe na Mwanza pamoja na mipaka ya Holili, Namanga, Tunduma na Mutukula.

236. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeajiri watumishi 201 katika ofisi za afya mipakani na hivyo kuongeza idadi ya watumishi kutoka watumishi 321 hadi 522 kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa katika maeneo ya mipakani. Aidha, kufuatia ongezeko hilo, Wizara imeanzisha ofisi mpya za Afya mipakani na katika maeneo ya kimkakati ambayo ni Bandari za Pangani, Kagunga na Bagamoyo, Mipaka ya Kilambo, Mkunya, Mkenda na Kyaka, Kiwanja cha Ndege Songea na Vituo vya Treni ya Mwendokasi (SGR) vya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam.

237. Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, Wizara imefanya utambuzi wa maeneo muhimu yanayowakutanisha wakazi wa mipakani pamoja na njia kuu wanazotumia na mienendo ya watu wanaoingia na kutoka nchini kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Kenya (Joint Population Connectivity Across Borders - PoPCAB). Aidha, Wizara imefanya tathmini ya athari za kiafya (Strategic Risk Assessment) na uandaaji wa mipango ya kukabiliana na dharura (Public Health Contingency Plan) katika mipaka kupitia zoezi la pamoja na nchi jirani za Burundi na Kenya. Matokeo ya tathmini zote hizo yameonesha kwamba mipaka yetu ni salama kwa viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa.

238. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeratibu mafunzo ya ana kwa ana ya matibabu ya magonjwa ya milipuko ya Kipindupindu, Mpox na Marburg kwa watoa huduma 2,581 katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Kigoma, Kagera, Dar es Salaam, Morogoro, Katavi, Mbeya, Songwe, Singida, Simiyu, Dodoma na Tabora. Vilevile, jumla ya watoa huduma 62

wamepata mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya operesheni za dharura na maafa katika Mikoa ya Tabora, Manyara, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Kigoma.

'Naomba kuwahakikishia wananchi kuwa, mipaka yetu ipo salama na Serikali imejipanga kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na ya kuambukiza kutoka nchi za jirani'.

Utoaji wa Huduma za Kinga Huduma za Chanjo

239. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha utoaji wa huduma za kinga ikiwemo kuhakikisha huduma za chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana muda wote kulingana na mahitaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, chini ya miaka mitano, wajawazito, wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14, wasafiri na makundi mengine yaliyo katika hatari ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo wanapata huduma hizo kwa wakati. Chanjo hizo zimekuwa zikitolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na ngazi ya jamii kupitia huduma mkoba na huduma tembezi.

240. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mnyororo baridi wa huduma za chanjo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imejenga maghala tisa (9) ya kuhifadhia chanjo pamoja na kununua magari 96 ambapo kati ya hayo, *Pick up Double Cabin ni* 68, malori 28 na pikipiki 300 kwa ajili ya kutoa huduma za chanjo nchini. Makabidhiano ya magari hayo na pikipiki yalifanywa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 1 Desemba 2024. Aidha, uimarishaji huo umesaidia kupunguza gharama za uendeshaji kutoka Shilingi Bilioni 18 hadi Shilingi Bilioni 1.8 mwaka 2024 pamoja na kuimarisha upatikanaji wa chanjo kwa wakati.

241. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha **chanjo za watoto** za kuwakinga na magonjwa 13 yanayozuilika kwa chanjo zinazopatikana bila malipo kulingana na mahitaji. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imeratibu ununuzi wa

chanjo za Rota; dozi 6,312,125 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuhara kwa watoto; PCV - 13 dozi 2,366,400 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Nimonia; chanjo za Surua Rubella; dozi 4,200,000 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Surua na Rubella; bOPV dozi 8,034,300 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio), Pentavalent dozi 3,034,300 kwa ajili ya kukinga Donda Koo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini, na Mafua ya Influenza, *Tetanus Diphtheria* dozi 1,400,000 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa Pepo Punda, BCG dozi 3,200,000 za kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na IPV dozi 2,304,200 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio).

242. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kulikuwa na jumla ya dozi za chanjo 13,416,045 nchi nzima katika maghala ya kuhifadhia chanjo. Kwa mgawanyo wa ROTA dozi 982,125, (MR) dozi 3,139,500, (PCV-13) dozi 4,583,200, (IPV) dozi 440,250, (PENTA) dozi 2,689,060, (Td) dozi 789,320, (bOPV) dozi 291,000, (BCG) dozi 96,000 na HPV dozi 396,590 baada ya kufanya usambazaji kwenye mikoa nchi nzima, hali hii inaonesha kuwa upatikanaji wa chanjo nchini ni wa kutosheleza.

243. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa **huduma za chanjo kupitia katika vituo vya kutolea huduma za afya** na katika huduma Mkoba na tembezi ili kuhakikisha watoto wote wanaohitaji huduma ya chanjo, wanafikiwa na huduma hiyo. Wizara iliweka lengo la kuchanja jumla ya watoto 3,114,061 ambapo hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya watoto 2,995,318 sawa na asilimia 96 walichanjwa chanjo ya Penta-3 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha utoaji wa chanjo nchini kwa watoto wa chini ya mwaka mmoja.

244. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Chanjo za kukinga ugonjwa wa Polio,** jumla ya watoto 2,896,495 sawa na asilimia 93 walipatiwa chanjo ya matone (OPV3) na watoto 3,025,922 sawa na asilimia 97 walipatiwa chanjo ya sindano (IPV). Aidha, watoto 3,094,604 sawa na asilimia 99 walipatiwa chanjo ya Surua Rubella dozi ya kwanza na Watoto 2,903,356 sawa na asilimia 93 walipatiwa chanjo ya Surua Rubella dozi ya pili. Vilevile, watoto 3,761,937 sawa na asilimia 114

walichanjwa chanjo ya BCG kwa ajili ya kukinga kifua kikuu. Kwa wastani hali ya utoaji wa chanjo nchini ni nzuri na inaendelea kuimarika kulingana na malengo yaliyowekwa.

245. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwalinda **wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14 dhidi ya Saratani ya mlango** wa kizazi kwa kununua na kusambaza chanjo ya *Human Pappiloma Virus* (HPV) dozi 4,763,180. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya wasichana wapatao 4,989,818 walipatiwa chanjo ya HPV sawa na asilimia 112 ya walengwa, ili kuwakinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Aidha, katika maghala ya chanjo kulikuwa na chanjo za HPV dose 659,470.

Huduma za Lishe

246. Mheshimiwa Spika, Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo huchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa pili wa Kitaifa wa Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan (2021/22 – 2025/26). Kupitia Mpango huo Wizara imekuwa ikitekeleza afua za lishe zilizothibishwa kuwa na matokeo makubwa ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo wa lishe duni na ule wa lishe ya kuzidi. Baadhi ya afua hizo ni pamoja na utoaji wa matone ya Vitamini A, kinga na matibabu ya utapiamlo mkali, uongezwaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwenye vyakula na utoaji elimu kwa jamii kuhusiana na masuala ya lishe kwa ujumla wake.

247. Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kuwa maziwa ya mama ni hitaji muhimu la mtoto pindi anapozaliwa hadi anapotimiza umri wa miaka miwili (2) au zaidi huku akiendelea kupewa vyakula mchanganyiko vya nyongeza kutoka katika makundi yote ya vyakula ili kupata virutubishi vyote muhimu kwa afya na ukuaji wake. Katika kutekeleza hilo, Wizara, imeendelea kusimamia miongozo inayosisitiza **unyonyeshaji sahihi wa Watoto**, ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **jumla ya Watoto 1,145,739 walinyonyeshwa maziwa ya mama pekee** ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, ambayo ni

sawa na asilimia 93 ya lengo, ikilinganishwa na asilimia 92 ya kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watoto 1,536,286 wamenyonyeshwa maziwa ya mama pekee sawa na asilimia 93 ya lengo. Ili kuhakikisha hali ya unyonyeshaji maziwa ya mama pekee inaongezeka, Wizara iliratibu maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Kitaifa Agosti 2024, ambayo yaliambatana na mkutano wa Maafisa Utumishi na Maafisa Sheria kwa lengo la kuhamasisha utekelezaji wa haki za uzazi mahala pa kazi ikiwemo kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kunyonyesha watoto wakiwa katika shughuli za kiuchumi au maeneo ya ajira.

248. Mheshimiwa Spika, huduma ya **utoaji wa matone ya Vitamini A** kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) hufanyika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa utaratibu wa kawaida ambapo mtoto akitimiza umri wa miezi sita (6) hupewa matone ya Vitamini A na huendelea kupatiwa matone hayo kila baada ya miezi sita (6) hadi atakapotimiza umri wa miaka mitano (5). Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto walio chini ya miaka mitano. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, malengo ya kampeni yalikuwa ni kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto 9,468,207 wenye umri wa kati ya miezi 6 mpaka miezi 59 nchi nzima. Jumla ya watoto 9,456,378 walipatiwa matone ya vitamin A ambayo ni sawa na asilimia 99.8 ya lengo.

249. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau mbalimbali, imeendelea kuhamasisha na kuelimisha makundi mbalimbali katika jamii kuhusu masuala ya lishe na mtindo bora wa maisha kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo maadhimisho ya **Siku ya Lishe Kitaifa** yaliyofanyika mwezi Oktoba 2024 katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara yakiwa na kaulimbiu isemayo **"Mchongo ni Afya Yako, Zingatia Unachokula"**. Lengo kuu la maadhimisho hayo lilikuwa ni kutoa elimu ya lishe kwa jamii. Kupitia maadhimisho hayo, jumla ya Watalaam wa afya na Lishe nchini wapatao 200 walijengewa uwezo kuhusu masuala ya ulaji unaofaa na mitindo bora ya maisha. Wakati wa maadhimisho hayo, jumla ya vipindi 208 vya masuala ya lishe viliandaliwa na kurushwa kwenye vyombo

mbalimbali vya habari vikiwemo redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii katika ngazi zote nchini.

250. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi **kutumia vyakula ambavyo vimeongezwa virutubishi muhimu** kwa maendeleo ya ukuaji wa afya ya watoto ili kuboresha afya zao na kuwakinga na maradhi mbalimbali yanayoweza kuzuilika kwa kula lishe bora yenye virutubisho vya madini na vitamini, iodini kwenye chumvi na vitamin A kwenye mafuta ya kula. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya mashine 230 za kunyunyizia virutubishi (Dosifiers) kwenye vyakula zimefungwa katika Mikoa 26 nchini na hivyo kufikia jumla ya mashine 1,402 ukilinganisha na machine 1,172 zilizokuwepo katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Aidha, kufuatia uwepo wa mazingira wezeshi ya uzalishaji wa virutubishi, jumla ya kilo 65,946 za virutubishi zimezalishwa na kusambazwa nchini.

Afya Mazingira na Usafi

251. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau pamoja na Mikoa na Halmashauri imeendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa afua mbalimbali zilizopo katika mradi wa Afya Mazingira na Usafi: *Sustainable Rural Water Supply and Sanitation* (SRWSS) 2020-2026, unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya 137. Lengo la Mradi ni kuvifikia vituo 2,636 vya kutolea huduma za afya ifikapo 2025, ambapo hadi kufikia Machi 2025 jumla ya vituo 2,740 vya kutolea huduma za afya vimefikiwa.

252. Mheshimiwa Spika, Afua zilizotekelezwa ni pamoja na kuwezesha ujenzi na matumizi ya vyoo bora, uwekaji wa vifaa vya kunawa mikono, udhibiti wa taka, usafishaji wa maeneo ya makazi, maeneo ya biashara na maeneo ya umma ili kuikinga jamii dhidi ya magonjwa mbalimbali kama vile Kipindupindu, Kuhara Damu, Dengue, Malaria na magonjwa mengine ya kuambukiza. Katika kuboresha suala la usimamizi wa mradi huo ngazi ya mikoa, Wizara imenunua na kusambaza jumla ya magari 21 na pikipiki 410.

253. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Kampeni ya ***FANYA KWELI USIBAKI NYUMA-MTU NI AFYA inayohamasisha*** ujenzi na matumizi ya Vyoo bora, kuzingatia kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni katika nyakati maalum, hedhi Salama, usafishaji wa maeneo ya makazi na kazi (Mita tano Usafi Wangu, Usafi Wangu Mita Tano, udhibiti wa utupaji ovyo wa taka, lishe Bora, mazoezi ya mwili, nishati Safi na maji salama ya kunywa). Utekelezaji wa Kampeni hii umesaidia kuongeza idadi ya kaya zenye vyoo bora kutoka kaya 8,277,206 mwezi Machi, 2024 na kufikia kaya 8,504,503 mwezi Machi, 2025 sawa na asilimia 78.4 ya lengo. Aidha, kaya zenye vifaa vya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni zimeongezeka kutoka asilimia 41.4 hadi asilimia 45.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDs)

254. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika kutekeleza afua za kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambayo ni Matende, Mabusha, Vikope, Trakoma, Usubi, Kichocho na Minyoo ya Tumbo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imetoa kingatiba dhidi ya ugonjwa wa matende na mabusha kwa jumla ya watu 530,034 sawa na asilimia 96.5 ya walengwa katika Halmashauri tano (5) za Mtama, Mikindani, Kinondoni, Pangani na Lindi. Aidha, jumla ya wananchi 1,603,419 sawa na asilimia 81.5 ya walengwa walipata kingatiba dhidi ya ugonjwa wa Trakoma katika Halmashauri saba (7) za Longido, Monduli, Ngorongoro, Kiteto, Mpwapwa, Simanjiro na Kalambo zenye maambukizi ya juu ya ugonjwa huo. Vilevile, Wizara ilitoa kingatiba kwa wananchi 5,456,029 dhidi ya ugonjwa wa Usubi sawa na asilimia 85 ya walengwa katika Halmashauri 24 za mikoa ya Ruvuma, Iringa, Njombe na Morogoro. Wizara imetoa **kingatiba ya kudhibiti ugonjwa wa kichocho kwa watoto** 7,134,762 sawa na asilimia 76 na kingatiba dhidi ya ugonjwa wa minyoo ya tumbo kwa Watoto 9,167,116 sawa na asilimia 83 ya walengwa.

255. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za tiba kwa kufanya upasuaji wa mabusha na vikope. Huduma za upasuaji wa mabusha zilitolewa kwa njia ya kambi katika Hospitali za Wilaya ya

Bagamoyo, Masasi Mji, Kisarawe, Handeni DC, Korogwe DC na Korogwe TC ambapo jumla ya wagonjwa 1,084 walipata huduma hiyo ikilinganishwa na wagonjwa 617 kipindi kama hiki mwaka 2024.

256. Mheshimiwa Spika, Wizara imewajengea uwezo watumishi katika vituo 40 vya kutolea huduma za afya juu ya kutoa huduma za matibabu ya matende. Aidha, Wizara imewajengea uwezo Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii 200 katika kuibua wagonjwa wa Matende na Mabusha katika Halmashauri za Bagamoyo, Masasi na Masasi Mji. Pia, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara ilitoa huduma za upasuaji mdogo wa usawazishaji wa Vikope kwa wagonjwa 1,772 katika Halmashauri za Wilaya 13. Lengo la upasuaji huo ni kuzuia wananchi walioathirika na ugonjwa wa vikope kupata ulemavu wa kutoona.

Elimu ya Afya kwa Umma na Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

257. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeendelea kutoa elimu kwa jamii, ili kuhakikisha jamii inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa yanayoambukiza na yale yasiyoambukiza. Hii inaenda pamoja na utoaji wa elimu kuhusu masuala ya lishe, mazoezi, magonjwa ya mlipuko, chanjo, afya ya uzazi, mama na mtoto.

258. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara inatekeleza Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ambapo kupitia mpango huo jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 12,832 katika Mikoa 12 ya Pwani, Mbeya, Kagera, Njombe, Songwe, Lindi, Geita, Kigoma, Tabora, Dodoma, Tanga na Ruvuma wamechaguliwa kuingia katika mafunzo maalum yanayohusiana na utoaji huduma katika ngazi ya jamii, pamoja na elimu. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 3,706 wamehitimu mafunzo hayo na wengine 4,309 wanaoendelea na mafunzo katika vyuo 45 nchini.

259. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imeanzisha programu ya elimu na hamasa ya matumizi ya huduma ya m-mama. Programu hiyo inakusudia kuiwezesha jamii kuwasaidia wajawazito, waliojifungua ndani ya siku 42 au watoto wachanga ndani ya siku 28 wenye changamoto ya dharura za kiafya kupata huduma ya usafiri na matibabu kwa haraka. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wanahabari 200 wamejengewa uwezo, vipindi 30 vya redio na runinga vimeandaliwa na kurushwa, vipeperushi mbalimbali vimeandaliwa na kusambazwa pamoja na uhamasishaji kupitia mitandao ya kijamii.

260. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa na kusambaza vielelezo vya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu elimu ya afya kwa Umma kulingana na kalenda ya matukio ya afya ya kitaifa na kimataifa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya picha mjongeo 920 na vipeperushi vya mtandaoni 1,440 vimesambazwa kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya matangazo ya redio 12 yamerushwa mara 22,680 kupitia vituo vya redio vinane (8), matangazo mafupi ya redio 10, vipindi vya redio 44, vipindi vya runinga 26, picha mjongeo 48 ambazo zimesambazwa kupitia mitandao ya kijamii na vipeperushi vya mtandaoni aina 26 vimeandaliwa na kusambazwa.

261. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa na kusambaza vielelezo vya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu tishio la ugonjwa wa *Mpox* na *Marburg*. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya vielelezo vilivyoandaliwa na kusambazwa ni mabango nakala 84,000, matangazo nane (8) ya redio yamerushwa mara 5,760, picha mjongeo 16 zimesambazwa kupitia mitandao ya kijamii sambamba na kuandaa kanzidata ya kidijitali ya kuhifadhi vielelezo vya uelimishaji na uhamasishaji jamii kuhusu masuala ya afya.

262. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kujikinga na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo kuwajengea uwezo viongozi 70 wa dini na waandishi wa habari 150 kuhusu utoaji wa elimu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko nchini. Wizara pia inaendesha kituo cha kupokea simu na

kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya afya (Afya Call Center) ambapo wananchi hupatiwa majibu ya maswali, ufafanuzi na hoja mbalimbali zinazoibuliwa katika jamii. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya wananchi 527,284 walipiga simu na katika simu hizo, simu 416,577 sawa na asilimia 79 zilipokelewa na kupatiwa huduma. Miongoni mwa masuala yaliyoulizwa kwa wingi ni magonjwa ya mlipuko asilimia 41, magonjwa ya kuambukiza asilimia 12, bima ya afya asilimia 21, magonjwa yasiyoambukiza asilimia 9, afya ya uzazi asilimia 7, lishe asilimia 4, afya ya akili asilimia 2 pamoja na matumizi sahihi ya dawa asilimia 4.

263. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kwa kipindi tajwa imefanya uhamasishaji na uelimishaji kupitia njia mbalimbali ikiwemo kampeni na kutembelea Shule za Msingi na Sekondari katika mikoa 19. Jumla ya wanafunzi 198,000 wameelimishwa kuhusu lishe, magonjwa ya milipuko, afya ya uzazi, chanjo dhidi ya HPV na kuhamasisha tabia zinazozingatia kanuni za afya na mitindo bora ya maisha.

Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

264. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara vyenye ubora, ufanisi na vilivyo salama kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kuzalisha, kununua, kutunza na kusambaza aina mbalimbali za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

265. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, Serikali imeendelea kutoa fedha za ruzuku kwenye vituo kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Katika Kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya Shilingi Bilioni 183.2 sawa na asilimia 91.6, zimetolewa kati ya Shilingi Bilioni 200 ya bajeti ya fedha za ruzuku. Aidha katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya katika Bohari ya Dawa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imefanikiwa kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 50 kama mtaji wa kuboresha upatikanaji wa dawa nchini. Vilevile, vituo vya

kutolea huduma za afya vimeweza kuchangia kiasi cha Shilingi Bilioni 126.6 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya. Katika kukabiliana na mabadiliko ya ufadhili na kisiasa kutoka kwa wadau, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi Bilioni 93.5 kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na vitendanishi vya maabara na hivyo kufikia jumla ya Shilingi Bilioni 370.1.

266. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini kununua maji tiba kutoka viwanda vya ndani ya nchi, kutoa msamaha wa kodi kwa vifungashio vya bidhaa za afya na Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma kuruhusu wazalishaji kulipwa malipo ya awali ya hadi asilimia 30 baada ya kusaini mkataba wa ununuzi.

267. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza viwanda vya dawa nchini, Jumla ya Shilingi Bilioni 10 zimetolewa na kuelekezwa kiwanda cha viuadudu kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani. Fedha hizo zimewezesha ununuzi wa lita 833,333.3 ambazo zinaendelea kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Aidha, upatikanaji wa fedha hizo zimeboresha uhusiano wetu na nchi ya Cuba na kupelekea kukamilika kwa makubaliano ya uhaulishaji wa teknolojia (Technology Transfer).

'Nitoe wito kwa Halmashauri zote zilizopokea na zinazoendelea kupokea viuadudu hivyo kutekeleza afua za unyunyuziaji katika maeneo yote yenye mazalia ya Mbu'.

268. Mheshimiwa Spika, kufuatia upatikanaji wa fedha hizo, hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi aina 382 nchini imeimarika kufikia wastani wa asilimia 86.2 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 79 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Hali ya upatikanaji wa dawa kwenye Zahanati asilimia 77, Vituo vya Afya asilimia 78, Hospitali za Wilaya asilimia 79, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 98 na Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa asilimia 99. Aidha, upatikanaji wa dawa muhimu za kipaumbele 382 katika Bohari ya Dawa (MSD) umefikia

asilimia 68 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 61 katika kipindi kama hicho Mwaka 2024.

269. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa bidhaa za afya katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini kwa lengo la kuhakikisha dawa na bidhaa nyingine za afya zinawafikia walengwa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya vituo 90 vya kutolea huduma za afya katika mikoa 14 vilifikiwa na zoezi hilo. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara iliweza kuwajengea uwezo watumishi 3,220 kutoka vituo 1,579 ili waweze kuimarisha usimamizi,upatikanaji na utolewaji huduma za dawa na bidhaa nyinginezo za afya kwa wananchi. Vituo ambavyo watumishi wake walijengewa uwezo, ni vile ambavyo vilikuwa vimebainika kuwa na upungufu kutokana na taarifa za usimamizi shirikishi, usimamizi wa ubora wa mnyororo wa ugavi pamoja na taarifa za mfumo wa kuagiza na kutoa taarifa za bidhaa za afya.

270. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa kampeni ya Kitaifa ya kujenga uelewa kwa jamii juu ya athari za **Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa.** Kampeni hii inaitwa **Holelaholela Itakukosti** ambayo imetekelezwa kwa kutumia majukwaa na njia mbalimbali za mawasiliano na kufikia jamii na rika mbalimbali. Aidha, kampeni hii imetajwa kuwa kampeni ya kipekee ya mfano wa kuigwa barani Afrika kwa mujibu wa taarifa ya *African CDC AMR Landmark report, August 2024*. *S*ambamba na hili, Tanzania imeshinda tuzo ya Afrika ya wanahabari kinara katika kampeni ya usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (UVIDA) kupitia kampeni ya "Holela-holela Itakukosti".

271. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imetoa mafunzo ya ufuatiliaji wa UVIDA katika hospitali za umma 23, Binafsi sita (6) na Mashirika ya dini nne (4). Mafunzo hayo yamewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa takwimu zinazohusu usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kuweza kutolewa taarifa kwenye mifumo ya kimataifa. Aidha, kufuatia jitihada zinazofanywa na Wizara, zimewezesha nchi kutambulika na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kushika nafasi ya kwanza barani Afrika kwa

kupata asilimia 80.3 kwenye eneo la ufuatiliaji wa matumizi ya dawa za *antimicrobials*. Vilevile, katika uimarishaji wa mfumo wa upimaji wa sampuli za UVIDA, Wizara imeongeza idadi ya upimaji kutoka sampuli 7,920 hadi 43,907 sawa na asilima 81.9 kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2023.

272. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti wa wizi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, Serikali imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika kusimamia uagizaji, utunzaji na matumizi kuanzia ngazi ya Bohari ya Dawa (MSD) hadi vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Sambamba na hilo Serikali imeweka alama ya utambuzi ya "GOT" (*Government of Tanzania)* kwenye bidhaa za afya ili kuzuia usambazaji usio halali. Aidha, Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji, usimamizi na kujenga uwezo kwa timu za ngazi ya Mkoa na Halmashauri ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na matumizi sahihi.

Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa

273. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, kwa kuwekeza kwenye maeneo makuu matatu ya maabara, radiolojia na matengenezo ya vifaa tiba.

274. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeongeza **maabara 883 na kufanya jumla ya maabara kufikia 11,665** ikilinganishwa na maabara 10,782 kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya maabara hizo, 7,383 ni za Serikali na 4,282 ni za binafsi. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 maabara 14 zilipata Ithibati na kufikia 89 kutoka maabara 75 kwa mwaka 2024. Kati ya maabara hizo, ngazi ya Taifa (03), Maalum (06), Kanda (05), Mikoa (31), Halmashauri (15), Binafsi (23) na sita (6) ni za Mpango wa Taifa wa Damu Salama ambapo vipimo vinavyofanyika katika maabara hizi vinaaminika na kukubalika duniani kote. Vilevile, kwa kuwa ubora wa huduma unaenda sambamba na usalama dhidi ya vimelea vya magonjwa, jumla ya makabati maalum 15 ya usalama wa vimelea yamenunuliwa na kusimikwa katika maabara ngazi ya Halmashauri ambazo hazikuwa na makabati hayo, ili kuimarisha

usalama wa watoa huduma dhidi ya vimelea vya magonjwa ya kuambukiza.

275. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha **huduma za radiolojia** nchini, Wizara imefanikisha kusimika Mashine za *Digital X-ray* katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Tabora - Kitete, Kigoma - Maweni na huduma tayari zimeanza kutolewa. Aidha, usimikaji wa *PET CT Scan* katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road* umekamilika na huduma za uchunguzi wa viashiria vya awali vya ugonjwa wa saratani tayari zimeanza kutolewa na hivyo kufikia jumla ya CT scan 45, MRI 13, *Digital X-ray* 491 na *Ultrasound* 970 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vilevile, Serikali imenunua na kusimika mashine 68 za *X-ray* za kidijitali zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.5 na kuzisimika katika hospitali na vituo vya Afya ngazi ya msingi katika mikoa ya Kigoma, Dodoma, Njombe, Katavi, Shinyanga, Tabora, Pwani, Tanga, Ruvuma, Lindi, Mwanza, Morogoro, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Arusha, Singida na Geita.

276. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Wizara imefanikiwa kusimika **mitambo 25 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni** nchini. Aidha, imefanyika tathmini ya mahitaji ya kupata chanzo mbadala cha kuzalisha na kusambaza hewa tiba ya oxygen katika mfumo wa kimiminika (Liquid Oxygen) kwa vituo 28. Awamu ya kwanza ya usimikaji wa matenki ya kuhifadhi hewa tiba ya Oksijeni katika mfumo wa kimiminika umeanza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Hospitali za Rufaa za Mikoa za Temeke na Mwananyamala.

277. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kwenye kuboresha huduma za uchunguzi nchini, Serikali imeajiri **wahandisi na mafundi Sanifu wa Vifaa tiba wapatao 81 na kufanya Idadi ya wataalam hao kufikia 490** katika ngazi zote za utoaji wa huduma za Afya. Jumla ya wataalam 40 wamejengewa uwezo katika maeneo mbalimbali ya usimikaji, matengenezo kinga na ukarabati wa vifaa tiba ndani ya nchi na nje ya nchi. Aidha, jumla ya watoa huduma za afya 16 kutoka vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini wamepatiwa mafunzo

ya matumizi na utunzaji wa mfumo wa kielektroniki wa kutolea taarifa za utendaji kazi wa vifaa tiba.

278. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha na kuimarisha karakana sita (6) zilizopo Hospitali za Bugando (Kanda ya Ziwa Victoria), Mbeya (Kanda ya Nyanda za Juu Kusini), Mtwara (Kanda ya Kusini), Hospitali ya Taifa Muhimbili (Kanda ya Mashariki), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (Kanda ya Kati) na Hospitali ya KCMC (Kanda ya Kaskazini) kwa ajili ya ukarabati na matengenezo kinga ya mashine na mitambo ilisimikwa nchini. Vituo hivyo pia vinatoa mafunzo kwa wataalam wa ufundi wa vifaa na vifaa tiba katika usimamizi na matengenezo kinga kwa vifaa tiba vyote. Aidha, Wizara imeendelea kuhuisha na kutoa miongozo mbalimbali ya kusimamia ubora wa mashine na mitambo hiyo. Vilevile, Wizara inaendelea kusimamia mfumo wa kieletroniki wa usimamizi wa vifaa tiba na miundombinu (MEIMIS) ili kuwezesha ufuatiliajia wa karibu na matengenezo kinga kwa wakati.

Mpango wa Taifa Wa Damu Salama

279. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa damu salama ya kutosha nchini ambapo**jumla ya chupa za damu 418,609 zilikusanywa nchini** ambazo ni sawa na asilimia 94.5 ya lengo la kukusanya chupa za damu 442,972 ikilinganishwa na malengo ya kukusanya chupa za damu 442,764 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Makusanyo hayo yametokana na jitihada za pamoja kati ya Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), Wadau mbalimbali, Madhehebu ya Dini, Timu za Ukusanyaji Damu za Halmashauri pamoja na Timu za Hospitali za Rufaa za Mikoa katika ukusanyaji wa damu salama nchini.

280. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Wizara imeanza taratibu za kuhakikisha vituo vya vya Damu Salama Kanda ya Kati Dodoma, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Benjamini Mkapa, Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Iringa, Njombe na Kigoma vinaanza mchakato wa kutambuliwa na kupata cheti cha ithibati katika utoaji huduma za damu salama kwa viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii

281. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025, Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii imefanikiwa **kupima jumla ya Sampuli 60,224 za magonjwa mbalimbali ya mlipuko pamoja na upimaji wa anuai za magonjwa hayo**. Sampuli hizo zinahusisha uchunguzi wa magonjwa yakiwemo Mpox, Marburg, mafua makali, Kipindupindu, Surua, *Rubella*, Kimeta, *Dengue*, kichaa cha mbwa (Rabies), matende, *Rotavirus, Human Papiloma*, wingi wa Virusi vya UKIMWI, utambuzi wa maambukizi ya VVU kwa watoto wachanga.

282. Mheshimiwa Spika, Wizara **imesimika mashine kwa ajili ya upimaji wa ugonjwa wa Saratani ya Shingo ya Kizazi "Alinity - M"** ambapo baada ya usimikaji zoezi rasmi la uchunguzi wa ugonjwa huo umeanza kufanyika kupitia Maabara ya Taifa. Aidha, Maabara ya Taifa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha huduma za Maabara nchini kwa kununua mashine za kisasa aina ya *Next Generation Sequencers* sambamba na mashine kubwa aina ya *Illumina Nextseq 1000* kwa ajili ya kuchakata sampuli nyingi na kwa kiwango cha juu kwa mara moja.

283. Mheshimiwa Spika, Wizara katika kuhakikisha inakabiliana na magonjwa ya mlipuko nchini, imeimarisha huduma za uchunguzi kwa kuwa na **mashine mbili (2)** za **iSeq 100** kwa ajili ya maabara jongezi (BSL-3 Mobile Laboratories) inayoweza kutumika mahali popote inapotokea mlipuko wa magonjwa. Maabara jongezi hiyo ndiyo iliyotumika kuthibitisha uwepo wa virusi vya ugonjwa wa *Marburg* katika milipuko ya mwaka 2023 na 2025 mkoani Kagera. Aidha, maabara hii imeendelea kutumika katika kubaini anuai za vinasaba vya vimelea vya magonjwa ya mlipuko ambayo ilisaidia wataalam wa afya kufanya jitihada za kutokomeza ugonjwa huo kwa muda mfupi.

284. Mheshimiwa Spika, Maabara ya Taifa imefanyiwa ukaguzi na kupata Ithibati ISO:15189:2022 kwa ajili ya usimamizi wa ubora wa vipimo wa Kitaifa na Kimataifa na ISO:17043:2010 kwa ajili ya kutengeneza na kusambaza sampuli za kuhakiki ubora wa huduma za

maabara nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi, 2025 maabara imefanikiwa kuandaa na kutuma sampuli za uhakiki ubora wa vipimo kwa vituo 600 nchi nzima kwa ajili ya kuhakiki ubora wa vipimo mbalimbali vinavyotolewa na Maabara nchini. Zoezi hilo linalenga kuendelea kupata na kudumisha ubora wa huduma za maabara katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Huduma za Uuguzi na Ukunga

285. Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kuwa huduma za Uuguzi na Ukunga ni mhimili muhimu katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini kwani asilimia 80 ya huduma za Afya zinatolewa na Wauguzi na Wakunga. Hivyo basi, Wizara imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa kuwajengea uwezo watoa huduma ili kuweza kutoa huduma zenye staha kwa **kuzingatia utu, heshima na mawasiliano madhubuti**. Hadi kufikia Machi 2025, **jumla ya madawati 400** ya Huduma kwa Mteja yameanzishwa katika vituo vya kutolea huduma kwa ngazi zote ili kusaidia wananchi kupata huduma kwa urahisi ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi changamoto mbalimbali wakati wa utoaji huduma. Aidha, watoa huduma 12,000 wamejengewa uwezo juu ya utoaji huduma staha ukilinganisha na watumishi 6,544 waliojengewa uwezo kwa mwaka 2024. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 83.

286. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwajibikaji wa watoa huduma katika kuimarisha ubora wa huduma, Wizara imezindua rasmi Kauli Mbiu ya Ubora wa Huduma katika Sekta ya Afya inayosema, **"HUDUMA BORA WAJIBU WANGU".** Kauli Mbiu hii ilizinduliwa rasmi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wauguzi Viongozi wa ngazi zote pamoja na taasisi za mafunzo uliofanyika kuanzia tarehe 18 hadi 20 Machi 2025". Kauli mbiu hii ambayo itawekwa kwenye mageti na milango ya vituo vyote vya kutolea huduma inalenga kuimarisha uwajibikaji kwa watoa huduma kutoa huduma bora.

287. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora wa utoaji huduma, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa kimatibabu katika vituo vya kutolea huduma. Kwa kipindi hiki, Wizara imefanya ukaguzi wa

kimatibabu kwa huduma za Uuguzi na Ukunga katika Hospitali 126 za Halmashauri. Matokeo ya ukaguzi huo yanaonesha kiwango cha ubora wa huduma za Uuguzi kimeongezeka kutoka asilimia 66 mwaka 2024 hadi asilimia 69 mwaka 2025 na huduma za Ukunga kutoka asilimia 75 mwaka 2024 kufikia asilimia 78 mwaka 2025. Ongezeko hili limechangiwa na kujengea uwezo Wauguzi na Wakunga 8,954 katika kutekeleza mipango kazi ya kushughulikia mapungufu yanayobainika pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma vituoni.

288. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za ushauri nasaha, upimaji wa VVU, kuanzisha dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati katika ngazi zote za kutolea huduma na kutoa rufaa kwa wakati kwa kuwatumia Wauguzi na Wakunga. Kwa kipindi hiki idadi ya Wauguzi na Wakunga waliopatiwa mafunzo ya kutoa huduma za VVU imeongezeka kutoka 3,769 mwaka 2024 hadi 5,056 Machi 2025, lengo ni kuendelea kusogeza huduma hizo kwa wagonjwa waliopo maeneo yenye upungufu wa matabibu. Aidha, programu hii imechangia kuongeza kasi ya upimaji wa VVU na uanzishwaji wa dawa pamoja na kuongezeka kwa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya vituo vipya 1,025 vya dawa za kupunguza makali ya VVU vinavyosimamiwa na Wauguzi vimeanzishwa katika maeneo yenye upungufu wa madaktari.

289. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuboresha vyumba vya kujifungulia ili kuweza kutoa **huduma za mama mwambata (Birth Companionship)** ambapo mama anaruhusiwa kukaa na msindikizaji aliyemchagua wakati wa kujifungua. Jumla ya vituo vya kutolea huduma 2,202 vimejengewa uwezo ambapo kwa sasa vituo 847 vinatoa huduma ya mama mwambata ikilinganishwa na vituo 42 kwa mwaka 2024 kipindi kama hiki. Sambamba na hili Wizara imewajengea uwezo watoa huduma 5,958 ikilinganishwa na watoa huduma 1,285 katika kipindi kama hiki mwaka 2024 juu ya matumizi sahihi ya chati uchungu ili kuendana na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani ya kuimarisha ubora wa huduma wakati wa kujifungua. Aidha, jumla ya Wakunga 181 katika Halmashauri za Kahama Mji, Ushetu, Kishapu, Shinyanga Vijijini, Ilala Jiji, Kinondoni na Temeke

walijengewa uwezo kutoa huduma za dharura kwa mama wakati wa kujifungua (Midwifery Emergency Skills Training).

290. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia ubora wa huduma kwa wagonjwa wa ndani katika **vitengo vya wagonjwa mahututi na dharura (ICU na EMD)**, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu matibabu ya hewa tiba ya Oksijeni kwa Wauguzi na Wakunga 760 kutoka Hospitali 16 za Rufaa za Mikoa ili kuimarisha huduma za wagonjwa mahututi. Aidha, Wizara imewajengea uwezo Wauguzi viongozi wa Mikoa na Halmashauri zote pamoja na Wauguzi Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa kufanya usimamizi shirikishi wa ndani kwa kutumia mfumo wa Usimamizi Shirikishi (AfyaSS) sambamba na miongozo ya kutoa huduma za Uuguzi. Jumla ya viongozi 302 waliweza kujengewa uwezo ili kuongeza ufanisi, tija na ubora wa huduma katika vituo wanavyosimamia sambamba na kuongeza usimamizi wa matumizi ya miongozo ya kutolea huduma za Uuguzi kama inavyoelekezwa na Shirika la Afya Duniani.

Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya

291. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kuhakikisha na kufuatilia utoaji wa huduma bora za afya katika ngazi zote nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara iliendelea kuimarisha Timu za Uimarishaji Ubora (Quality Improvement Teams) kwa kuwajengea uwezo watoa huduma 510 kutoka Timu za Uendeshaji Huduma za Afya za Mikoa, Halmashauri na vituo vya afya katika Halmashauri 35 za Mikoa ya Mtwara, Singida, Lindi, Manyara na Shinyanga. Kwa upande wa huduma kwa wateja, Wizara imeendelea kusimamia vituo vya kutolea huduma katika ngazi zote kwa kuhakikisha vituo vinaweka mazingira rafiki ya huduma kwa wateja. Mazingira hayo ni pamoja na kuboresha mifumo ya kupokea malalamiko, watoa huduma kuzingatia maadili ya kazi na kuhakikisha usalama wa huduma kwa mteja.

292. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora wa huduma za kimatibabu, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imefanya ukaguzi wa kimatibabu (Clinical Audit) katika hospitali za

rufaa za mikoa 28, hususan kwenye huduma za mama na mtoto pamoja na huduma za dharura. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kuwa miongozo ilifuatwa kwa asilimia 67 katika huduma za mama na mtoto na asilimia 64 katika huduma za dharura. Sambamba na hilo, Wizara ilitoa mafunzo ya ukaguzi kwa watoa huduma 288 ambapo 163 walipata mafunzo ya ana kwa ana na 125 kwa njia ya mtandao. Aidha, Wizara imeboresha nyenzo za ukaguzi na kuwajengea uwezo watoa huduma ili waendelee kufanya ukaguzi kwa ufanisi na kupanua wigo wa ukaguzi hadi vituo vya afya vya ngazi ya msingi ambako wananchi wengi hupatiwa huduma.

293. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma zinazotolewa kwenye vituo zinakidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa, Serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha taasisi maalum ya kutoa ithibati kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Lengo kuu la kuanzisha taasisi hii ni kuhakikisha huduma zinazotolewa zinazingatia viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuweka viwango, kufanya tathmini huru, na kutoa ithibati kwa vituo vitakavyokidhi vigezo. Pia, uanzishwaji wa taasisi hii utapunguza gharama kubwa zinazolipwa kwa taasisi za nje na kusaidia vituo vitakavyopewa ithibati kutoa huduma bora, salama na zenye kuheshimu haki na utu.

294. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza afua za kukinga na kudhibiti maambukizi (Infection Prevention and Control) pamoja na kuhakikisha usalama wa huduma kwa wateja. Katika muktadha huo, jumla ya watoa huduma 3,304 wamepatiwa mafunzo ambapo 1,852 walihudhuria mafunzo darasani na 1,452 walipata mafunzo kwa njia ya mtandao katika mikoa ya Mara, Dar es Salaam, Kigoma, Shinyanga, Singida, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera, Morogoro, Mbeya na Katavi. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo watoa huduma ili waweze kukinga na kudhibiti maambukizi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na ya milipuko kama Marburg, Kipindupindu, Mpox, pamoja na maambukizi yanayotokana na huduma za afya (Healthcare Associated Infections).

295. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufuatiliaji wa maambukizi yanayohusiana na huduma za afya, Wizara imetoa mafunzo kwa watoa huduma 317 kutoka vituo 53 vilivyopo katika mikoa sita (Lindi, Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Manyara na Kilimanjaro). Viashiria vya ufuatiliaji vimeingizwa kwenye mfumo wa kidijitali wa DHIS2 ili kurahisisha ukusanyaji na ufuatiliaji wa taarifa hizo. Vilevile, Wizara inaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma waliopo kwenye ngazi ya afya ya msingi ili waweze kuanza kutoa taarifa za magonjwa husika katika mifumo ya kutolea taarifa.

296. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha **usimamizi shirikishi** kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea na utekelezaji wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa *Afya Supportive Supervision System* (AfyaSS) ambapo mfumo huo umeweza kutumika katika ngazi zote za kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, jumla ya simamizi shirikishi 14,186 kati ya 25,147 sawa na asilimia 56.4 zilifanyika kupitia mfumo huo. Aidha, hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya watoa huduma 13,134 wamefundishwa na kusajiliwa katika mfumo huo. Mfumo huo umesaidia kuongeza ufanisi wa usimamizi shirikishi kwa kusaidia kutunza kumbukumbu, kuongeza uwajibikaji na kupunguza gharama za matumizi ya karatasi.

Rasilimali Watu Katika Sekta ya Afya

297. Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma bora kwa wananchi unategemea uwepo wa watoa huduma za afya wenye ujuzi na weledi wa kazi. Lengo hilo litawezekana iwapo vyuo vya afya vitaendelea kuzalisha wataalam wenye ujuzi na weledi, kuwaendeleza wataalam waliopo pamoja na kuajiri watumishi wa kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

298. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Serikali **imeajiri jumla ya watumishi 13,564** katika Sekta ya Afya na kufanya **jumla ya watumishi katika Sekta ya Afya kufikia 177,711**. Ongezeko hili la watumishi **limepunguza upungufu wa watumishi wa Sekta ya Afya kutoka asilimia 64 hadi kufikia asilimia 55 ya mahitaji**

ya watumishi wote 391,950 wanaohitajika katika Sekta ya Afya. Kati ya watumishi waliopo, watumishi 136,739 sawa na asilimia 77 wapo katika ngazi ya afya ya msingi na watumishi 33,765 sawa na asilimia 19 wanafanya kazi katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum za Rufaa na Hospitali ya Taifa na asilimia 4 ya watumishi wapo katika Mashirika na Taasisi. Pamoja na juhudi hizi Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Afya imeendelea kutoa ajira za mikataba ili kukabiliana na upungufu wa watumishi uliopo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 8,146 waliajiriwa kupitia utaratibu huu kwa ajili ya kufanya kazi kwenye vituo vya kutolea huduma.

299. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kuweka mazingira mazuri na yenye kuvutia kwa watumishi wa Sekta ya Afya ili kuwabakiza watumishi katika maeneo yao ya kazi. Wizara inaendelea kuwakumbusha waajiri mbalimbali kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia na kuwabakiza watumishi wa Sekta ya Afya kama vile kujenga nyumba za makazi karibu na maeneo ya kutolea huduma, kununua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwahudumia watumishi, kuendelea kutoa posho ya masaa ya ziada na posho za kuitwa kazini (Oncall Allowance), kutoa mikopo kwa watumishi wa afya na kuwaendeleza watumishi hao ili wabaki katika maeneo yao kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi.

300. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uwepo wa wataalam wa kutosha, kwa uwiano sahihi na wanaotoa huduma zilizo bora za afya kwa wananchi, Wizara imeendelea kusimamia vyuo vyote vya mafunzo vya kada zaa kati vinavyomilikiwa na Serikali, taasisi za dini na watu binafsi ili kuhakikisha vinazalisha wataalam wenye ujuzi na weledi. Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 33,353 sawa na asilimia 36 ya waombaji 92,820 waliotuma maombi ya kujiunga na vyuo vya afya ngazi ya kati. Kati yao wanafunzi 3,209 sawa na asilimia 10 walichaguliwa kujiunga na vyuo vya Serikali na wanafunzi 30,144 sawa na asilimia 90 walichaguliwa kujiunga na vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi na taasisi za dini katika programu za

Sayansi Shirikishi za Afya, Uuguzi na Ukunga. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watalaam 17,850 wamehitimu katika fani mbalimbali za kada za kati za Afya ikilinganishwa na wataalam 15,475 katika kipindi hicho kwa mwaka 2024. Wahitimu ngazi ya shahada kwa kipindi hicho ni 5,415 ikilinganishwa na wataalam 2,891 katika kipindi hicho kwa mwaka 2023. Vilevile, wahitimu wa ngazi ya Shahada ya Uzamili wameongezeka kutoka 540 mwaka 2023 hadi kufikia 889 mwaka 2024.

301. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na kuratibu uendeshaji wa mafunzo ya muda mfupi ya Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya washiriki 3,631 wamepatiwa mafunzo hayo. Pamoja na mafunzo hayo, Wizara imeanzisha mitaala ya kada zenye uhaba mkubwa nchini ikiwa ni pamoja na Mtaala wa Stashahada ya Saikolojia Tiba (Clinical Psychology) ambao upo kwenye hatua za mwisho za ukamilishwaji. Mitaala hii imeanzishwa ili kuzalisha wataalam wa kutosha kukabiliana na changamoto za matibabu ya afya ya akili na utengemao kuanzia kwenye ngazi ya msingi. Vilevile, Wizara imehuisha mitaala ya Stashahada ya Optometria na Utunzaji Kumbukumbu na Taarifa za Afya (Health Record and Information Technology) baada ya iliyokuwepo kuisha muda wa matumizi.

302. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia ufadhili wa masomo wa ***Samia Health Super-specialization Program*** umewezesha ufadhili wa masomo kwa **watalaam wapya wa Sekta ya Afya 544** na kufanya jumla ya wataalam wanaofadhiliwa kusomea fani za ubingwa na ubingwa bobezi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi kufikia 1,420. Kati ya wataalam wapya waliopata ufadhili, 517 wamepata ufadhili wa kusoma vyuo vikuu vya ndani na watalaam 27 wamepata ufadhili wa kusoma nje ya nchi. Vilevile, Watumishi 47 wamepata ufadhili wa mafunzo kwa mfumo wa seti unaowezesha huduma mpya za ubingwa na ubingwa bobezi kuanza kutolewa zikiwa na wataalam wote wanaohitajika kwa ajili ya utoaji wa huduma hizo. Aidha, kutokana na **kuongezeka kwa kiwango cha fedha ya ufadhili kutoka Shilingi Bilioni 10.95 mwaka 2023/2024 hadi kufikia Bilioni 14** mwaka

2024/2025, idadi ya wanufaika wa ufadhili imeendelea kuongezeka hadi kufikia wataalam 1,420 mwaka 2024/2025.

303. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mpango wa kuwajengea uwezo wataalam wa Sekta ya Afya ili waweze kutoa huduma zinazokubalika kitaifa na kimataifa sambamba na kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao kwa Sekta ya Afya (*National e-Learning Platform for Health)*. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya moduli 42 za mafunzo mbalimbali ya afya ziliongezwa kwenye mfumo na kufanya jumla ya moduli zilizopo katika mfumo kufikia 298.** Katika kipindi hicho watumishi wapya waliosajiliwa kwenye mfumo huo ni 9,751 na kufanya jumla ya watumishi wote kufikia 129,663. Wizara kwa kushirikiana na mabaraza ya kitaaluma itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuwaendeleza wataalam wa Sekta ya Afya ili waendelee kuwa na weledi unaokubalika katika kutoa huduma za afya nchini.

304. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imewajengea uwezo wakufunzi 92 wa vyuo vya afya vya kada za kati nchini kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za ufundishaji na upimaji wa wanafunzi *(Teaching Methodology and Students Assessment)*. Pia, katika kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti ubora wa mafunzo, Wizara imehuisha miongozo mbalimbali ya mafunzo ikiwemo Mwongozo wa Mitihani ya Kitaifa ya Kada za Kati za Afya, Mwongozo wa Ulinzi na Usalama wa Mitihani ya Kitaifa ya Muhula wa Pili na Mwongozo wa Matumizi ya Hospitali za Mafunzo (Clinical Placement Guide).

305. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo ya Viashiria vya Mahitaji ya Watumishi kwa kulingana na kazi yaani ***Workload Indicators of Staffing Needs (WISN)*** kwa wakufunzi 128 kutoka kwenye Mikoa yote nchini. Mafunzo hayo, yamezingatia maboresho ya kidigitali yaliyofanyika ili kurahisisha kukusanya na kuchakata taarifa za viashiria vya kazi zilizofanyika kwenye kituo kwa ajili ya kupima uzito wa kazi kwenye vituo na kutoa taarifa ya uhitaji wa watumishi kulingana na uzito wa kazi zilizopo. Mafunzo hayo yatawezesha

kuendelea kupanga mipango ya mahitaji ya watumishi yenye uhalisia kwa kuzingatia uzito wa kazi na sio kuzingatia hadhi au ukubwa wa kituo bila kujali idadi ya wagonjwa, huduma zinazotolewa na uzito wa kazi kwa watumishi waliopo kwenye kituo husika.

Matumizi ya TEHAMA

306. Mheshimiwa Spika, Wizara imesimika Mfumo wa Afya eHMS katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 28 na kuunganisha na mifumo mingine ikiwemo mfumo wa Taarifa za Utoaji wa Huduma za Afya (DHIS2), mfumo wa kukusanya mapato Serikalini (GePG), Bohari ya Dawa (MSD), Wakala ya Usajili wa Ufilisi na Udhamini (RITA) na mifumo ya Bima za afya, ikiwemo mfumo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Aidha, Mfumo huo pia umeunganishwa na Mifumo ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda (MNH, JKCI, MOI, BMH, BMC, ORCI) na mfumo wa kutolea huduma za afya ngazi ya msingi (GOTHOMIS).

307. Mheshimiwa Spika, Mfumo jumuishi wa kukusanya na kuhifadhi taarifa za afua mbalimbali za afya ngazi ya jamii (Unified Community System - UCS) umeboreshwa. Hadi sasa mfumo huo umesimikwa katika jumla ya mikoa 26 ikiwemo Arusha (vituo vya afya 108), Dar es Salaam (vituo vya afya 52), Dodoma (vituo vya afya 105), Geita (vituo vya afya 90), Kagera (vituo vya afya 120), Kigoma (kituo cha afya 75), Kilimanjaro (vituo vya afya 62), Lindi (vituo vya afya 102), Manyara (vituo vya afya 52), Mbeya (vituo vya afya 172), Morogoro (vituo vya afya 79), Mwanza (vituo vya afya 178), Njombe (vituo vya afya 79), Pwani (vituo vya afya 129), Shinyanga (vituo vya afya 128), Singida (vituo vya afya 62), Tabora (vituo vya afya 174) na Tanga (vituo vya afya 130).

308. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha ufungaji wa huduma za Tiba Mtandao katika hospitali ya Rufaa Mkoa wa Songwe na kufanya hospitali zinazotumia Huduma ya Tiba Mtandao kuwa 25 (Hospitali za Rufaa ya ngazi ya Mkoa 18, Hospitali za Rufaa ngazi ya Kanda tatu (3), Hospitali Maalum tatu (-3), Hospitali ngazi ya Taifa moja (1).

Matumizi ya mfumo huu yatasaidia katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini.

Ufuatiliaji na Tathmini

309. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na Tathmini, Wizara imeunda timu ya wataalam 126 wa Ufuatiliaji na Tathmini kutoka katika Idara, Vitengo, Programu, Mabazara na bodi, Taasisi na Hospitali zilizo chini ya Wizara. Utekelezaji huu umefanyika kwa kuzingatia agizo lililotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya ufuatiliaji na tathmini. Lengo la timu hiyo ni kuimarisha utendaji kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na *champions* ambao wamebobea katika eneo ya tathmini na ufuatiliaji, Wizara imeandaa mwongozo wa mafunzo ambao utatumika kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa wataalam hao 126 kuwa na ujuzi wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao haswa katika eneo la afya.

310. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara imekamilisha kuandaa machapisho manne (4) ya Takwimu na kuyasambaza katika Idara na Vitengo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya takwimu ikiwemo jarida la Takwimu za hali ya utoaji wa huduma za Afya nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024, *Annual Health Sector Performance Profile 2023, Health Statistical Table and Figure 2023 na National Health Facility Atlas 2023.* Taarifa hizi zinapatikana katika Tovuti ya Wizara na Tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Taarifa zinazopatikana katika majarida na machapisho hayo inawezesha Wizara, wadau na jamii kufahamu kuhusu mwenendo wa utoaji huduma za afya na kutumia taarifa hizo katika kutoa ushauri na kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kisayansi katika kutatua changamoto za Sekta ya Afya.

311. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa taarifa na takwimu za utoaji huduma za afya nchini ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, imeandaa na kusambaza nyenzo 314,413 za ukusanyaji taarifa (MTUHA tools) katika

vituo vyote vya kutolea huduma nchini. Nyenzo hizo ni pamoja na Rejesta, Fomu za Muoanisho na Fomu za Taarifa za kila mwezi, ambazo zimeshajumuishwa katika mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji taarifa. Zana hizo zitasaidia kuimarisha upatikanaji wa takwimu katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Ugharamiaji wa Huduma za Afya

312. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza Mikakati mbalimbali ili kuwezesha wananchi kupata huduma za afya kwa kuzingatia Sera ya Afya ya Mwaka 2007. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya nchini na kuimarisha mfumo wa Bima ya Afya kwa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura 161 yenye lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi wanapohitaji huduma hiyo.

313. Mheshimiwa Spika, kufuatia tangazo la **Serikali Na. 700A la mwaka 2024** la kuanza utekelezaji wa **Sheria ya Bima ya Afya kwa wote** kwa awamu**,** Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya kabla ya kuanza kutekelezwa kwa takwa la ulazima wa bima ya afya kwa wote. Uelimishaji wa wananchi unahusisha viongozi wa ngazi zote ikiwemo ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwa na uwajibikaji wa pamoja. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika na utekelezaji wa Sheria hii inaendelea kuimarisha mifumo itakayosaidia kuongeza ufanisi katika kuandikisha wanachama na uchakataji wa madai. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mfuko wa kugharamia kaya maskini (TASAF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Tanzania (NIDA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

314. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2024/25 kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.54** kilitengwa kwa ajili ya kugharamia vipaumbele mbalimbali katika Sekta ya Afya ikiwemo ujenzi na ukarabati wa

miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Trilioni 2.46 kilichotengwa mwaka 2023/24. Aidha, Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ambapo hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha Shilingi Bilioni 243.5 kimetolewa kwa ajili ya ununuzi, ugomboaji, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

315. Mheshimiwa Spika*,* katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya Sera za Kimataifa katika ufadhili wa Sekta ya Afya, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya tathmini ya namna ya kukabiliana na changamoto ya athari hizo kwa kutenga kiasi cha Shilingi Bilioni 202 kwa ajili ya kutumika katika kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2025. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi Bilioni 93 tayari zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa za ARVs, bidhaa za Kifua Kikuu na Malaria. Aidha, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kwa Wizara hadi kufikia Shilingi Bilioni 300 kwa mwaka 2025/26 kutoka Shilingi Bilioni 200 za mwaka 2024/25. Ongezeko hili litawezesha ununuzi wa dawa za ARVs pamoja na dawa nyingine muhimu.

'Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Serikali imejipanga katika kuhakikisha dawa hizo muhimu zinapatikana kwa walengwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kama kawaida'.

Miradi ya Maendeleo

316. Mheshimiwa Spika**,** katika kuboresha huduma za afya nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususan ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalumu na Hospitali ya Taifa pamoja na vyuo vya Afya na utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali.

317. Mheshimiwa Spika*,* Miradi 11 imefikia zaidi ya asilimia 80 ya utekelezaji ikiwemo; ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu; ujenzi

wa awamu ya pili wa jengo la wodi za wagonjwa, jengo la huduma za Radiolojia katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Chato; jengo la kutolea huduma za wagonjwa wa nje awamu ya kwanza na jengo la Damu Salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa KigomaMaweni; jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi na Mtwara, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara awamu ya nne; ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro-Mawenzi, ujenzi wa jengo la Radiologia katika Hospitali ya Magonjwa ambukizi ya Kibong'oto na ujenzi wa jengo la kutolea huduma za wagonjwa wa nje awamu ya pili katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma - Songea**.**

318. Mheshimiwa Spika, Miradi mitatu (3) inayoendelea na utekelezaji imefikia wastani wa asilimia 60 ambayo ni ujenzi wa jengo la huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora-Kitete, ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe na ujenzi wa jengo la damu salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa.

319. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza miradi mitano (5) ambayo utekelezaji wake umefikia wastani wa asilimia 40, ikiwemo ujenzi wa jengo la magonjwa hatarishi ya kuambukiza katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida; ujenzi wa jengo la afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, ujenzi wa kituo cha umahiri kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na milipuko Kisopwa, ujenzi wa jengo la tiba mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa na ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Kanda Chato.

320. Mheshimiwa Spika, miradi (52) utekelezaji wake upo katika hatua za awali kwa wastani wa asilimia 20; Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Hospitali ya mama na Mtoto Nala-Dodoma, Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Magharibi-Kigoma, Ujenzi wa jengo la utawala katika ya Hospitali ya magonjwa ambukizi Kibong'oto, Uhuishaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), ujenzi wa kituo cha mionzi

kwa ajili ya matibabu ya Saratani – Mbeya, ujenzi wa jengo la huduma ya afya ya mama na mtoto katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Shinyanga, Tanga, Kagera na Morogoro ni ***kama inavyoonekena katika Kiambatisho Namba 2.***

Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo Chini ya Wizara Bohari ya Dawa (MSD)

321. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa (MSD) ni Taasisi iliyoanzishwa mwaka 1993 kwa mujibu wa Sheria ya Bohari ya Dawa Na.13 iliyofanyiwa marekebisho mbalimbali na ina majukumu ya msingi manne (4); Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za afya na vile vilivyoidhinishwa na Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2025, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vinavyohudumiwa na Bohari ya Dawa vimeongezeka na kufikia 8,619 kutoka vituo 8,276 vilivyorekodiwa Juni 30, 2024 sawa na ongezeko la vituo 343. Ongezeko hili limetokea kwenye mikoa yote inayohudumiwa na Bohari ya Dawa kupitia kanda 10 zilizopo katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mtwara, Mwanza, Tabora,
Kilimanjaro, Tanga, Kagera, Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya imeendelea kuimarika kwa kuzingatia upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria 382 na bidhaa za Mradi Misonge 73. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2024/25, upimaji wa hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria umeendelea kuzingatia bidhaa za afya 382. Lengo likiwa ni kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya ambazo ni muhimu zaidi kwenye utoaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

322. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya kwenye maghala ya Bohari ya Dawa pekee umeendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria 382 kwenye maghala ya Bohari ya Dawa umefikia asilimia 68 kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya mwezi mmoja ikilinganishwa na asilimia 61 kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, upatikanaji wa bidhaa za dawa pekee umeendelea kuwa

asilimia 68 kwa mwezi Machi 2025 kwa kiwango kinachokidhi mwezi mmoja. Upatikanaji huu wa bidhaa za afya umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka licha ya kuwepo kwa changamoto ya uwezo mdogo wa uzalishaji wa bidhaa za afya nchini na migogoro mbalimbali inayoathiri mnyororo wa ugavi duniani na hivyo kuhitajika kwa muda mrefu kati ya uagizaji na mapokezi ya bidhaa za afya.

323. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za Miradi Misonge – "Vertical Programs" umeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi 2025, upatikanaji wa bidhaa hizi umefikia asilimia 92.5 kutoka asilimia 82 iliyofikiwa mwezi Machi 2024. Bidhaa hizi za Miradi Misonge zinahusu magonjwa ya UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, Ukoma na Afua nyinginezo ambazo zimekuwa zikipatikana kupitia Serikali na Wadau mbalimbali. Sambamba na hili, Utimizaji wa mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya umeendelea kuwa wastani wa asilimia 79 hadi kufikia mwezi Machi 2025, sawa na kiwango kilichoripotiwa mwezi Julai 2024. Utimizaji huu unahusu mahitaji yaliyoombwa kupitia Bohari ya Dawa pekee.

'Nichukue fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa dawa za miradi misonge zitaendelea kupatikana kama kawaida katika vituo vya kutolea huduma za afya'.

324. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Bohari ya Dawa imeendelea kufanya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi vituo vinavyotoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za kuchuja damu (dialysis), vifaa tiba vya utoaji wa huduma ya kinywa na meno kama vile viti vya meno vya kisasa pamoja na mashine maalum za mionzi kwa utoaji wa huduma za kinywa na meno 'dental x-ray', mashine za usingizi, 'Ultrasound' na 'Digital X-Ray'. Uwepo wa mitambo hii umeimarisha utambuzi wa magonjwa kwa usahihi na kutolewa kwa tiba sahihi. Vilevile, Bohari ya Dawa imeendelea kusambaza bidhaa za afya kwa lengo la kuokoa maisha ya mama na mtoto, majenereta kwa ajili ya kuhakikisha huduma hazikwami pale ambapo kunatokea

changamoto za umeme, mashine za kufulia na majokofu ya kuhifadhia miili.

325. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bohari ya Dawa inatekeleza mpango maalum wa kuongeza upatikanaji wa huduma za uchujaji damu ikiwa ni sehemu ya matibabu ya figo, hivyo kupunguza gharama za huduma hiyo. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 idadi ya mashine imeongezeka na kufikia mashine 137 kutoka mashine 60 na hivyo kuongeza hospitali zilizopokea mashine hizi kupitia Bohari ya Dawa kutoka hospitali 7 na kufikia hospitali 15. Uwekezaji huu umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 7.7. Katika hospitali hizi, hospitali 11 zimeanza kutoa huduma na hospitali 4 zipo katika hatua za mwisho za matengenezo. Baadhi ya hospitali zinazotoa huduma hizi ni pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Amana, Mwananyamala, Temeke, Morogoro, Katavi, Tumbi, Chato, Sekou Toure pamoja na hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, Mkakati huu wa usambazaji wa mashine za uchujaji wa damu unalenga kupunguza gharama na adha zilizopo kwa sasa.

326. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa imesambaza jumla ya *kits* 144 ya bidhaa za *hemodialysis* kwa ajili ya vipindi 100 kila kimoja kwa hospitali zinazotoa huduma za uchujaji wa damu. Usambazaji huu utawezesha utoaji wa huduma kwa vipindi 14,400. Katika kuhakikisha huduma hizi hazikwami, Bohari ya Dawa imeagiza na inatarajia kupokea shehena nyingine ya *kits* 504 ifikapo mwezi Juni 2025, ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma za uchujaji damu.

327. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuhakikisha bidhaa za afya ya kinywa na meno zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya. Thamani ya bidhaa hizo zilizosambazwa imeendelea kuongezeka kutoka Shilingi milioni 598.19 kwa mwaka 2022/23 na kuweza kufikia Shilingi Bilioni 9.46 mwaka 2024/25. Hali ya upatikanaji wa bidhaa za meno ashiria imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi 2025 imefikia 88% ikilinganishwa na 75% katika kipindi kama hichi kwa mwaka 2024 na hivyo kuwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuweza kutoa huduma hizi kwa ubora na ufanisi zaidi.

328. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha bidhaa za afya zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kufanikisha usambazaji wa bidhaa za afya nchi nzima kwa mizunguko sita kutoka mizunguko minne. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi mwezi Machi 2025, Bohari ya Dawa ilifanikiwa kusambaza bidhaa za afya kwa kuzingatia muda uliopangwa kwa wastani wa asilimia 98 ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 kutoka asilimia 92 katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024.

329. Mheshimiwa Spika, kutokana na jukumu la ununuzi wa bidhaa za afya, sambamba na fedha ya Serikali inayopelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ambapo mwaka huu wa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 200 kilitengwa na mpaka sasa MSD imeshapokea kiasi cha Shilingi Bilioni 183.2 sawa na asilimia 91.6. Hata hivyo, Bohari ya Dawa hukusanya fedha (*cash collection)* kutoka vituo vya kutolea huduma za afya ambazo hupatikana kupitia vyanzo vingine vya vituo hivyo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kiasi cha Shilingi Bilioni 126.64 zilikusanywa sawa na asilimia 64 ya lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 198.40. Aidha, kiasi hiki kimeongezeka kwa asilimia 110 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 60.3 kilichokusanywa kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha uliopita.

330. Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali, mapato ya Bohari ya Dawa yameendelea kuongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Bohari ya Dawa imepata mapato ya Shilingi Bilioni 438.14 sawa na asilimia 108 ya lengo la kusambaza bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi Bilioni 389.94. Mapato haya ni ongezeko la Shilingi Bilioni 90.68 kutoka Shilingi Bilioni 347.46 sawa na asilimia 26 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2023/2024. Ongezeko hili limesababishwa na maboresho ya kiutendaji na usimamizi wa mnyororo wa ugavi, ununuzi na usambazaji wa bidhaa za afya kupitia bajeti ya vituo vya kutolea huduma inayotengwa kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya RaisTAMISEMI, kuimarika kwa makusanyo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya za

Miradi Msonge. Aidha, mapato mengine yaliyokusanywa kwa kipindi hiki cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025 ni kiasi cha Shilingi Bilioni 16.37 sawa na asilimia 108 ya lengo la Shilingi Bilioni 15.07 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

331. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, Bohari ya Dawa inaendelea na mkakati wake wa kuhakikisha uwepo wa Mikataba ya Muda Mrefu - *Framework Agreements,* kutoa kipaumbele kwa wazalishaji wa ndani, kuanzisha na kutekeleza mkakati wa kununua moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji au wazabuni walioidhinishwa na wazalishaji husika, na kusimamia utendaji wa wazabuni kwa kuzingatia mikataba iliyopo.

332. Mheshimiwa Spika, ufanisi unaopatikana Bohari ya Dawa ni matokeo ya Serikali kuwekeza kwenye maboresho na kuhakikisha Taasisi hii nyeti inatekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwemo kuipatia MSD kiasi cha Shilingi Bilioni 100. Aidha, katika kuhakikisha utendaji wa Bohari ya Dawa unaimarika, kuanzia mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imeamua kutenga fedha kwa ajili ya kulipia gharama za bidhaa za Miradi Msonge ambazo zinahusu utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya kwa ajili ya magonjwa ya UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, Ukoma na bidhaa za mama na mtoto.

333. Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la watu, na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika Sekta ya Afya umesababisha ongezeko la mahitaji ya maghala ya kuhifadhia bidhaa za afya ili kuimarisha mnyororo wa ugavi. Serikali imejenga maghala ya kisasa yenye viwango vya kimataifa katika Mikoa ya Dodoma na Mtwara ambapo yameshakamilika na yataanza rasmi kutumika mwezi Juni,2025.

334. Mheshimiwa Spika, Maghala haya mapya yatapunguza gharama za usambazaji ambapo ghala lililopo Dodoma litakuwa linapokea bidhaa zake kupitia reli ya kisasa kituo cha Dodoma kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kuwezesha bidhaa hizo kusambazwa moja kwa moja kwenda kwenye Kanda nyingine nchini. Aidha, Bohari ya Dawa inaendelea kutekeleza ujenzi wa maghala kwa awamu

ambapo awamu ya pili itahusu ujenzi wa ghala la Mwanza na Chato, Mkoa wa Geita, ambapo Serikali imeweza kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 24.6 na hatua za kuwezesha kuanzishwa kwa ujenzi wa ghala la Dar es Salaam zinaendelea. Awamu ya tatu itatekelezwa katika Mikoa ya Arusha na Ruvuma.

335. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa bidhaa za afya nchini, Bohari ya Dawa imeanzisha Kampuni Tanzu inayoitwa "MSD Medipharm Manufacturing Company Limited" ambayo ina jukumu kubwa la kufanya uzalishaji wa bidhaa za afya. Kampuni hii, ina uwezo wa kufanya uwekezaji kwa kushirikiana na Sekta binafsi kwa mfumo wa uwekezaji wa pamoja yaani *Joint Venture Investment* na kuiwezesha Serikali kunufaika na faida inayopatikana moja kwa moja.

336. Mheshimiwa Spika, Kampuni hii kwa sasa inamiliki Kiwanda cha Barakoa cha MSD Medipharm ambacho kina takribani miaka minne (4) toka kuanzishwa kwake na kinazalisha barakoa za kawaida (Surgical mask) na barakoa maalum (N95) kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya njia ya hewa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini pamoja na Kiwanda cha Glovu kilichopo Makambako Mkoa wa Njombe.

337. Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai 2024 hadi Mwezi Machi 2025, kiwanda kimeweza kuzalisha jumla ya Barakoa 1,119,778 sawa na asilimia 124 ya lengo, na kufanya mauzo ya jumla ya Shilingi 588,930,035.00 sawa na asilimia 130.9 ya malengo ya kiwanda, na ikilinganishwa na barakoa 732,800 zilizozalishwa kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kufanya mauzo ya Shilingi 366,400,000.00. Vilevile, hadi kufikia mwezi Machi 2025, Kiwanda cha Glavu(Gloves) Idofi kimeweza kuzalisha na kuuza jumla ya glavu milioni 5.6 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.9 sawa na asilimia 50 ya matarajio ya uzalishaji kwa mwaka wa kwanza wa kiwanda.

338. Mheshimiwa Spika, Kampuni hii inatekeleza mradi mkubwa wa viwanda vya dawa na vifaa tiba katika eneo la viwanda la MSD, Zegereni Mkoa wa Pwani, mradi unaotekelezwa kwa kushirikiana na

wabia wenza kutoka sehemu mbalimbali duniani. Aidha, MSD kupitia Kampuni hii inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kuzalisha bidhaa za afya zitokanazo na malighafi ya pamba ambao unalenga kutumia pamba inayolimwa nchini na kuchangia sio tu kupunguza uagizaji wa bidhaa hizi kutoka nje ya nchi bali pia kutoa soko la uhakika kwa wakulima wa zao la pamba nchini na ajira kwa vijana.

339. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuongeza ununuzi wa bidhaa za afya kutoka kwa wazalishaji wa ndani ambapo katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025, bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi Bilioni 56.7 zimenunuliwa kutoka kwa wazalishaji wa ndani ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 16.93 zilizonunuliwa katika kipindi kama hichi kwa mwaka wa fedha 2023/24 ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 39.77.

Aidha, MSD imeendelea kununua maji tiba kwa asilimia 100 kutoka kwa wazalishaji wa ndani. Dhamira hii itasaidia kuongeza uzalishaji na kuvutia wawekezaji ambapo matumizi ya fedha za kigeni yatapungua na ajira zitatengenezwa nchini.

340. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Serikali imewezesha Bohari ya Dawa kuanza usimikaji wa mfumo wa TEHAMA ambao utakuwa na thamani ya Shilingi Bilioni 4. Mfumo huu unatarajiwa kuongeza ufanisi katika mnyororo wa ugavi, kuboresha matumizi ya takwimu na upashanaji taarifa. Katika jitihada za kuhakikisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA yanaimarishwa, hadi sasa, matumizi ya TEHAMA kwa Bohari ya Dawa yamefikia kiwango cha asilimia 95 ambapo sehemu kubwa ya michakato inafanyika katika mfumo wa Epicor 10 – ERP na kupelekea MSD kutambulika na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kiwango cha *Level 4* katika matumizi ya Tehama.

341. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2025 miongoni mwa mifumo iliyotengenezwa ili kuimarisha utendaji ni mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa magari (Real time Fleet Management System), mfumo wa ununuzi wa bidhaa za afya kwa nchi za SADC kwa njia ya

kielektroniki (Electronic SADC Pool Procurement - eSPPS), Mfumo wa "*Proof of Delivery*" unaotumika kusainisha vituo baada ya kufikishwa mzigo vituoni na kupokelewa na mfumo wa kuhudumia wateja, (Customer Portal) ambao hutumika na vituo vya kutolea huduma za afya kutambua bidhaa za afya zilizopo MSD, gharama yake na hatua zilizofikiwa katika uchakataji wa maombi ya wateja yalipofikia.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

342. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Sura ya 395 kwa lengo la kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa Umma na wategemezi wao kupitia bima ya afya. Sheria ya Mfuko imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuwezesha kupanua wigo wa walengwa kwa kuingiza makundi mbalimbali. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya, Mfuko unajumuisha watumishi katika Sekta ya Umma, wafanyakazi kutoka katika Sekta Binafsi na makundi mbalimbali ya jamii katika Sekta isiyo rasmi. Majukumu ya Kisheria ya Mfuko ni pamoja na kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuitunza, kusajili watoa huduma na kufanya malipo kwa watoa huduma za afya. Majukumu mengine ni kuwekeza fedha za ziada katika vitega uchumi mbalimbali ili kujiongezea uwezo wa kifedha unaowezesha kutoa huduma, kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma ili kuhakikisha wanazingatia miongozo iliyopo, kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko na kutoa elimu kwa Umma.

343. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko umesajili wanachama wapya 462,408 sawa na asilimia 78 ya lengo la kusajili wanachama wapya 593,654. Kulinganisha na wanachama 337,834 waliosajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Idadi ya wanachama waliosajiliwa imewezesha Mfuko kuwa na wanachama wachangiaji 1,255,813 wenye jumla ya wanufaika 5,161,281 sawa na **asilimia 8.1** ya Watanzania wote. Mfuko unaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wanachama ikiwemo kutoa elimu mijini na vijijini ili kuhakikisha

wanachama wengi wanajiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya.

344. Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika, Mfuko umekusanya mapato jumla ya Shilingi Bilioni 619.8. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi Bilioni 579.9 ni kutoka katika michango ya wanachama, Kiasi cha Shilingi Bilioni 36.3 ni mapato yatokanayo na uwekezaji na kiasi cha Shilingi Bilioni 3.5 ni kutoka katika vyanzo vingine vya mapato. Mapato yaliyokusanywa ni ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 560.8 kilichokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2023/24 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7**.

Jedwali Na. 7. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Mfuko kati ya mwaka 2023/24 na mwaka 2024/25.

Mapato	MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2023/24			MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2024/25			ONGEZEKO/ PUNGUFU (%)
	Malengo (in '000) TZS)	Halisi (in '000) TZS)	Asilimia ya lengo	Malengo (in '000) TZS)	Halisi (in '000) TZS)	Asilimia ya lengo	
Michango	534,963,054	521,980,614	98%	603,032,075	579,999,093	96%	10%
Uwekezaji	50,238,195	34,257,837	68%	42,680,244	36,316,438	85%	6%
Mapato	**MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2023/24**			**MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2024/25**			**ONGEZEKO/ PUNGUFU (%)**
	Malengo (in '000) TZS)	**Halisi (in '000) TZS)**	**Asilimia ya lengo**	**Malengo (in '000) TZS)**	**Halisi (in '000) TZS)**	**Asilimia ya lengo**	
Mengineyo	1,125,000	4,617,053	410%	5,352,224	3,493,138	65%	-32%
Ufadhili	7,687,500	-	-	16,447,376	-	-	-
Jumla	**594,013,749**	**560,855,504**	**94%**	**667,511,919**	**619,808,669**	**93%**	**10%**

345. Mheshimiwa Spika, michango kutoka kwa wanachama imeendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 ilikuwa ni asilimia 93 ya mapato yote yaliyokusanywa ikiwa ni asilimia 92 ya lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 603. Kiasi hicho ni ongezeko la

asilimia 6 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 521 kilichokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24.

346. Mheshimiwa Spika, Mfuko umetumia jumla ya **Shilingi Bilioni 506**, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 438.1 ni kwa ajili ya ulipaji wa madai kwa watoa huduma, kiasi cha Shilingi Bilioni 66.4 ni matumizi ya kiutawala ikijumuisha malipo ya mishahara na kiasi cha Shilingi Bilioni 1.7 ni matumizi mengineyo ikijumuisha miradi ya maendeleo. Matumizi ya malipo ya madai kwa watoa huduma yamepungua kwa asilimia 34 kwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Billioni 587.7 kilicholipwa kwa watoa huduma kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Vilevile, matumizi ya uendeshaji wa Mfuko yameongezeka kutoka asilimia 74 ya matumizi mwaka 2023/24 hadi kufikia asilimia 83 ya matumizi mwaka 2024/25 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8**.

Jedwali Na. 8. Mwenendo wa Matumizi ya Fedha ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka 2023/24 na mwaka 2024/25.

MATUMIZI	MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2023/24			MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2024/25			ONGEZEKO/ PUNGUFU (%)
	Malengo (in '000) TZS)	Halisi (in '000) TZS)	%	Malengo (in '000) TZS)	Halisi (in '000) TZS)	%	
Malipo ya Madai	444,417,275	587,737,296	132%	432,000,000	438,083,6858*	101%	**-34%**
Matumizi ya kiutawala	70,493,489	52,408,512	74%	79,645,115	66,383,405	83%	**21%**
Miradi ya maendeleo	1,989,560	690,513	35%	143,176,867	1,744,07	1%	**60%**
Jumla	**516,900,324**	**640,836,321**	**124%**	**654,821,982**	**506,211,169**	**77%**	**-27%**

347. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya madai 55,817** yamechakatwa na jumla ya kiasi cha Shilingi Bilioni 438 sawa na asilimia 101 ya lengo kimelipwa. Aidha, kiasi kilicholipwa ni asilimia 91 ya madai yote yaliyowasilishwa na hivyo

kufanya madai yaliyokataliwa kuwa ni asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 22 ya madai yaliyokataliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Madai hayo yalichakatwa kwa wastani wa siku 58 ikilinganishwa na siku 66 kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Vilevile, asilimia 40.8 ya madai yalilipwa kwa vituo vya kutolea huduma vya Serikali na asilimia 59.2 yalilipwa kwa vituo vya kutolea huduma vya binafsi. Takwimu zinaonesha kuwa, fedha za NHIF kwa sasa zinachangia wastani wa asilimia 80 ya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

348. Mheshimiwa Spika, Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa **usajili wa vituo** vya kutolea huduma za afya ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Mfuko umesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 397 ambapo vituo 97 ni usajili wa mara ya kwanza, vituo 279 vilihuisha usajili na vituo 9 vilibadilishiwa hadhi, vituo 12 viliongeza huduma na kubadilisha umiliki. Aidha, usajili huu umefanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa na Mfuko kufikia 10,004 ikiwa asilimia 72 ni vituo vya Serikali, asilimia 20 ni vituo binafsi na asilimia 8 ni vituo vya madhehebu ya kidini.

349. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za matibabu nchini, Mfuko unatoa mikopo nafuu ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo, jumla ya vituo 431 vilivyokidhi vigezo vimenufaika na mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 50.3. Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, vituo 5 vimepatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi Millioni 449.2 ikiwa ni pungufu ya asilimia 89 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 2.6 kilichotolewa mwaka 2023/24 kipindi kama hicho. Aidha, kati ya mikopo iliyotolewa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Shilingi Billioni 428.2 sawa na asilimia 95 zilitolewa kwa vituo vinavyomilikiwa na Serikali na kiasi cha Shilingi Millioni 21. sawa na asilimia 5 Kituo cha mtu binafsi. Utaratibu huo umesaidia kujenga uwezo wa vituo katika kutoa huduma za afya kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

350. Mheshimiwa Spika, Mfuko umeendelea **kupambana na kudhibiti udanganyifu** kutoka kwa watoa huduma, waajiri binafsi, wanufaika

wa huduma na watumishi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko ulibaini kiasi cha Shilingi Bilioni 5.7 kinachotakiwa kurejeshwa kilitokana na madai yenye udanganyifu kutoka kwa watoa huduma. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kusitisha matumizi ya kadi za wanachama 983 wasiostahili na wanachama wanaotumia kadi zao kufanya udanganyifu na vituo vinne (4) vimesitishiwa mikataba ya huduma.

351. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza takwa la kisheria la kufanya **tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko**, kila baada ya miaka mitatu, mfuko unatekeleza takwa hilo kwa kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wake (actuarial valuation). Kwa kipindi cha kuishia Juni 2021. Matokeo na mapendekezo ya taarifa ya tathmini hiyo yametumika katika kufanya mapitio ya vifurushi vinavyotumiwa na wanachama binafsi pamoja na familia zao. Mnamo tarehe 17 Desemba 2024, Mfuko ulizindua vifurushi vipya viwili ambavyo ni Serengeti, Ngorongoro na kurejesha kifurushi cha Toto Afya Kadi (TAK). Kifurushi cha **Serengeti Afya** kina wigo mpana wa huduma za msingi, huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zaidi ya huduma 1,800 ambapo mchango unaanzia Shilingi 660,000 kwa mwaka kwa mtu mmoja. Kifurushi cha **Ngorongoro Afya** kina wigo mpana wa huduma za msingi, kibingwa na ubingwa bobezi, huduma zaidi ya 440 ambapo mchango unaanzia Shilingi 240,000 kwa mwaka kwa mtu mmoja na **Toto Afya Kadi (TAK)** ni kifurushi kwa ajili ya watoto chini ya umri wa miaka 17 wanaosajiliwa mmoja mmoja au kwa makundi kupitia shule. Kwa watoto wanaosajiliwa mmoja mmoja mchango kwa mwaka ni Shilingi 150,000 ambapo wanasubiri kwa miezi 3 kabla ya kuanza kunufaika na huduma. Michango ya watoto wanosajiliwa kwa makundi kupitia shule wanazosoma ni Shilingi 50,400 kwa mtoto mmoja. Watoto wanaosajiliwa kwa makundi, uanachama wao unaanza kwa pamoja na hakuna muda wa kusubiri ili kupata huduma. Aidha, wanachama wenye vifurushi vya Najali, Wekeza na Timiza wataendelea kupata huduma hadi muda wa uanachama wao utakapokoma na kisha kujiunga na vifurushi vipya vilivyopo.

352. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi kwenye Mfuko na kuhakikisha azma ya bima ya afya kwa wote inatimia, Mfuko

umefanya maboresho ya mifumo ya TEHAMA katika eneo la uandikishaji wa wanachama na uchakataji wa madai ambapo **Mfumo wa uandikishaji** umeboreshwa na kumwezesha mwanachama kujiandikisha na kujihudumia bila kulazimika kufika katika Ofisi za Mfuko. Mfumo huo unapatikana kupitia kiunganishi cha https://selfservice.nhif.or.tz. na **Mfumo wa Uchakataji Madai** umeongeza ufanisi kwa kuchakata madai kwa haraka kwa kutumia Akili Unde, hivyo kuharakisha malipo ya madai ya Watoa Huduma.

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)

353. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilianzishwa kwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219. Jukumu kuu la taasisi ni kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya maombi 1,113 ya usajili wa dawa za binadamu yalipokelewa, kati ya hayo maombi 1,005 sawa na asilimia 90 yalifanyiwa tathmini. Maombi 540 sawa na asilimia 54 ya maombi yaliyotathminiwa yaliidhinishwa na hivyo dawa husika kusajiliwa. Aidha, kulikuwa na jumla ya maombi 124 ya usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi 114 (asilimia 92) yalifanyiwa tathmini na maombi 83 (asilimia 92) yaliidhinishwa baada ya kukidhi vigezo. Pia, kulikuwa na maombi 390 ya usajili wa maeneo ya biashara zinazohusiana na dawa na vipukusi ambapo maombi 384 sawa na asilimia 94 yalifanyiwa tathmini na 374 kati yake sawa na asilimia 97 yalikidhi vigezo vya usajili na hivyo kupewa vibali vya biashara. Vilevile, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda na maeneo 6,708 ya biashara ya dawa na vipukusi ambapo maeneo 5,853 sawa na asilimia 87 yalisajiliwa.

354. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha **usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi**, jumla ya maombi 585 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi (vifaa tiba 379 na vitendanishi 206) yaliwasilishwa ambapo maombi 527 (vifaa tiba 341 na vitendanishi 186) sawa na asilimia 90 yalifanyiwa tathmini na maombi 193 (vifaa tiba 137 na vitendanishi 56) yaliidhinishwa. Aidha, maombi yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 273 ikilinganishwa na

maombi 254 yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2024. Vilele, Mamlaka ilipokea na kutathmini maombi 531 ya usajili wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba na vitendanishi ambapo maeneo 519 sawa na asilimia 98 yalikidhi vigezo na kusajiliwa. Maeneo yaliyotathminiwa ni ongezeko la maeneo 60 ikilinganishwa na maeneo 471 yaliyotathminiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji kupitia elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na hivyo kuongezeka kwa uelewa wa wafanyabiashara wa bidhaa husika.

355. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilikagua maeneo 492 yanayojihusisha na biashara za vifaa tiba na vitendanishi ambapo maeneo 478 sawa na asilimia 97 yalikidhi vigezo. Idadi ya maeneo ya biashara yaliyokidhi vigezo ni ongezeko la maeneo 61 sawa na asilimia 15 ikilinganishwa na maeneo 417 yaliyokidhi vigezo mwaka 2024. Ongezeko hili limechangiwa na uhamasishaji wa wadau kukidhi matakwa ya Sheria na kuimarika kwa shughuli za udhibiti.

356. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa bidhaa zinazodhibitiwa, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 6,574 ya kuingiza na 648 ya kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa, vipukusi, vifaa tiba na vitendanishi na kufanya jumla ya maombi yaliyopokelewa kuwa 7,222. Kati ya maombi hayo, jumla ya vibali 6,458 vilitolewa (5,853 ni vibali vya kuingiza nchini na 605 ni vibali vya kusafirisha nje ya nchi). Kati ya vibali vilivyotolewa, vibali 6,174 (5,803 vibali vya kuingiza nchini bidhaa na 371 ni vibali vya kusafirisha nje ya nchi) vilikaguliwa katika vituo vya forodha. Aidha, idadi ya vibali vilivyokaguliwa katika kipindi hiki ni ongezeko la vibali 518 ikilinganishwa na vibali 5,656 vilivyokaguliwa kipindi kama hiki mwaka wa fedha uliopita. Hii imetokana na kuongezeka kwa wakaguzi na hivyo kuimarika kwa shughuli za udhibiti katika vituo vya forodha.

357. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilifanya tathmini ya bidhaa za dawa, vifaa, vifaa tiba na vipukusi vilivyoko sokoni ili kujiridhisha na ubora wake ambapo jumla

ya sampuli 260 zilifanyiwa uchunguzi na kati ya hizo 252 sawa na asilimia 97 zilikidhi vigezo. Mafanikio hayo yanaashiria uwepo wa ubora na usalama wa bidhaa zilizopo katika soko zinazodhibitiwa na mamlaka. Aidha, Mamlaka imeendelea kulinda mipaka ya nchi kwa kuzuia uingizwaji wa bidhaa duni, bandia na ambazo hazijasajiliwa kwa kufanya doria na ukaguzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

358. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 elimu kwa umma ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi pamoja na kutangaza huduma za Mamlaka kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mihadhara 160, vipindi vya redio na runinga na matangazo mafupi ya redio na runinga. Mihadhara ya utoaji elimu ilifanyika kwa vikundi mbalimbali vya wananchi wakiwemo wazalishaji wa bidhaa, vijana, wanawake, wanafunzi na walimu kutoka Shule mbalimbali ambapo jumla ya washiriki 76,358 walifikiwa. Aidha, jumla ya wateja 9,535 walihudumiwa kupitia madawati ya huduma kwa wateja Makao Makuu na Ofisi za Kanda.

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

359. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Sura 177 yenye jukumu la kufanya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo, utoaji ushahidi wa kitaalam mahakamani na usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na nyumbani.

360. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kufanya uchunguzi wa kisayansi wa maabara wa sampuli na vielelezo nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli 133,852 kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara** ambazo zinajumuisha sampuli za sumu, dawa za kulevya, mauaji, majanga, ubakaji, utambuzi wa uhalali wa wazazi kwa mtoto na jinsi tawala, vyakula, dawa za binadamu na mifugo, dawa asili, maji, kemikali, maji taka, na bidhaa nyingine za viwandani. Sampuli zilizofanyiwa

uchunguzi ni 132,737 sawa na asilimia 99.3 ya sampuli zilizopokelewa na asilimia 63.7 ya lengo la mwaka la kuchunguza sampuli 208,322.

361. Mheshimiwa Spika, Sampuli zilizofanyiwa uchunguzi zilipungua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na sampuli 141,683 zilizochunguzwa kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024. **Kupungua kwa sampuli zilizochunguzwa kunatokana na juhudi za Serikali za kuzuia uhalifu na biashara haramu ya madawa kulevya nchini**. Matokeo ya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli na vielelezo umeiwezesha Wizara kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuchangia katika kulinda afya za wananchi na mazingira pamoja na utoaji wa haki katika vyombo vya maamuzi kwa kutoa ushahidi wa kitaalam katika mahakama mbalimbali nchini.

362. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ubora wa matokeo ya uchunguzi yanayokubalika kitaifa na kimataifa, Mamlaka imeendelea kutekeleza viwango vya Mifumo ya Ubora ya Maabara (ISO 17025:2017) na kufanikiwa kuendelea kuwa na vyeti vya ithibati vya Maabara za Vinasaba, Chakula, Mazingira, Toksikolojia na Maabara zilizopo ofisi ya Kanda ya Ziwa.

363. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka iliendelea na usajili wa wadau 1,295 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali sawa na asilimia 86.3 ya lengo la kusajili wadau 1,500 kwa mwaka. Wadau waliosajiliwa waliongezeka kwa asilimia 32.9 ikilinganishwa na Wadau 974 waliosajiliwa kwa kipindi kama hicho katika mwaka 2024. Lengo la kusajili wadau hawa ni kuendelea na juhudi za kulinda afya, mazingira na usalama wa nchi dhidi ya kemikali hatarishi na bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya au silaha za kemikali. Pia, Mamlaka ilitoa mafunzo juu ya usafirishaji salama wa Kemikali nchini kwa wadau wa kemikali 7,969 sawa na asilimia 128.5 ya lengo la kuelimisha wadau 6,200 kwa mwaka. Mafunzo hayo yamesaidia kuwapa uelewa wa namna bora ya kujilinda, kulinda watu wengine pamoja na kulinda mazingira wakati wa usafirishaji wa kemikali hizo.

364. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga Ofisi na Maabara pamoja na ununuzi wa vifaa na mitambo ya maabara. Katika kipindi hiki Mamlaka imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika Kanda ya Mashariki Dar es Salaam na Kanda ya Kusini Mtwara. Aidha, Mamlaka imeendelea kukamilisha mipango ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika mipaka ya Mtukula, Kabanga, Namanga na Holili.

365. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Mamlaka inakuwa na Vifaa vya kutosha kulingana na mahitaji na teknolojia ya kisasa, Wizara imeiwezesha Mamlaka kununua mitambo mikubwa minne (4) aina ya *Fourier Transform Infrared Spectrometer (FTIR), Inductively Coupled Plasma Optical Emission spectrometer (ICP-OES), Portable Gas Chromatography, Gas Chromatography* na mitambo midogo 20. Mitambo hii ya maabara imeongeza ufanisi na kasi ya utoaji wa matokeo ya uchunguzi wa kimaabara kwa wakati kwani baadhi ya mitambo imesimikwa kwenye Ofisi za Kanda kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi na hivyo kutolazimika kufuata huduma Makao Makuu.

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

366. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya Mwaka 1979 ikiwa na jukumu la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali za afya hapa nchini, Taasisi imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa watafiti mbalimbali waliopo katika Taasisi za tafiti ndani na nje ya nchi, watalaam kutoka katika vyuo vikuu na watu wengine wenye nia ya kufanya utafiti katika eneo la afya. Taasisi kupitia Kamati ya Uratibu wa Tafiti za Afya imekuwa ikipitia maombi yote yanayowasilishwa, baada ya kuyapitia na kujiridhisha, yale yanayokidhi vigezo hupatiwa kibali (Ethical Clearance) kwa ajili ya kuanza kufanya tafiti husika. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Taasisi ilitoa vibali 519 kati ya maombi 534 yaliyowasilishwa sawa na asilimia 97.

367. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kufanya tafiti mbalimbali na kutumia matokeo ya tafiti hizo kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Taasisi imetekeleza miradi ya tafiti 133 kati ya 150 iliyopangwa kwa mwaka 2024/25 ambayo ni sawa na asilimia 89. Aidha, tafiti hizo zililenga magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, uimarishaji wa mifumo ya afya na pia kuelewa viashiria vya kijamii na mazingira pamoja na Tiba Asili. Aidha, Taasisi inaendelea na **Utafiti wa kufuatilia hali ya maambukizi ya Malaria** nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika mikoa 13 ya Tanzania Bara (MSMT) ulioanza mwaka 2020. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mabadiliko ya vimelea vya malaria ili kubaini kama mbinu tunazotumia kupambana na ugonjwa huu zinafanya kazi ipasavyo, kufuatilia ubora na uwezo wa dawa za kutibu ugonjwa wa malaria na ufanisi wa vipimo vya haraka vya kupima malaria (mRDTs). Vilevile, Taasisi imefanya **majaribio ya dawa mpya** zitakazofupisha muda wa matibabu ya kifua kikuu kutoka miezi sita (6) hadi minne (4). Matokeo ya awali ya tafiti hizi yameonesha kuwa dawa mpya zina uwezo wa kufupisha muda wa matibabu toka miezi sita hadi miezi minne kwa wagonjwa wasio na kifua kikuu sugu.

368. Mheshimiwa Spika, Taasisi imetekeleza **utafiti wa kuangalia hali ya afya baada ya matibabu ya kifua kikuu.** Matokeo yameonesha asilimia 70 ya wagonjwa wanaomaliza dawa za kifua kikuu mapafu yao yanakuwa hayafanyi kazi vizuri. Utafiti zaidi unaendelea kuangalia madhara mengineyo ya kiafya na kugundua mbinu za kuboresha afya ya mapafu baada ya kumaliza dawa za kifua kikuu ili kuboresha huduma kwa wagonjwa wenye kifua kikuu na waliomaliza tiba hiyo.

369. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kufanya **tafiti katika eneo la tiba asili na tiba mbadala** ambapo dawa nne (4) za tiba asili za NIMREGENIN kwa ajili ya kutibu tezi dume, TANGESHA kwa ajili ya kutibu seli mundu, PERSIVIN kwa ajili ya kutibu tezi dume na WARBUGISTAT kwa ajili ya kutibu magonjwa nyemelezi zinaendelea kufanyiwa uchunguzi wa usalama. Matokeo ya awali ya utafiti huu yameonesha kuwa dawa hizi ni salama katika hatua za majaribio kwa wanyama. Kuhusu Dawa ya tiba asili ya NIMREGENIN imeonekana

kuwa na nguvu ya kupunguza uvimbe unaotokana na saratani na inatoa mchango mkubwa katika kupambana na magonjwa ya saratani nchini. Hivyo, Wizara imeendelea na utafiti wa kuangalia ikiwa dawa ya NIMREGENIN inaweza kusaidia tiba ya saratani za Tezi Dume, saratani ya shingo ya kizazi na saratani ya ubongo.

370. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea na **utafiti wa kuzuia ugonjwa wa Kisukari** ambapo tafiti hizi zimeonesha kuwa wagonjwa wenye virusi vya UKIMWI wapo katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa wa kisukari. Aidha, Taasisi inafanya utafiti wa jaribio nasibu la awamu ya tatu ili kuangalia ikiwa matumizi ya dawa ya *Metformin* kwa watu wenye virusi vya UKIMWI wenye dalili za awali sana za kisukari yanaweza kupunguza uwezekano wa watu hawa kupata ugonjwa wa kisukari. Jaribio hilo linafanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam. Washiriki 1,634 wameandikishwa na ufuatiliaji utafanyika kwa miaka minne (4) ili kuweza kujua ikiwa dawa hii inasaidia kukinga watu kupata ugonjwa wa kisukari.

371. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa kushirikiana na wadau imeendelea na utafiti wa kupunguza magonjwa nyemelezi yanayotokana na maambukizi ya fangasi ya uti wa mgongo (Cryptococcal Meningitis). Kupitia matokeo chanya ya utafiti huu, Shirika la Afya Duniani na Wizara zimeboresha Miongozo ya Utambuzi na matibabu ya magonjwa nyemelezi ya maambukizi ya uti wa mgongo.

372. Mheshimiwa Spika, Taasisi inaendelea kufanya **utafiti wa miaka mitano (2021 mpaka 2025)** katika Mikoa ya Mbeya na Songwe ili kutathmini kama asilimia 2 (kwa kipimo cha OV-16 ELISA) inafaa kuwa kiwango cha juu cha maambukizi ya ugonjwa wa Usubi. Matokeo ya utafiti wa awali yanaonesha kuwa maambukizi yapo chini ya asilimia 2. Kama matokeo ya tathmini ya mwisho wa mwaka 2025 yatahakiki kiwango hicho cha maambukizi, utafiti huu utasaidia katika kufanya maamuzi ya kusitisha ugawaji wa Kingatiba katika maeneo yenye maambukizi na kuokoa pesa inayotumika katika kutekeleza afua hii.

Utekelezaji wa Majukumu ya Bodi za Usajili na Mabaraza ya Kitaaluma

373. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya. Katika kutekeleza hilo, Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili wa Vituo ziliundwa kwa mujibu wa Sheria kwa ajili ya kusimamia maadili ya Kitaaluma, kusajili wataalam na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Wataalam wa Kada husika.

374. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jumla ya Mabaraza ya Kitaaluma nane (8) na Bodi za Usajili mbili (2). Mabaraza na Bodi hizo ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Optometria, Baraza la Wataalam wa Radiolojia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi.

375. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mabaraza ya Kitaaluma yalisajili jumla ya watalaam **31,315**, usajili wa Maduka ya Dawa **509**, usajili wa watarajali **3,076**, Mashauri ya Kinidhamu yaliyofanyiwa kazi ni **135**, mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) yametolewa kwa watalaam **84,947** na ukaguzi wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya **3,483.** Aidha, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma yametekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Baraza la Uuuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)

377. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Jumla ya Wauguzi na Wakunga **4506** wamesajiliwa, sawa na asilimia 90 ikilinganishwa na lengo la kusajili wataalam 5,000. Kati yao, Wauguzi Wasajiliwa 4,399 (14) wataalam wa dawa ya usingizi na ganzi tiba, 107 wameorodheshwa (EN). Hili ni ongezeko la wataalam 2,327 ikilinganishwa na wataalam 2,179 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Idadi hiyo inafanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi sasa kufikia 57,200. Aidha, Wauguzi na Wakunga Watarajali 745 wamepewa usajili wa awali ikilinganishwa na watarajali 576 katika kipindi kama hicho 2023/24. Watarajali wanaendelea na

mafunzo ya vitendo katika Vituo 31 zikiwemo Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda (4) na Hospitali za Rufaa za Mikoa 27.

378. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Baraza la Uuguzi na Ukunga lilipokea maombi manne (4) ya kuanzisha huduma binafsi za Uuguzi na Ukunga katika Mikoa ya Dar es Salaam na Tabora. Vituo vyote vilikaguliwa na kuonekana kuwa vimekidhi vigezo na hivyo kupewa vibali. Hii inafanya jumla ya *Nursing and Maternity Homes and Services* zilizosajiliwa kutoa huduma kufikia 94 kwa nchi nzima.

379. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025, Wauguzi na Wakunga 37,405 wamefanya mafunzo ya kujiendeleza (CPD) kwa njia tofauti tofauti ili kujengewa uwezo wa kutoa huduma, na uwezo wa kufanya tafiti mbalimbali. Idadi hii imeongezeka ikilinganishwa na Wauguzi na Wakunga 32,643 katika kipindi cha 2023/24. Ongezeko hili limetokana na elimu na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa wataalam kujiendeleza kwa ajili ya kujengewa uwezo wa kutoa huduma bora za uuguzi na ukunga pamoja na kukidhi vigezo vya kuhuisha leseni za kutolea huduma. Aidha, jumla ya moduli 42 za mafunzo ya kujiendeleza zilipokelewa na kuhakikiwa na kupata ithibati ya Baraza. Moduli zililenga katika maeneo ya afya ya mama na mtoto, magonjwa ya mlipuko na yasiyoambukiza, chakula na lishe, kukinga na kudhibiti maambukizi (Infection Prevention and Control), huduma za upasuaji na utoaji salama wa dawa za ganzi tiba, afya ya akili, huduma za wagonjwa mahututi (Critical Care) na mbinu za ufundishaji (Teaching Methodology).

380. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha Wataalam wa kada ya Uuguzi na Ukunga wanazingatia maadili, sheria na miongozo ya taaluma yao. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya mashauri saba (7) ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yalipokelewa. Mashauri haya yako katika hatua mbalimbali za uchunguzi na kisha hatua stahiki kuchukuliwa kulingana na Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010. Aidha, idadi ya

mashauri ya ukiukwaji wa maadili imepungua ikilinganishwa na mashauri 11 yaliyopokelewa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24.

Baraza la Madaktari Tanganyika

381. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia usajili, utendaji na maadili ya watalaam pamoja na Taaluma ya Udaktari kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza la Madaktari Tanganyika limesajili jumla ya watalaam 3,794 kati ya 6,610 waliotarajiwa kusajiliwa sawa na asilimia 57. Hii ni pungufu ya wataalam 2,414 ikilinganishwa na wataalam waliosajili katika kipindi kama hicho mwaka 2024 ambapo walisajiliwa watalaam 6,208. Hadi kufika Machi 2025, Jumla ya wataalam waliosajiliwa imefika 42,937. Aidha, jumla ya watalaam 674 wamepatiwa leseni kwa mara ya kwanza na watalaam 5,621 wamehuisha leseni zao na hivyo kufanya jumla ya watalaam waliopatiwa Leseni na kuhuisha Leseni kufikia 18,700.

382. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu lake la usimamizi wa mitihani ya watarajali Baraza huandaa mitihani kabla watarajali hawajaanza mafunzo na baada ya kumaliza mafunzo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watalaam 1,193 walifanya mtihani wa kabla ya mafunzo ya utarajali, kati yao watarajali wa Udaktari walikuwa 1,053, Udaktari wa Meno 58, Fiziotherapia 43 na wataalam wa lishe na tiba ya chakula 39. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya watarajali 1,278 waliomba na kukidhi sifa za kufanya mtihani wa baada ya mafunzo ya utarajali kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya waliofanya mtihani, watarajali wa Udaktari ni 1,209, Udaktari wa Meno 64, Fiziotherapia wane (4) na Mtaalam wa tiba kwa vitendo mmoja (1).

383. Mheshimiwa Spika, Baraza linatambua usajili wa mafunzo ya *fellowship* kama mbadala wa Shahada ya Uzamili (MMed). Mafunzo haya yalianza kutambulika rasmi nchini mwaka 2020 ingawa yalikuwa yakitolewa katika nchi nyingine tangu mwaka 2012. Mafunzo ya *fellowship* yamejikita zaidi katika njia ya vitendo na yanalinganishwa

na Shahada ya Uzamili inayotolewa katika vyuo vikuu. Mafunzo hayo yamegawanyika katika makundi ya Watalaam wanaopata usajili wa shahada ya kwanza ya uzamili na kutambuliwa kama Bingwa na Watalaam wanaopata Shahada ya pili ya Uzamili na kutambuliwa Bingwa bobezi. Aidha, Baraza limeandaa miongozo tisa ya kupima na kutathmini sifa za ziada kwa njia ya *fellowship* ili kuhakikisha ubora na ulinganifu wa mafunzo hayo. Hadi Machi 2025, jumla ya watalaam 59 wamekamilisha mafunzo ya *fellowship* na kutambuliwa kuwa na sifa za ziada katika taaluma zao.

384. Mheshimiwa Spika, jumla ya watoa mafunzo endelevu 82 walisajiliwa ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2024/25 ambapo watoa mafunzo 37 walisajiliwa. Watoa mafunzo hao wanahusisha Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za wilaya, Vituo vya afya, Zahanati, Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Taasisi za Serikali, Taasisi zisizo za Serikali na Makampuni. Aidha, jumla ya kozi 515 zilipewa ithibati ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2024/25 ambapo kozi za mafunzo endelevu 292 zilipatiwa ithibati. Vilevile, jumla ya watalaam 19,600 walifanya mafunzo mbalimbali ya kitaaluma ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2024/25 ambapo jumla ya watalaam 16,116 walifanya mafunzo endelevu ya kitaaluma.

385. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ambapo jumla ya malalamiko 22 yalipokelewa. Kati ya hayo Malalamiko 19 yalichunguzwa na Kamati ya Uchunguzi wa Mashauri ya Kitaaluma na mashauri 10 yalisikilizwa na Baraza dhidi ya wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma zao. Maamuzi yaliyotolewa ni pamoja na walalamikiwa wawili (2) kupewa onyo, watano (5) kufungiwa leseni za kutoa huduma kwa muda wa miezi sita (6) na kuelekezwa kwenda kwenye mafunzo ya lazima ya weledi kwa kipindi cha miezi mitatu (3) wakiwa chini ya uangalizi kwa kipindi cha miaka miwili (2). Mlalamikiwa mmoja (1) amefungiwa Leseni kwa kipindi cha miezi tisa (9) na mmoja (1) kwa kipindi cha miaka miwili (2). Walalamikiwa wanne (4) hawakukutwa na hatia yoyote na kuachiwa huru.

Baraza la Famasi

386. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limesajili jumla ya wafamasia 148, fundi sanifu dawa 820 wameandikishwa na fundi sanifu dawa wasaidizi 75 wameorodheshwa na kufikisha jumla ya wataalam 14,322. Kati yao, wafamasia ni 3,937; fundi sanifu dawa ni 9,252; fundi sanifu dawa wasaidizi ni 1,133 wanaotambuliwa. Aidha, asilimia 70 ya watalaam wamehuisha na kuwa na leseni hai za utendaji. Katika kuhakikisha kada inatoa watoa huduma wenye vigezo, Baraza limefanikiwa kusimamia jumla ya watarajali 456 katika vituo 36 vya kutolea huduma za afya.

387. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, maduka ya dawa 509 (rejareja 412, Jumla 35 na jumla na rejareja 53 na maghala 09) yamesajiliwa kutoa huduma ya dawa nchini, hivyo kufanya jumla ya maduka ya biashara ya Famasi kuwa 3,345. Vilevile, jumla ya watalaam 10,026 walishiriki mafunzo endelevu (CPD) katika maeneo mbalimbali ambapo Wafamasia 3,072, Fundi Sanifu Dawa 6,506 na Fundi Sanifu Dawa Wasaidizi 448.

388. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya mashauri ya kinidhamu 99 yalipokelewa, kati ya hayo malalamiko 25 yanaendelea na hatua ya uchunguzi. Malalamiko 74 uchunguzi wake ulikamilika na maamuzi yaliyotolewa ni pamoja na walalamikiwa 31 kupewa onyo, tisa (9) walifungiwa Leseni za kutoa huduma katika maduka ya famasi kwa kipindi cha miezi 12, mmoja (1) alitakiwa kulipa fidia ya hasara aliyosababisha, mmoja (1) aliongezewa muda wa mafunzo kwa vitendo na watalaam 31 hawakukutwa na hatia.

Baraza la Wataalam wa Radiolojia

389. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza lilipitia maombi ya usajili wa wataalam wa Radiolojia kwa kada mbalimbali. Aidha, Wataalam waliokidhi vigezo walisajiliwa kulingana na usajili walioomba. Usajili wa matazamio (wataalam 176),

usajili kamili (161), usajili wa muda (Mtaalam mmoja), uandikishaji (5) na uorodheshaji (5) na kufanya idadi ya wataalam waliosajiliwa kwa kipindi hicho kufikia 344. Idadi hiyo inapelekea jumla ya wataalam wote waliosajiliwa na Baraza tangu kuanza usajili mwaka 2011 kufikia 1,840. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya wataalam 810 kati ya wataalam 1,400 walihuisha leseni zao sawa na asilimia 58 ya waliotegemewa kuhuisha leseni kwa mwaka 2023/24.

390. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kusimamia watarajali wa kada za Radiolojia nchini ambapo jumla ya watarajali 49 walipewa mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili na kupangiwa vituo vya utarajali. Aidha, mafunzo juu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili (HPRS) yameendelea kutolewa kwa wataalam wa radiolojia nchini. Jumla ya wataalam 1,450 kati ya 1,840 sawa na asilimia 78 wameweza kutumia mfumo kujisajili na kuhuisha leseni. Pia, jumla ya wahitimu 49 wa ngazi ya shahada wameweza kuchagua vituo vya utarajali kwa njia ya mfumo huo.

391. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilitoa mafunzo kuhusu sheria, kanuni, miiko na maadili kwa wahitimu 307 wa shahada, na stashahada katika fani za Radiolojia nchini. Aidha, Baraza lilishiriki kuandaa Kongamano la Siku ya Radiografia nchini lililofanyika Arusha na Dar es Salaam ambapo jumla ya Wataalam 750 walipatiwa mafunzo mbalimbali.

392. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilipokea jumla ya mashauri matatu (3) ya uvunjifu wa miiko na maadili ya kitaaluma. Mashauri yote yapo katika hatua za uchunguzi, yatakapokamilika hatua stahiki zitachukuliwa kulingana na sheria, kanuni, miongozo ya miiko na maadili ya taaluma.

Baraza la Wataalam wa Macho (Optometria)

393. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limesajili jumla ya wataalam 40 kwa usajili wa kudumu na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa usajili wa kudumu kufikia 453.

394. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wataalam 420 walipatiwa elimu kuhusu mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) ya fani ya Optometria katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Baraza lilifanikiwa kufanya kikao na wataalam wa Optometria waliopewa usajili wa kudumu na usajili wa awali mkoani Dodoma ambapo jumla ya wataalam 80 walikumbushwa juu ya kuzingatia maadili, kutoa huduma bora, Sheria ya Optometria, matumizi ya Mfumo wa usajili wa wataalam (HPRS) ili kuongeza ufanisi na kuboresha huduma za macho. Katika kuhakikisha kada inatoa watoa huduma wenye vigezo, Baraza limefanikiwa kusimamia jumla ya watarajali watano (5) katika vituo vya kutolea huduma.

Baraza la Wataalam wa Maabara ya Afya

395. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 1,221 wapya wa maabara wamesajiliwa kwa usajili wa kudumu na kuandikishwa, hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia 16,655. Aidha, katika kipindi hiki, wataalam 5,981 wamehuisha leseni zao na katika kipindi cha mwaka 2024/25, wataalam 6,862 wamehuisha leseni zao. Hivyo kufanya Wataalam wenye leseni hai kufika 9,596 hadi Machi 2025.

396. Mheshimiwa Spika, Baraza lilisimamia mitihani ya usajili kwa ngazi zote (Astashahada, Stashahada na Shahada) ambapo jumla ya maombi 1,299 yalipokelewa kati yao wataalam wa Astashahada walikuwa 108; Stashahada 875 na Shahada 316. Ufaulu wa jumla ulikuwa asilimia 60 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 54 mwaka 2023/24. Baraza limeongeza kituo kimoja (1) cha mafunzo ya utarajali cha Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara na kufanya jumla ya vituo vinavyotambuliwa na Baraza kuwa 25. Vilevile, Baraza lilitoa mafunzo endelevu (CPD) kwa wataalam wa Maabara 10,954.

397. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limefanya ukaguzi katika vituo 214 vya Maabara pamoja na vyuo katika Mikoa ya Dodoma, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Manyara, Mwanza, Arusha, Iringa, Kagera, Mara na Singida. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kuangalia viwango vya ubora katika utoaji wa

huduma kwenye vituo na utoaji wa mafunzo kwenye vyuo. Zoezi hili lilienda sambamba na utoaji wa elimu kuhusiana na Sheria, Kanuni na mwongozo wa mafunzo endelevu ya taaluma. Aidha, kuna ongezeko la uhuishaji wa leseni na kusoma mafunzo endelevu ya taaluma (CPD) kwa wataalam 1,558 waliopata alama za CPD Mwaka 2023/24 hadi wataalam 10,954 kufikia Machi, 2025. Katika kipindi hiki, Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ambapo jumla ya mashauri manne (4) yalifunguliwa, kati ya hayo mashauri matatu (3) yanaendelea na uchunguzi na shauri moja (1) limefungwa.

398. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limesajili watarajali 398 ambao wamepangwa katika vituo vya mafunzo 25. Watarajali 376 walianza mafunzo Mwezi Novemba, 2024 na Watarajali 22 walianza mafunzo Mwezi Aprili, 2025.

Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira

399. Mheshimiwa Spika katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, idadi ya wataalam wapya waliosajiliwa na Baraza la Afya Mazingira ni 448 ikilinganishwa na wataalam 382 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa kufikia 4,997. Kati ya wataalam 4,997 waliosajiliwa, wenye usajili kamili ni 2,057, Usajili wa kuorodheshwa 2,215, Usajili wa kuandikishwa 581 na Usajili wa Muda 144.

400. Mheshimiwa Spika, Baraza limeratibu mafunzo ya utarajali ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watarajali 145 wanaendelea na mafunzo katika mikoa 25 ya Tanzania Bara na Vyuo Sita (6) vinavyotoa taaluma ya Afya Mazingira Ngazi ya Stashahada na Watarajali 164 wamehitimu mafunzo hayo mwezi Oktoba, 2024 ikiwa ni ongezeko la wahitimu 55 kutoka mwaka 2024. Aidha, Baraza limeendelea kufanya ufuatiliaji wa usajili, uhuishaji wa leseni na watarajali katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

401. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha Wataalam wa kada ya Afya Mazingira wanazingatia maadili, sheria na

miongozo ya taaluma yao. Katika kipindi hicho, jumla ya wataalam 670 wa shahada na stashahada ya Afya Mazingira walipatiwa mafunzo maalum kuhusu sheria, kanuni, miiko na maadili ya taaluma. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hapakuwa na taaarifa za uvunjifu wa maadili iliyowasilishwa katika Ofisi ya Msajili.

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

402. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wataalam (waganga na wasaidizi wa tiba asili na tiba mbadala na wauza dawa za asili) 6,713 wamesajiliwa, sawa na asilimia 149 ya lengo la kusajili wataalam 4,500 kwa mwaka, na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi sasa kufikia 59,878. Kati ya wataalam 6,358 waliosajiliwa, wataalam 4,880 walipatiwa usajili wa awali na 1,468 usajili wa kudumu. Aidha, Baraza limesajili vituo vya tiba asili 273 na kufanya jumla ya vituo kuwa 2,108 hadi Machi 2025.

403. Mheshimiwa Spika, Baraza lilitekeleza zoezi la ukaguzi wa maduka ya kuuza dawa za asili, vituo vya kutolea huduma katika mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma. Dhumuni kuu lilikuwa ni kukagua ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi na kutoa mwongozo wa uboreshaji wa huduma hizo. Ukaguzi huu ulifanyika katika maduka 165 ya kuuza dawa za asili na vituo 57 vya kutolea huduma. Aidha, wauzaji wa maduka ya dawa asili pamoja na maduka ambayo hayakuwa na leseni walielimishwa na kuwasajili papo hapo.

404. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ambapo jumla ya malalamiko manne (4) yalipokelewa. Kati ya hayo uchunguzi wa malalamiko mawili (2) umekamilika na hatua stahiki zimechukuliwa.

Bodi ya Maabara Binafsi za Afya

405. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, idadi ya vituo vilivyosajiliwa na Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ni 317

ikilinganishwa na vituo 238 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 sawa na ongezeko la vituo 79, hivyo kufanya jumla ya Maabara Binafsi nchini kufikia 4,353. Kati ya hizo, maabara zinazojitegemea ni 1,555 na zilizojishikiza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ni 2,798.

406. Mheshimiwa Spika, Bodi imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa huduma na kutoa elimu ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayotumika katika usimamizi na uendeshaji wa huduma zitolewazo kwenye maabara binafsi za afya 844 katika mikoa nane (8) ambayo ni Morogoro, Mbeya, Katavi, Rukwa, Songwe, Geita, Mwanza na Arusha. Kati ya hizo, maabara 676 sawa na asilimia 80 zilikidhi vigezo.

Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

407. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025 Bodi ilikuwa imesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 3,483 kati ya vituo hivyo vituo vinavyofanya kazi ni 3,328, vilivyofungwa moja kwa moja vituo 36 na vituo 119 vimefungwa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, katika vituo vinavyofanya kazi Hospitali ni 224, vituo vya afya 309, Zahanati 1,954, Kliniki 402, *Polyclinics* 395, Kliniki za kuchuja damu 22 na vituo vya uchunguzi 22.

408. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya maombi 339 ya vituo binafsi yaliwasilishwa, kati ya hayo maombi 204 yalikuwa maombi ya vituo vipya, maombi 49 yalikuwa ya vituo vinavyoomba kupandishwa daraja na maombi mengineyo vituo 86. Kati ya maombi hayo, vituo 262 vilisajiliwa (Kliniki 23, *Polyclinics* 38, Hospitali ngazi ya Mkoa 10, Hospitali ngazi ya Kanda tatu (3), ngazi ya Wilaya tisa (9), vituo vya afya 19 na Zahanati 159 na kituo cha Uchunguzi kimoja (1), sawa na asilimia 77 ya maombi yote.

409. Mheshimiwa Spika, Bodi iliendelea na zoezi la ukaguzi wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam ambapo jumla ya vituo 523 vilikaguliwa ikilinganishwa na vituo 272 vilivyokaguliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024 ikiwa ni

ongezeko la vituo 251. Kati ya vituo hivyo, vituo 495 sawa na asilimia 95 vilikidhi vigezo vya uendeshaji wa vituo.

SEHEMU YA V: VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26.

410. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mapinduzi ya Sekta ya Afya yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya sita, Wizara imeainisha Vipaumbele kumi (10) vitakavyotekelezwa kwa mwaka 2025/26 ambavyo ni:-

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe;
ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa;
iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;
iv. Kuendelea kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa maeneo ya kimkakati;
v. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga;
vi. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;
vii. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini;
viii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;
ix. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko; na
x. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

411. Mheshimiwa Spika, Kiasi cha **Shilingi Trilioni moja, Bilioni mia sita kumi na nane, milioni mia moja tisini na moja, laki mbili na elfu thelathini na tano (1,618,191,235,000.00)** kimekadiriwa kutumika kutekeleza vipaumbele hivyo na afua mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 166.01 zitatumika kutekeleza afua zifuatazo:

a. Kuendelea kuimarisha usimamizi katika Mikoa 20 na kuanzisha vituo vya Operesheni ya Matukio ya Dharura za Afya (PHEOCs) katika mikoa sita (6) ya Simiyu, Geita, Pwani**, Njombe, Singida** na Shinyanga kwa ajili ya kuratibu, kujiandaa, kukabiliana na dharura za afya ikiwemo milipuko ya magonjwa;

b. Kuendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha jamii kuhusu ulaji unaofaa, kufanya mazoezi, kuzingatia lishe bora kwa watu wa rika zote, matumizi sahihi ya sukari, chumvi, mafuta, athari zitokanazo na matumizi ya tumbaku, pombe ili kuzuia na kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza;

c. Kukamilisha uanzishwaji wa Programu ya Taifa wa Lishe nchini;

d. Kuendelea kuimarisha huduma za afya mipakani kwa kujenga Miundombinu ya kuwatenga wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza katika mipaka 16 na ununuzi wa magari matano (5), Ambulance boat tatu (3) na vipima joto tembezi (Walkthrough thermoscanners) 28;

e. Kuendelea kutekeleza Programu ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Serikali kwa kuwajengea uwezo Wahudumu 28,000 kutoka Mikoa;

f. Kuendelea kuimarisha huduma za chanjo kwa kuwafikia Watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wasichana na mama wajawazito.

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 309.51 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-

a. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA ikiwemo matumizi ya akili mnemba (Artificial Intelligence) ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kuunganisha mifumo iweze kusomana, kubadilishana taarifa na kupunguza gharama za huduma za afya nchini;

b. Kuhuisha na kuzindua Sera ya Afya pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter);

c. Kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Afya ya Jamii (National Public Health Institute);

d. Kuimarisha Hospitali ya Benjamin Mkapa ili kuwa na hadhi ya Hospitali ya Taifa;

e. Kuanzisha kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya magonjwa ya damu na uloto katika hospitali ya Benjamin Mkapa;

f. Kuanzisha kituo cha kimataifa cha upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Kituo hicho kitakuwa ni kituo kikubwa na kitaongoza katika ukanda wa kusini mwa jangwa la sahara;

g. Kuzitangaza na kuzipa hadhi ya kuwa taasisi Hospitali za Afya ya Akili Mirembe na Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya;

h. Kuimarisha ufuatiliaji, uratibu na udhibiti wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Antimicrobial Resistance) na kusimamia uingizaji na matumizi sahihi ya Antibiotics nchini;

i. Kuongeza kasi ya matumizi ya Tiba Mtandao (Telemedicine) ili kusaidia utoaji wa huduma za ushauri, ubingwa na ubingwa bobezi kwa maeneo yasiyo na wataalam hao;

j. Kuweka mazingira wezeshi ya viwanda vya ndani vya kuzalisha bidhaa za afya ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hizo kwa urahisi na unafuu wakati wote;

k. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya (dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi) kwa kuboresha mifumo ya maoteo, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na bidhaa nyingine katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya;

l. Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua za kukabiliana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Anti-Microbial Resistance);

m. Kuwezesha Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa kujiunga katika mchakato wa kupata ithibati ya kimataifa hivyo kuongeza viwango vya ubora wa huduma na kukuza utalii wa tiba nchini;

n. Kuongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa zenye uwezo wa kutoa huduma za ubingwa muhimu nane (8) kutoka hospitali moja (1) hadi kufikia tisa (9). Huduma hizo ni Magonjwa ya ndani, Magonjwa ya watoto, Magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, huduma za upasuaji, huduma za dawa za usingizi na ganzi, upasuaji wa mifupa, radiolojia na Magonjwa ya dharura; na

o. Kuwezesha upatikanaji wa huduma za mama mwambata na matumizi ya chati ya uchungu iliyoboreshwa katika ngazi zote za kutolea huduma za kujifungua kwa akina mama wajawazito.

iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 49.80 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya Sera yasiyotarajiwa kutoka kwa nchi za magharibi; na

b. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote nchini kwa kuanza kutoa kadi za Bima ya Afya kwa makundi mbalimbali.

iv. Kuendelea kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa maeneo ya kimkakati, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 4.46 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo Saratani na afya ya akili;
b. Magonjwa ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko;
c. Usugu wa vimelea dhidi ya dawa; na
d. Dawa za tiba asili na tiba mbadala.

v. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 76.57 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuendelea na ununuzi na usambazaji wa dawa muhimu za uzazi salama (Magnesium sulphate, Oxytocin, FeFo na SP) pamoja na dawa za uzazi wa mpango, dawa kinga za minyoo, dawa za kuongeza damu, dawa za Malaria, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi;

b. Kuimarisha upatikanaji wa dawa ya vidonge myenyuko vya amoxycillin, ORS/zinc kwa ajili ya kutibu nimonia na kuhara kwa watoto, dawa za Surfactant na vifaa vya kusaidia upumuaji (CPAP) ili kusaidia changamoto za upumuaji kwa watoto waliozaliwa kabla ya wakati na waliozaliwa na uzito pungufu; na

c. Kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Unit - NCU) na waliozaliwa na uzito pungufu.

vi. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 80.38 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa utaratibu wa Seti kwa wataalam wa ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi na kufadhili mafunzo ya kada za kati za kimkakati;

b. Kuendelea kutoa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya vya umma; na

c. Kusimamia ubora wa mafunzo katika vyuo vya umma na binafsi.

vii. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini, ili kutekeleza afua hizi kiasi cha Shilingi Bilioni 123.93 kimetengwa: -

a. Kuendelea kutoa huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa pamoja na kuanzisha na kuimarisha huduma mpya kulingana na mahitaji zikiwemo**:**

- Upandikizaji wa ini katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kampasi ya Upanga na Kuanzisha huduma bobezi za mfumo wa mkojo na uzazi kwa wanaume (Uro-andrology) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kampasi ya Mloganzila.

- Kuanzisha upasuaji na ubadilishaji wa mabega na viwiko (Shoulder and Elbow Replacement) katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili.

- Kuendelea kutoa huduma ya upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo, nyonga na magoti kwa kutumia mfumo wa akili mnemba katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili MOI.

- Kuanzisha huduma ya matibabu ya wagonjwa waliopata kiharusi na mishipa ya damu ndani ya ubongo bila kufungua fuvu

(Interventional Neuro-radiology) katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

- Kuanzisha huduma sita za kibingwa kwa fani za Radiolojia, Usingizi, Ngozi, Macho, Magonjwa ya akili na Magonjwa ya Damu Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni Kigoma.

- Kuanzisha huduma za kibingwa za upasuaji wa taya na uso (Maxillofacial Surgery) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa

- Kuanzisha huduma za kibingwa za masikio, pua na koo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kitete (Tabora).

b. Kuendelea na hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa maboresho makubwa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili;

c. Kuanzisha kiwanda cha kuzalisha viungo tiba na viungo saidizi (Prostheses Manufacturing Plant) katika Hospitali ya Kanda KCMC. na

d. Kuendeleza na kuimarisha huduma za mkoba za kimkakati za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi (International Medical Camps).

viii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala, ambapo kiasi cha Shilingi milioni 937.29 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-

a. Kuongeza Hospitali zinazotoa huduma jumuishi za Tiba Asili kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa 14 hadi 21; na

b. Kuendeleza huduma za Tiba Asili kwa kufanya tafiti, kuongeza na kuendeleza mashamba ya miti dawa kwa kila kanda ili kuhamasisha uzalishaji endelevu wa dawa za tiba asili;

ix. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya

mlipuko, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 173.94 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-

a. Kuendelea kutekeleza afua za udhibiti na kutokomeza Malaria kwa kuua mazalia ya mbu, kuimarisha uzalishaji wa viuadudu katika viwanda vya ndani ikiwemo kiwanda cha Viuadudu Kibaha, kununua na kusambaza vyandarua, vitendanishi na dawa za Malaria.

b. Kuendelea kutekeleza afua za kudhibiti na kutokomeza Kifua Kikuu na Ukoma, UKIMWI, Homa ya Ini na magonjwa ya ngono kwa kuimarisha uwezo wa utambuzi na tiba ya magonjwa hayo kwa kununua vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na dawa;

c. Kufufua kiwanda cha *Tanzania Pharmacetical Industry* (TPI) kilichopo Arusha kuanza kuzalisha ARV.

x. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 6.61 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-

a. Kuimarisha utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu kwa kununua vifaa vya uchunguzi wa usikivu na macho kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa 14 na Hospitali za Kanda tano (5) na kuimarisha huduma za utengamao katika Hospitali za Halmashauri 50.

b. Kuongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa zinazotoa huduma tatu za utengamao za Viungo tiba na viungo Saidizi (Prosthetics and Orthotics), Fiziotherapia (Physiotherapy), Tiba kwa Vitendo (Occupational Therapy*)*, kutoka nane (8) hadi 18;

c. Kuendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa kituo cha umahiri cha huduma za utengamao katika Mkoa wa Tabora; na

d. Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Klabu za Afya za Wazee (Healthy Ageing Clubs) katika ngazi ya Halmashauri ili kuongeza idadi kutoka 14 hadi 30;

SEHEMU YA VI: SHUKRANI

412. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee natoa shukran zangu kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambao ni **Bw. Mavere Ali Tukai (MSD), Dkt. Irene Charles Isaka (NHIF), Bw. Adam Mitangu Fimbo (TMDA), Prof. Said Shebe Aboud (NIMR), Dkt. Fidelice Mbaruku Mafumiko (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali)**. Pia, nichukue fursa hii kuwashukuru Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda ambao ni **Prof. Mohamed Yakub Janabi** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Mhe. Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Dkt. Peter Richard Kisenge** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Diwani Bakari Msemo,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Leonard Maduhu Subi** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dkt. Paul Sarea Lawala** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Fred Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Prof. Abel Nkono Makubi** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Caesar Mawalla** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Herbert George Msigati** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara), **Dkt. Bahati Mgeni Wajanga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando), **Prof. Gileard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC) na **Bi. Brenda Kinemo Msangi** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda CCBRT).

413. Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru **Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara, Wasajili wa Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma, Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi.** Natoa shukrani kwa Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

414. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na wadau mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa nchi zinazochangia Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund) zikiwemo **Canada**,

Denmark, **Ireland**, **Uswisi**, **Korea Kusini**, **Uingereza** pamoja na Mashirika ya Kimataifa ambayo ni **Benki ya Dunia**, **UNFPA** na **UNICEF** kwa mchango wao ambao umechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya, hususan katika ngazi ya afya ya msingi.

415. Mheshimiwa Spika, napenda kuzitambua nchi nyingine za Umoja wa Falme za Kiarabu, Serikali ya Watu wa China na Uturuki pamoja na mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao muhimu kwa Wizara katika kuboresha huduma za afya nchini. Mashirika hayo ni pamoja na yale yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa kama vile, **WHO, UNAIDS, UNDP, UNFPA, UNICEF, UN-WOMEN, na IAEA; Jumuiya ya Ulaya (EU); IMF; BENKI YA DUNIA; BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AfDB);** pamoja na mashirika mengine ya Kimataifa na wadau wa maendeleo kama **GLOBAL FUND, GAVI, PEPFAR (CDC na USAID), KOICA, PMI, SUSAN THOMPSON BUFFET FOUNDATION, GATES FOUNDATION, GLOBAL AFFAIRS CANADA, ABBOTT FUND, NUTRITION INTERNATIONAL, GIZ, KfW, JICA, KOFIH, FLEMING FUND** pamoja na taasisi mbalimbali za kifedha za ndani. Ushirikiano wao umeendelea kuwa nguzo muhimu katika mafanikio ya Sekta ya afya nchini.

416. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa watu binafsi, asasi za kiraia, vyama vya kitaaluma, na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa mchango wao mkubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini. Mashirika haya yamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Serikali kuleta maendeleo katika sekta ya afya. Baadhi ya mashirika hayo ni BENJAMIN MKAPA FOUNDATION, AGOTA, AGA KHAN FOUNDATION, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, NEST 360, FOUNDATION FOR CANCER CARE IN TANZANIA, LHL INTERNATIONAL, MDM, COUNSENUTH, ELCT, IFAKARA HEALTH INSTITUTE, LIONS CLUB, MAT, PST, TAPHATA, GOOD SAMARITAN FOUNDATION, WALTER REED, EGPAF, JHPIEGO, JSI, FHI, AFRICARE, MSALABA MWEKUNDU, PLAN INTERNATIONAL, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, PATHFINDER, PATH, CHAI, AMERICARES, MELSAT, TARA, TAWOPHA, PASADA, NACOPHA, PAT, PSI, PRINMAT, ROTARY CLUB INTERNATIONAL, SIKIKA, SHREE HINDU MANDAL, TANNA, TPHA, TANZANIA SURGICAL ASSOCIATION (TSA), SATA, TANZANIA DIABETIC ASSOCIATION, TANESA,

THPS, TUNAJALI, TANZANIA MIDWIVES ASSOCIATION, TAYOA, TDA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, WHITE RIBBON ALLIANCE, LSF, CIHEB TANZANIA, STARLINK GULF TRADING LTD , KIVULINI, WILDAF, HAYDOM LUTHERAN HOSPITAL, GSM FOUNDATION, MO FOUNDATION, VODACOM FOUNDATION, TCRF, FSDT, JAI, TOUCH FOUNDATION pamoja na asasi nyingine zilizoshirikiana na Sekta ya Afya kwa namna moja au nyingine. Ushirikiano wao ni wa kupongezwa na unaendelea kuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya afya nchini.

417. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Vyuo vya elimu ya juu vinavyoshirikiana na Sekta ya Afya katika kuimarisha huduma za afya nchini. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Kairuki, Chuo Kikuu cha Tumaini, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino, Chuo Kikuu cha Katoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi, Chuo Kikuu cha KCMC, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, Chuo Kikuu cha Aga Khan, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro, Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, Vyuo Vikuu vya Sayansi na Teknolojia Mbeya na Arusha, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Chuo cha Kumbukumbuku ya Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mtakatifu Franscisco pamoja na vyuo vya kati vinavyotoa mafunzo ya sayansi katika eneo la afya kwa ushiriki wao katika kukuza elimu, utafiti, na utoaji wa huduma za afya una mchango mkubwa na wa kupongezwa.

SEHEMU YA VII: MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26

Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/26

418. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/26 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha Shilingi **819,977,862,602.14**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **74,207,303,307.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya

Wizara, Shilingi **153,792,696,693.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, Shilingi **591,977,862,602.14** zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara.

Matumizi ya Kawaida

419. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 626,433,136,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **Asilimia 39** ya bajeti iliyotengwa, ambapo kiasi cha **Shilingi 475,418,119,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha **Shilingi 151,015,017,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Miradi ya Maendeleo

420. Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga kutumia **Shilingi 991,758,099,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 61 ya bajeti iliyotengwa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 564,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 427,299,490,000.00.**

421. Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni **Shilingi 1,618,191,235,000.00** ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea.

Na	Fungu	Matumizi ya Kawaida	Miradi ya Maendeleo	Jumla
1	Fungu 52	626,433,136,000.00	991,758,099,000.00	1,618,191,235,000.00

422. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya www.moh.go.tz.

423. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsanteni sana, Mheshimiwa Waziri ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwanza kabla sijamwita Mwenyekiti, nimeletewa ujumbe hapa kuna wageni wa Mheshimiwa Shigongo kutoka Buchosa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa ninaomba kuleta Mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, sitaweza kusoma taarifa yote hivyo, ninaomba Taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee sana ninaomba niungane na Bunge lako Tukufu, niungane na wewe kwa kutumia nafasi hii kumpongeza sana Profesa Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani. Pia, niungane nawe kumpongeza Dkt. Ntuli Kapologwe kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Mheshimiwa Spika, taarifa yangu imegawanyika katika sehemu kuu tatu: kuna utangulizi; sehemu ya pili ni utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa Mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi minne ilitembelewa na kukaguliwa katika Mkoa wa Mara, Simiyu, Geita na Dodoma. Miradi hiyo ni ya Hospitali ya Rufaa ya Mara, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, Hospitali ya Kanda Maalumu ya Benjamini Mkapa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika miradi hiyo iliyokaguliwa, ipo baadhi ya miradi ambayo haijakamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya fedha. Moja ya mfano wa miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la tiba ya mionzi katika Hospitali ya Kanda ya Benjamini Mkapa, Dodoma ambapo mradi ulianza 7Juni, 2022 na ulitarajiwa kukamilika 6 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi Kamati inatembelea mradi huu mwezi Machi, 2025 mradi ulikuwa umefika 57% badala ya kuwa 91%. Aidha, mradi umepokea shilingi 8,412,869,672.12 sawa na 27.65% ya shilingi 30,421,863,042.69 zilizokuwa zimetengwa ambazo zilitarajiwa kutolewa katika kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi wa Maendeleo iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2024. Kufuatia ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Fedha za miradi kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(b) Fedha kutolewa kwa kiwango kidogo chini ya 50% hadi kufikia mwezi Machi, 2025 katika miradi tajwa; na

(c) Upungufu wa Wataalam wa Afya, Mfano, Madaktari bingwa wa magonjwa ya Ngozi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla imebainika kuwa mwenendo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo siyo wa kuridhisha ikilinganishwa na muda uliobaki kabla ya mwaka wa fedha kwisha. Hali hii imesababisha miradi kutokukamilika ndani ya muda uliopangwa na kutokufikia matarajio ya miradi hiyo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, makusanyo na maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika uchambuzi wa Kamati Fungu Na. 52 makadirio ya Wizara yalikuwa ni kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 819,977,862,602.14 kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu imebaini kuwa katika vyanzo vya maduhuli vilivyodhanishwa na Wizara. Chanzo cha Hospitali ya Kanda, Maalum, Hospitali za Taifa, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara ndicho kilichochangia kwa kiasi kikubwa ambapo hadi mwezi Februari, chanzo hicho kimekusanya jumla ya shilingi 340,162,500,399.79 ambazo ni sawa na 62% ya lengo la chanzo hicho kama ilivyoonyeshwa katika Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya makusanyo ni ya kuridhisha. Uchambuzi unaonyesha makadirio ya makusanyo ya mapato yatokanayo na huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kipindi cha Juni, 2024 hadi Februari, 2025 yamefanya vizuri sana katika makusanyo kwa kuvuka 80% ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, hospitali hizo kwa mfano ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe ambapo wamekusanya 104%, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu 89%, Hospitali ya Rufaa ya Mirembe 84%, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha - Mt. Meru 83% katika kipindi cha hadi mwezi tulioutaja hapo katika taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni ya wastani kiasi cha shilingi 470,173,048,480.05

ambacho ni sawa na 69% ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilizopokelewa ni shilingi 242,265,195 sawa na 58%; na fedha za nje zilizopokelewa ni shilingi 227,907,853,372.00 sawa na 87% kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utolewaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa wastani, kwani uchambuzi unaonyesha kuwa miradi 55 ya maendeleo iliidhinishiwa. Hata hivyo, miradi 24 tu ndiyo ilipokea fedha hadi kufika Januari, 2025 ikiwa ni sawa na 44% tu ya miradi yote iliyoidhinishiwa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi 24 iliyopokea fedha za ndani, miradi tisa imepokea fedha zote kwa 100% za ndani iliyoidhinishiwa. Baadhi ya miradi iliyopokea fedha zote zilizoidhinishiwa, hadi kufika Februari, 2025 ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* Hospitali ya Magonjwa ambukizi ya Kibong'oto, Hospitali ya Kanda ya Kaskazini *(KCMC)* na Hospitali ya Mifupa ya *(MOI)*.

Mheshimiwa Spika, imebainika kuwa miradi 31 ya maendeleo haikupokea kiasi chochote cha fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo. Baadhi ya miradi hiyo ni Hospitali ya Mama na Mtoto Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga kwa maana ya Bombo, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro kwa maana ya Mawenzi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha - *Mount* Meru, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Kanda ya ziwa Bugando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu wa utoaji fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni kiashiria cha kuwepo kwa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni muhimu sasa, Serikali kuhakikisha fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge

zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2024 kwisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Makadirio na makusanyo ya maduhuli katika Wizara ya Afya katika mwaka 2025/2026 ni shilingi 819,977,862,602.14.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba lipo ongezeko la 8% ambalo ni shilingi 63,184,156,104.56 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2024/2025 kama ilivyoonekana katika Kielelezo Na. 4.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada mbalimbali zinazofanywa kuhakikisha kiwango cha makadirio ya makusanyo kinaongezeka kila mwaka. Ni vema Serikali kuhakikisha kwamba inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji na upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa Sekta ya Afya na kuongeza bajeti ya Afya kila mwaka ambapo kwa miaka mitano mfululizo kumekuwa na ongezeko la fedha zinazotengwa kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kama inavyoonekana katika kielelezo namba tano.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2025/2026 fedha zinazoombwa na kuidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) ni shilingi 1,618,191,235,000.00. Hili ni sawa na ongezeko la 23% ikilinganishwa na shilingi 1,311,837,466,000.00 zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya Wizara ya Afya shilingi 626,433,136,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 991,758,099,000.00 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 151,015,017,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 471,418,119,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 564.4 na fedha za nje ni shilingi 427,299,490,000.00 ambazo mchanganuo wake unaonekana katika Kielelezo Na. 6.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la fedha za bajeti asilimia zinazoombwa kwa ajili ya Wizara ya Afya Fungu Na. 52 kwa mwaka 2025/2026 ni 23%, ongezeko hili lipo katika Fungu la Matumizi ya Mengineyo ambapo limeongezeka kwa asilimia mbili ukilinganishwa na mwaka wa fedha 2024.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, fedha za ndani za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa 36%, na fedha za nje za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa 62%.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kamati yetu kuwa, Serikali itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya Wizara ya Afya ili kuendelea kuongeza kasi ya kuboresha Sekta hii muhimu inayogusa maisha ya kila Mtanzania. Aidha, fedha zote zitolewe kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Taarifa ya Utendaji ya Bohari ya Kuu ya Dawa, kwanza tukiri ufanisi umeongezeka sana katika Bohari ya Dawa chini ya usimamizi wa Mkurugenzi Mavere, wameongeza kiwango cha mapato na usambazaji wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Kamati imebaini zipo changamoto za mtaji, ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023, ombi la kupewa mtaji liliwasilishwa kupitia Wizara ya Afya. Lengo la mtaji unaoombwa ni kuongeza ufanisi wa *MSD* ili itekeleze vema majukumu yake iliyokasimiwa ambayo ni uzalishaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za afya na vile vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika taarifa ya Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Afya kwa miaka miwili mfululizo (2023/2024 na 2024/2025), Kamati imekuwa ikitoa msisitizo kuwa Serikali itoe mtaji wa shilingi bilioni 561. Kamati inaishukuru sana Serikali katika kuchukua hatua za awali ambapo mwaka wa fedha 2023/2024 wametoa mtaji wa shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi za Serikali, Bohari Kuu ya Dawa pia wamefanya juhudi na kupata kiasi cha shilingi bilioni 162. Hivyo, kwa sasa mtaji unaoombwa ni shilingi bilioni 300 kwa mchanganuo ufuatao: Shilingi bilioni 150 zinahitajika kuwezesha ununuzi wa dawa, shilingi bilioni 110 kwa ajili ya kulipa madeni ya washitiri na shilingi bilioni 24 kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya *MSD,* wakati huo huo shilingi bilioni 15.4 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikiidai Serikali ambapo kumewepo na madeni yanayoongezeka kila mwaka kwenye vituo vya afya, yaliyogawanyika kwenye makundi mawili. Moja ya kundi hilo ni bidhaa zinazotolewa kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa matarajio ya kulipwa pindi vituo vitakapokuwa na fedha, na kundi la pili ni gharama za utunzaji na usambazaji wa bidhaa za Miradi Misonge ambapo Serikali iliingia makubaliano ya kuchangia gharama hizi. Jumla ya madeni yote yanayohusu ununuzi, utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya ni shilingi bilioni 434.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2025 changamoto ya madeni ya bidhaa zilizosambazwa unaonyesha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo chini ya Wizara ya Afya vinadaiwa shilingi bilioni 46.4 na vituo vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI vinadaiwa shilingi bilioni 83.1.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bidhaa za afya za Miradi Misonge, Serikali inadaiwa shilingi bilioni 305 kwa ajili ya huduma za utunzaji na usambazaji wa bidhaa hizo za afya.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali sasa ikatoa kipaumbele kwa kutoa mtaji kwa Bohari Kuu ya Dawa kwani ikiwa kiasi kilichoombwa cha mtaji kitapatikana, kitaiwezesha Bohari ya Dawa *(MSD)* kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya, japo na wao wanao wajibu kulipa madeni haya. Madeni yote inayodaiwa Serikali, yatafutiwe ufumbuzi ili kunusuru ustawi wa Bohari ya Dawa *(MSD). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokabili Mfuko huu. Moja ya changamoto hizo ni madeni ya muda mrefu ambayo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilitoa kwa taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, ulitolewa Mkopo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ajili ya ununuzi wa magari ya Polisi shilingi bilioni 45; mwaka 2012, ulitolewa mkopo kwa ajili ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* shilingi bilioni 17; mwaka 2012, ulitolewa mkopo kwa ajili ya Taasisi ya Mifupa ya *MOI* kwa ajili ya ujenzi wa jengo pacha ambapo ni shilingi 18,164,741,000.00. Mwisho, mwaka 2010 ulitolewa mkopo kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, shilingi bilioni 129.

Mheshimiwa Spika, mikopo hiyo yenye thamani ya jumla ya shilingi 210,291,301,794.89 inasababisha mzigo mkubwa wa kifedha na upungufu wa uwezo wa Mfuko kuwekeza katika kuhudumia miundombinu ya sekta hii ya Bima ya Afya na tulitamani sana Waziri wa Fedha asikie huu mchanganuo.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Wizara ya Afya (Fungu 52), Kamati inaipongeza Serikali sana kwa hatua kubwa waliyochukua kuhakikisha maboresho makubwa yanafanyika na hatimaye kuwa na huduma bora za afya, kwani afya

ndiyo msingi wa uhai na maendeleo ya mtu mmoja mmoja na katika *level* ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ambao unalenga kuboresha zaidi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kwanza: -

(i) Kiwango kidogo cha utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyokusudiwa ikamilike mapema na kuwanufaisha wananchi. *(Makofi)*

(ii) Uhaba wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kutoa vibali vya ajira kwa sekta ya afya kwani sekta hii ndiyo msingi wa nguvu kazi ya Taifa.

(iii) Ukosefu wa mtaji wa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe mtaji wa shilingi bilioni 300 kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD),* ili kuongeza ufanisi na kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya, kusaidia uwekezaji katika viwanda na kuongeza uwezo wa uhifadhi bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kutosha. Kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

(iv) Madeni ya Bohari ya Dawa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia tunaisihi ilipe deni inalodaiwa na Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* kiasi cha shilingi bilioni 434.2, kwa mchanganuo ufuatao shilingi bilioni 46.4 kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya Wizara ya afya, shilingi bilioni 83.1 kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na shilingi bilioni 305 za Miradi Misonge. Ni muhimu sana madeni haya yakalipwa katika kuendelea kuulinda mnyororo wa

ugavi na kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa utoshelevu.

(v) Madai ya fedha za Mfuko wa Bima ya Afya tumeeleza pia.

Mheshimiwa Spika, tunashauri Serikali iweze kulipa deni la shilingi bilioni 210 ambapo zilitoka *NHIF* ili kuimarisha utendaji wa mfuko huu na kutokwamisha uendelevu wa mfuko huu hili ni muhimu sana.

(vi) Katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwashirikishe wadau kutoka sekta binafsi katika kuchangia fedha za mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa wote kwa watu wasio na uwezo kwa lengo la kuongeza fedha za kusaidia matibabu na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ambayo imeishasainiwa na Mheshimiwa Rais.

(vii) Kutokukamilika kwa Miradi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwekeze kipaumbele cha kutoa fedha katika miradi ambayo imeanza muda mrefu ili ikamilike na kuanza kutoa huduma. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaatiba ili kuleta tija kwa jamii, tumeona mabadiliko makubwa na mageuzi makubwa, basi tunaisihi Serikali iendelee kununua vifaatiba ili kuendana na kasi ya mabadiliko na ujenzi wa vituo hivyo.

(viii) Serikali isimamie matumizi ya TEHAMA kwenye Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Kitaifa kwa kufungwa mifumo ya *Electronic Health Management System (eHMS)* kama ilivyo kwenye Hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Spika, nataka nichomekee hapa, tulipotoa maoni ya kufungwa kwa mifumo ya eHMS takwimu zinaonyesha mapato, usimamizi na utendaji, mapato yameongezeka kwa 14% katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa sababu ya matumizi ya mifumo bora ya kisasa. Kwa hiyo, hili linatakiwa liendelezwe kufanyika bila kusubiri

mpaka Mamlaka za juu zitoe maelekezo watu wamsadie Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba haya mambo yanatimia katika Wizara yake.

(ix) Sheria ya kusimamia huduma za uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe za viungo vya mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa sheria inayosimamia huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya binadamu ili kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hii kwa wananchi.

(x) Katika magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali kupambana na tatizo la magonjwa yasiyoambukiza na tunaishauri ifanye yafuatayo:-

(a) Ifanye tafiti kubaini ukubwa wa tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

(b) Itoe elimu kwa jamii kuhusu vyanzo vya magonjwa hayo na namna ya kuyaepuka hususan kwa kuzingatia mazoezi na lishe; na

(c) Ishirikishe sekta nyingine katika utekelezaji wa afua za kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa.

(xi) Tunaishauri Serikali iunde bodi moja ya usajili wa vituo vya kutolea huduma ya afya nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itaweka ulazima wa vituo vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali kusajiliwa kwa kukidhi vigezo kabla ya kuanza kutoa huduma.

(xii) Katika uimarishaji wa viwanda vya ndani na kuzalisha bidhaa za dawa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa uweze kuleta tija kwa Watanzania Serikali ifanye yafuatayo:-

(a) Iongeze kodi kwa bidhaa za dawa zinazotoka nje ya nchi ambazo zinazalishwa na viwanda vya ndani. Ninarudia, Serikali iongeze kodi kwa bidhaa za dawa zinazotoka nje ya nchi ambazo zinazalishwa na viwanda vya ndani; *(Makofi)*

(b) Serikali ifufue Kiwanda cha Dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* ambapo Serikali ina umiliki wa hisa za 40%;

(c) Serikali iongeze kiwango cha uzalishaji wa dawa katika viwanda vya dawa vya Keko *(Keko Pharmaceutical Industries)* ambacho Serikali ina umiliki wa hisa za 70%; na

(d) Serikali itoe msamaha wa kodi kwa malighafi zinazoagizwa nchini kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za dawa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi kuwasilisha hii Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uzalendo wako na umahiri wako namna unavyoliongoza Bunge letu wewe pamoja na Naibu wako Spika na Wenyeviti wetu wote wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee sana ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama - Mbunge na Waziri wa Afya kwa namna ambavyo ameweza kuipatia Kamati yetu ushirikiano mkubwa sana, pia Waziri huyu kwa muda mfupi kwa Kamati tunaosimamia sekta hii ameonesha ufanisi wa hali ya juu sana katika kuwa msikivu, kupokea na kuchakata maoni ya Kamati yeye pamoja na Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tunampongeza sana Katibu Mkuu wetu wa Wizara, Dkt. Seif Abdallah Shekilage, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ismail Rumatila na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Elias Magembe pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Afya na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati inapotekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano mzuri ambao wamenipatia wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina wa masuala mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika uandishi wa taarifa hii. Nawapongeza sana na ninaomba majina yao yatambuliwe katika orodha kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru sana Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake. Baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Fungu Na. 52 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha
2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu (3) zifuatazo: -

(a) **Sehemu ya Kwanza** - Utangulizi;

(b) **Sehemua ya Pili** - Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(c) **Sehemu ya Tatu** - Maoni na Ushauri wa Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

2.1 Mambo yaliyozingatiwa Wakati wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Ili kuliwezesha Bunge kufuatilia Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na kushauri ipasavyo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mambo makuu matatu (3) ambayo ni: -

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya uliotolewa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, uchambuzi huu unalenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti husika.

2.2 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Kwa Mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Jumla ya miradi minne (4) ilitembelewa na kukaguliwa katika Mkoa wa Mara, Simiyu, Geita na Dodoma, lengo likiwa ni kujiridhisha na mwenendo wa utekelezaji wa Miradi hiyo na kupima endapo utekelezaji wake utaweza kuyafikia malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa wananchi. Miradi hiyo ni pamoja na uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara (Mradi Namba 5411), Uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu (Mradi Namba 5411), Uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita (Mradi Namba 5411), na Uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamini Mkapa (Mradi Na. 5428).

Mheshimiwa Spika, Naomba kulijulisha Bunge kuwa, katika miradi hiyo iliyokaguliwa, ipo miradi ambayo haijakamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya fedha. Miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la tiba ya mionzi katika hospitali ya kanda ya Benjamini Mkapa, Dodoma ambapo mradi ulianza 7Juni 2022 na ulitarajiwa kukamilika 6 Juni 2025. Hata hivyo, hadi Kamati inatembelea mradi huu mwezi Machi, 2025 mradi ulikuwa umefika **asilimia 57** badala ya **asiilimia 91**. Aidha, mradi umepokea **Shilingi 8,412,869,672.12** sawa na **asilimia 27.65** ya **Shilingi 30,421,863,042.69** zilizokuwa zimetengwa ambazo zilitarajiwa kutolewa katika kipindi cha miaka mitatu.

Aidha, mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Mara; ambayo ujenzi wake ni awamu na ulianza mwaka 1980. Hivi sasa mradi upo katika awamu ya tano na unatekelezwa chini ya mkandarasi mkuu Prince *General Investment Ltd* kwa gharama ya **Shilingi 14,739,338,399.21** ambapo ameshalipwa **Shilingi 4,000,000,000.00.** Vilevile, katika awamu ya tano Wizara iliingia Mkataba wa kuingiza umeme na TEMESA kwa gharama ya **Shilingi 4,388,665,587.57** ambapo hadi sasa bado hajalipwa na utekelezaji wake umefika **asilimia 58**. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kumalizika 2025 na ujenzi umefika asilimia **15**.

Mradi mwingine ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita ambayo inamradi wa ujenzi wa jengo la maabara na jengo la mama na mtoto sambamba na ujenzi wa ukuta, ujenzi wa barabara ndani ya hospitali na njia ya watembea kwa miguu na mfumo wa maji taka. Gharama

za mradi ni **Shilingi 13,213,606,303.33** ambapo hadi sasa zimetolewa **Shilingi 4,505,583,851.67** na ujenzi umefika **asilimia 50**

2.2.1 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Kufuatia ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

(a) Fedha za miradi kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(b) Fedha kutolewa kwa kiwango kidogo chini ya asilimia 50 hadi kufikia mwezi Machi, 2025; na

(c) Upungufu wa Wataalam wa Afya, Mfano, Madaktari bingwa wa magonjwa ya Ngozi.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla imebainika kuwa mwenendo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo si wa kuridhisha ikilinganishwa na muda uliobaki wa miezi miwili tu kwa mwaka wa fedha wa utekelezaji wa miradi hiyo kuisha. Hali hii inasababisha miradi kutokukamilika ndani ya muda uliopangwa na kutokuyafikia matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora zilizokusudiwa. Vile vile kusababisha mabadiliko katika gharama za utekelezaji wa miradi hiyo endapo haitakamilika ndani ya muda uliopangwa.

2.3 Utekelezaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati Mwaka 2023/2024

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kamati ilitoa ushauri katika maeneo kumi na tisa (19). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi, Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati na inaendelea kutekeleza kwa yale ambayo bado hayajatekelezwa. Katika taarifa hii, Kamati itaendelea kuyasisitiza maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu.

2.4 Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Kamati wa Fungu 52 makadirio ya Wizara yalikuwa ni kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 819,977,862,602.14** kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa katika vyanzo vya maduhuli vilivyobainishwa na Wizara, chanzo cha hospitali za Kanda, Maalum, Taifa, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara ndicho kinachangia kwa kiasi kikubwa ambapo hadi mwezi Februari, 2025 chanzo hicho kimekusanya jumla ya **Shilingi 340,162,500,399.79** sawa na **asilimia 62** ya lengo la chanzo hicho. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli.

Kielelezo Na: 1 Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Kipindi cha Mwaka 2024/2025 hadi Machi, 2025

NA	CHANZO CHA MAKUSANYO	KIASI KILICHOIDHINISHWA KUKUSANYWA	KIASI KILICHOKUSANYWA HADI FEBRUARI 2025	ASILIMIA (%)
1.	Makao Makuu ya Wizara	70,756,146,439.69	42,076,503, 664.72	59
2.	Hospitali za Rufaa za Mikoa	134,171,499, 810.31	84,971,219,144.71	63
3.	Taasisi zilizo chini ya Wizara	551,866,060,247.58	340,162,500,399.79	62
JUMLA		**756,793,706,497.58**	**467,210,223,209.22**	**62**

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti (Fungu 52) hadi Februari 2025 iliyowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla hali ya makusanyo ni ya kuridhisha. Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Mapato yatokanayo na utoaji wa Huduma kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kipindi cha

Julai 2024 hadi Februari 2025 unaonesha baadhi ya hospitali zimefanya vizuri sana katika makusanyo kwa kuvuka asilimia themanini (80%) ya makusanyo. Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe (104%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu (89%), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (84%) na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha - Mt. Meru (83%).

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini pia maeneo ambayo hayakufanya vizuri kwa kigezo cha makusanyo yake kutokuvuka asilimia hamsini (50%) hadi mwezi Februari 2025 ambayo ni Maabara ya Taifa (2%), Elimu ya Afya kwa Umma (31%), Baraza la Mazingira (31%), Baraza la Optometri (33%), Baraza la Uuguzi na Ukunga (39%),Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu - NIMR (43%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma - Maweni (47%), Hospitali ya Kanda ya Burigi Chato (42%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga (47%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi (48%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya (49%) na Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Bugando (49%).

Mheshimiwa Spika, Ni rai ya Kamati kuwa, pamoja na kwamba umebaki muda mchache kufika mwisho wa mwaka fedha 2024/2025; ipo haja ya kuhakikisha makusanyo yanapatikana hasa kwa maeneo ambayo hayajavuka asilimia hamsini (50%).

2.5 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Katika Bajeti ya mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Afya (Fungu 52) iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 1,311,837,466,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 632,267,220,000.00** ambazo ni sawa na **asilimia 48** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kiasi cha **Shilingi 679,570,246,000.00** ambazo ni sawa na **asilimia 52** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2025 hali ya utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ni ya kuridhisha kwani fedha zimetolewa kiasi cha **Shilingi**

340,362,963,132.00 sawa na **asilimia 54** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni ya wastani kwani kimetolewa kiasi cha **Shilingi 470,173,048,480.05** ambazo ni sawa na **asilimia 69** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi 242,265,195,109.00** sawa na **asilimia 58**; na fedha za nje zilizopokelewa ni **Shilingi 227,907,853,372.00** sawa na **asilimia 87** kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 2.

Kielelezo Na: 2 Mchanganuo wa Fedha zilizoidhinishwa 2024/2025 na Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2025



Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliyowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa utolewaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa wastani kwani uchambuzi unaonesha miradi hamsini na tano (55) ya maendeleo iliidhinishiwa fedha za ndani. Hata hivyo, miradi ishirini na nne (24) tu ndio iliyopokea fedha hadi mwezi Februari, 2025 ikiwa ni sawa na **asilimia**

44 tu ya miradi yote iliyoidhinishiwa fedha za ndani. Kati ya miradi 24 iliyopokea fedha za ndani, miradi tisa (9) imepokea fedha zote (100%) za ndani iliyoidhinishiwa. Baadhi ya miradi iliyopokea fedha zote ilizoidhinishiwa hadi kufika Februari 2025 ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, Taasisi ya Saratani - Ocean Road, Hospitali ya Magonjwa ambukiziKibong'oto, Hospitali ya Kanda Kaskazini (KCMC) na Hospitali ya Mifupa Muhimbili (MOI).

Mheshimiwa Spika, Imebainika kuwa miradi thelathini na moja (31) ya maendeleo haikupokea kiasi chochote cha fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo. Baadhi ya miradi hiyo ni Hospitali ya Mama na Mtoto Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga - Bombo, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro - Mawenzi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha - Mount Meru, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Kanda ya ziwa Bugando.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwenendo huu wa utoaji fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni kiashiria cha kuwepo kwa ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni muhimu sasa, Serikali kuhakikisha fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2024/2025 kuisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa.

2.6 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa taarifa ya Kamati umezingatia miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka Mmoja (2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (HSSP-V

2021-2026), Mpango Mkakati wa Wizara 2020/2021-2025/2026 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030).

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi pamoja na shughuli za Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo: -

2.6.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2025/2026 ni **Shilingi 819,977,862,602.14**. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo kutoka katika kila chanzo.

Kielelezo Na: 3 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Fungu 52 kwa Mwaka 2025/2026

CHANZO CHA MAKUSANYO	KIASI
Makao Makuu ya Wizara	74,207,303,307.00
Hospitali za Rufaa za Mikoa	153,792,696,693.00
Taasisi, Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda	591,977,862,602.14
JUMLA	**819,977,862,602.14**

Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2025/2026 ambapo zimeongezeka **Shilingi 63,184,156,104.56** sawa na ongezeko la **asilimia 8** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hili lipo katika vyanzo vyote vya makusanyo ambapo ongezeko kubwa ni la Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo makusanyo yake yameongezeka kwa **asilimia 14** kama inavyoonekana katika kielelezo namba 4.

Kielelezo Na: 4 Mchanganuo wa Ongezeko la Fedha za Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka 2025/2026

Maelezo	Makadirio ya Makusanyo 2024/2025	Makadirio ya Makusanyo 2025/2026	Kiasi Ongezeko	Asilimia Ongezeko
Makao Makuu	70,756,146,439.69	74,207,303,307.00	3,451,156,867.31	**+5**
Hosp za Rufaa za Mikoa	134,171,499,810.31	153,792,696,693.00	19,621,196,882.69	**+14**
Taasisi	551,866,060,247.58	591,977,862,602.14	40,111,802,354.56	**+7**
JUMLA KUU	**756,793,706,497.58**	**819,977,862,602.14**	**63,184,156,104.56**	**+8**

Chanzo: *Randama ya Wizara ya Afya 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada mbalimbali zinazofanyika na kuhakikisha kiwango cha makadirio ya makusanyo kinaongezeka kila mwaka. Ni vema Serikali kuhakikisha inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato. Vilevile, ipo haja ya Serikali kuangalia kwa kina kiasi cha makadirio yanayotengwa kwa baadhi ya vyanzo ambavyo havifanyi vizuri ili kupunguza kiwango cha makadirio hayo badala ya kuwa na makadirio ya makusanyo makubwa ambayo hayatekelezeki. Kwa Mfano, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2024/2025 ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 3,271,941,747.00** ambapo hadi mwezi Februari 2025 ilikusanya **asilimia 49** tu. Hospitali hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imekadiriwa kukusanya **Shilingi 4,000,000,000.00** ikiwa ni ongezeko la **Shilingi 728,058,253.00**.

Mheshimiwa Spika, Maeneo mengine ambayo hayakufanya vizuri lakini yameongezewa makadirio kwa mwaka 2025/2026 ni Baraza la Uuguzi na Ukunga, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu - NIMR, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Bugando.

2.6.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa Sekta ya Afya na kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya kila mwaka ambapo kwa miaka mitano mfululizo kumekuwa na ongezeko la fedha zinazotengwa kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya (fungu 52) kama inavyoonekana katika kielelezo namba 5.

Kielelezo Na: 5 Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026



Chanzo; Randama 2021/2022 hadi 2025/2026 zilizowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka 2025/2026 fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) ni **Shilingi 1,618,191,235,000.00.** Hili ni ongezeko la **asilimia 23** ikilinganishwa na **Shilingi 1,311,837,466,000.00** zilizoidhinishwa mwaka 2024/25. Kati ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya Wizara ya Afya **Shilingi 626,433,136,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 991,758,099,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 151,015,017,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 475,418,119,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, fedha za ndani ni **Shilingi 564,458,609,000.00** na fedha za

nje ni **Shilingi 427,299,490,000.00**. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchanganuo wa fedha zilizotengwa.

Kielelezo Na: 6 Asilimia ya Mgawanyo wa Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2025/2026



Chanzo: Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, Ongezeko hili la **asilimia 23** ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026; lipo katika Fedha za Matumizi ya Mengineyo ambapo zimeongezeka kwa **asilimia 2** ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2024/2025. Vilevile, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, fedha za ndani za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 36**, na fedha za nje za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 62**.

Mheshimiwa Spika, Ni imani ya Kamati kuwa, Serikali itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya Wizara ya Afya ili kuendelea kuongeza kasi ya kuboresha Sekta hii muhimu inayogusa maisha ya kila Mtanzania. Aidha, fedha zote zitolewe kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika.

2.6.3 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Taarifa ya Utendaji ya Bohari ya Kuu ya Dawa, Kamati imebaini changamoto ya mtaji, ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23, ombi la kupewa mtaji liliwasilishwa kupitia Wizara ya Afya. Lengo la mtaji unaoombwa ni kuongeza ufanisi wa MSD ili itekeleze vema majukumu yake iliyokasimiwa ambayo ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za Afya na vile vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Itakumbukwa kuwa katika taarifa ya Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Afya kwa miaka miwili mfululizo (2023/2024 na 2024/2025), Kamati imekuwa ikitoa msisitizo kwa Serikali kutoa mtaji kiasi cha **Shilingi Bilioni 561.5.** Kamati inaishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za awali ambapo mwaka wa fedha 2023/2024 umetolewa mtaji wa kiasi cha **Shilingi bilioni 100.** Pamoja na jitihada za Serikali, Bohari kuu ya Dawa imefanya jitihada na kufanikiwa kupata kiasi ya **shilingi bilioni 162.5.** Hivyo, Kwa sasa mtaji unaoombwa ni **Shilingi bilioni 300** kwa mchanganuo wa **Shilingi bilioni 150** zinahitajika kuwezesha ununuzi wa dawa, **Shilingi bilioni 110** kwa ajili ya kulipa madeni ya washitiri, **Shilingi bilioni 24.1** kwa ajili ya ujenzi wa Maghala, **Shilingi bilioni 15.4** kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, Bohari Kuu ya Dawa imekua ikiidai Serikali ambapo yamekuwepo madeni yanayoongezeka kila mwaka kwenye vituo vya afya yaliyogawanyika kwenye makundi mawili. Moja ya kundi hilo ni bidhaa zinazotolewa kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa matarajio ya kulipwa pindi vituo vitakapokuwa na fedha, na kundi la pili ni gharama za Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Miradi Misonge ambapo Serikali iliingia makubaliano ya kuchangia gharama hizi. Jumla ya madeni yote yanayohusu Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za afya ni **Shilingi bilioni 434.2**.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Machi, 2025, mchanganuo wa madeni ya bidhaa zilizosambazwa unaonesha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo chini ya Wizara ya Afya vinadaiwa **Shilingi**

bilioni 46.4 na vituo vilivyopo chini ya OR-TAMISEMI vinadaiwa **Shilingi bilioni 83.1**. Kwa upande wa bidhaa za afya za Miradi Misonge, Serikali inadaiwa **Shilingi bilioni 305** kwa ajili ya huduma ya utunzaji na usambazaji wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Ni vema Serikali ikatoa kipaumbele kwa kutoa mtaji kwa Bohari Kuu ya Dawa kwani ikiwa kiasi kinachoombwa cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za Afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za Afya. Aidha, madeni yote inayodaiwa Serikali yatafutiwe ufumbuzi ili kunusuru ustahimlivu wa Bohari ya Dawa.

2.6.4 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazoukabili Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Moja ya changamoto kubwa ni madeni ya mikopo ya muda mrefu ambayo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilitoa kwa taasisi mbalimbali za Serikali. Mwaka 2010, ulitolewa Mkopo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ajili ya ununuzi wa magari ya polisi **Shilingi bilioni 45,445,479,256.77**. Mwaka 2012, ulitolewa mkopo kwa Mamlaka ya Taifa ya Vitambulisho (NIDA) **Shilingi bilioni 17,329,680,538.12**. Mwaka 2012, ulitolewa mkopo kwa Taasisi ya Mifupa ya MOI kwa ajili ya ujenzi wa jengo pacha **Shilingi bilioni 18,164,741,000.00**. Mwisho, mwaka 2010 ulitolewa mkopo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa **Shilingi 129,351,401,000.00**.

Mheshimiwa Spika, Mikopo hiyo yenye jumla ya **Shilingi bilioni 210,291,301,794.89** inasababisha mzigo mkubwa wa kifedha na kupunguza uwezo wa Mfuko kuwekeza katika huduma muhimu na miundombinu.

2.6.5 Huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi

Mheshimiwa Spika, Huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ni huduma zinazotolewa na wataalamu waliobobea katika maeneo maalum ya tiba zinazojumuisha huduma ya uvunaji, utunzaji

na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu zinazolenga kusaidia na kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Uanzishwaji wa huduma ya matibabu ya kibingwa na bingwa bobezi imekuwa ni hatua muhimu na chachu katika kuboresha afya ya wananchi na kuimarisha mfumo wa afya nchini. Faida ya kuwapo kwa huduma hizi ni pamoja na kutoa matibabu ya hali ya juu kwa magonjwa kama Saratani, matatizo ya moyo, figo, mishipa ya fahamu na upasuaji wa hali ya juu na hivyo kupunguza gharama za matibabu nje ya nchi. Aidha, huduma hizi pia zimekuwa kichocheo cha kuvutia wagonjwa kutoka nchi jirani kama vile Kenya, Uganda, Malawi na Zambia kuja kupata matibabu.

Mheshimiwa Spika, Wakati Serikali inaendelea na kuboresha huduma hizi kwa kusomesha madaktari pamoja na kuendelea kuwekeza kwa kununua vifaa, ni vema kuhakikisha kunakuwepo na sheria mahsusi kwa ajili ya huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu. Sheria hii itasaidia sana kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hii pamoja na maslahi ya pande zote mbili kwa wananchi na hata wageni toka nje ya nchi.

2.6.6 Uwekezaji wa Viwanda vya Kuzalisha Bidhaa za Dawa

Mheshimiwa Spika, Azma ya Serikali kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 ni kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji/sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini. Kamati imebaini kuwepo kwa maendeleo makubwa yaliyofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Afya ambapo sekta binafsi imewekeza kwa kiwango kikubwa kwa kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa ambavyo vimechochea upatikanaji wa bidhaa za dawa nchini.

Mheshimiwa Spika, Licha ya Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za dawa nchini, bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazoathiri uzalishaji wa

bidhaa hizo na uwekezaji kwa ujumla. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo; -

(a) Bohari Kuu ya Dawa kucheleweshaji malipo ya fedha kwa wazalishaji wa bidhaa za dawa;

(b) Kuwepo kwa Mamlaka nyingi za udhibiti wa bidhaa za dawa na malighafi za kutengeneza bidhaa za dawa, kwa Mfano, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba -TMDA, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania-TAEC, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa SerikaliGCLA, Bodi ya Sukari Tanzania-SBT, Shirika la Viwango Tanzania-TBS na Wakala wa Vipimo-WMA;

(c) Uwepo wa utitiri wa kodi wakati wa uingizaji wa malighafi za kuzalisha bidhaa za dawa na baada ya kuzalisha bidhaa za dawa;

(d) Kukosekana kwa masoko ya uhakika ndani ya nchi kutokana na ushindani mkubwa wa bidhaa za dawa kutoka nje ya nchi ambapo bidhaa hizo huuzwa kwa bei ya chini. Mfano bidhaa za dawa kutoka India na China; na

(e) Kukosekana kwa nishati (umeme) ya uhakika viwandani jambo linalosababisha shughuli za uzalishaji kusimama kwa saa kadhaa.

Mheshimiwa Spika, Ili kuendelea kulinda wawekezaji wa ndani na kuboresha mazingira ambayo yatavutia wawekezaji wengi zaidi, ni vema Serikali kutafuta ufumbuzi kwa haraka na kutatua changamoto zote zinazowakabili wawekezaji hao ili kuweza kuimarisha zaidi uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa za dawa nchini.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025,

pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/2026 kwa Wizara ya Afya (Fungu 52), Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua kubwa ya kuhakikisha maboresho makubwa yanafanyika na hatimae kuwa na huduma bora za afya, kwani afya ndio msingi wa uhai na maendeleo ya mtu mmoja mmoja na hata taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ambao unalenga kuboresha zaidi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.

3.1 Kiwango Kidogo cha Utoaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2024/2025

Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyokusudiwa ikamilike mapema na kuwanufaisha wananchi.

3.2 Uhaba wa Rasilimali Watu

Serikali iendelee kutoa vibali vya ajira kwa sekta ya Afya kwani sekta hii ndio msingi wa nguvu kazi ya Taifa.

3.3 Ukosefu wa Mtaji Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Serikali itoe mtaji wa **Shilingi bilioni 300** kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ili kuongeza ufanisi na kuboresha upatikanaji wa bidhaa za Afya, kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kutosha. Kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

3.4 Madeni ya Bohari kuu ya Dawa (MSD) kwa Serikali

Serikali ilipe deni inalodaiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) lenye thamani ya **Shilingi bilioni 434.2**, kwa mchanganuo wa **Shilingi bilioni 46.4** kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya Wizara ya afya, Shilingi **bilioni 83.1** kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya OR-TAMISEMI na **Shilingi bilioni 305** za miradi

Misonge. Ni muhimu sana madeni haya yakalipwa katika kuendelea kuulinda mnyororo wa ugavi na kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa utoshelevu.

3.5 Madai ya Fedha za Mkopo za Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF)

Serikali ilipe **Shilingi bilioni 210,291,301,794.89** ambazo ilizikopa kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kuimarisha utendaji wa Mfuko huo na kutokwamisha uendeshaji wa mfuko huu.

3.6 Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

Serikali iwashirikishe wadau kutoka sekta binafsi katika kuchangia fedha za mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo, kwa lengo la kuongeza fedha za kusaidia matibabu kwa watu wasio na uwezo wakati wa utekelezaji wa sheria ya bima ya afya kwa wote nchini.

3.7 Kutokukamilika kwa Miradi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa

Serikali iweke kipaumbele cha kutoa fedha katika miradi ambayo imeanza muda mrefu ili ikamilike na kuanza kutoa huduma. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaa tiba ili kuleta tija kwa jamii.

3.8 Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA

Serikali isimamie matumizi ya mifumo ya TEHAMA kwenye Hospitali za Rufaa za Kanda kwa kuanzisha mfumo uitwao *Electronic Health Management System(eHMS)* kama ilivyo kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa, kwa kuwa mfumo huo umeonekana kuwa msaada mkubwa katika kurahisisha utoaji wa huduma na pia kuongeza mapato.

3.9 Sheria ya kusimamia huduma ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa Chembechembe na Viungo vya Mwili wa Binadamu

Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sheria inayosimamia huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na

viungo vya binadamu ili kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hii kwa wananchi.

3.10 Magonjwa Yasiyoambukiza

Ili kupambana na tatizo la magonjwa yasiyoambukiza, Serikali ifanye yafuatayo: -

a) Ifanye tafiti kubaini ukubwa wa tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza nchini;

b) Itoe elimu kwa jamii kuhusu vyanzo vya magonjwa hayo na namna ya kuyaepuka hususan kwa kuzingatia mazoezi na lishe; na

c) Ishirikishe sekta zingine katika utekelezaji wa afua za kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

3.11 Usajili wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

Serikali iunde bodi moja ya usajili wa vituo vya kutolea huduma za Afya nchini. Hatua hii itaweka ulazima wa vituo vya kutolea huduma za Afya vinavyomilikiwa na Serikali kusajiliwa kwa kukidhi vigezo kabla ya kuanza kutoa huduma.

3.12 Uimarishaji wa Viwanda vya ndani vya kuzalisha bidhaa za dawa

Ili uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa uweze kuleta tija kwa watanzania, Serikali ifanye yafuatayo: -

a) Iongeze kodi kwa bidhaa za dawa zinazotoka nje ya nchi ambazo zinazalishwa na viwanda vya ndani;
b) Ifufue kiwanda cha dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* ambacho serikali ina umiliki wa hisa za asilimia 40;
c) Iongeze kiwango cha uzalishaji wa dawa katika kiwanda cha dawa cha Keko *(Keko Pharmaceutical Industries)* ambacho Serikali ina umiliki wa hisa za asilimia 70; na
d) Itoe msamaha wa kodi kwa malighafi zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za dawa.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee nawashukuru sana Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama (Mb)-Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb)-Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Abdallah Shekalage, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ismail Rumatila na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Elias Magembe pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati inapotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina wa masuala mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika uandishi wa Taarifa hii. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - Mjumbe
7. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe

12. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Seif Salum Seif, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Agness Mathew Marwa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Jacquline Andrew Kainja, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Elibariki I. Kingu
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI
2 Juni, 2025

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii, kabla ya kuanza uchangiaji huo, nimejulishwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga kwamba kuna wageni wake 14, nao ni Walimu kutoka Makambako. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia, Mheshimiwa Waziri katika kitabu ambacho tumekipokea na hotuba uliyoisoma uliyosema iingine kwenye *Hansard*, ukurasa wa 16 kichwa cha habari pale juu utakuja uangalie kilipaswa kuandikwaje ili

uje ufanye marekebisho wakati unafanya hitimisho ili yaingie rasmi kwenye Taarifa Rasmi za Bunge hayo marekebisho utakayokuwa umeyaleta.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata fursa ya kuanza kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya. Ukweli ni kwamba, mengi yamefanyika, Wizara inafanya vizuri na Wabunge wenzangu ninadhani hii ni Wizara ya kuwapatia tu ushauri, lakini wanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na Jimbo langu la Musoma Vijijini. Ninasema inaenda vizuri na uthibitisho ni huu. Huduma za afya toka niwe Mbunge wa Musoma Vijijini ni kwa miaka hii minne, mitano mambo yamebadilika kweli kweli. Musoma Vijijini tuna Hospitali ya Halmashauri yenye hadhi ya Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vituo vya afya sita, tumepata tena fedha tunajenga kituo cha afya cha saba. Zahanati zinazotoa huduma ni 28, zahanati 24 ni za Serikali na zahanati tatu ni za binafsi. Sasa kwa mtindo wetu wa Musoma Vijijini huwa tunaanza kujenga sisi, halafu baadaye tunaomba Serikali itusaidie. Sasa hivi tunajenga zahanati mpya 18, lakini malengo yetu ni kujenga zahanati kila kijiji. Kwa hiyo, Musoma Vijijini tunajenga Shule ya Sekondari kila Kijiji na Zahanati kila Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magari ya wagonjwa tunayo saba; mawili mapya ya Serikali, matano Mbunge na rafiki zake waliyanunua. Kwa hiyo, kwa yote haya ninatoa shukrani kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais amewekeza na Wizara inafanya kweli kweli. Kwa hiyo, acha niende kwenye maombi mepesi ambayo ninajua na Wabunge wengine wataomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi waongezwe na madawa yaongezwe. Sasa, kitu cha muhimu sana ni kutoa ushauri. Ushauri wa kwanza ni hivi, kwa mazuri tunayoyafanya, tunapasa kujipima na tutumie hata vigezo ambavyo sisi tulishiriki kuvitengeneza.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kwanza kabisa, na Wizara hii tulishiriki vizuri sana mwaka 2015 *UN* zile *Sustainable Development Goals,* sasa ya afya ni namba tatu *SDG No. 3* ambayo ni *good health and wellbeing*. Hii ni kubwa mno, ninaomba Wizara kila tunavyokwenda mbele, rudini kweye hii *SDG No. 3* mwangalie kama tunaenda vizuri. Ikifika 2030, tutafanya kupitia mafanikio, lakini katika nchi za Kiafrika na labda duniani Tanzania itaonekana inafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipimo cha pili, sisi ni wanachama wa *WHO,* tena Mheshimiwa Profesa rafiki yangu, hongera sana. Sasa huko *WHO* lazima nako tuongalie wanatoa mapendekezo gani? Kwa mfano, uwiano wa daktari na wananchi wanaopaswa kutibiwa. *WHO* inapendekeza daktari mmoja kwa watu 1,000. Wengine wanasema, daktari mmoja kwa watu 4,000.

Mheshimiwa Spika, ninapenda hii ya daktari mmoja, watu 1,000. Maana ya daktari hapa ni yule mwenye shahada kutoka kwenye Chuo Kikuu kinachotambulika, ndiyo maana yake hiyo. Kwa hiyo, tukichukua mapendekezo hayo, sasa hivi Tanzania tupo watu takribani milioni 70, kwa hiyo, daktari mmoja kwa watu 1,000 Mheshimiwa Waziri anapaswa kuwa na Madaktari 70,000. Sasa, mimi sikutaka kwenda kwenye *database* yao, siwezi kulumbana nao, afadhali niongee haya mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2050 kwenye dira yetu ya maendeleo, tukifika mwaka 2050 kama tunazaliana sana na itategemea na *speed* yetu ya kuzaliana, lakini tuchukulie tutakuwa watu milioni 140. Kama ni watu milioni 140 ifikapo mwaka 2050 tunapaswa nchini kuwa na madaktari 140,000 kulingana na mapendekezo ya *WHO*.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ni lazima tujipime nacho ni uwiano wa ma-*nurse* kwa wagonjwa. *WHO* inapendekeza *nurse* mmoja kwa wagonjwa wanane, tunafanya vizuri lakini tunapaswa kujipima na kwenye maeneo kama ya *emergency;* na *Psychiatric Hospital* kama Milembe hapa wanataka *nurse* mmoja kwa wagonjwa wanne. Kwa hiyo, ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge, ukweli ni kwamba tunayo safari ndefu tumeanza kutembea, tusikate tamaa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la pili ni kwenye vifaa. Vifaa lazima tujipongeze, tumefanikiwa sana. Tukiviongea kwa lugha nyepesi nyepesi, mtu ataviona ni vyepesi vyepesi. Nimeshukuru kumsikia Mheshimiwa Waziri anasema tuna *CT-Scans* 45. Sasa ninaona niyaseme kwa kirefu ndiyo utaona umuhimu wake. *CT-Scanner* hiyo ni *Computed Tomography* ndiyo kule huwa ninawaeleza mambo ya *science*. Tunazo *MRI*, Mheshimiwa Waziri ametuambia tunazo 13 sasa hivi. Sikiliza, hii *MRI* ni *Magnetic Resonance Image*. Watu wa Sayansi tupo hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuna mambo ya *X-Rays* ambazo hata kule kwangu zipo. Mheshimiwa Waziri ameenda mbali, tumechukua ambazo ni *digital* za kisasa kweli kweli ambazo nyingine ni *fixed* na nyingine ni *mobile* za kumfuata mgonjwa alipo. Halafu kifaa cha nne kikubwa ni *ultrasound machines*. Mheshimiwa Waziri ametuambia tunazo 970.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa mchango wangu mimi hapa, hivi vifaa vyote vinne vikubwa wanasayansi watajua ni mambo ya *rays,* lakini *imaging techniques* ni *techniques* za *imaging,* kuona mwili kwa undani wake.

Mheshimiwa Spika, hapa pendekezo langu ambalo ni muhimu na lilifanya niombe kuchangia ni wataalam, ambapo tunao wachache sana. *Specifically,* hili eneo litatusaidia hawa lazima tusomeshe vijana kwenye eneo la *radiology*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu yatakuwa kama yale ambayo wakati sisi tulipoingia Chuo Kikuu tukiwa hatuna wataalam

wa madini, Serikali ikasema tusomeshwe kwa haraka sana, na tukasomeshwa kwa *speed* kweli kweli. Sasa, pendekezo langu, hii *radiology* ninapendekeza tuwe na vijana wanaosoma hii Shahada *GACC in Radiology* angalau 100 kila mwaka na tuwapeleke kwenye vyuo ambavyo ni vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa nini? Kwa sababu hivi vitatu vyote *CT-Scan, MRI, X-Rays* and *Ultrasound* tunavyo, tatizo huwa ni tafsiri sasa. Wameshapiga picha, wanakupatia wewe utafsiri, uweze kupendekeza matibabu. Hapo ndiyo penye kazi hapo, kuhusu tafsiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni sawasawa kama kwenye sekta mafuta unaweza ukafanya *exploration,* ukaenda kutafsiri ukasema hakuna mafuta, mwingine akarudi hapo hapo akatafsiri akasema kuna mafuta. Sasa ndiyo kama hii ya *radiology,* anaweza akatafsiri asione kuna ugonjwa, mwingine akatafsiri hicho hicho akasema kuna ugonjwa. Kwa hiyo, hapa tunahitaji wataalam, na ndiyo ninasema kwa lugha nyingine, tuwe na *marshal plan,* watu wasomeshwe kwa kasi kubwa sana kwenye shahada ya kwanza 100, kwa miaka mitano tutakuwa na watalaam 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nimalizie dakika moja. Hospitali zetu hizi mbili lazima tuzifanyie kazi. Kuna *Teaching Hospital* na *General Hospital.* Ni lazima tuwekeze sana kwenye *Teaching Hospital* kwa sababu inatoa kazi mbili, inatibu na kutoa elimu, na hapo ndiyo ninapendekeza na Hospitali ya jina la Mwalimu Nyerere, ile ya Mkoa wa Mara, *Memorial Regional Hospital,* tunaomba iwe ni *Teaching Hospital,* iwe ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Mwalimu cha Kilimo na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kuzungumza ndani ya Bunge hili Tukufu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake wa kipekee, pia ninawashukuru sana wananchi wa Buchosa kwa heshima waliyonipa ya kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyoongea leo, ninaweza nisipate tena nafasi ya kuongea hapo mbele; ninaomba nianze kwa kusema, nilipokuja Bungeni hapa, nilikuja na ajenda tano. Ajenda ya kwanza ni ajenda ya ku-*empower* wazawa wa nchi hii. Ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, tumefanikiwa kubadilisha Sheria ya Manunuzi na kwamba tumekubaliana bilioni 50 ni wazawa watakaofanya kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuja na ajenda ya *RPL* pamoja na kubadilisha *curriculum* zetu. Ninashukuru sana Serikali, kupitia Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba tumefanikiwa kurejesha *RPL* na sasa *curriculum* zimebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyingine ilikuwa ni kuhusu *National Innovation Fund*. Ninashukuru sana Serikali tumeanzisha Samia *Innovation Fund* kuwasaidia vijana wetu wabunifu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nyingine ilikuwa ni utumiaji wa rasilimali za nchi yetu kwa maendeleo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya jambo hili kwa umakini mkubwa, sasa tunaona utalii unachangia mapato makubwa kwa nchi yetu. Nina uhakika kabisa tunapokwenda ni kuzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajenda nyingine ilikuwa *NHIF;* nilipata nafasi ya kuzungumza na dada yangu Mheshimiwa Jesnista hasa ilikuwa ni juu ya mifumo kusomana. Mifumo kusomana ilikuwa ni changamoro kubwa. Nikienda Hospitali ya Kairuki kutibiwa, nikienda Muhimbili ninahitaji kurudia vipimo, matokeo yake ilikuwa inatokea *duplication*

of care na *NHIF* ikawa inaingia kwenye matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajenda yangu ya tano ambayo inafanya nizungumze leo ilikuwa ni juu ya ugonjwa wa Homa ya Ini. Mtakumbuka kabisa zungumzo langu la kwanza Bungeni lilikuwa ni kuhusiana na Homa ya Ini. Nilipata nafasi ya kusoma *data* moja mtandaoni mwaka 2014 iliyonionesha kwamba *prevalence rate* ya Homa ya Ini ilikuwa kubwa sana, na Tanzania ilikuwa ni asilimia sita. Jambo hilo lilinifanya mimi na wenzangu tuamue kufanya kampeni nchi nzima kuwaelimisha watu kuhusu ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, wakati ninafanya jambo hilo, dada yangu Grace Magembe alikuwa ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alikuwa Meck Sadick, na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Ilala alikuwa Meshack Shimwela. Tulifanya kampeni ile, lakini baadaye tuliambiwa tulikuwa tunasababisha taharuki kubwa, tukaamua kuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ninapozungumza *prevalence rate* ya *Hepatitis* katika Taifa letu bado ipo juu. Ninavyozungumza, *prevalence rate* ya Homa ya Ini ni sita mpaka nane. Hii inaonesha kwamba tatizo hili ni kubwa na Shirika la Afya Duniani limetamka kwamba, kufikia mwaka 2030 ugonjwa huu uwe *eliminated*. Imebaki miaka mitano tu, na ninavyotazama mimi ninaona kama haitakuwa rahisi kwetu ku-*eliminate* ugonjwa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini nimesimama kuzungumza? Nimesimama kuzungumza kuikumbusha Serikali yangu na nchi yangu juu ya umuhimu wa kutoa chanjo ya Homa ya Ini kwa watu wetu. Nimeshazungumza huko nyuma na ninazungumza tena leo. Ninaomba sana tuwachanje watu wetu, kwani ugonjwa huu upo na unazidi kuenea na watu wanapoteza uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumtibu mgonjwa wa *cancer* ya ini iliyosababishwa na Homa ya Ini inagharimu dola 50,000 kwa nchi kama Marekani, kwa India ni dola 20,000, kwa Tanzania hapa

inagharimu siyo chini ya milioni 30 kumtibu mgonjwa mwenye *cancer* ya ini na inawezekana asipone, lakini kumzuia mtu asiugue *cancer* ya ini inagharimu siyo zaidi ya shilingi 4,000 peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, nilishazungumza huko nyuma na ninaomba nizungumze tena leo. Ninakwenda kugombea Ubunge, nitarudi mwezi wa 11, nitaendelea na ajenda hii mpaka mwachanje watu wetu dhidi ya ugonjwa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kabisa; ninaomba nitoe historia fupi tu kidogo hapa ili niweze kueleweka. Chanjo ya Homa ya Ini mwaka 2002 Hayati Benjamin Mkapa aliamua kuwachanja watoto wote kwenye Taifa hili, kila mtoto anayezaliwa anachanjwa. Kuanzia mwaka 2002 mpaka leo 2025 ina maana ya kwamba watoto wote, vijana wote wenye umri wa miaka 25 ambao ni 70% ya watu wetu wamekwishachanjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, ninachokizungumza hapo ni nini? Ninaomba nisikilizwe vizuri hapo. Ili uweze kuwachanja watu wako wote unahitaji kuchanja 90% tu ya watu. Hiyo inaitwa *Herd Immunity*. *Herd Immunity* usichanje watu wote 100%, chanja 90% peke yake.

Mheshimiwa Spika, sasa, kwa *data* tulizonazo hapa sisi ni kwamba, ukichanja 90% ya watu milioni 60 Watanzania unatakiwa kuchanja watu milioni 54 peke yake. Milioni 54 ukiwachanja, katika milioni 54 hiyo ukiondoa watu ambao ni vijana wa miaka 25, unatakiwa kuchanja watu 37,800,000 ambao ni 70%. Ukitoa 54 ukatoa 37 unabaki na watu 16,200,000 peke yake, ambao ukiwachanja hao utakuwa umechanja 90% ya Watanzania wote. Maana yake ni kwamba, utakuwa umesababisha *Herd Immunity* kwenye nchi yako, utakuwa ume-*eliminate* kabisa ugonjwa wa *Hepatitis* katika nchi yetu. Sasa, kwa nini hatuchanji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niongee jambo moja, linaweza likawasikitisha watu wengi. Ni kwamba, ukinunua chanjo India leo ya *Hepatitis* kutoka Kiwanda cha *Serum India* utanunua kwa nusu ya dola, ambayo ni sawa sawa na shilingi 1,400 *approximately* (chanjo

moja kuinunua). Mtu anahitaji chanjo tatu ili aweze kuwa *fully recovered*. Kwa hiyo, tafsiri yake ni nini? Shilingi 1,400 mara tatu, ni kama shilingi 4,200. Mtu anachanjwa na anakuwa *fully protected,* lakini kwa nini hapa Tanzania tunashindwa kuchanja watu wetu wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mtu mmoja ana *monopoly* ya chanjo ya *Hepatitis* (kampuni moja tu). Ukienda kununua chanjo India leo kwenye Kiwanda cha *Serum* watakwambia hapana; chanjo hii kule Tanzania anashughulika nayo Bilakwate. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba huwezi kununua mpaka uje kwa Bilakwate. Huyu mtu mwenye *monopoly* hapa Tanzania anauza chanjo yake kwa bei kubwa, shilingi 10,000 kwa chanjo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba nisaidiwe, *MSD* waende moja kwa moja kiwandani wakanunue moja kwa moja kiwandani hii chanjo. Nimejipanga na nimejiandaa. Huyu mtu mwenye *monopoly* tunataka tumpeleke kwenye *Fair Competition Tribunal*, ili aweze kuondolewa hiyo kinga ya kununua peke yake. Tusipofanya hivyo watu wetu watazidi kuumia. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri anisikilize. Tumeongea jana kirefu sana mimi na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo langu hapo ni kuwa-*protect* watu wetu. Katiba yetu inatamka wazi kwamba, kazi ya kwanza ya Serikali itakuwa ni uhai, ni kushughulika na ustawi wa watu wake. Tukiokoa maisha ya mtu mmoja ni faida kubwa sana kwa Taifa letu. Sasa, hatuwezi kuwa nchi ambayo mtu mmoja ana *monopoly* ya kuuza chanjo ya *Hepatitis* katika nchi yetu, halafu ameachwa aendelee kufanya hivyo. Ninamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, yeye ni mzalendo katika nchi yetu. Tusaidiane kwenye jambo hili, *MSD* wakanunue wenyewe chanjo kiwandani ili chanjo hii iwe ya bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mtu mmoja, watu wetu wanashindwa kuimudu hii chanjo, wanashindwa kuimudu. Chanjo moja shilingi 10,000, chanjo tatu shilingi 30,000. Wangapi wataweza kumudu? Kama hilo haliwezekani, kama watashindwa

kumnyang'anya huyu mtu *monopoly*, basi *NHIF* wachukue dhamana ili chanjo iweze kutolewa na *NHIF* moja kwa moja kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema, ninafurahi ninazungumza mbele ya Profesa Janabi na Dkt. Shekalaghe wananisikiliza. Ninawaombeni sana tukafanye kazi ya kuwalinda na kuokoa maisha ya watu wetu. Tusipofanya hivyo watu wataendelea kupoteza uhai na sisi tupo tunaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niunge mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato ajiandae.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona kunipa nafasi hii ili nichangie, niungane na Wabunge wenzangu. Kwanza nianze sana kwa kumshukuru Mungu. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwaletea Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tumeona wakati Waziri anawakilisha kwamba kuna 1,600,000,000,000 na ushehe. Hii yote inaonyesha Rais ana dhamira nzuri na Watanzania kuhakikisha anawaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako watu wanasema kila kitu tunasema ameleta Rais Samia. Unajua hapa leo tunapitisha bajeti hii ya 1,600,000,000,000. Sisi tunapitisha, nani sasa mwenye kuidhinisha hela ziende? Watu wasijizime *data*. Mwenye kupitisha hela ziende kwa wananchi ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, niombe sana waone kwamba Rais anafanya kazi kubwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako watu wanamchora kama kamdoli fulani hivi. Niiombe Wizara hii ya Mawasiliano washughulike nao. Rais huyu ni tunu ya Watanzania, washughulike nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama pamoja na Naibu Waziri wake, pamoja na Katibu Mkuu. Kwa kweli tumeona tangu ameingia kwenye Wizara hii tumeona mageuzi makubwa sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Jenista na timu yake, anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi letu sisi kama Wabunge wenzako, tunamwombea sana kwa wananchi wa Peramiho kwa sababu yeye ni Waziri anafanya kazi katika Tanzania. Tunamwombea wananchi wa Peramiho, tunawaomba wananchi wa Peramiho waone kwamba iko haja urudi uweze kuwatumikia Watanzania wakiwepo na wa Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo wamesema wenzangu hapa, niseme mambo machache. Kwenye Wizara ya Afya kama tulivyosema wanafanya kazi nzuri, tuna tatizo sasa la ugonjwa wa watu, magonjwa ya figo. Sasa yamekuwa ni makubwa sana, tatizo hili limekuwa ni kubwa katika nchi yetu. Tuiombe Wizara ione kwa sababu tatizo hili sasa linahudumiwa na Mkapa, linahudumiwa na Kanda kule Mbeya na Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, tuombe sasa waone iko haja sasa ya kupeleka huduma hii kila mkoa kwa sababu hospitali za mkoa zipo nyingi, zimejengwa kila mkoa hospitali nzuri. Kwa hiyo, tuombe kila mkoa suala hili la wagonjwa wetu wa figo lishughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie sasa kwenye Jimbo la Makambako ambalo wananchi wake ninawapenda sana na wao wananipenda sana; lazima niwe mkweli. Kwa kazi nzuri iliyofanyika niliyosema ya afya, Makambako tuna vituo vipya vitano vya afya. Tuna zahanati zaidi ya 17. Kwa hiyo tunaipongeza sana Wizara pamoja na TAMISEMI kuhakikisha kwamba sisi Makambako tuna vituo vya afya na zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara, tuna Kituo cha Afya pale Ikelu ambacho Mheshimiwa Waziri alikuja yeye mwenyewe tuliungana na mimi kwenda wakati ule kwenda kuona ujenzi ambao unaendelea. Tunaomba washirikiane na Wizara ya TAMISEMI kuhakikisha tunapata fedha ili kituo hiki kiweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna kituo cha afya vilevile kule Usetule Kata ya Mahongole, kinaendelea. Tunaomba tupate fedha ili kituo hiki pia kiweze kukamilika. Pia, tuna kituo kingine ambacho kilianzwa kimesimama kule Kitandililo. Tunaomba washirikiane na TAMISEMI kuona kituo hiki kinaweza kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Ukanda huu wa Kusini Makambako pale tuna kiwanda cha dawa. Kiwanda hiki tunaomba waendelee kuhakikisha kinapata fedha kuhakikisha lile kusudio waliloanza kinaweza kukamilika, hasa kutengeneza dawa za vidonge pamoja na *syrup* kwa sababu kiwanda kipo. Watu wa Makambako na ukanda huu tunategemea sana kuona kwamba kiwanda hiki kitakamilika ili kiweze kutoa ajira za ndani na nje ya Mji wa Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Bima ya Afya. Suala la Bima ya Afya baadhi ya watumishi wetu unakuta wanapokwenda watu wenye bima hawahudumiwi kama ambavyo sawa na mtu anayetoa fedha taslimu. Jambo hili Wizara waliangalie wakishirikiana na TAMISEMI, kuhakikisha kwamba Bima ya Afya ni bima ambayo mtu amelipia, ni sawa na fedha taslimu. Kwa hiyo, isimamiwe kuona watu hawa wenye bima wanahudumiwa kama sawa na mtu ambaye amepeleka fedha pale dirishani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu; Serikali sasa imejenga vituo vingi, hospitali nyingi na zahanati nyingi. Tuhakikishe tunapeleka watumishi wa kutosha ili waweze kuwahudumia Watanzania katika vituo hivi ambavyo vimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, hili haliko kwenye Wizara yako lakini kwa sababu Serikali iko hapa. Mheshimiwa Waziri, pale

Makambako tuna madai ya fidia ya muda mrefu. Tunadai la fidia la umeme wa upepo ambalo wananchi wake sasa takribani zaidi ya miaka 10 na kitu wamezuiliwa hawawezi kufanya jambo lolote na nimekuwa nikifuatilia juu ya kulipa fidia wananchi hawa ili shughuli zao ziendelee, waweze kupata fedha waweze kufanya majukumu mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tuna fidia ya soko la Kimataifa ambalo Serikali ilishalipa fidia. Kuna wananchi walibaki 18 ambao uhakiki wao ulikuwa bado. Kwa hiyo, kwa sababu Serikali iko hapa Mheshimiwa Waziri, shirikiana na wenzako kuhakikisha wananchi hawa wanapata fidia, stahiki zao za watu 18 hela zilizobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna fidia nyingine ambayo ilikuwa kwa ajili ya kujenga ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa. *(Makofi)*

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, dakika moja ni *summary*. Fidia ya mwisho ni Idofi, kwa kujenga *One Stop Centre* kwa ajili ya kuondoa yale makaburi zaidi ya shilingi milioni 100 na kitu watu wa *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo nikupongeze wewe binafsi sana kwa kazi kubwa unayofanya. Kwa kweli lazima tuwe wakweli. Tunapata heshima sisi wenzako hata tukitembea. Juzi nilikuwa nchi moja huko, nilikuwa nchi za nje, wanasema unatoka kule anakotoka Spika Tulia? Nikasema ndiyo. Kwa hiyo, umetupa heshima kubwa sana kwa kuwa Mbunge wa Bunge la Dunia. Sisi wenzako tunakupongeza sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunampongeza vilevile, Rais wetu kwa kazi kubwa anazofanya za kuletea Tanzania maendeleo. Tunamwombea kule Mbeya, kule Mbeya, wasikie kule Mbeya. Kwa kweli kwamba wewe ni tunu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, Uyole, Uyole! Wananchi wa Uyole tunawaomba sana waone kwamba umuhimu wa kukupatia wewe. Ninakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe; Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato ninakuomba radhi kwa sababu muda uliobaki hutaweza kuchangia, utaanza kuchangia mchana.

Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo jipya la Uyole ujaye nakushukuru sana kwa nafasi. Pia, tuliona uliwauliza Wanauyole pale, wamekwishakuchagua tumeona kabisa hadharani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa, nimemsikia Mheshimiwa Waziri akisoma hotuba yake na akisema mafanikio makubwa sana ya kimbunga cha *Tsunami*. Nami kwa mafanikio hayo hayo ambayo yamefanywa na Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na mwanamke jemedari na mahiri sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Serikali yake yote kwa ujumla ya chama chetu, kwa kuendelea kuwekeza sana kwenye afya ya Watanzania ambapo tukiamini kwamba afya ndiyo msingi wa mafanikio yote. Mtu anaweza asiende shule, lakini akiwa na afya anaweza akatafuta njia mbadala ya kuweza kuishi. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa uwekezaji mkubwa sana kwa ajili ya ustawi mkubwa wa Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo unafanya na kipekee hapa Mheshimiwa Waziri

ninaomba nikushukuru sana. Tunashukuru sana kwa ile *ambulance* aliyotupatia Kituo cha Afya Kapele. Sisi Wanakapele na Wanamomba tunashukuru mno na tunaamini kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI wataweza kutusaidia kupata *ambulance* kwenye hospitali ya wilaya pale Chitete pamoja na *ambulance* kwenye Kituo cha Afya Mkulwe. Shangazi katika hilo tunakutegemea sana utaongea na pacha wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee sana ninaomba nimpongeze Naibu Waziri wake. Mheshimiwa Dkt. Mollel ni mtu muungwana ambaye kwa kweli ana mazuri yake. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mollel. Kwa kweli amekuwa ni daktari. Tunapompigia simu hata usiku wa manane tunapokwama na wagonjwa wetu kwenye hospitali za mikoa, amekuwa ni mtu mwenye msaada, anapokea. Amewasaidia Wabunge wengi sana. Kwa kweli katika wema huu ambao amewatendea watu, Mwenyezi Mungu azikumbuke na kuzitakabali hizo sadaka zake, amkumbuke Naibu Waziri Dkt. Mollel, aendelee kupokea simu hivyo kwa sababu unapomsaidia mgonjwa yule ni mhitaji, umekuwa umemkopesha Mwenyezi Mungu. Mungu ambariki sana na aendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi tunaomba tushauri mambo kadhaa kwenye eneo hili. Tunatambua kwamba wako kwenye mkakati wa namna gani tulete huduma ya afya kwa wote, kwenye Bima ya Afya kwa wote, lakini tuombe, kwa kuwa afya haiwezi kusubiri, wananchi wa Tanzania wameamua kuwasubirisha ili mambo yakamilike, lakini kuna mtu mwingine ameumwa leo, yawezekana Mwenyezi Mungu alikuwa amempa siku saba tu za ku-*survive* kwenye huo ugonjwa. Sasa na kama jambo hili litakamilika miezi mitatu ijayo au mwaka mzima ujao, mtu huyo anaendeleaje kupata huduma? Mtu huyo anaendeleaje kusaidika?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba, wakati michakato yote inaendelea na maboresho mengine kwenye Bima ya Afya yanaendelea, tunaomba vile vifurushi walivyovitoa vya Watanzania kupata huduma ambao wako kwenye Bima ya Afya ya *NHIF* tunaomba virudishwe, virejeshwe kwa sababu, siyo Watanzania wote

ambao wana uwezo na Watanzania wengi kwa ujumla matibabu yamekuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba hivi vifurushi virejeshwe kama ilivyokuwa hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mtu anapoenda kupima umeme kwenye moyo ana bima, lakini inabidi tena aongeze pesa nyingine aweze kurejesha. Mtu alijinyima akakata bima na familia yake ili iweze kumsaidia. Kwa hiyo tunaomba na nimekuwa nikiongea hapa na nimeuliza swali la nyongeza, vifurushi hivyo ambavyo wameviengua viweze kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa ambayo yameweza kutajwa hapa; kuongeza majengo, kuongeza vifaa tiba, kuongeza na mambo mbalimbali, viko baadhi ya vifaa hapa Mheshimiwa Waziri amevitaja kwamba Tanzania ndiyo nchi peke yake ambayo tuna hivyo vifaa (tunaongoza kwenye baadhi ya hizo nchi ambazo zinamiliki hivyo vifaatiba).

Mheshimiwa Spika, sasa, sisi tuwaombe. Wapo vijana wenzetu wa Kitanzania ambao wamesoma vizuri na wamemaliza masomo ya udaktari. Tunaomba katika ile changamoto ya kupungukiwa na watumishi, tunaomba vijana hawa waajiriwe kwa wingi ili tunatamani kwa kuwa vifaa vile vimeweza kuongezeka, matibabu yaweze kufanyika masaa 24. Kwa sababu, kuongezeka kwa vifaa hivi pia hatuwaombei Watanzania waumwe, lakini tunaamini na nchi za jirani ambao watakuja kutibiwa kwenye nchi yetu tutumie kama chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Spika, sasa, ninashauri, watu wakienda kutibiwa usiku kunakuwa tu kuna lile dirisha la *Emergency*. Baadhi ya kliniki zinafungwa, ni mpaka pawe asubuhi. Kama tumeongeza majengo, kama tumeweza kuongeza vifaa, tuwaajiri na vijana wa Kitanzania ambao hawajaajiriwa na wamesoma na wengine wamesoma kwa kutumia kodi za Watanzania walipewa mkopo, waingie kwenye ajira rasmi hospitali zetu ziweze kufanya masaa 24, ili hata watu wengine ambao wanatoka huko nje waje watibiwe tuendelee kujiongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wakija kutibiwa wenyewe asubuhi, sawa, lakini mtu mwingine akija akifika labda na basi saa 12, *whether* ametoka, Kenya ametoka Malawi, apate huduma atibiwe ili asubuhi aweze kurudi kwao.

Mheshimiwa Spika, tusitegemee dirisha la *Emergency* peke yake katika kutoa huduma, kwa sababu kliniki zingine zinafungwa kwamba daktari mpaka siku fulani na wakati mwingine hata wagonjwa kupangiwa ratiba, kwamba kuna daktari bingwa aje aonwe baada ya wiki mbili. Kama Mungu alimpa siku sita za huyu mtu kuweza kuishi, kwa hiyo mtu huyu ataweza kwenda kuondoka japokuwa Mwenyezi Mungu hapangiwi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ambayo tunayataja, yako baadhi ya magonjwa hapa nchini kwetu ambayo kwa kweli yamekuwa tishio. Katika hili pia tunaomba Serikali iendelee kuweka msamaha kwa sababu magonjwa haya yameonekana kuendelea kuchukua watu sana.

Mheshimiwa Spika, mwezi ulioisha tu mwezi Mei Jimboni kwetu Momba watu ambao wamekufa kwa kukosa matibabu ya kufanya *dialysis* ya figo, ni zaidi ya watu nane, unapokea na ndiyo hizo simu zingine ambazo tumekuwa tunampigia Mheshimiwa Dkt. Mollel.

Mheshimiwa Spika, sasa tutapigia watu wangapi? Ni watu wangapi ambao hawawezi wakamfikia Mbunge? Ni watu wangapi ambao hawawezi kuwapigia Wabunge wengine waweze kusaidika?

Mheshimiwa Spika, tunaomba matibabu, kwenye kufanya *dialysis* kwenye figo, aidha yawekewe msamaha au yapunguzwe gharama, ni kubwa. Watanzania wengi hawawezi kumudu hayo matibabu halafu ni *consecutively;* wiki hii uweze kufanya, uweze kusafishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anatoka Momba anaambiwa akafanye *dialysis* rufaa. Kutoka Sanja tu kufika Mlowo nauli ni karibu shilingi

20,000; utoke Mlowo uende Mbeya, hakuna Watanzania ambao wanaweza.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumefanya msamaha kwenye baadhi ya magonjwa tukatafuta, *whatever,* wahisani sijui kwenye *TB*, kwenye *HIV,* watu wanapata matibabu bure, tunaomba na kwenye figo iwe hivyo hivyo. Watanzania wengi wanakufa, kwa ajili ya kukosa matibabu ya kusafisha figo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili tunaomba sana. Miongoni mwa vitu ambavyo Waziri avipe kipaumbele kwenye bajeti yake, Mheshimiwa Waziri, kipaumbele kiwe ni kusafisha figo. Iwe bure kabisa na elimu kuenea namna ambavyo watu tuendelee kutunza figo zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugonjwa mwingine ambao tunaomba pia, tupate msamaha ni saratani. Kufanya hizo *chemo,* mionzi, kwa kweli, ni gharama sana. Watanzania wengi wanakufa, kwa ajili ya kwenda kufanya mionzi kwenye *cancer.* Licha ya kwamba, kuna Watanzania ambao hawana uwezo wa kufika huko India na maeneo mengineyo, lakini kufika tu hapo *Ocean Road,* mimi ninatolea mfano kwa sababu, ninatoka jimbo la kijijini na ni mbali sana; anafika hapo mtu hana ndugu Dar es Salaam, amechukua muuguzi akaendelee kumuuguza, wamepangiwa leo ufanye, baada ya wiki moja, baada ya wiki moja; matibabu yenyewe ni gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi tuombe watu wajitafutie nauli ya kufika huko *Ocean Road,* wajitafutie gharama kidogo namna ya kula, kama watachangiwa na ndugu, lakini matibabu haya yapunguzwe, kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. Kama tumewekeza miundombinu yote hii, tumeweka vifaa tiba vyote hivi, tunamaanisha kwamba, Mheshimiwa Rais wetu nia yake ni kuokoa maisha ya Watanzania wengi. Wakati mwingine hata mtu akiambiwa tu ana kansa, labda kansa ya uzazi, ameambiwa tu pale Meta, anaishia hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nauli tu ya kufika Dar es Salaam, vipimo hivyo atakavyoenda kutajiwa, namna ya kumwona daktari, mpaka amalize hiyo tiba miezi mitano, zote hizo ni pesa na ndiyo vifurushi hivyo vingine

wamevitoa kwenye bima. Kwa kweli, tunaomba haya magojwa mawili, figo na saratani, waweke msamaha Watanzania watibiwe bure kwa sababu, ni magonjwa ambayo yanaua watu na watu hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana hili lichukuliwe kuwa ni kipaumbele. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa, tunaomba atoe matumaini, ili wale wagonjwa ambao wako *Ocean Road* saa hizi wasikie kabisa kwamba, Wizara ya Afya imekusudia kuwasaidia, kwa ajili ya jambo fulani. Pia, hawa ambao wanafanya *dialysis* wanasubiri, wamepangiwa tarehe, wasikate tamaa, yaani mtu akitajiwa pesa tu anakata tamaa anaenda kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tulifanya jitihada kwenye *TB,* kwenye UKIMWI, watu wakaanza kuishi kwa matumaini na wanaishi na virusi. Watu wanasomesha watoto wanakufa uzee, tunaomba na kwenye haya magonjwa yasiyoambukiza tuweze kuyachukua kwa umuhimu wake, ili tusipange foleni kuendelea kuwapigia Mawaziri, kwa ajili ya kuomba msamaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu siku ya leo. Ninalo tangazo la wageni; leo tuna wageni wengi kidogo hapa Bungeni:-

Wapo wageni wangu wanne ambao wameingia baada ya tangazo la awali wakiongozwa na Saada Nasoro, ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Saada *Foundation*. Wasimame wote kwa pamoja. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Pamoja na kwamba, huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Waziri, lakini nimtambue kipekee kabisa; Dkt. Godlove Fred Mbwanji, huyu ni Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya. Sijui amekaa sehemu gani?

Haya, pengine ni kati ya wale ambao walishatangazwa wakati uliopita, lakini pamoja na hayo ninampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhudumia mikoa mingi kabisa ya Nyanda za Juu Kusini. Anajitahidi sana kwa kweli, anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii haimaanishi kwamba, wengine hawajashukuriwa, wameshashukuriwa na Mheshimiwa Waziri kwenye Ukurasa wa 218 kwa hiyo, wote mko humu, msijisikie vibaya. Huyu nimemtaja maalum kwa sababu, anatoa huduma moja kwa moja ambayo na mimi nafaidika. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine ambao wamekaa Jukwaa la Spika:-

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Afya. Yupo Profesa James Mdoe, Mwenyekiti wa Bodi, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NMRI). Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Sophia Janabi, hili jina mmeandika hapa, labda Janabi litakuwa la mwisho; Sophia Byanaku Janabi, Mke wa Profesa Janabi. Karibu sana, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Asimame tena, hatujamwona

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, aaha! Amesimama haraka?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Haya karibu tena Sophia, usimame tena, hawajakuona Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya wananchi. Haya, ahsante sana. Nadhani Wabunge hapa na wananchi wote wana jambo la kujifunza na ndiyo mlichokuwa mnasisitiza. Sasa mmejifunza kwamba, siyo mambo ya, "ninachosema nini usifuate, fuata nini? Haya, ninachosema na Kutenda ndiyo hicho hicho. Kwa hiyo, karibu sana Sophia, Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia, wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri. Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Maafisa kutoka Wizarani. Wasimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Waganga wafawidhi hospitali za rufaa za mikoa. Karibuni sana Bungeni. Ahsanteni sana, ninyi pia, kwa sehemu yenu mnafanya kazi nzuri sana. Waheshimiwa Wabunge huwa hawapigi makofi mengi hivi bure bure kwa hiyo, tunawashukuru na ninyi kwa kazi nzuri mnayofanya kwenye hospitali zetu za rufaa za mikoa. *(Makofi)*

Wapo Viongozi wa Shirika la Dawa Asili na Ulinzi wa Mazingira. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wadau wa Maendeleo kutoka Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa; *UNICEF, UNFPA, World Bank, United Kingdom Embassy, Health Summit, COFI* na *MDH*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Madaktari Bingwa wa Kampeni ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakiongozwa na Dkt. Caroline Mayengo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, madaktari hawa pia, wamefanya kazi kubwa sana kwenye hii kampeni na wamepita maeneo mengi, ambayo kwa kweli, wameleta suluhu katika changamoto nyingi kabisa za wananchi ambazo hazikuweza kupatiwa ufumbuzi kwa utaratibu ule wa kawaida. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tunaamini mtaendelea kufanya kazi hiyo, hata kama kampeni itakuwa imekwisha. Tunaamini mtakuwa mmejiwekea mazingira ambayo mmetengeneza mtandao, ambao mnaweza kufanya kazi pamoja, mkawa mnasafiri huko mikoani na kuendelea kutoa huduma kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wenyeviti wa Bodi wa Mabaraza ya Kitaaluma. Karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Viongozi wa Chama cha Wauguzi Tanzania *(TANA)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wadau wa Taasisi za kifedha kutoka Benki ya *NMB* na *CRDB.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunalo Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi *(NACOPHA)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 18 wa Mheshimiwa Deo Sanga. Nilikuwa nimeshawatangaza na walisimama tayari.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, ambaye ni Ndugu Vincent Saguda kutoka Chuo cha Diplomasia Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge tutakaoanza nao michango mchana. Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokwenda.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

(Saa 7.11 Mchana, Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kwenye hoja iliyo mbele yetu. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge ajiandae.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi mchana huu au jioni hii kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya Afya. Awali ya yote ninapenda sana kumshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele. Ninapenda sana kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano kwa pongezi nyingi alizozifanya katika sekta ya afya na sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuwashukuru sana, kuwapongeza sana Mawaziri. Waziri Jenista Mhagama ambaye ni dada mchapakazi. Mwanafunzi mwenzake kipindi cha nyuma aliwahi kusema, Jenista aliwahi kusema; *"I am born a Leader and I'll die a Leader."* Leo katika umri huu ninamwona akiwa *a Leader*, mengine ya mbele sisemi. Ninapenda kumpongeza Naibu Waziri Dkt. Mollel, kwa jinsi anavyopangua maswali kisomi kwelikweli. Anaitendea haki taaluma yake, anakitendea haki Chuo chake cha Muhimbili na mimi nikiwa sehemu ya chuo hicho. Hongera sana kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninaomba nijikite mchango wangu katika Wizara hii. Baada ya pongezi zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa Rais kwa jitihada zake za kuboresha sekta ya afya, mimi leo ninaomba nijikite katika

mwendelezo wa kazi katika Wizara hii ya Afya. Nitajikita katika jambo moja la kuzuia, au kinga. Katika afya kuna kutibu na kukinga, hivi vyote vinakwenda sawa, lakini moja inatakiwa iwe juu zaidi ya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu, au kwa tafiti nyingi zinaonyesha kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Kama tutaweza kuwekeza zaidi katika kinga tutaokoa fedha nyingi sana katika tiba. Sasa basi, nianze kwa kusema kwamba, Wizara ya Afya, hebu tujikite zaidi katika suala la visababishi vya magonjwa. Magonjwa mengi au takriban yote yana visababishi; na hii siyo kwa Wizara ya Afya tu, ni kwa wizara zote, kwamba zinachangia katika usababishi wa magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni kisababishi vya magonjwa, *waterborne diseases*; barabara ni visababishi vya magonjwa, ajali nyingi za bodaboda; ukienda kwenye Wizara zote za viwanda ni visababishi; ukienda kwenye shughuli zote za kibinadamu, wanyama, mifugo ni visababishi vya magonjwa, *Rift Valley Fever*. Tukiwekeza zaidi katika visababishi tutaokoa fedha nyingi na wagonjwa watapungua hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mfano mmoja, mtu unapokwenda kuchota maji kwenye bomba lenye koki, ukifika pale unafungua koki, maji yanajaa kwenye ndoo. Ukiondoka na ile ndoo ukaacha koki na maji yanaendelea kutiririka na ukaenda kuyatumia maji na huku koki hujafunga maji yale yatatiririka bila sababu, halafu unarudi tena unakuta maji yanaendelea yamepungua. Kwa hiyo cha msingi katika mfano huo, ni kufunga koki pale unapojaza ndoo yako ya maji; ukayatumie, halafu ukirudi ufungue tena koki utumie. Ninamaanisha nini, wagonjwa walioko hospitali waendelee kupata tiba na wale walioko nje wasiendelee kupata magonjwa ili kwenda kujazana hospitali. Tuwekeze katika visababishi vinajulikana. Magonjwa yote yanajulikana, iwe malaria iwe *cancer*; iwe figo; iwe *pressure*; iwe moyo, vyote vina visababishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Profesa Janabi. Profesa Janabi popote alipo ninampongeza sana asisahau kutuhimiza, kutuelezea visababishi vya magonjwa ili tusirundikane hospitali. Ninasisitiza kwamba tuendelee kuwekeza katika afya ya jamii, afya ya jamii itatusaidia kupunguza wagonjwa hospitalini. Mgonjwa mmoja anapokuwa hospitalini anakuwa na wategemezi wa kumhudumia, anakuwa na wategemezi wa kumpelekea chakula na kwenda kumwona, muda ule mwingi wa watu kurundikana hospitali unapunguza nguvu kazi. Kwa hiyo tukipunguza kuwa na wagonjwa wengi watu muda mwingi watautumia kufanya kazi badala ya kuwa hospitalini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Muhimbili katika Kitengo cha Mifupa, walioko pale wamejazana ni wagonjwa wa ajali za bodaboda. Ajali za bodaboda zinazuilika; kwa nini hawa watumia bodaboda wasichukue tahadhari? Kwa nini wasivae *helmet*? kwa nini wabebane mishkaki? *Balance* ya pikipiki inakosekana. Mtu ameweka mtoto mgongoni, amebeba mzigo, mama yeye, wakianguka ni watu wanne hapo wameumia, Serikali inabeba mzigo mzito. Hebu Wizara zote ziingie katika vita ya kupunguza visababishi vya magonjwa ili Wizara hii fedha inazopewa iweze kutumika ipasavyo na kusiwe na manunguniko katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari hawatoshi kwa sababu wagonjwa wanaongezeka; lakini visababishi vikipungua tukiwekeza zaidi katika kinga madaktari watafika mahali hata wao watakuwa wanawasikiliza Wabunge, watakuwa wanasoma magazeti, watakuwa wanachangia vitu vya maana. Kwa sasa madaktari wako *busy*, wahudumu wako *busy*, kwa sababu kila dakika hawa wanaingia, hawa wanatoka, hawa wanaingia hawa wanatoka. Ifike mahali mahali watu wabaki wafanye kazi za uzalishaji mali na hawa walioko hospitalini, kwa sababu hatuwezi kuzuia kabisa, waendelee kupata tiba vizuri, tutakuwa tumeokoa pesa nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika vyuo vikuu; kama mwakilishi wa vyuo vyote kuanzia vya chini mpaka vyuo vikuu, hebu tuongeze udahili wa wanafunzi watakaoenda kusomea masuala ya

kinga, waongezeke. Ili hawa wafanye kazi ya kurudi katika vijiji mpaka sehemu zozote kutoa elimu juu ya visababishi vya magonjwa mbalimbali. *Public health* (afya ya jamii) nayo ipate kipaumbele katika vyuo vyetu vyote vinavyotoa wauguzi na madaktari. Hawa watakaporudi kule watasaidia kuchagiza elimu ya afya ya kujikinga na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi niseme tu kwamba, hivi visababishi vikidhibitiwa na siyo kwa Wizara ya Afya tu; Wizara ya Mambo ya Ndani ikidhibiti; Wizara ya Maji, ikidhibiti; Wizara ya Mifugo, ikidhibiti, Wizara zote haya ya Elimu ikidhibiti, ninamwona Waziri wangu wa Elimu pale; vyote vikidhibiti tutakuwa tumepunguza visababishi vya magonjwa, wagonjwa wale ambao walikuwa wanaumwa kwa sababu kuumwa mtu huwezi kuchagua, nitaumwa tu, lakini tutapunguza msongamano wa magonjwa na tutapunguza gharama ya matibabu, tutaipunguzia Serikali mzigo wa fedha nyingi ambazo zinatumika isivyo lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu wengi hawajui, mtu akiumwa kitu fulani anakimbilia "ooh! leo ninaumwa, ninaumwa shingo, Mheshimiwa nitumie hela, ninataka nikapime *CT scan*, ninataka nianze *chemo*, hata hajui *chemo* ni nini, hata hajui hiyo shingo ni nini, kwa sababu hatujui visababishi vya magonjwa, mtu anakuja kujua visababishi ameshachelewa; kwa hiyo anaanza matibabu kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi watu wameongea kuhusu mambo ya figo ambayo yanazuilika. Figo zinajulikana visababishi vyake ni nini, Kisukari inajulikana, lishe duni, hebu tuwaelimishe watu kuhusu lishe, hii imesemwa sana Bungeni. Lishe ni moja ya visababishi vya magonjwa mengi. Watu wanafikiri kwa kula vizuri, kwa kula hivi basi hapo wamefika, visinia mtu anafakamia tu kila aina ya msosi mwenye umri mkubwa kama mimi, kumbe anajiingiza katika matatizo ambayo tiba yake ni gharama kubwa. Ninawaomba Mawaziri hebu tuzingatie suala la lishe ili watu wajue, kwamba katika umri fulani wanatakiwa kula nini. Pawe kabisa na vijarida vinavyoonyesha mtu anakula nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ninawapa hongera sana Mawaziri, wachape kazi, tuko nyuma yao. Mungu awabariki sana pamoja na Mawaziri wengine. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Nahato, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Tabasam Hamis, wajiandae Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila na Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa sehemu ya wachangiaji katika bajeti hii ya Wizara ya Afya. Ni kwamba, Wizara ya Afya imebeba dhamana kubwa sana katika nchi yetu; lakini ni Wizara ambayo hivi tunavyozungumza yako mambo mengi sana ambayo Wizara ya Afya, bado Serikali yetu haijaweka kipaumbele kikubwa sana katika Wizara hiyo. Tunaipongeza Wizara ya Afya, pamoja na kuwa na watumishi wachache, lakini wameweza kufanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kuwa Watanzania wanakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mbadala katika afya, binadamu anatibiwa, lakini binadamu hana *spare* kwamba unaweza ukaweka *spare* mpya akarudi kuwa mpya, linakuwa ni jambo kubwa sana. Ikifikia mtu kuumwa, akaugua mtu au wazazi au nani, kwa hiyo ni jambo ambalo familia yote inakosa amani; na hasa wakiugua watoto wadogo na wakiugua akinamama. Halikadhalika sisi ambao labda ndiyo nguvu kazi ya familia, ukaugua baba, ukawa uko kitandani. Kwa nini ninayasema haya, ni kwamba Serikali imejitahidi sana kuboresha miundombinu ya afya nchini, hakuna mahali katika nchi hii ambako Serikali haijaweka mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana katika miundombinu. Kwa mfano, mimi tu nimeingia katika Jimbo la Sengerema, tumejenga hospitali ya wilaya mpya kabisa. Katika hiyo hospitali ya wilaya bado pamoja na kujengwa kwake ina mambo mengi sana ambayo bado yamepungua, lakini ina vifaa vingi sana vipya vimepelekwa pale katika ile hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, tumekwenda naye katika hospitali ya wilaya, tumekwenda naye *DDH* ameona, lakini tumekwenda naye katika hospitali ya wilaya iliyojengwa kwa ajili ya halmashauri yetu. Tumepewa mitambo mingi, vifaa viko vingi, lakini tumejengewa vituo vya afya, tumejenga vituo vya afya zaidi ya sita. Wizara ya Ujenzi ilitupatia majengo kwa ajili ya kituo cha afya sehemu inayoitwa Busisi, pia pale tulikwenda na Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda kuangalia wakati wanapokea majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini ninasema hivyo; sisi tuna zahanati kama 31, tuna zahanati mpya tena zimepata fedha, zimejengwa kama zahanati 13. Katika vijiji tulivyonavyo, vijiji 71 pia navyo vina ujenzi wa maboma unaendelea. Tuna zaidi ya maboma 30 ya zahanati hizo mpya, tuna vituo vya afya na vyenyewe vimeshapata vifaa vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri zaidi tunaishukuru Wizara ya Afya, wametuletea majokofu kwa ajili ya mochwari mpya. Tumepata majokofu katika Vituo vya Afya vya Kagunga pamoja na Katunguru; na hivi tunategemea Mungu akijaalia tunapata katika Kituo cha Afya cha Ngoma; Butimba; na Kituo cha Afya Kijuka; Kituo cha Afya Kanyerere; na Sima. Hii inaonyesha kwamba Serikali imefanya jitihada za kuwekeza miundombinu kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii madaktari imekuwa shida kubwa. Pamoja kuajiri wahudumu wa afya na madaktari, lakini huwezi kuwa na vituo vya afya saba, ukiweka na vituo vilivyokuwepo vitatu na vituo vya afya 10, hospitali ya wilaya lakini hakuna daktari bingwa katika wilaya. Sisi katika Sera ya Afya tulikuwa tumekubaliana kwamba kila wilaya itapata angalau *surgeon* mmoja na itapata *physician* mmoja. Sasa imekuwaje kwa hili jambo kukosekana? Kwa sababu kuna magonjwa ambayo yangeweza kutibika huko huko katika wilaya zetu, lakini sasa tunalazimika kwenda katika hospitali za rufaa, hali inakuwa ni mbanano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaonekana tumebanana kifedha, kwamba bajeti yetu si nzuri, hizi hospitali za wilaya katika nchi, kwa nini hawa madaktari bingwa wasiwe wanakwenda kwenye hizi wilaya? Kwa mfano, siku ya Jumatano labda, tunajua leo daktari bingwa atakuwepo siku ya Jumatano, madaktari bingwa wawili kila mwezi wanakwenda angalau wanakuwepo pale mpaka hapo tutakapokuja kupata madaktari bingwa. Inakuwaje mifumo haisomani kati ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya? Hili jambo Serikali ni moja, baba mmoja, mama mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo tunaomba sana Bunge lako lielekeze kwamba hao madaktari bingwa sasa wawe na siku maalum, tujue kama ni *surgeon* anakuja wa mifupa anapatikana Jumamosi ya kila wiki, wananchi wenye matatizo badala ya wote kurundikana Muhimbili; kurundikana Benjamin Mkapa; kurundikana *Mbeya Hospital*; kurundikana labda Mount Meru sasa hivi vitu vya namna hii tunaona kama vile tunajikwamisha sisi wenyewe wakati tumetekeleza mambo makubwa sana katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka nilizungumze katika hili suala ni kwamba, sisi Sengerema pale tuna hospitali yetu *DDH*. Hii hospitali imeanza kutoka huduma tangu mwaka 1953, mwaka 1953 mpaka leo ni zaidi ya miaka 72; leo ndiyo tunakuja kupata mwaka huu sisi hospitali yetu ya wilaya. Kwa hiyo hawa wenzetu *Roman Catholic* wamefanya kazi ya kuihudumia jamii katika Kanda ya Ziwa kwa muda mrefu, miaka 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameomba tu nafasi kwamba, wao wawe hospitali ya rufaa, wasajiliwe kuwa hospitali ya rufaa kwa sababu wana kila kitu. Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuja Sengerema na ameona wana *theatre* za kisasa; wana umeme wao *megawatt* kama tano ambazo wanaweza wakahudumia ile hospitali; wana mifumo ya maji; wana kila kitu *tools* za macho, yaani kila kinachoweza kufanywa katika hospitali ya rufaa wale *DDH* Sengerema wanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda huo sasa mpaka uje uvuke kuja kuingia Mwanza tunamshukuru Mungu tumepata daraja lakini hata

kama hawa wanaoletwa kutoka Kigoma, kutoka Ngara wapi lazima wavuke Sengerema. Kwa nini wasiifanye Sengerema ikawa hospitali ya rufaa? Hatukatai, tunakubali wameweka Ukerewe lakini na sisi Sengerema tupo ng'ambo kuna wilaya zinazoweza kuhudumiwa na ile *DDH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo ukija kwenye majumuisho yake tuone kwa sababu wamejitahidi wameshapeleka kusomesha madaktari wanne kuwa *specialist,* wao wenyewe kwa pesa zao. Kwa nini Serikali isije ikawapa wale ma-*specialist* watatu tu tuka-*qualify* ili iweze kusajiliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ambayo tumeyaomba hapa sisi tuweze kuhudumiwa kama Hospitali ya Rufaa *DDH* Sengerema. Ina vitanda zaidi ya 400 ina kila kitu ile hospitali. Mheshimiwa Waziri kama atakubali hiki kipindi ambacho tunakimalizia hiki cha muda wa mwisho, aje Sengerema yeye mwenyewe aje ajionee. Katibu Mkuu anajua hii hospitali, yeye anajua, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua hilo jambo, tunawaomba sana kwamba wangekuja Sengerema tukaja tukaona na sisi wakatupa nafuu, tuna visiwa, tuna nini. Kwa hiyo moja ya tatizo letu kubwa ni hilo ambalo limebaki lakini kwa shughuli zingine zote sisi tunaipongeza sana Wizara ya Afya kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini tunaiomba Serikali iongeze bajeti hii bajeti iliyotajwa kwa Wizara ya Afya sisi tunaona kama haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imesikia hapa kila Mbunge anayesimama hapa anaona kama bado tuna matatizo makubwa hasa katika magonjwa haya haya makubwa kama magonjwa ya figo. Tulizungumza mwaka jana wakasema watalifanyia kazi, sasa tunaomba mwaka huu Serikali iliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninataka kuzungumzia ni suala la tiba asili. Ndugu zangu bila kufichana mwaka jana na mwaka juzi *CORONA* ilitutesa sana hapa Tanzania, lakini tiba asili ilifanya kazi. Tulichemsha chai za rangi hapa, chai dawa tukaweka vitunguu swaumu, tukaweka tangawizi, limao, ndimu, na majani ya ndimu tukajifusha sisi wenyewe. Watu wa tiba asili wamefanya kazi kubwa

sana lakini hatujajua je, hawajagundua tu kwamba tiba asili imesaidia kiasi gani? Mbona wakija hapa wanatoa maelezo, nimesoma hotuba yako Mheshimiwa Waziri hakulizungumza kabisa suala la tiba asili hawa watu anawasaidia namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tu wametambulishwa hapa watu wa tiba asili, lakini yapo magonjwa kama kifafa hayatibiki hospitalini hawa wanatibu. Sasa hivi wanatibu mpaka kisukari, wanatibu magonjwa mengi sugu, mpaka ini wanatibu watu wa tiba asili. Hebu sasa tuwatambue vizuri na leseni zao huko vijijini zimekuwa shida sana kupatikana, kwa hiyo unakuta mganga...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Tabasamu.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja nimalizie.

MWENYEKITI: Ninaomba malizia hiyo.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia tu; ni kwamba hebu wapunguze hizi leseni na huu urasimu wa kupata leseni watu wa tiba asili wauondoe. Kwanza leseni za tiba asili zingekuwa bure tu hawa watu wanatusaidia sana maeneo ambapo hakuna hospitali wametulinda kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge. Mheshimiwa Neema Mwandabila Mheshimiwa Jacqueline Kainja na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu wajiandae.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mungu mwenye enzi na utukufu kwa kuniwezesha kusimama mahali

hapa muda na wakati kama huu. Pia, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu wake kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii ya Afya, hakika mimi sina mashaka na uzoefu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwa kushirikiana na watendaji wote wa Wizara ya Afya katika Mkoa wetu wa Tanga, hakika wananchi wa Mkoa wa Tanga tumejawa na shukrani nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeletewa zaidi ya shilingi bilioni 158 kwa ajili ya miundombinu ya afya pamoja na vifaatiba. Tumeweza kujenga zahanati 72, lakini na kuweza kukarabati hospitali za wilaya sita pamoja na hospitali nyingine tatu. Vilevile, tumeweza kutengenezewa vituo vya afya 23 ndani ya Mkoa wetu wa Tanga hakika mioyo yetu imejawa na shukrani na hatuna namna nzuri ya kumzungumzia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zaidi ya tunu ya Taifa hili ambalo tutailinda na kuitetea kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile niseme kwamba, licha ya mambo mazuri ambayo wametufanyia bado wananchi wa Mkoa wa Tanga *especially* Wilaya ya Korogwe pale Hospitali ya Magunga, tunaomba sana Wizara hii ya Afya iendelee ku-*influence* hospitali ile kongwe ya muda mrefu sana ambayo mara zote imetengewa fedha na fedha zile haziendi kwa hiyo matengenezo hayajaweza kufanyika Hospitali ya Wilaya ya Magunga – Korogwe. Tunaomba sana hospitali ile na yenyewe ipewe kipaumbele ili kuendelea kuzienzi fikra za viongozi watangulizi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiangalia hospitali ile ipo kwenye *highway* ya kutoka Tanga kwenda Kilimanjaro ambapo ajali nyingi zinatokea. Wametuwezesha tumepata idara ya dharura tunashukuru sana, lakini bado jengo lile kwa maana ya *main building* ya hospitali ile. Tunaomba msaada ili tuweze kuishi kwa kupata huduma nzuri za afya kama ambavyo zimetamalaki sehemu zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka niliwahi kuuliza swali hapa na Mheshimiwa Dkt. Mollel alilijibu vizuri kuhusiana na Benki ya Kijerumani ambayo inaitwa *KfW – Germany* ambayo imekuwa ikitoa huduma za bima za afya kwa mama na mtoto. Benki ile ilikuwa inafanya kazi kwa muda mrefu Mkoani Tanga na wanawake na watoto waliweza kunufaika, lakini baadaye walisitisha huduma ile na kwenda kwenye mikoa mingine. Niliomba kujua ni kwa nini huduma ile imesitishwa Tanga na Mheshimiwa Dkt. mollel alijibu vizuri kwamba tutaweza kufanya mazungumzo na benki ile ili huduma ile irejee Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye katika kufuatilia hospitalini nilipata taarifa kwamba wameshakubaliana na Benki ile ya *KfW – Germany* kurudisha huduma ile Mkoani Tanga, lakini mpaka sasa ni kimya sijapata mrejesho wowote, nitaomba sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa ku-*wind up* hoja yake nisikie neno kuhusiana na jambo hili kwa manufaa na mustakabali mpana wa wanawake wa Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile kuchangia kipengele cha 41 cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Jenista Muhagama. Amezungumza vizuri kwamba kama Taifa tumeimarika katika huduma za ubingwa bobezi na amezitaja huduma za ubingwa bobezi ambazo tumeimarika nazo ni pamoja na upandikizwaji wa vifaa vya usikivu. Niipongeze Serikali hakika tume-*save* fedha nyingi kwa suala hili la upandikizaji wa vifaa vya usikivu. Watu walikuwa wanapelekwa India na *surgery* ile ya *cochlea implant surgery* ni milioni *35 USD* ninakumbuka, *35 thousand USD* ni gharama ya *cochlea implant surgery* moja. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali imefanya jitihada kubwa kutatua changamoto hii, lakini niseme kwamba Serikali bado haijakwenda kwenye chanzo cha tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha tatizo si kwa watoto wetu kufanyiwa *cochlea implant surgery*; chanzo cha tatizo ni kujua ni kwa nini watoto wetu wanachelewa kujulikana kama wana usikivu hafifu wakati wanapozaliwa. Ninaiomba Serikali kama ambavyo wameweza kuanzia *ABR test* pale Muhimbili kwa maana ya *Auditory Brainstem*

Response test Muhimbili, tunaomba kwenye wilaya zetu vifaa vile vya kupima usikivu watoto mara tu watoto wanapozaliwa viende kwenye wilaya zetu yote hili jambo linawezekana. Serikali inatumia fedha nyingi kwa wenye ububu na uziwi wanajenga shule lakini *not only that* tumeona jinsi ambavyo ububu unaongezeka. Niliwahi kutoa *records* hapa, hela Serikali inayotumia ilitoka kutoka bilioni tatu mwaka 2022 imefika mpaka bilioni sita imeji-*double*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake idadi ya bubu na viziwi nchini inaongezeka, maana yake ni nini? Tunakwenda kuathiri *human resource* ya nchi hii na tunakwenda kuwapa ugumu uzito wazazi wanahangaika na watoto wa namna hii. Niiombe Serikali iseme kitu itakapokuja ku-*wind up* ni nini mpango wake katika jambo hili? Wanafanya katika *level* ya juu sana, lakini mtoto mara anapozaliwa iwe ni *compulsory* kupimwa usikivu na kupimwa usikivu katika nchi za wenzetu siyo hata *expensive* ni kama shilingi 15,000 ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuzungumza na Dkt. Edwin, Dkt. Edwin ambaye ni bingwa wa *ENT* amewahi kusema kile kifaa cha kupima usikivu mtoto anapozaliwa ukiacha hii *ABR Test* haizidi milioni 15. Ninaomba Serikali katika vifaatiba ambavyo watavipa kipaumbele kwenye wilaya zetu. Ninaomba na vifaa hivi vya usikivu ili kukuza Taifa la watoto wenye weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie, ninazungumza kitu ninachokijua vizuri mimi na mume wangu kama tungekuwa ni wazazi ambao hatuna uelewa wa kutosha, mtoto wangu wa kwanza mimi angekuwa bubu au kiziwi kama siyo kuhangaika kufika mpaka India na hali kadhalika, mpaka leo tunapata *challenge* ya kumfundisha...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa wapi? Mheshimiwa Esther Taarifa.

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza ninampongeza kwa mchango anaotoa Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, lakini ninataka tu nimpe taarifa tunavyo-*address* wenzetu ni vyema kusema watu wenye ulemavu wa kusikia *either* kuona na kuongea kuliko kusema ububu, na; uziwi watu wenye ulemavu wa kusikia, watu wenye ulemavu wa kuongea na watu wenye ulemavu wa kuona. Ahsante!

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Injinia Ulenge unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipokee tu kwa maana ya tafsiri kila mtu anaweza akaizungumza anavyoweza yeye, ninashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachoweza kusisitiza ni kwamba vifaa vile vya kupima usikivu mara mtoto anapozaliwa siyo ghali kiasi ambacho Taifa letu kushindwa kuvinunua. Ninaomba msisitizo huu, vifaa hivi viweze kupatikana katika hospitali za wilaya jitihada walizozifanya ni kubwa sana katika *level* ya hospitali ya Taifa, ninaomba hili jambo nilisikie likisemwa katika vipaumbele vya Wizara wakati watakapo-*wind up* hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri, dada yangu...

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ikupa, Taarifa.

TAARIFA

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niweke *record* sawa kwa sababu Mheshimiwa Ulenge amepokea taarifa, lakini jinsi ya tunavyoyatumia maneno haya zamani tulikuwa

tunasema wasiosikia, lakini sasa hivi tunaita viziwi. Kwa hiyo, hatuiti tena wasiosikia, tunaita viziwi na wale wenzetu ambao wana ulemavu wa macho tunaita wasioona na kwa sisi walemavu wa viungo (waliokuwa wanaitwa viwete) sasa hivi tunaitwa walemavu wa viungo. Kwa hiyo, *terminologies* zipo hivyo sasa hivi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Ulenge unaipokea?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa tafsiri hizo nzuri, ninaomba ulinde muda wangu tafadhali. Ninataka kusema kwamba hili la vifaatiba hivi vya usikivu kwa maana vipimo vile vya awali mara mtoto anapozaliwa nina hakika dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama analimudu. Kama ambavyo alisimamia hoja yangu ya muda mrefu ya ufuatiliaji na tathmini na ulipokuwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na leo Serikalini kumekuwa na vitengo vya *monitoring and evaluation* kwenye kila taasisi ya umma nina hakika kabisa dada yangu na hili analiweza, ninaomba akalisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya mwisho, ninaomba kusema kwamba ninampongeza sana Daktari Janabi kwa nafasi aliyoipata na tunamtakia kheri kubwa sana katika hatua hizo anazoziendea na hakika Tanzania tunaona fahari sana kwa hatua hizi ambazo tunazipiga kwa madaktari wengi na Dkt. Regasha hali kadhalika tunamkumbuka sana ametutibu sana *H.pylori.* Tunashukuru sana waendelee, wakapambane na wakalitangaze Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme tu kwamba sisemi kwa dhamira yoyote ya kwamba nina wasiwasi na yaliyofanyika, lakini tu ni katika *curiosity* ya kawaida, ninaomba hawa watu *sensitive* kwenye Taifa letu sasa waangaliwe *with a specific attention* suala la kwamba mtu ameshakuwa Mkurugenzi wa *WHO* hata kama ni daktari, hata kama mke wake ni daktari anakwenda India peke yake bila kuwa na *escort* ya daktari yoyote huku nchini wakati tunaamini hii nafasi ni nafasi *sensitive* kwa Taifa letu. Ninaomba Serikali waiangalie kwa aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka zamani mtu alikuwa akienda hospitali India yule mtu ambaye ni *sensitive* kama kina Mafuru walikuwa wanapata ma-*escort* ya madaktari wetu na maamuzi yanayofanyika yanaendana na mashauriano ya madaktari wetu wa Tanzania; lakini watu wanainuka wanakwenda wenyewe India, mwisho wa siku tunapoteza watu. Sisemi kwamba kuna uzembe uliofanyika, lakini ninaomba tuiangalie hii kwa namna ya aina yake ili twende kulinda vichwa hivi vya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la mwisho ambalo ninaweza kulizungumza ni Hospitali ya Taifa Muhimbili…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, malizia tu hiyo hoja haraka haraka.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwamba suala la Hospitali ya Taifa Muhimbili kulipiwa *parking* kwa muda wote mgonjwa anapokwenda hospitalini pale, ninaomba liangaliwe kwa namna yake. Mtu anapokwenda Muhimbili haendi kama anakwenda *Milimani City* haendi kwa *relaxation* wala haendi aki-*determine time* atakayoitumia pale, yeye anakwenda lakini atakaa muda gani inategemea na daktari ambaye anampa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekwa *parking* pale*, I do appreciate* kuona kwamba ma-*chief executive* wanatafuta namna ya kuongeza fedha kwenye taasisi zao, lakini hiki siyo chanzo *genuine* cha fedha, tunawaumiza Watanzania ambao wanakwenda Muhimbili kwa shida, hawaendi ku-*relax*, hawaendi kutembea. Ninaomba mtafute chanzo mbadala kuliko kuwadai wananchi waliokwenda Muhimbili kwa matibabu *parking* muda wote watakaoishi Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante! Nilimwita Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi jioni hii ili niweze kuchangia katika Wizara yetu hii muhimu kwa Watanzania, Wizara ya Afya. Awali ya yote pia niweze kutumia nafasi hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Jenista na timu yake kwa kuendelea kufanya kazi nzuri. Tunajua kusimamia Wizara hii siyo kazi nyepesi kwa sababu ni Wizara *sensitive* yenye mahitaji muhimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, kazi iliyofanyika katika kuboresha utoaji wa huduma ni nzito. Tumeona hospitali zinaendelea kujengwa pale kwetu Mbeya tuna jengo kubwa la kisasa kabisa limejengwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Meta upande wa wazazi. Kwa hiyo, ukienda upande wa majengo mengine, huduma zingine ukiacha hii ya wazazi majengo pia yameongezeka mengi ya kisasa. Ninajua siyo kwa Mkoa wa Mbeya tu ambao unahudumia sisi watu wa Nyanda za Juu Kusini, lakini na maeneo ya kanda zingine pia yameendelea kufanyiwa uboreshaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi ya kusema ila kuna vitu ambavyo vichache ninataka kufanya kama angalizo, nilikuwa ninasoma taarifa hii nilikuwa ninatafuta kuona ni wapi Wizara hii na TAMISEMI kuna *connection*. Sijaona eneo ambalo lina-*clarify* ni kwa namna gani Wizara ya Afya inaisimamia TAMISEMI kwenye utoaji wa huduma zake. Mfano, kule TAMISEMI tuna vituo vya afya ambavyo vimechakaa sana, lakini tuna zahanati ambazo zimechakaa sana sasa kama hakuna hawa watunga sera ambao ni wasimamizi wa mambo ya afya na kule watekelezaji nikaona kama hapajakaa sawa. Kwa hiyo, kupitia bajeti hii tulitakiwa tuone hata ni sehemu gani inaonesha ushirika wake na wapi na TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri aende akahakikishe vituo vya afya vyote chakavu zahanati na hata kama kuna hospitali nyingine

ambazo ni za *level* za wilaya zina uchakavu uliokithiri, basi zikafanyiwe maboresho. Hili tunamwomba aende kulisimamia. Nina mfano wa vituo vya afya kwetu kule Songwe, mfano pale Mbozi kuna kituo kinaitwa Masangula ukikiona kabisa unaona kabisa hiki kituo kwa kweli majengo yake yamechakaa kitu ambacho tungependa kuona yanaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani pia kuongelea kwenye kipengele cha magojwa ya mlipuko. Unapoongelea magonjwa ya mlipuko ni magonjwa ambayo kiukweli ni rahisi kuenea hata kwa watu wengine inakuwaje kituo cha *isolation* kinawekwa katikati ya mji? Mimi nina mfano mzuri pale Kata ya Makambini sisi kama wananchi tuliomba kituo cha afya, lakini ajabu na kweli tumewekewa *isolation centre*. Hivi ni nani ambaye aliwahi kumwomba baba yake mkate akapewa jiwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Wanamakambini, Wanatunduma tuliomba kituo cha afya. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie ile *isolation* walipoiweka pale si sehemu sahihi, watafute sehemu ya kuiweka ambapo kutakuwa hakuna watu wengi. Watupe kituo cha afya Makambini ndilo lilikuwa ombi letu. Kwa hiyo, katika hilo suala la *connection* ya Wizara hii na kule TAMISEMI watusaidie wakaondoe ile *isolation* watupe kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kupitia ripoti sehemu ya ubora wa huduma. Kumekuwa na changamoto ya wananchi kutokuwa na imani na hospitali zetu na hii naiongea kwa moyo mkunjufu kabisa kwamba wananchi wale ukiwaambia nenda hospitali za Serikali unakuta wanabisha. Utashangaa kwa sisi watu wa Nyanda za Juu Kusini wanasema bora niende Ikonda au niende *private hospital* nyingine, lakini ukimwambia nenda kwenye hospitali za Serikali wanakataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nimeiona kwa watu wanaokuwa wamepata ajali za mifupa, lakini hata tu kwa wale wagonjwa, unakuta anaumwa unamwambi nenda hospitali hizi za Serikali wanakuwa ni wabishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai, juzi nilikuwa na mgonjwa wangu wa karibu kabisa ambaye yeye alikuwa analalamika kizunguzungu na maumivu ya mifupa na nyama (*muscles*) amefika hospitali ambayo ni ya kuaminika siwezi kuitaja hapa kwa ajili ya heshima yake. Anaenda kupewa dawa za kutuliza maumivu na kuambiwa kwamba mifupa imekaza. Hivi mifupa inakaza bila sababu? Badala ya kwamba aende akapimwe ijulikane ni kwa nini hiyo mifupa imekaza, hakuna. Akaenda *private* sekta akapimwa anaonekana ana *uric acid. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *uric acid* tu hospitali za rufaa zingine wanashindwa ku-*identify*. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri niseme tu kwamba ubora wa hospitali zetu tunaomba uwe unafuatiliwa kwa ukaribu. Wamesema wamefanya *monitoring* ya ubora wa huduma kwenye hospitali 28 ambapo waliangalia katika huduma za mama na mtoto, lakini wakaangalia kwenye kitengo cha dharura. Kwenye huduma ya mama na mtoto *score* ilikuwa ni 67%, lakini kwenye huduma ya kidharura *score* ilikuwa ni 64%. Sasa ninajiuliza hapo hii huduma haifanyiki mara kwa mara maana watalaam walioonyesha wamewasomesha ni wachache ina maana hii huduma haifanyiki mara kwa mara kufuatilia ubora wa huduma zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanatuhakikishia vipi wananchi tuendelee kuwa na imani na hizi hospitali? Kama vitengo tu ambavyo hata havina shughuli nzito sana sana kama huduma ya mama na mtoto ina-*score* 67%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwenye magonjwa mengine magumu huduma zinaendaje? Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba tusaidie kitengo cha ubora wa huduma kiboreshwe, kiongezwe wataalam, watu wapatiwe *training* za kutosha ili waweze kusimamia hospitali zetu ili ninapokwenda kama ni hospitali ya mkoa ninapata huduma ileile, ya wilaya ninapata huduma ileile na kituo cha afya ninapata huduma ileile. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri hili aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye kipengele kimoja cha Hospitali ya Muhimbili. Hospitali ya muhimbili kwa kweli ni hospitali ambayo inafanya kazi kubwa sababu inapokea wagonjwa wengi wengi unakuta watumishi wa pale wako *busy* muda mwingi. Hata hivyo, kuna hiki kitengo ambacho kimeanzishwa kinaitwa kitengo cha *IVF*, kitengo cha upandikizaji wa mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata nafasi ya kuwasiliana na daktari mmoja wa eneo lile akaniambia kwamba ni kweli huduma imeanza na tunatoa na hapa inaonyesha wamehudumia wagonjwa nane, lakini wana changamoto zao. Huduma imeanza, lakini dawa na vitendea kazi ambavyo vinatumika kwa ajili ya utoaji wa huduma hizi haviko-*registered MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekanaje huduma ianze halafu hizo dawa na vitendea kazi wanasema *lab media* na hizo dawa zake mpaka waagize Ujerumani ndiyo wazipate halafu tena ndiyo zinatakiwa zisafirishwe kwa mnyororo baridi. Sasa unaweza uka-*imagine* mnyororo baridi kutoka Ujerumani hiyo dawa mpaka ije ifike huku ubora wake unakuja unafika ukiwa una ngapi, lakini gharama yake inaongezeka inakuwa kubwa zaidi. Ni wananchi wangapi wanaweza ku-*afford* hiyo dawa au hiyo huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe, Madaktari walisema wanaomba dawa hizi yaani vifaa tiba na dawa zake ambazo zinatumika katika zoezi zima la upandikizaji wa mimba ziwe *registered, MSD* waweze kuziagiza wanunue ili wawe na urahisi wa kuzipata ili tuweze kuwasaidia wanawake wengi au wanaume wengi ambao hawana watoto. Tunajua kabisa kukosa mtoto ni mojawapo ya vitu vinavyoweza vikampelekea mtu kuwa na msongo wa mawazo. Kwa hiyo, hilo pia tunaomba wawasaidie wafanye kazi nzuri wahudumie watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kusisitiza kwamba Kituo chetu cha Afya cha Tunduma kinaendelea kuelemewa pamoja na kwamba wametujengea hospitali tunawashukuru inasaidia, lakini pamoja na kwamba wamejenga vituo vingine vya afya

tunawashukuru, bado wananchi wengi wanaendelea kuamini Kituo cha Afya cha Tunduma kwa sababu huku bado wengine madaktari siyo wa kutosha na majengo bado hayajakamilika, yaani vifaa vya utoaji huduma na watalaam bado hawajapelekwa kwenye vituo vingine vya afya. Kwa hiyo, tunaomba Wizara waweze kutusaidia kwa sababu tunajua kuna vifaa vingine vinatoka *direct* kutoka kwao kwenda TAMISEMI. Kwa hiyo, waendelee kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo, niseme ninashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwandabila. Nilimwita Mheshimiwa Jacqueline Andrew Kainja, atafuatiwa na Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu na Mheshimiwa Anatropia Theonest, ajiandae.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Afya mama yangu Jenista Mhagama pamoja na Naibu Waziri wake, lakini vilevile watendaji wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu wetu Mkuu wa Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya hususani sisi wananchi wa Mkoa wa Tabora tunampongeza na tunamshukuru kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kupitia sekta hii ya afya kwa maana ya kwamba Mkoa wetu wa Tabora tumepokea bilioni 33.2 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali tano za wilaya katika wilaya saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukarabati wa hospitali kongwe mbili za wilaya ikiwemo Hospitali ya Urambo pamoja na ya Igunga. Vilevile tumekuwa na vituo vipya vya kutolea huduma za afya, vituo vya afya na zahanati kwa maana kwamba 2021, 2023, 2024 kutoka vituo 348 mpaka vituo 428 kwa kweli sisi wananchi wa Mkoa wa Tabora tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pia pesa za bajeti ya ruzuku za dawa na vifaa tiba kutoka bilioni nne kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 bilioni 9.8. Hayo kwetu ni maendeleo makubwa na hii inatusaidia sisi wananchi wa Mkoa wa Tabora kupata hali nzuri ya upatikanaji wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumepata huduma nyingi ambazo sitaweza kusema zote, tuna *CT-scan* tulitumia bilioni 1.8, inaweza kuwasaidia wananchi wetu wa Mkoa wa Tabora, lakini tumeweza kupokea *ambulance* 23 katika Mkoa wetu wa Tabora, hayo sisi ni mafanikio makubwa na tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na tunamwambia aendelee kuchapa kazi mitano tena tutamhakikishia na atashinda kwa kishindo kwa kura za kutosha kutoka Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri yote hayo ambayo yanafanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita, lakini vilevile niweze kujielekeza katika kushauri Serikali katika taarifa ya Kamati ambayo imesomwa na Mwenyekiti wa Kamati, nimeona ukurasa wa 16 imejielekeza kwa miaka miwili mfululizo nyuma Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuweza kuisaidia mkopo *MSD* bilioni 561 ambazo zilikuwa zinahitajika ili wao waweze kujisimamia kwa ajili ya mtaji mkubwa wa kuendesha huduma zao na tumeipa *MSD* kazi kubwa ya uzalishaji, uhifadhi, usambazaji na ununuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuiwezesha *MSD* Mheshimiwa Waziri hapa tutakuwa bado hatujafanya kazi vizuri na tukategemea matokeo mazuri kutoka *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ikiwa inasisitiza Wizara na Serikali kutoa pesa hizo Wizara walikuwa wasikivu na Serikali ilikuwa sikivu ikatenga bilioni 100 kwa ajili ya kuisadia *MSD*. Kwa hapa kwa kweli niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kupongeza taasisi hii ya *MSD* chini ya Mkurugenzi Mavere Tukai, pamoja na timu nzima ya *MSD* wao walifanikisha kupata milioni 162.4 kwa ajili ya

kuendelea kupambana na changamoto mbalimbali zilizopo ndani ya *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona vilevile namna ambavyo *MSD* hii ikiwezeshwa inaweza ikajisimamia. Ukurasa wa 17 taarifa ya kamati inaonyesha kwamba *MSD* inadai Serikali; mbali na kwamba *MSD* inahitaji mtaji, lakini vilevile tunaweza tukajikita kwenye kulipa madeni ambayo *MSD* inadai ya bilioni 434.2 hivyo tukiwapatia wanaweza wakajiendesha kwa sababu waliomba 561 ikatoka bilioni 100, lakini bado bilioni 300 basi Serikali tuangalie tulipe madeni ya *MSD* wanayodai yote ili tuweze kuona ikifanya kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iweze kuwekeza pesa kwa ajili ya kiwanda chetu kile cha *TPI* ili kiweze kufanya kazi na tuweze kuzalisha *ARVs* ili tuweze kuondokana na kutegemea wafadhili na kama tunavyoona sera za kinchi, sera za nchi za Marekani ambazo zinabadilika zisije zikatuingiza kwenye changamoto kubwa. Kama tuna uwezo huo ni vema basi tukajielekeza pia kuhakikisha kiwanda hiki kinaweza kusimama vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nihamie kwenye suala lingine kwa sababu ya muda. Suala hili niliwahi kuliongea mwaka jana 2024 wakati Waziri wa Afya akiwa ni Ummy Mwalimu na alilipokea na akasema atalifanyia kazi. Hata hivyo, leo hii ninaomba kwa sababu Waziri wetu wa Afya mama yetu Jenista Mhagama yuko hapa na mama yangu ni mfuatiliaji na ni msikivu ninamwomba kwa unyenyekevu mkubwa sana alibebe hili alipeleke Wizarani na wakakae walifanyie kazi. Suala hilo si lingine ni Kurugenzi ya *Pharmacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea Kurugenzi ya *Pharmacy* kwa maana katika utendaji wa muundo mzima wa Wizara yetu ya Afya na hasa kwenye hospitali zetu huwa kuna kurugenzi katika idara zote, lakini kuna baadhi ya idara hazijawekewa kurugenzi kwa maana ya wale wasimamizi kuingia kwenye vikao vya maamuzi kama Bodi au Menejimenti ya Hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa tuna Mfamasia Mkuu wa Serikali, ambaye yeye amekuwa Mkurugenzi Msaidizi lakini yule anaishia kule Wizarani huku chini kwenye watendaji na wananchi wote tunaishia kwenye hospitali kuhakikisha tunaenda kutibiwa bado kurugenzi hiyo haijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa nini ninaomba kurugenzi ya *pharmacy?* Ni kwa sababu 50% ya bajeti za dawa zinaenda kwenye idara ya *pharmacy* na msimamizi mkuu ni Mfamasia, lakini Mfamasia huyu kwa Hospitali ya Muhimbili au hospitali zozote zile za kanda hana uwezo wa kuingia kwenye vikao vya bodi vya ndani, badala yake anawakilishwa na kurugenzi ya tiba chini ya daktari ambaye hana utaalam wa *pharmacy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia 95% ya wagonjwa wanaoenda hospitali wanahitaji kutumia dawa na vifaa tiba na tukisema vifaa vya tiba vyote viko chini ya *pharmacy* msimamizi ni Mfamasia, lakini kwa nini inashindikana? Mfamasia huyu kuingia kwenye Bodi ya Hospitali au Menejimenti ya Hospitali ili kuweza kupeleka mawazo yake moja kwa moja ya idara ambayo idara hii ya *pharmacy* 40% ya mapato ya hospitali yanatoka katika idara ya *pharmacy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini kinachoshindikana? Nimwombe Mheshimiwa Waziri, jambo hili dogo sana, hatutaweza kupata tija kubwa ya matokeo chanya kama asilimia kubwa tunategemea upande wa *pharmacy* lakini mfamasia huyu hapewi dhamana ya kuingia kwenye vikao vya maamuzi makuu ndani ya hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe, hizo kurugenzi ni Hospitali ya Muhimbili na Hospitali zote za Kanda na Benjamini zinatakiwa zitengenezwe Mfamasia Mkuu wa Serikali mmempa nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi kwa ngazi ya Wizara je, huku ambako kuna watendaji hawa kada ya *pharmacy* tunawashirikishaje? Ikiwa kama tuna wafamasia wameweza kujiendeleza sana? Tunao wengi wa kutosha kwa nini tusiwatumie kupata mawazo yao moja kwa moja

badala ya kuwakilishwa na daktari ambaye yeye pia hana taaluma ya *pharmacy? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, ajiandaye.

MHE. BENARDETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza kabisa ninapenda nimpongeze Waziri wa afya Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi nzuri sana anayofanya katika Wizara hii. Kwa kweli sishangai kwa sababu kwenye Wizara zote alikopelekwa amefanya vizuri sana, kwa kweli yeye ni jembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Mollel, yeye akiwa kama daktari ana mchango mkubwa katika mambo mazuri ambayo tunaona kwamba na mafanikio yametokea katika Wizara hii hongera sana. Ninampongeza Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi wa taasisi mbalimbali ndani ya Wizara hii na watendaji wote kwa mafanikio mkubwa sana katika hii sekta ya afya. Hongera sana kwa Mheshimiwa Mohamed Yakub Janabi kwa ushindi na vilevile kwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika kwa kweli ametuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na mapinduzi makubwa ndani ya sekta ya afya, kwa hiyo tunasema mama ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Afya, tumesikia kilio kikubwa cha Bohari Kuu ya Dawa *MSD* unajua kwamba ina majukumu makubwa ya uzalishaji, ununuzi, utunzaji, na usambazaji

wa vifaa tiba ikiwemo madawa. Hata hivyo, hawa wamepungukiwa mtaji na kila mwaka wamekuwa wakiomba lakini mwaka juzi 2023/2024 wakapewa bilioni moja na mkaona mambo makubwa ambayo walianza kufanya, nina uhakika kwamba wakiongezewa mtaji watafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kukosekana kwa mtaji sasa kunafanya hii bohari kuu ifanye kazi kama si kama bohari kuu ni kama duka la kawaida la dawa. Sasa hivi mnaona *tendency* ya wafadhili wanaanza kujitoa, Tanzania 90% ya afua za UKIMWI na *TB* zilikuwa zilikuwa zinafadhiliwa na Mfuko wa Rais wa Marekani na wanaona jamaa Mheshimiwa anaanza kujitoa kama anavyojitoa sasa itakuwaje kama sisi hatutakuwa tumeiwezesha taasisi yetu ya *MSD* ikawa na madawa ya kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mwanakamati tunaleta ombi kwa Serikali kwamba kwa kuwa wanadaiwa na *MSD* bilioni 434.2, tunaomba hizo zikalipwe. Lakini vilevile hii *MSD* ipewe mtaji wa kutosha kusudi hata hawa wafadhili wakija kujitoa hawa wagonjwa wetu karibu milioni1.5 ambao ni wagonjwa wa UKIMWI wanaendelea kutumia *ARVs* na wagonjwa wa *TB* wanaopata matibabu ya muda mrefu tuwahakikishie kwamba madawa yatakuwepo wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa maana ya *NHIF* na yenyewe inaidai Serikali bilioni 210.29. Ni ukweli usiopingika kwamba Serikali imeboresha huduma za afya, tumejenga zahanati kila kona, kuna vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mkoa, hospitali za Taifa, hospitali za kanda zote zimeboreshwa ili kusudi Watanzania waweze kupata huduma iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona vifaa tiba vimenunuliwa ma-*CT-scan* na *digital x-rays, pet-scan, dialysis machines* karibu kila mkoa *MRI* na kadhalika, lakini matibabu bado ni ghali ndiyo maana Serikali mkaja na Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote ili kusudi Mtanzania

asife kwa kukosa matibabu kila Mtanzania aweze kutibiwa kwa kupitia bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bima ya afya iwezekane, inabidi Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uwe na ukwasi ambao unatosha. Hivyo, tunaiomba Serikali ilipe deni hilo la Bima ya Afya shilingi bilioni 210 ili kusudi tuweze kuongeza ukwasi katika hii mifuko; itaongeza uhimilivu na uhai wa Mifuko na hivyo waweze kutoa huduma zilizo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sekta ya afya imeendelea sana kwa sababu sasa hivi tunapandikiza uroto, tunapandikiza figo na tunaelekea kwenda kupandikiza ini na moyo, Serikali tunaomba haraka sana ilete sheria ya kuwawezesha hawa wataalam wetu waweze kupandikiza hivyo viungo pamoja na chembechembe hai kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera umepakana na nchi nyingi ikiwepo Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na kadhalika, kwa sababu ya mwingiliano mipakani unakuta kwamba magonjwa ya mlipuko na hasa yakiwa kwenye nchi hizo jirani kama *Marburg, Mpox, Ebola* na kadhalika yanaweza yakaingia Tanzania kwa kupitia mipaka ambayo iko katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi Wabunge wa Mkoa wa Kagera tumekuwa tukiomba tujengewe *isolation centres,* lakini vilevile tujengewe na hospitali kubwa ya kuweza kutibu haya magonjwa ya mlipuko. Kwa niaba ya wananchi wa Kagera tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea *isolation centre* pale Mutukura, ambao ni mpaka uliopo kati ya Uganda na Tanzania kule Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba *isolation centres* nyingine ziendelee kujengwa kwenye mipaka ambayo ni rasmi kwa mfano kwenye mpaka wa kati ya Tanzania na Uganda ulioko kule Kyerwa, mpaka uliopo kati ya Tanzania na Rwanda uliopo pale Rusumo - Ngara na mpaka uliopo kati ya Tanzania na Burundi uliopo

kule Kabanga tujengewe *isolation centres* ili kusudi wale wasafiri wakifika pale mpakani wakihisiwa kwamba wana haya magonjwa ya mlipuko waweze kutengwa kwenye hizo *isolation centres* kabla hawajaja Tanzania kuchanganyikana na Watanzania na kuambukiza hayo magonjwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumekuona Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Jenista Mhagama ukiwa unatia saini mkataba wa kutujengea hospitali kubwa ya kisasa ya magonjwa yasiyoambukiza Mkoani Kagera, tunasema ahsante sana Mheshimiwa Waziri na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujali wananchi wa Kagera. Sisi tunachoweza kumuahidi ni kwamba itakapofika mwezi Oktoba tunaenda kumlipa, tutampigia kura nyingi, kura za kishindo, kura za ushindi ili kusudi ashinde aendelee kuwa Rais na aendelee kutuletea maendeleo katika Mkoa wetu wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kwa kweli umetuongoza vizuri sana. Ninawashukuru na ninawapongeza na Wajumbe wote wa Kamati, Sekretarieti yetu kwa kutuongoza vizuri pamoja na ushirikiano tuliokuwa nao ambao ndiyo mambo yaliyotuwezesha kuyafanikisha yale yote ambayo tumeyafanikisha kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mushashu.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni ndani ya Ukumbi ambao wameingia mchana huu, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wetu wa Afya ambao ni Ndugu Hilda Mkwabe, huyu ni Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza *Autism Foundation;* Ndugu Sedio Mandigo, Balozi wa Kupambana na Saratani; Ndugu Abdulmalik Mollel, Mkurugenzi Mtendaji wa *Global Medicare* - taasisi

inayoshirikiana na Wizara ya Afya kutangaza tibaasili. Karibuni sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara nyeti. Nitaanza kwa ku-*quote,* nitam-*quote* William Graham, huyu ni mwandishi wa vitabu na ni *motivation speaker,* alisema hivi: "*When wealth is lost, nothing is lost; when health is lost something is lost; and when character is lost all is lost*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaonesha mkazo kwenye *wealth*. *Weath* ni mali, *weath* ni utajiri, *wealth* ni uchumi. Unaweza kupoteza kila kitu lakini hujapoteza kila kitu. Ninakuja kwenye afya, ukipoteza afya kuna kitu kitakuwa kimepotea. Ukipoteza *character* kwa maana ya sifa kuna kitu au kila kitu kitakuwa kimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini nimeongea haya? Katika vitu vyote tunavyovifanya msingi wake ni afya, sisi tunao msemo unasema: "Kwa sababu nina nguvu nitapambana", lakini ukipoteza kitu kinaitwa nguvu mapambano yote yamefikia ukingoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninam-*quote* mzungumzaji ambaye amenitangulia, amesema: "Gharama ya matibabu hapo nchini ni ghali". Nami ninaomba nirudie kwamba, ugharamiaji wa matibabu hapa nchini ni ghali sana. Katika kila tunachokifanya na katika kila tunachokifikiria tuwaze ni namna gani tunaweza kupunguza gharama ya matibabu hapa nchini. Haya yote nitayaongea leo utaona kwamba kutibiwa ni rahisi kwa sababu leo una fedha *you have wealth,* lakini ikifikia wakati ambapo hauna *wealth* na hauna *health* ndiyo utaelewa ninamaanisha nini nikisema gharama ya matibabu ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama hauna chochote unaumwa ukaambiwa piga *X-Ray, CT-Scan* na *Ultrasound* ndiyo utaelewa

ninamaanisha nini nikisema gharama ya matibabu iko juu. Siyo hiyo tu, ukiambiwa mwone Daktari kwa kiasi fulani, nenda kamwone daktari ukimaliza kumwona daktari nenda kwenye vipimo, ukatoka, nenda kwenye dawa rudi kwa Daktari, utaelewa gharama ya matibabu ni kubwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tunafika hapa? Wakati mwingine nikifika kwenye hospitali hizi kubwa kubwa nikafurahia uwekezaji uliofanyika na Serikali za awamu mbalimbali nikasema kweli Watanzania wameweka kitu, kweli kodi za Watanzania zimefanya kitu na kweli zinaonekana kwa macho. Uwekezaji wa Watanzania uliofanyika basi *return* yake iwe upungufu au kupunguza gharama za matibabu ambazo wanapaswa kuzipata wakati afya zao zimetetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ninayaongea nikilinganisha na vifurushi au *package* za bima ambazo leo tuko nazo na tunazi-*market* au Wizara imekuwa ikizisemea. Ukiangalia gharama za vifurushi leo tunavyoongelea kuna kifurushi cha Ngorongoro, Serengeti. Nikawa ninaangalia kwenye *age group* nikaona katika *age* kati ya *0* mpaka *17* unaona kwamba *package* ya vifurushi viko nafuu kidogo. Ukija kwenye *age* kati ya miaka 18 mpaka 35 unaona kwamba inapanda, unavyoendelea kupanda inakuja 36 mpaka 59 ambao pengine wengi wetu hapa ndiyo tuna-*belong* unaona kwamba inapanda. Mzani unavyoshuka kwanza wanasema *sixty* yaani ukianza kupanda ngazi ya *sixty* unaona kwamba gharama ya matibabu inaendelea kuwa kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *mind you,* hawa watu wa miaka 60 *plus* ni watu ambao leo hawana ajira, ni watu wamestaafu! Ni watu ambao hawana kipato, lakini huduma zao za matibabu ukiangalia kifurushi cha Ngorongroro mtu mmoja inakuwa ni shilingi laki saba na elfu nane. Serengeti ni shilingi 3,306,000. Unaona kwamba huyu Mzee ambaye najua gharama yake ya matibabu ni kubwa hakuna shida, lakini kwa miaka yake 60 ameshalitumikia hili Taifa. Hiyo miundombinu mnayoiona na majengo mnayoyaona, *CT-Scan, ultrasound* na yote yaliyonunuliwa ni kwenye kodi alizo-*contribute* kwenye miaka nenda

miaka rudi. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie tunapojadili hapa tufanye gharama za matibabu hapa nchini ziwe *affordable,* isiwe *luxury*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu unawasikia, unaweza kukutana na mtu anasema, "Mheshimiwa Anatropia ninaumwa", "Unaumwa kwa nini huendi hospitali?", "Sina gharama za kwenda hospitali". Ina maana kuna magonjwa mtu akipata yeye hatima yake ni kusubiri Mungu atakavyoamua, Mungu akiamua apone atapona, Mungu akiamua vinginevyo hata magonjwa ambayo angeweza kutibiwa hawezi kutibiwa ni kwa nini huduma za matibabu ziko aghali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunaenda hospitali, huduma za bima za afya ni aghali, na hii tena ndiyo inaniumiza! Mtu anaweza kukata kifurushi cha shilingi laki sita au laki saba, yeye anajua akishakata bima kazi imeisha, ukifika unaambiwa kifurushi ulichokata dawa hizo hazipo! Hilo suala linaumiza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani Wizara wa5fanye *computation* ambayo inaweza kueleweka ambayo hata Serikali inaweza kui-*facilitate* kwamba mtu akikata bima ya afya ajue kwamba nimemaliza na niwekeze kwenye bima ya afya, kila mwaka nilipie ni-*renew* ili nitibiwe kwa sababu *there is no guarantee* kwamba nilivyokata kwenye mwaka husika nimeumwa, sasa kwa nini siku nikiumwa niambiwe hizo dawa hazipo kwenye hii *package* ziko kwenye hii *package* ambayo hukukata? Ninadhani ni kitu ambacho hakiko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ninataka kukileta kwenu ningetaka Mbunge anayeweza kusimama hapa kwenye hii *podium* akasema yeye kwenye Jimbo lake mama mjamzito anatibiwa bure, yaani anapofika na tumbo lake anatibiwa anaenda nyumbani, anyanyuke hapa wapiga kura wake wamwone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inayosema, huduma ya Mama Mjamzito na watoto chini ya miaka

mitano itakuwa bure, haitekelezeki! Serikali iseme wazi. Tusiwadanganye akinamama tunapoenda kwenye majukwaa na tunapoenda majimboni tunaishia kusema maneno ambayo ni ya uwongo. Tunaanza kujichanganya! Tuwaambie ukweli kwamba ukienda hospitali nenda na taulo lako, nenda na *gloves* zako, nenda na vile vifaa vyote vya kujifungulia.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hizi habari za kusema kwamba vitakuwa ni bure siyo kweli! Tuwaambie wananchi ukweli. *(Makofi)*

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa wapi?

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwa Mwenyekiti wa Kamati, Kingu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kingu.

TAARIFA

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa dada yangu na rafiki yangu ninayempenda sana na kwa kweli anachangia kwa uzalendo mkubwa, ni Mbunge makini sina shida naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa kwamba rekodi zinaonesha kwamba kwa mwaka wa fedha uliokwisha wazee zaidi ya milioni 3.4 wametibiwa bila malipo kwa mujibu wa *statistics* za Serikali. Kwa hiyo, kusema kwamba sheria hii ya kuwatibu wazee na akinamama kwamba haitekelezeki ndiyo tunaweza tukawa na changamoto katika Taifa letu, lakini kwa kiwango kikubwa sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imeendelea kutekeleza kuwasaidia

wazee huduma za matibabu bila malipo, *statistics* hata tulipokuwa tunasomewa utekelezaji wa Ilani, moja ya vitu ambavyo Rais ame.....

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Theonest, unapokea taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Kingu?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Wazee wa Jimbo lake ambao wamenufaika na hayo matibabu, lakini ninawaomba wasipewe matibabu Wazee wa Jimbo lake la Singida, Wazee wa Kyerwa pia wapewe matibabu hayo, kwa sababu nina uhakika pengine aliowataja milioni tatu siyo takwimu tu ninadhani wazee wanazidi hiyo takwimu, pengine ni wa kwake wamenufaika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza hapa, kama huduma ni bure tunaelewa ni kwa nini sera imekuja namna hiyo, ni kwa sababu ya umahsusi wa kundi husika, umahsusi wa akinamama wajawazito, umahsusi wa watoto chini ya miaka mitano. Kwamba kama ukizuia hili kundi, kama ukitanguliza fedha kwenye hili kundi, *risk* ni kwamba wanaweza kuacha kwenda hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kuwatoza fedha *risk* itabaki palepale. Kwa hiyo, kama tunataka tuondoe *risk* hizo *delivery kit* tuzi-*offer for free,* na nina uhakika Serikali ikiamua inawezekana kabisa na tukajua kwamba tunavyoenda kujifungua *we are free* tunajifungua, hiyo tutakuwa tunasema tumeweza katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye jambo jingine kuhusu suala la malaria. Hakuna kitu kinasikitisha katika karne tuliyonayo leo bado tunaongelea changamoto ya malaria. Ukisoma hotuba ya Wizara ukasoma na randama inaonesha gharama ambazo zimewekwa kwenye kupambana na malaria. Ninataka nisome kidogo tu kwenye randama, inasema mapambano dhidi ya malaria, Wizara

ilinunua na kusambaza dozi milioni nne za dawa mseto, dozi za malaria, dozi za sindano mahesabu yako hapa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajiuliza kweli katika karne hii tunapaswa kuendelea kupambana na malaria? Ni kwa nini ninasema haya? Serikali ilifanya uwekezaji mkubwa wa kiwanda cha viuatilifu unaitwa *biotech product* kwa ajili ya kuchukua zile dawa kusambaza na kuua vimelea vya malaria. Ni kwa kiwango gani hizo dawa tumezinunua na kuzisambaza kwenye Halmashauri ili tuondokane na changamoto ya malaria? Leo malaria wanasema ni *killer disease*, inaua kwa 33% ukilinganisha na magonjwa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tuna uwezo wa kupambana na malaria lakini hatupambani na malaria. Tunaongelea vyandarua, tumesambaza vyandarua kadha wa kadha kwenye Mikoa lakini kwa nini tusiongelee tumesambaza zile dawa za kupambana na vijidudu vya malaria? *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Jenista Mhagama.

TAARIFA

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tutasubiri ili tuweze kutoa majibu ya kina, lakini katika maeneo ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amevunja rekodi na kufanya vizuri sana na kwenye hotuba yangu nimeiweka wazi labda Mheshimiwa Mbunge hakupata nafasi ya kupitia, ni pale alipoingia madarakani na kuamua kuhamisha nguvu ya mapambano dhidi ya malaria kwenye udhibiti na kuendelea na tiba pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatoa shilingi bilioni 10 na tumekwishanunua zaidi ya lita laki 833.333 za dawa ya kuua viutilifu ambavyo vinazalisha mbu wa malaria. Kwa hiyo, jambo hilo tayari Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshafanya hiyo kazi. Dawa

zimeshasambazwa na sasa hivi tunasubiri mvua ziishe dawa zitaanza kunyunyizwa kwenye halmashauri zote nchini.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Anatropia taarifa hiyo unaipokea?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiipokea sasa hivi atajibu nini wakati wa ku-*wind up?* Wakati wa ku-*wind up* anapaswa kujibu hayo niliyoya-*raise* kwenye mjadala. Ninataka kusema hivi, tangu tumekuwa na kiwanda pale Kibaha zaidi ya miaka nane, leo tungekuwa tunaongelea changamoto ya malaria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa leo tunawekeza fedha kwenye vyandarua? Tungekuwa leo tunajivunia kununua zile *rapid test* kadhaa? Kupanga ni kuchagua! Yeye ni Waziri wa Wizara hii na anafanya kazi, anafanya kazi, anapambana! Kwa hiyo, akiamua kununua zile dawa akazisambaza, leo hatutaongelea tena vyandarua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia ulitakiwa ukatae au ukubali hiyo taarifa, lakini malizia mchango wako.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ananipotezea muda. Ninapokea kwamba sasa wanaweka mikakati, tunaanza kuona tukitokomeza malaria, tunaacha biashara ya chandarua, tunaacha biashara ya kuuza dozi za malaria kwa maana ya kuhangaika na hizi dawa wakati tuna uwezo wa kutokomeza malaria kupitia kiwanda ambacho tunacho nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweka fedha tumewaleta watu wa Cuba na badala yake nilikuwa hapa, kuna ziara kuna baadhi ya wanasiasa huwa wanafanya ziara kwenye hicho kiwanda halafu wanawaeleza wale wa kiwanda kwamba fanyeni jitihada za

kujitangaza. Hivi kweli leo tunakiambia kile kiwanda kujitangaza? Au sisi ni kazi yetu kukitangaza na kuuza zile *products* kwenye nchi mbalimbali zinazotuzunguka ambazo pia zinapata changamoto ya malaria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kama muda wangu upo, nitaongea kwa kusikitika tena.

MWENYEKITI: Muda wako umeisha na nilikuwa nimekuongezea kidogo, muda wako umeisha.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Samwel Hhayuma na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya. Kwanza, ninaomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Moja kwa moja nianze pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana ambayo ameifanya katika Wizara hii ya Afya, pia kwa tuzo nyingi sana ambazo amezipata ikiwemo tuzo ya kupunguza vifo vya akinamama na watoto nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Watanzania wote waliompongeza Profesa Janabi kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, kwa kweli ametuheshimisha Watanzania kwa mara nyingine tena, hongera sana. Pia, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Afya Mheshimiwa Jenista Mhagama, ambaye kwa kweli amekuwa Waziri wa muda mrefu, amefanya kazi kwenye Wizara nyingi na tunamshukuru tena anaendelea kupambana kwenye hii Wizara kuhakikisha kwamba tunaendelea pia pamoja na kupunguza vifo vya akinamama na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel ambaye kwanza majibu ya kila siku hapa Bungeni, amekuwa akitujibu pia amekuwa na utayari wakati wote tukimpigia simu hata akiwa nyumbani. Tunakumbuka kuna mtoto mmoja wa Kilolo aliumwa na nyuki alilazwa pale Muhimbili alikuwa hatarini kufa kwa sababu ya kusafishwa damu. Tulipompigia Dkt. Mollel hatutamsahau, alipiga simu saa hiyo hiyo wakaenda kumsafisha damu na huyo mtoto nitamleta Bungeni kwa sababu alitaka kufa. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Afya, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Afya kwa kazi nzuri ambayo imesababisha hata Serikali ya Awamu ya Sita kufanya vizuri sana. Nitakuwa sijatenda haki kama nisipompongeza Daktari wetu wa Mkoa, Dkt. Mwakalebela. Kwa kweli huyu Daktari amekuwa akitusaidia sana wananchi wa Iringa, ni Daktari ambaye amekuwa akitusikiliza na akitusaidia sana katika mkoa wetu, tunamshukuru. Tunatamani hata miaka irudi nyuma asiweze kustaafu ili aendelee kuhudumia katika mkoa wetu na pengine hata akistaafu basi endeleeni kumpa mikataba kwa sababu uwezo anao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali yetu, lakini ziko baadhi ya changamoto ambazo na mimi ningetamani niziseme. Katika Mkoa wetu wa Iringa kwanza, kuna ufinyu mkubwa sana wa eneo kwenye Hospitali ile ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa. Hii inatokana na mwingiliano ambao kila siku wanauzungumzia kati ya Gereza la Mkoa na Hospitali yetu ya Rufaa. Kwa hiyo, tunaona majengo mengi hayajengwi kwa sababu ya ule mwingiliano; eneo ni finyu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikuta wafungwa wanatoka na *ambulance* zinakuja unaweza ukajisikia vibaya sana. Ninashukuru nilipoongelea kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani niliwaomba kwamba, gereza lile sasa lihame na ninashukuru pia niliongea siku ile na Mkuu wa Magereza akanihakikishia kwamba sasa hivi watapata bajeti na gereza litahama. Tunaomba kwa kweli kazi hiyo ifanyike ili

majengo mengi yajengwe ikiwa ni pamoja na nyumba za madaktari wetu wakae jirani na hospitali waweze kusaidia wagonjwa waliopo katika Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pale Iringa tuna ukosefu wa jengo la kisasa la mama na mtoto. Hii ni kutokana na ongezeko kubwa sana la mama wanaojifungua na kwa kweli Iringa tunajitahidi tunajifungua sana. Kwa hiyo, tunaomba wodi ile watuletee pesa ili tuweze kuongeza kwa sababu halitoshi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu gharama za huduma za kusafisha figo *(dialysis)*. Kwa kweli wananchi wengi, uwezo wao ni mdogo sana kiasi kwamba, watu wengine wanashindwa kwenda kufanya hiyo huduma kwa sababu hawana uwezo wa pesa na hawana bima ya afya. Kwa hiyo, inakuwa ni shida mno, wananchi wengi wanapoteza maisha na wananchi wengi hawajui wafanye nini wanaotoka vijijini na wengine hawajui wafanyeje. Kwa hiyo niombe hebu iangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hospitali inashindwa kujiendesha kwa sababu wananchi wanashindwa kwenda kupata hiyo huduma. Kwa hiyo pesa inakuwa haipo ya kujiendesha kwenye hiyo huduma. Ninaomba Serikali iangalie upya huduma za usafishaji wa figo ikiwepo Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu upungufu wa watumishi katika Wizara ya Afya katika Mkoa wetu wa Iringa ambao ni karibu 50%. Kwa hiyo, niombe waangalie kwa sababu ni muhimu sana kupata hao watumishi kwenye Sekta ya Afya na hasa madaktari kwenye vituo vya afya na zahanati wawepo ili waweze kusaidia huduma katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano; kwa kweli tunashukuru kwani kwenye Hospitali ya Rufaa kuna *ambulance* sita, kuna magari manne, lakini kuna dereva mmoja tu ambaye ameajiriwa. Kwa hiyo hii inasababisha hata saa nyingine kukimbiza mgonjwa kuleta huku

Benjamini Mkapa inakuwa shida. Niombe hata madereva pale wapatikane wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu majengo yaliyojengwa na wadau. Katika Mkoa wetu wa Iringa sisi kwanza, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. Tunaye mdau ambaye ni Mkurugenzi wa ASAS ambaye ni m-*NEC* na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais juzi alimteua kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu na Wajumbe wa Halmashauri Kuu wakamchagua kwa kura nyingi. Kwa kweli hii tunampongeza amekuwa akifanya kazi kubwa sana katika Serikali hii na katika Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikupa tu mfano maana yake watu wasije wakafikiri labda ninasemaje; amejenga jengo la benki ya damu salama ya mkoa; amejenga jengo la watoto wachanga; ametujengea jengo maalum la wagonjwa mahututi *(ICU)*; amejenga jengo la viungo bandia na vifaa saidizi; ametujengea jengo la wagonjwa maalum. Majengo haya yote ni mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri mara nyingi tumekuwa tukiongea na yeye kuhusiana na hili jambo. Ningeomba hebu kitu kifanyike pale Iringa ili tuendelee na wadau wengine wajitokeze kwamba wanapoisaida Serikali mambo makubwa kama haya kuponyesha maisha ya watu basi angalau tuzo maalum na itambulike ili wengine waendelee kusaidia katika Wizara hii ya Afya ambayo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaomba madaktari wa magonjwa ya *physiotherapy* hasa kwa wazee, watoto na watu wenye ulemavu. Kwa kweli hili ni jambo ambalo linahitajika. Unaona tuna jengo zuri sana, lakini naona vifaa pamoja na wataalam wanakuwa wanakosekana na sasa hivi watu wengi wanaugua ugonjwa wa kupooza, lakini wanaona kwamba wakienda hospitali wanakuwa hawawezi kufanyiwa mazoezi. Kwa hiyo, inawachukua muda mrefu sana wa kupona *BP*. Vilevile tuna watoto wamezaliwa na ulemavu, tukipata wataalam wakawasaidia inasaidia pengine wengine wanakuwa wananyooshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa na mimi nizungumzie vifurushi vya bima ya afya, hebu viangaliwe upya. Mbunge aliyepita amezungumza sana. Kuna vifurushi vingine unakuta kweli umenunua, lakini hupati vile vipimo, hupati zile dawa, inabidi viangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma atafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara yetu ya Afya. Awali ya yote kwanza, nitoe shukrani za Wanahanang kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya kwani wakati tunapata changamoto ya maporomoko ya mlima yeye ndio alikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu na tulikuwa naye. Ninafikiri zaidi ya siku karibu 40, tumekesha naye na tumepambana wote. Mheshimiwa Waziri, Wanahanang wanasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wenzangu wa Wizara ya Afya ambao tumefanya nao kazi zaidi ya miaka 12 kwamba ni mtu sahihi na mchapakazi; wampokee na pia wamuunge mkono. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Mollel, tunashirikiana mambo mbalimbali ambayo nimemletea ya Wanahanang amekuwa akiyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu Dkt. Shekalaghe, siku ambayo tuko tunapambana na maporomoko ya Hanang, yeye ndiye alikuwa anaratibu hilo zoezi la wananchi kwa sababu wakati ule alikuwa upande wa masuala ya jamii. Kwa hiyo, alifanya kazi nzuri sana na niseme tu ahsanteni sana kwa Wizara ya Afya kwa kazi kubwa ambayo wametufanyia sisi watu wa Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza mchango wangu kwa maana ya suala ambalo tunalo hapa mezani; Mheshimiwa Waziri tumekuwa na utaratibu wa kujenga kituo cha afya kila kata, baadaye tukasema tuanze na vituo vya afya ambavyo vipo kwenye maeneo ambayo yana watu wengi hasa makao makuu ya tarafa. Pia, tuna maeneo ambayo tayari yana zahanati na yana watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu kwenye eneo hili badala ya kufikiria kutafuta milioni 500 yote iliyokamilika, tuangalie namna ya kuboresha zahanati ambazo ziko kwenye makao makuu ya kata, tuboreshe hasa eneo la huduma ya mama na mtoto ili tuweze kuboresha huduma za afya za msingi kwenye ngazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo langu la Hanang kwa mfano, ukienda pale Dirma tuna zahanati; tuboreshe angalau tuweke huduma ya afya ya mama na mtoto pamoja na maeneo ya Ishponga, Laghanga, Getanuwas na Lalaji yenye mahitaji yanayofanana ili wakati tunaelekea kila kata kuwa na kituo cha afya tuwe tumeanza na zile huduma za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka kuongelea ni suala la mapambano dhidi ya malaria. Nipongeze juhudi kubwa ambayo imefanyika kwamba, tumepeleka dawa za mseto 4,567,020 na tumepeleka dawa zile za chupa zaidi ya karibu 900,000 hivi. Tumepeleka vile vipimo vya *MRDT* zaidi ya 10,000,000 na upatikanaji wake ni zaidi ya 95%. Niwapongeze sana kwa mafanikio hayo kwa sababu inawezesha watu wetu ambao wameugua wanapata matibabu kwa wakati na matibabu ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye eneo hilo ninaomba tujielekeze kwenye uelekeo wa kuangamiza vile vijidudu vinavyosababisha malaria. Twende sambamba; nilipata bahati ya kutembelea kile kiwanda chetu pale Kibaha; changamoto wanayolalamika ni kupata masoko. Tujielekeze kwenye hatua ya kuhakikisha kwamba, mbu wote wanaoambukiza malaria wanaangamizwa ili tusihangaike na dawa, tusihangaike na vipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nilipata bahati ya kuhudumu Kamati iliyokuwa ya Huduma na Maendeleo ya Jamii karibu miaka miwili na nusu hivi na mara zote nimekuwa nikisemea Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara. Yamefanyika mambo mengi, hospitali ile kwa sasa ukiitazama pale ninafikiri imeboreka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameanzisha huduma ya *dialysis* karibuni na imeanza kufanya kazi Mkuu wa Mkoa amezindua. Wametuletea vifaa vya kisasa, wametupa *digital x-ray* ya kisasa. Vipimo vya kuangalia mfumo wa chakula wametuletea. Pia, suala la *sickle cell* na kuchambua mazao ya damu yamefanyika mengi. Kwenye eneo lile bado tunayo changamoto ya jengo la *emergency*. Tuna changamoto ya jengo la *ICU,* jengo la *radiology* kwa maana ya mionzi na wodi bado hazijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Manyara ina changamoto ya eneo. Mji wa Babati unakua kwa kasi sana, tukichelewa kutafuta eneo la ziada baada ya muda itakuwa ngumu kupata eneo. Ninaomba lile eneo lipanuliwe ili mahitaji ya baadaye ya ile hospitali yaweze kukidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya 2024/2025 tumetengewa shilingi bilioni mbili, lakini mpaka sasa hata senti moja haijaenda. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri iangalie ile hospitali kwa sababu ndio inayotegemewa. Ina huduma nzuri, kwa sasa Wanamanyara wameanza kuamini kama ndio hospitali ya rufaa na watu wote ambao wananiuliza mimi ni sehemu gani ambako tunaweza kupata huduma fulani Fulani, mimi nina wa-*refer* pale na kwa kweli huduma ni nzuri sana; tuwaboreshee mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari wa mkoa, wale madaktari bingwa ambao Waziri ametuletea wamezunguka wilaya zote za Mkoa wa Manyara. Wametoa huduma kwa Wanamanyara na Wanamanyara wamefurahia ile huduma; ile huduma iendelee. Ninachoomba tu ni kwamba, haya mapungufu ambayo nimeyasema Mheshimiwa Waziri utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la vifaa na vifaatiba. Kila mtu amekuwa akiongea kwamba huduma za afya ni ghali. Tumepeleka vifaa kwenye ngazi ya wilaya, mikoa, hospitali zetu za rufaa na hospitali za kanda. Ombi langu kwenye eneo hili tunao wataalam wetu wa vifaa na vifaatiba, tuendelee kuwajengea uwezo na tuwape elimu ya kutosha. Waziri amekuwa akishirikiana nao ninazo taarifa kwa sababu ni wenzangu nimefanya nao kazi. Aendelea kushirikiana nao, awape elimu ya kutosha. Changamoto zinazokuja hapa nchini ni teknolojia mpya; waendelee kufundishwa wawe wabobevu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akipiga *x-ray* Katesh hiyo iaminike mpaka Hospitali ya Rufaa Muhimbili ili kusiwe na gharama za kujirudia. Nimepiga *x-ray* Katesh, nikienda Muhimbili iwe ni hiyo hiyo kusiwe na gharama za kujirudia. Watanzania tulionao ni watu maskini, hivyo fedha zinazotumika zitumike kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuhakikishe kwamba hili linafanyika, boresha eneo la *Telemedicine* (waboreshe wataalam). Mtu yeyote ambaye amepiga labda Bunda *x-ray* akifika Muhimbili aweze kuaminika. Akipiga *x-ray* Singida iaminike kokote nchini na hizi taarifa ziende kusiwe na gharama za kujirudia. Tukiboresha kwenye eneo hili tutapunguza gharama za matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kuongea kwenye hilo hilo la vifaa tiba; tunayo Taasisi yetu ya Mamlaka ya Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi *(TMDA)*. Kwa sababu vifaa tunavyoviagiza hapa nchini 90% mpaka 95% vinatoka nje. Dawa tunazoagiza hapa nchini sehemu kubwa inatoka nje na vitendanishi vivyo hivyo. Hawa tuendelee kuwajengea uwezo waendelee kufanya ukaguzi wa viwanda wa vifaa na vitendanishi vinavyokuja hapa nchini ili tuwe na uhakika na ubora wake, usalama wake na ufanisi wake kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu sehemu kubwa; nimemsikia mwenzangu akichangia suala la kuangalia kuhakikisha kwamba tunakuwa na namna ya kuhakikisha dawa tunazozitumia

zinasimamiwa vizuri. Hata hivyo, tukisimamia eneo la uchunguzi vizuri ambako tunategemea vifaa na vitendanishi, yawezekana tukapunguza matumizi ya dawa kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ninataka niisemee ni suala la bima ya afya kwa wote. Wakati nikiwa kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo baadaye imegawanyika ikapata Kamati tatu, hili eneo tulilijadili kwa kina na Watanzania sehemu kubwa ndio tumaini lao. Mheshimiwa Waziri tunachoomba aiharakishe ili hatimaye kila Mtanzania aweze kuwa na bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu sana kwa mazingira tuliyonayo mtu kuwa na fedha mfukoni muda wote utakapoumwa ujitibu. Bima iwe ndiyo daktari, bima iwe ndiyo njia ya kujichunguza kwa maana ya ukitakiwa *x-ray* ndiyo bima yako inakusaidia; ukitakiwa *MRI* bima ndiyo inakusaidia; na *CT-Scan* pia bima ndiyo iwe inakusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipata changamoto ya kansa unaenda kwenye *PET-Scan,* bima ndio iwe inaweza kumsaidia Mtanzania ambaye ni maskini. Kwa mazingira tuliyonayo tunapoteza Watanzania wengi kwa sababu ya kushindwa kulipia matibabu. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri hii aharakishe. Akiifanya, yeyote yule hapa ataniambia Mheshimiwa Mbunge ambaye amefanya ziara kwake jambo la kwanza ambalo ataulizwa ni matibabu kwa wazee; eneo hilo lina changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na bima ya afya kila Mtanzania akiwa yuko *covered,* itatusaidia kuwapunguzia Watanzania gharama. Ninaamini baada ya Watanzania kuwa na uhakika wa matibabu na wakapata matibabu kwa wakati, uchumi wa kila mmoja utaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma. Nilimwita Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi ajiandae.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Kwanza kabisa nimtangulize sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na hatimaye tunasimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri dada yangu Mheshimiwa Jenista kwa kazi nzuri. Amekuwa ni mwalimu kwa sisi wanawake wenzake na anafanya kazi nzuri sana. Mimi katika Mawaziri bora, Mheshimiwa Jenista ni Waziri bora pia yumo. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Wamekuwa wakimsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa mama yetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Katibu wa Wizara, watumishi wote na wataalam wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanazofanya. Pia, nimpongeze Mganga Mkuu wa Mkoa wetu wa Rukwa Dkt. Ibrahim Isack na Katibu wa Afya wa Mkoa kaka yangu Masusu Ramadhani. Wamekuwa ni msaada mkubwa sana kwa wanawake wa Mkoa wa Rukwa; kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Rais wetu mpendwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Hakika mama amefanya kazi kubwa sana katika Wizara hii ya Afya. Wanawake tulikuwa na changamoto nyingi sana za afya, lakini mama amepunguza sana vifo vya mama na mtoto. Hongera sana kwa Rais wetu, aendelee kuchapa kazi, sisi tuko nyuma yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye Mkoa wangu wa Rukwa. Tunashukuru sana Serikali imetujengea hospitali za wilaya.

Ndani ya kipindi kifupi tumepata wilaya nne, lakini bado tumepata katika Wilaya yangu ya Sumbawanga Vijijini. Juzi kati hapa katika kituo cha afya kipya tumepata shilingi milioni 700 katika Kituo cha Mbui na tumepata vifaatiba vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ni wataalam. Mama amejenga, tumepata fedha nyingi sana za kujenga vituo vya afya, tumejengewa hospitali za wilaya na tumejengewa zahanati. Katika Wilaya yangu ya Sumbawanga Vijijini tumepata zahanati 18 kwa muda wa ndani ya miezi sita. Hongera sana Serikali yangu, hongera sana Rais mpendwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali yetu iangalie; wataalam wamekuwa ni changamoto sana. Tuna majengo mazuri, vifaatiba vimefika, lakini tatizo wataalam, madaktari bingwa hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Rukwa tuna upungufu mkubwa sana wa wataalam wa meno na wauguzi; ni changamoto kubwa sana. Tunaomba sana watakapokuwa wana-*windup wa*tuambie ni lini sasa wataalam wataongezeka katika Mkoa wetu Rukwa? Pia, *specialists* wa maabara hatuna, tunaomba sana watuangalie katika Mkoa wetu wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ushauri. Hapa katikati pamekuwa na wimbi la wafadhili, wafadhili walitia mgomo kuendelea kutuletea dawa. Ninaishauri Serikali yangu kwamba, tuendelee kujiwekeza, tuanzishe viwanda, tutengeneze viwanda vya kutengeneza dawa sisi wenyewe nchini, ili wafadhili wetu kama wakitia mgomo sisi wenyewe tuendelee kujiwekeza kutoa dawa kwa magonjwa mbalimbali, yakiwemo magonjwa ya *TB,* upungufu wa kinga na magonjwa mbalimbali ambayo yanaleta shida sana katika nchi yetu. Ninaomba tuanze kujiwekeza wenyewe kutengeneza, kujenga viwanda vyetu, tujitegemee wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika Mkoa wetu wa Rukwa ni tuna changamoto, siyo kubwa, lakini ni changamoto. Tulitenga eneo

la kujenga hospitali ya rufaa, kuna sehemu inaitwa Milanzi, Serikali ililipa wananchi, wananchi wale waliachia lile eneo, lakini mpaka sasa bado ujenzi huo haujaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru, nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametenga fedha, tunaomba ujenzi huu aanze haraka. Kwa sababu, eneo lilipo tunalo eneo la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, limekuwa ni finyu na majengo yamekuwa ya zamani. Tunaomba lile eneo liendelee kutumika, hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa ujenzi uanze haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bupe, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul ajiandae.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Afya, nianze tu kwanza kwa shukurani. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, sisi Moshi Mjini kwa kipindi hiki tulikuwa hatuna Hospitali ya Wilaya; tunajengewa, tena ya ghorofa na kazi inaendelea. Mheshimiwa Waziri alikuja pale aliiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna vituo vya afya viwili, lakini tumepata vingine viwili na cha tatu, nimeambiwa muda wowote hela itakuja, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha kule Kata ya Kiboroloni. Zimefanyika kazi nyingi sana kwenye Hospitali yetu ya Mawenzi na pia, zimefanyika kazi nyingi sana, hata nikizitaja sitaweza kumalizia, katika Hospitali yetu ya Kanda ya *KCMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu pamoja na Naibu Waziri kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana. Ni watu wasikivu, wanafikika muda wote na wanatusaidia sana. Ninampongeza sana Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, bahati nzuri Katibu Mkuu alishakuwa *RAC* pale Mkoa wa Kilimanjaro, kila

ninapomgusia jambo, Dkt. Shekalaghe, anakuwa analijua kichwani kwake na kwa kweli, wamekuwa msaada mkubwa sana pamoja na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda moja kwa moja kwenye Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya *KCMC*. Nimesema hapo awali kwamba, kazi nzuri kubwa sana imefanyika pale na haya ambayo ninakwenda kusema ni ya kuboresha tu; kabla sijayasema nampongeza Profesa Gileard Masenga, ambaye ni Mkurugenzi wa hospitali pamoja na timu yake yote. Kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili moja ni ombi; lile eneo la uzazi pamoja na chanjo kwa watoto ni finyu sana na ile sehemu ya kusubiria haina paa, sasa unajua mimi bado ni mzazi, ambaye nina watoto wadogo. Kutokana na Sera ile ya Serikali ya kwamba, mwanaume akienda kwenye kupeleka mtoto chanjo hapangi foleni, basi ninaenda pale. Sasa nikienda nimekuwa nikipata hizo changamoto, wananiambia lile eneo liboreshwe, liongezwe ukubwa na kupauliwa, hasa lile eneo la kusubiria, ile sehemu wanayosubiria wale akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo tumeliombea muda mrefu, najua Waziri analijua, Naibu Waziri, najua hata Wizarani limekwenda kupitia kwa Katibu Mkuu, wote wanalijua. Ni suala la *wage bill;* ninajua siyo suala rahisi kwa sababu, bado kuna hospitali nyingine za kanda nazo zinahitaji, lakini ninaomba waiangalie changamoto ya *KCMC,* Moshi Mjini na Mkoa wa Kilimanjaro kipekee, kwa sababu ya ukaribu wake na Arusha. Arusha *population* ni kubwa na *purchasing power* ni kubwa kwa sababu, uchumi wake ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa madaktari wetu bingwa pale *KCMC* hawatulii, maana baada ya muda wa kazi wanawahi Arusha kufanya tena kliniki nyingine, ili waweze kupata fedha za ziada. Sasa hiki kitu kwa kweli, kinafanya ubora wa kazi pale unapata

changamoto, hebu waiangalie kiupekee, zipo nyingine ninajua, lazima tuanze Kibong'oto, twende Kanda nyingine, Mbeya, wapi!

Mheshimiwa Spika, lakini sisi ukaribu wetu na Arusha unatuletea shida. Hebu watuangalie kwa jicho la kipekee tuweze kuboresha yale mazingira, vinginevyo tunasubiri tu kwa hamu uzinduzi wa lile banka na matibabu ya *cancer* kwa mionzi pale *KCMC,* tunawasubiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi, ambayo iko Moshi Mjini. Kwa kweli na yenyewe imewekezwa sana, tunayo changamoto kidogo ya *man power,* hebu tuangalieni, vifaa vimewekwa, kumekuwa na maboresho mazuri, *manpower* kidogo ni tatizo. Ninampongeza sana Mkurugenzi pale, Dkt. Edna Joy Munisi, anafanya kazi kubwa sana, anafikika, anajaribu kupambana, lakini bila *manpower* sasa liko kwenu, naomba muangalie namna ya kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuendelea kurekebisha ile *master plan*. Ile hospitali ni ya Mwaka 1922, yale majengo pale ni ya zamani, tunaendelea, kuna *master plan* ambayo walishaichora, wanajenga majengo ya ghorofa pale, ili tuendelee kuboresha ile huduma. Sasa ni lazima Wizara walete hela kuendana na ile *plan* ilivyo, vinginevyo vile vijengo vya zamani tukiendelea kuvikarabati tutachukua muda mrefu. Kwa hiyo, ninaomba sana tulizingatie hilo kwenye Hospitali yetu ya Mawenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye Bima ya Afya kwa Wote. Ninajua kuna watu wameongelea vifurushi kwa ujumla wake na mimi siko mbali na yale wanayosema. Ninampongeza sana Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Irene Kisaka, anajitahidi kwa kweli, kwenda na kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ya harakaharaka, moja ni TEHAMA. Ukienda *KCMC,* Idara ya Macho, kabla hujapata huduma kule unaambiwa urudi *mile* kadhaa tena, ili kadi iangaliwe halafu sijui wa-*verify, paper work* nyingi jamani! Hatuko kwenye karne hiyo tena!

Ni vizuri wa-*integrate* mifumo yao idara zote za hospitali hiyo, ukifika kwenye idara husika hulazimiki tena kutoka. Inabidi sasa kila mgonjwa akienda awe na mtu wa kumpa kampani, kwa ajili ya kwenda kupeleka hizo hela kwenye bima ku-*verify,* kurudi huku na nini! Hebu waangalie namna ya kuboresha matumizi ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye vifurushi. Sasa kwenye vifurushi mimi niko tofauti kidogo na yale yaliyosemwa na wenzangu, siyapingi, nafikiri ni hisia za jumla na zinatakiwa ziangaliwe. Kuna mahali ninaona kuna shida kidogo, hapa kwenye watu wazima wa miaka ya 60 kwenda juu, kifurushi cha mtu mmoja na cha mwanandoa hakuna tofauti! Sasa sijui tuna *encourage* watu wakifika miaka 60 waachane au iweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa tu mfano, kifurushi cha Serengeti kwa mtu mmoja wa miaka 60 *and above* ni shilingi 3,336,000 lakini wanandoa ni shilingi milioni 6,338,000; yaani kuna *discount* ya shilingi 300,000 tu, sasa sioni kama kuna pointi hapo na ni vizuri wajue haya. Kuna wakati kada fulani za Watumishi wa Umma kwenye mikoa fulani, sitaitaja, hasa walimu walikuwa wanaolewa; pamoja na mambo mengine na uzuri na nini, ni kama lile la afya. Mtu anajua nikiolewa au nikioa Mwalimu, pamoja na mambo mengine, mambo yetu ya afya yatakuwa yamekaa vizuri kwa sababu ya kile kifurushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki cha wanandoa wastaafu, miaka 60 kwa mfano, hiki cha Serengeti, Tanzanite, mwanandoa mmoja 60 *years and above* ni shilingi milioni 6,708,000 wakiwa wawili ni shilingi milioni 13,400,000 hakuna *discount* yoyote! Sasa sijajua kina maana gani, kama siyo ku-*discourage* ndoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi watuambie ni vizuri *discount* ya wawili ionekane kubwa, ili ku-*encourage* watu waweze kuingia kwa wingi zaidi, lakini hapa hamna tofauti kati ya kuingia mmoja na kuingia wanandoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwa *MSD*. Ninampongeza sana Tukai Mavere, kaka yangu, kwa kweli, anafanya kazi nzuri. Zipo changamoto, ninakumbuka kwenye hotuba zilizopita tulishafikiria kuifanya *MSD* ifanye kazi kibiashara hasa kwa kuangalia maeneo ya *SADC* na ninadhani mpaka mkataba ulishasainiwa. Sasa haya matatizo tunayayaona hapa ya bajeti, ingekuwa imewezeshwa kufanya kazi kule *SADC,* faida inayopatikana kule, ingetupunguzia mzigo huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lile suala la ku-*supply* kwenye nchi za *SADC,* na ni lazima niseme ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, na wao wenyewe hapa asubuhi wamesema, wamekuwepo Watanzania wengi ambao wameweza kufanya kazi kwenye kada za afya Kimataifa maana kidiplomasia tuko vizuri, tulimalizie. Tumalizie hiyo *effort* ya kufanya biashara kule *SADC,* ili ikipata faida huko, basi huku nyumbani tuendelee kupata unafuu, lakini zaidi nisisitize kuangalia namna ya kulipa lile deni lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda *Ocean Road*. Napo kwa kweli, ni eneo tegemeo ninaipongeza sana Serikali. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea kile kipimo cha *PET Scan* na kwa kweli, Dkt. Diwani Msemo anafanya kazi nzuri pale, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninaloenda kusema nimeshamfikishia Dkt. Molel *in personal,* kile kipimo cha *PET scan* ambacho ni cha bei kubwa sana. Serikali imewekeza, kimesaidia na kimepunguza hata *referral* kwa zaidi ya 67%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyongeza kidogo kwa baadhi ya magonjwa. Kwa mfano *Hodgkin lymphoma* hauwezi kupima pale kwa sababu, kuna nyongeza kidogo inatakiwa u-*upgrade*. Hebu, tafadhali, kwa sasa *Hodgkin* nayo imekuwa ni tishio, watu wengi sana wanaumwa ugonjwa huo. Hebu tuangalie namna ya kuboresha tuweze kupima mpaka *cancer* pale, ili tuweze kuhudumia wananchi wengi zaidi na ku-*save* fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni la ujumla, la *manpower,* ninaipongeza sana Serikali. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, ninakupongeza Waziri pamoja na timu yenu yote, wamepunguza lile *gap* kutoka 64% ya uhitaji mpaka 55%, ni kazi nzuri sana. Sasa ninawaomba tuendelee kuongeza nguvu. Kwa mfano, sisi kwenye Kamati yetu ya *LAAC* tuliwahi kutoa ushauri kwamba, baadhi ya mapungufu yanaonekana, kwa mfano, kwenye Serikali kwa ujumla linaloleta shida kwenye *wage bill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kumalizia, watu ambao wanapandishwa cheo. Kwa mfano, Mkurugenzi wa Halmashauri alikuwa ni mwalimu, anapandishwa anakuwa Mkurugenzi; anapoondolewa kwenye ile nafasi, tena kwa sababu ya uzembe, ule mshahara unabaki pale, amezuia *wage bill* za watu wengine hapo chini, wengi sana. Tuangalie namna, akipandishwa, akishushwa, basi ashuke kwenye ule mshahara ule wa chini kwa sababu, hapa tunataka tuangalie kazi iweze kuwahudumia Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Priscus Tarimo, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa *Engineer.* Stella Martin Manyanya ajiandae.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hii Wizara muhimu. Moja kwa moja ninaanza kwa kumpongeza sana dada yetu, Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama, Mlezi wa Mkoa wetu wa Kilimanjaro, Kiserikali kwa hiyo, Waziri ndiyo mlezi wangu kule Kilimanjaro. Pongezi sana kwako dada Mheshimiwa Mhagama kwa kazi nzuri anayoifanya Wizarani na mkoani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza kwa namna ya pekee, kidiplomasia yuko vizuri, anaona mambo, nilimwona alivyokuwa anapambana Marehemu Dkt. Ndugulile apate ule u-*director,* Profesa

Janabi na hata mama sasa amepewa *Award* ya *Bill Gates,* ambayo tunaita ni *Goalkeepers Award*. Inaonesha kwamba, kwenye diplomasia uko vizuri. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeze pia rafiki yangu, Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Kilmanjaro, Mheshimiwa Dkt. Molel, watu wa Siha wajue wana jembe. Nina siri kubwa sana na Mheshimiwa Mollel, mwaka 2009 aliokoa maisha yangu, hatakumbuka, lakini mimi ninajua; nilivyorudi kumletea suti akawa ameshahama, nikiwa ninafundisha *South Africa*. Kwa hiyo, tuna jembe, tena zuri sana, hongera sana. Pia, ninampongeza Katibu Mkuu – Dkt Shekalaghe, Makamu wake, Naibu wake pamoja na watu wengine wote wa Wizarani kwa kazi nzuri wanazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali, imewekeza vizuri pale kwenye Hospitali yetu ya *KCMC,* kama alivyosema Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Priscus Tarimo wa Moshi Mjini. Pale tunaona Serikali imewekeza shilingi bilioni nne kwenye lile Jengo la Mionzi na wamewekeza kwenye jengo moja, bado kuna majengo manne yako tu kwa hiyo, tuwaombe, hakuna hasara hata kidogo kuwekeza *KCMC* kuna wabobezi wa hali ya juu ambao wanatoa tiba ya kubadilisha nyonga; ukishazeeka, nyonga ikikataa, nenda pale utapata tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya upasuaji kwenye mfumo wa chakula, tezi dume wanafanya oparesheni, wanatibu ugumba, wanapandikiza *cornea* na wanatengeneza viungo bandia. Kwa hiyo, ni hospitali ambayo hutashangaa kwenda pale, kusema ukweli, wanatoa huduma nzuri kwa hiyo, ninaiomba Serikali tuendelee kuwa-*support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Profesa Masenga. Kupitia msamaria mwema wametoa, wame-*waive,* msamaha kwa wagonjwa wengi sana, kama 4,002, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2.1 wamesamehe bure. Kwa hiyo, tuna Profesa, Mungu ambariki kuendelea kusaidia watu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla sijaanza mchango, ninaomba mambo ya kwenye jimbo langu kwanza. Mheshimiwa Waziri nilimwomba anisaidie *Digital X-Ray,* kwa ajili ya Hospitali ya Kibosho, ambayo ni *Referral Hospital* ya Wilaya ya Moshi, ilikuwa ni Bajeti ya 2023/2024. Alivyokuja Mabogini nilimwomba, yaani ni kama nimeonekana mtu wa ajabu ni kwamba, hawa watu hawajapata kile kifaa na wananilaumu sana. Ninaomba jamani, aandike mahali tu, wasije wakawasahau tena hawa jamaa zangu, ni hospitali muhimu sana inasaidia Watanzania *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba vifaatiba, ninajua mengine ataongea na pacha mwenzake. Vifaatiba katika Vituo vya Afya vya Uru Kusini, Uru Shimbwe, Uru Kyaseni na Kibosho Umbwe; Kituo cha Afya cha Kibosho Ubwe ni cha zamani kinahitaji vifaatiba na pia, kwenye ile Hospitali ya Wilaya ya Mabogini bado vifaa tiba havijafika pale. Tunaomba watusaidie ikiwa ni pamoja na magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kiujumla utahusu changamoto za tiba hapa nchini. Ninaanza kwa kusema kwamba, huduma ya afya ni haki ya binadamu. Hata kwenye Biblia kuna mistari 108 inayoongelea kuhusu afya ya mwili na tujikumbushe hapa, hata Yesu Kristo alivyokuja duniani hapa alitibu watu kwa kutumia nguvu zake za Kimungu, alijua nini maana ya afya na alitoa tiba ya magonjwa mbalimbali, sote tunafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mungu mwenyewe alituhurumia sisi wanadamu akatutibu, ninaiomba Serikali, ambayo ni mamlaka iliyowekwa na Mungu yuleyule, tujitahidi kabisa tuwasaidie wananchi wetu wapate tiba, ili tupate baraka za Mungu, Serikali yetu ipate baraka za Mungu. Ninamshukuru Rais anajitahidi kusema ukweli, wamefanya vitu vingi vizuri sana, tuweke nguvu kwenye hizi changamoto nitakazozisema, ili tusaidie wananchi wapate tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza hapa nchini ni gharama kubwa ya matibabu kwa baadhi ya magonjwa. Mtu akiugua ugonjwa kama figo, wenzangu wameshasema, *cancer*,

moyo, kubadilisha damu na ugonjwa wa selimundu, wewe ujue unakwenda, kama usipokuwa na pesa unakwenda kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu kidogo niongelee ugonjwa wa selimundu ambao wachangiaji wenzangu hawajausema. Katika ripoti ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, 15% ya Watanzania wana vinasaba vya selimundu kwa hiyo, huko mbele ya safari nina hakika tutakuwa na wagonjwa wengi sana wa selimundu kwa sababu, tutakuwa tunaoana kati ya mtu mwenye selimundu vinasaba na mwingine mwenye selimundu, tutakuwa na wagonjwa wengi. Sasa hivi wame-*identify* watu 34,220 wenye selimundu na 60% wanaowatibu kwa kutumia *hydroxyurea*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safi kabisa, lakini ni watu 11 tu katika hao watu 34,000 ambao wameishawafanyiwa upandikizaji wa uroto, ambayo ni sawa na asilimia 0.03 ya watu wote ambao wamekutwa na ugonjwa huu. Ninaiomba Serikali, haya magonjwa ni makubwa, magonjwa aliyoyataja Waziri ikiwepo selimundu, wataalam tunao, vifaa tunavyo; ninaipongeza sana Hospitali ya Benjamini Mkapa, wanafanya kazi nzuri, tusitibu watu 11 tu, tutoe ruzuku ya kutibu hawa watu, ili nao wapate maisha na wafurahie kuwa Watanzania. Ninaiomba sana Serikali itoe ruzuku, kwa ajili ya haya magonjwa makubwa niliyoyataja ukiwepo huu wa selimundu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine, ya pili, ni ukosefu wa vifaatiba, ukosefu wa dawa na chanjo kwenye baadhi ya maeneo ambayo yako vijijini. Tukiondoa yale maeneo, ambayo ni hospitali mpya, tumezijenga au vituo vya afya vipya tumevijenga, vile vya zamani vingi vina uhaba wa vifaa tiba. Kwa mfano, vitanda vya kulaza wagonjwa kusema ukweli, ni shida katika baadhi ya maeneo; majokofu ya kutunza dawa, kutunza maiti, magari, dawa, hata chanjo, ninaiomba Serikali, hebu tujiongeze, tuwekeze kwenye haya maeneo tusaidie vile vituo vya vijijini ambako ndiko wanakoishi watu wengi. Tukishasaidia kule vijijini idadi ya watu watakaokuja Mjini kupata tiba itapungua na tutakuwa tumewasaidia sana Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kubwa ambayo iliyopo kule vijijini au kwa Watanzania kwa ujumla ni uwepo wa wanachama wachache waliojiandikisha kwenye Mfuko wetu wa Bima ya Afya. Watu wengi hawajajiunga na mfuko huu kutokana na gharama kubwa ambazo zimeainishwa. Ninaomba nitoe mifano, japokuwa wenzangu wamekwishasema, ninataka tu tuangalie umuhimu wa hiki kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Ngorongoro Afya na kuna Serengeti Afya. Sasa kwa watoto wadogo kati ya umri wa 0 – 17 *years* akichukua kifurushi cha Ngorongoro ni shilingi 240,000, akichukua cha Serengeti ni Shilingi 660,000. Kwa miaka 18 – 35 hapa kwenye hii *age* ndipo tuna idadi kubwa ya Watanzania. Akichukua cha Ngorongoro ni 432,000 na Serengeti ni 792,000. Akiwa na mke vyote vinapanda zaidi, kama alivyoongelea mchangiaji mmoja aliyepita. Miaka 36 – 59 Ngorongoro ni 540,000 na Serengeti 1,620,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale watu wazima kama mimi. Ukishakuwa mtu mzima kama mimi Ngorongoro ni shilingi 708,000 na Serengeti ni shilingi 3,336,000. Ukiwa na mwenzako Ngorongoro ni 1,345,000/- na Serengeti ni 6,338,400. Hizi data nimezipata kutoka kwenye *website* ya *NHIF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tuwe wakweli; watu wengi kule vijijini uwezo wao wa kununua hivi vifurushi ni mdogo sana, huo ndio ukweli wa Mungu. Kwa hiyo, niiombe Serikali hebu chondechonde, ninajua kuna gharama zinatakiwa mtu alipe ili atibiwe, lakini Watanzania ni hawa hawa uwezo wao ndiyo huo. Sasa tusipofanya kitu kurekebisha mambo watakuwa wanafia kule nyumbani kwa sababu hawawezi kukata hivi vifurushi. Watakuwa wanafia nyumbani badala ya kwenda hospitali kwa sababu kama mtu hana bima ya afya na hana fedha ya kwenda kujitibu itakuwa ni ngumu sana. Niiombe Serikali kwanza itafute namna ya kusaidia hawa watu ili waweze kumudu hivi vifurushi, virekebishwe *if possible;* wafanye marekebisho fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhamaishe; tufanye uhamasishaji wa hali ya juu kwa sababu inaonekana watu wengi hawajaingia kwenye bima ya afya. Tuhamasishe watu watu wajiunge na hii mifuko, ili mtu atakapougua kama ana bima ya afya akienda kupata tiba hospitali hatapata shida, hatarudishwa, atatibiwa na ataishi kama ambavyo Mungu amempangia awe na maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, ninaomba niseme tu mengine nitachangia kwa maandishi. Baada ya kusema hayo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wake wote. Sisi tunawatakia kila la kheri; lakini ninaomba yale niliyomwomba kwenye jimbo langu na yale ambayo nimependekeza ayachukulie *seriously* ili Watanzania wanufaike na kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa Patrick Ndakidemi. Nilimwita Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Francis Isack Mtinga

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi. Jioni ya leo nichangie Wizara ya Afya *Vote* 52 katika bajeti yao hii muhimu ambayo inagusa maisha ya Watanzania. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupatia nafasi kuendelea kutimiza wajibu wetu kama Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni shukrani. Nimshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ametuheshimisha na kutukimbilia Wanababati kwa sekta hii ya afya. Sisi Wanamkoa wa Manyara tunamshukuru na tuna deni la kulipa kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa mambo ambayo yamefanyika na ambayo muda wote yalikuwa hayajawahi kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali yetu ya Mkoa ni juzi tu ametupatia vipimo vya *dialysis* (mashine za *dialysis*), pia kwa mfumo mzima wa chakula ili wananchi waweze kupata matibabu hayo na maendeleo yanaonekana katika Hospitali yetu ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wetu Jenista atufikishie salamu zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwamba Wanamanyara tunamshukuru kwa hospitali ile. Matibabu yanatolewa na majengo yanaendelea. Niombe tu hizo bilioni mbili ambazo zimepangwa katika bajeti hii katika miradi 55, ambapo miradi 31 ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Manyara hazijapata, tunaomba ikiwapendeza katika hizi siku 20 zilizobaki basi watupatie hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hospitali ya wilaya tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa miaka hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia tumepata hospitali ya wilaya pale majengo yenye thamani ya zaidi ya *1.4 billion,* wametupatia. Mpaka wametupatia Kangaroo *room* kwa ajili ya wale watoto njiti, wamekuwa sasa wanahudumiwa pale. Pia, tumejengewa wodi ya wanawake kwenda kujifungua zaidi ya shilingi milioni 500. Tumepatiwa *emergence ward* yenye thamani ya milioni 300; na sasa *1.4 billion* inaendelea pale, majengo yetu yameboreka sana. Tusipokuwa na shukrani kwa kweli hata Mwenyezi Mungu hawezi kutubariki. Mheshimiwa Waziri atufikishie shukrani hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vituo vyetu vya afya. Mimi nina kata nane, katika kata hizo ni kata mbili tu zimebaki. Kata ya Nagala pamoja na Kata ya Singe vituo vya afya ambako hizo hela Mheshimiwa Waziri niliongea naye pia kwamba, tupatiwe ili vile vituo viwili viweze kukamilika. Kwa kweli kwa jimbo letu tuna moyo wa shukrani kwa Mheshimiwa Rais wetu, Serikali yetu pamoja na Mawaziri wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri yeye na msaidizi wake, wamekuwa wasikivu, wanafikika na tunapokuwa na shida yoyote tukiwapigia simu kwa kweli wamekuwa wakitusaidia;

hasa wagonjwa wale ambao wameshindwa kutibiwa, wamekuwa wakitusaidia sana. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa uzoefu alionao ninaamini atasaidia hii Wizara ya Afya; akisaidiana na Dkt. Mollel. Tunawashukuru sana kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakituhudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la pili, kuhusu hizi fedha za *MSD,* ambapo wanaomba wapatiwe deni hili la bilioni 434, na *NHIF* bilioni 210. Kwa kuwa sekta hii bado wahitaji ni wengi tunaomba basi fedha hizi zitolewe na Wizara ya Fedha ili taasisi zetu hizi ziweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusiana na suala la Sera ya Afya Bure kwa wajawazito, watoto chini ya miaka mitano pamoja na wazee. Juzi niliuliza swali; kwamba ni nini hasa ambacho ni bure? Kwa sababu tumekuwa tukipata sana simu za akinamama wajawazito wanaojifungua. Nimshukuru sana Dkt. wetu wa Hospitali ya Mrara pale Babati, amekuwa akitusaidia sana Madiwani pamoja na Mbunge. Mama anakwenda kufanyiwa *operation; operation* ni bure, lakini akitoka tu kule *theatre* vifaatiba, sindano dawa, kila kitu anachajiwa *(to be charged)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri amesisitiza kwamba sera hii bado ipo pale pale na ndiyo tunayoisimamia. Basi ninamwomba ikimpendeza dada yetu wakati wa ufafanuzi atuambie tu, kwamba ni bure kweli au kuna vifaa vinakuwa *charged? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kuwa 60% ndiyo ambayo Serikali inachangia, 40%; kwenye swali la nyongeza niliiloliuliza ndiyo yule mama anayochangia. Basi atuweke wazi ili iepushe usumbufu tunaowapatia madaktari wetu na kuwaambia tibuni bure, sera ni bure, kwa nini wanawa-*charge*? Tukiweka hili huru litatuweka huru. Tunaomba siku ya leo wawatangazie Watanzania kwamba kuna mtu mwenye uwezo anakuwa *charged*, kuna mtu asiyekuwa na uwezo anakuwa *charged* hata kama yupo kwenye hiyo

package. Itatusaidia sana na itabariki kazi njema tunayoifanya katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana pia atupatie ufafanuzi, kwamba, baada ya kuleta hivi vifurushi vya bima ya afya; je, bado tunasimamia hii sera yetu ya afya bure kwa wale au kuna *change* sasa; kwamba tunahama sasa wote ni lazima twende kwenye bima ya afya? Sasa, wakati tukisema sera yetu inasema tunawatibu bure wakati huu tume-*introduce* vifurushi vya bima ya afya kwa wote na sheria tumepitisha, hapa atatusaidia ufafanuzi. Tunaenda na lipi, wote twende kwenye bima au bado hii timu inatibiwa bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hivi vifurushi; Mheshimiwa Waziri ana vifurushi vya Tarangire, Ngorongoro, Mikumi, Serengeti na *Tanzanite*. Ni jambo jema kabisa. Tulipopitisha Sheria hii ya Bima ya Afya kwa Wote Mwaka 2023 tuliomba Serikali yetu na Mheshimiwa Waziri watuletee hivi vifurushi kupitia kanuni. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, Kamati yetu ya Bunge ya Huduma za Jamii pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo wapitie hivi vifurushi waone *affordability* ya hivi vifurushi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye vifurushi hivi; mfano, mzee mwenye miaka *60 plus* ukimlipia kifurushi cha Tarangire shilingi 240,000 anapata huduma zifuatazo; anamwona daktari bingwa, lakini huyu mzee mwenye *60 plus* anakosa huduma ya *dialysis*. Mheshimiwa Waziri anafahamu kuwa wazee wengi wa *60 plus* wana matatizo ya sukari*, pressure,* magonjwa ya moyo na wanahitaji mazoezi tiba; lakini wanakosa vipimo vya *MRI, CT-Scan*, mazoezi tiba, saratani na cha *dialysis*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifurushi cha tarangire ndicho ambacho wananchi wetu wengi wa hali ya kawaida wakisaidiwa na vijana wao kuwalipia labda, maana ni mzee tunataka awe na bima, hiki ndicho kifurushi ambacho ni *affordable* kwa vijana na familia wanaweza wakamlipia huyu mzee ambaye ni *60 plus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama huyu mzee ambaye yupo kwenye *60 plus* yupo kwenye ndoa; hawa wawili kwenye kifurushi cha tarangire analipa 472,800/-; lakini akienda kwenye kifurushi ambacho kinamsaidia kupata tiba za *dialysis,* saratani, mazoezi, tiba ya *MRI*, *CT-Scan* na kadhalika analipa milioni 13,214,760/-. Hayo ndiyo mahitaji ya wananchi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wazee ambao wapo kwenye ndoa, Mungu kawajaalia, wanalipa milioni 13. Maana yake ni kwamba watoto wao wanapaswa watafute, *per month,* isipungue milioni moja, ili waweze kupata hizi milioni 13 kwa mwaka. Bado tunaona hivi vifurushi ni ghali sana. Niombe na niishauri Serikali yetu, kwamba, kwa kuwa hivi vifurushi siyo *affordable* kwa wananchi, tuone sasa tuangalie jinsi gani tunaweza tukachangia matibabu, sisi Watanzania kwa wote. Hii ni kwa sababu lengo la bima ni kuchangiana, kusaidiana. Yule ambaye hajiwezi tumsaidie au asaidiwe na wale ambao wanajiweza. Huyo asiyejiweza ukimpeleka milioni 13 maana yake hawezi kwenda hospitali akatibiwa, akapata hayo matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Waziri wasi-*hesitate* kuleta vyanzo ambavyo Watanzania wote tutavichangia. Kama kwenye barabara tulikatwa shilingi 100 ikatusaidia katika kujenga barabara zetu *why not* kwenye *line* za simu milioni 90 tulizonazo tukahitaji hata shilingi 500, ili hiyo isaidie mtu mwenye moyo, saratani, sukari ambapo hayo magonjwa yanaendelea kwa kasi kubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri kwenye bajeti ya Mheshimiwa amesema hivi, kwamba amesamehe wagonjwa zaidi ya 3,000, zaidi ya bilioni tatu; maana yake Mheshimiwa Waziri amezitafuta na kuzilipa, wale ambao tunamwambia hawajiwezi. Sasa, ili taasisi zisiendelee kulipa hizi fedha kwa machungu makubwa kwamba mtu amefariki, imeletwa milioni sita, wanajamii hawana, tunawashukuru tunawapigia wanatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tusi-*hesitate*, twendeni tuka-*identify* chanzo ambacho Watanznaia watachangia wote. Tunaweza tukaenda kwenye *crop cess.* Kwa sababu watumishi wa Serikali…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nimwite *Engineer* Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na mchangiaji wa mwisho Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

MHE. ENG. STELLA N. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na vilevile nikushukuru wewe kwa kazi kubwa anayoifanya na ninaamini kule Njombe hawatamsumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida nitaanzia kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu pamoja na wote wanaomsaidia katika kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinazidi kuimarika. Pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mdogo wangu Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake. Ninaamini leo kule Songea yule mwanaye Ibrahim kwa jina maarufu *tall* leo atakuwa ana furaha sana, kwa sababu kila wakati *tall* akimwandika kwenye mtandao hajawahi kubadilika kumsifu kwa kazi zake nzuri. Kwa hiyo, ninamuunga mkono leo na ninasema watu wenye roho nzuri kama hao, leo Ibrahim nimeona aingie kwenye *Hansard* za Bunge, ni mtu mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo yaliyozungumzwa nianzie na pale alipoishia Mheshimiwa Gekul kwa sababu muda ulimwishia. Kwa kweli hali ya hivyo vifurushi vilivyopangwa haioneshi sisi Watanzania kuthamini utu na utu uzima. Kwa sababu huyu mzee mara nyingi ndiye aliyestaafu. Amestaafu kutoka kwenye aidha ajira rasmi

au hata kama alikuwa kwenye ajira zake binafsi za kilimo na kadhalika. Ametumika miaka yote ya umri wake katika kuisaidia nchi hii halafu mwishoni anaambiwa sasa wewe kwa sababu umeshakaa sana tunakuwekea hiki kifurushi kikubwa kikusaidie. Hivi maana yake ni nini ndugu zangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani waliopanga walikuwa hawajajua hali halisi. Huyu mzee anahitaji kusaidiwa, hana kitu halafu ndipo kifurushi chake kinakuwa cha milioni. kwanza hata kula yake ni tatizo, sasa hizo milioni kadhaa zinatoka wapi? *Simply* kwa sababu tunamhofia atakuwa anaumwaumwa kila wakati, ana magonjwa yale mazito mazito. Ndiyo gari bovu limeshatumika, kwa hiyo inabidi wote wenye nguvu tumsaidie na hiyo ni heshima na hekima kubwa mbele za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, ninamwamini, pamoja na Naibu wake na timu yao yote wayasikie haya maneno yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si mara ya kwanza tunazungumzia juu ya umuhimu wa kuwa na utaratibu wa kuchangia hizi bima kiurahisi zaidi kuliko kung'ang'ania kuweka fedha nyingi kwa mtu mmoja. Jamani sisi tunaotoka vijijini tunashuhudia watu wanakufa kwa kushindwa kupata huduma na tena hizo huduma zinapatikana mbali, inabidi asafiri. Kwanza nauli ni nyingi halafu akifika hapo anatakiwa tena kutoa hizo gharama nyingine. Tafadhali, kwa namna ya kipekee ninaomba tuliangalie hilo suala upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwanza pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa jitihada kubwa walizozifanya. Wilaya yangu ya Nyasa sasa hivi ina sehemu nyingi za kutolea huduma za afya ikiwemo zahanati; tunazo sasa 40, vituo vya afya tulikuwa navyo vitano, sasa hivi tunaenda kwenye saba. Pia, hospitali ukijumlisha na zile za Makanisa tutakuwa nazo sasa tatu; na *ambulance* wametuletea. Hata hivyo kuna changamoto ya wataalam. Tunaomba sasa tusiangalie tena vijijini kama wakati ule. Watu wameelimika, wanahitaji kupata zile huduma mbalimbali zinazojitosheleza, ikiwemo huduma za kibingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo huduma za kibingwa katika mwongozo walionao, wanasema kwamba kwenye wilaya hakuna huduma za kibingwa; kwa hali hiyo mtu mwenye bima ya afya akienda kutibiwa na bingwa katika eneo lile, anaambiwa huyu daktari bingwa huyu kama yupo kwenye hospitali ya wilaya ni sawasawa na ameenda pale kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, hawezi kumwandikia mgonjwa wake dawa zile zinazoandikwa na daktari bingwa *simply* kwa sababu yupo katika hospitali ya wilaya. Hiyo inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa tumeifanya na Serikali yetu imefanya kazi kubwa. Sasa, ipunguze gharama za watu kuendelea kuhangaika kwenda mpaka mijini mbali huko wakati tayari wangeweza kupata huduma hizo kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao mabingwa uzuri wake hata wakienda kwenye maeneo haya ya wilayani wanapenda kabisa kwa sababu sasa hivi wilaya zote ni nzuri. Wilaya kama ile ya Nyasa wewe mwenyewe unaona *Maasha Allah,* wilaya nzuri. Mtu atapenda tu kukaa kule siyo? Sasa vitu vidogovidogo vinakwamisha. Yeye akimtibu mgonjwa eti kwa sababu yupo wilayani alipwe 7,000, huyu aliyeko mkoani au maeneo mengine alipwe 25,000 (yaani inalipwa kutoka kwenye hospitali). Sasa, hiyo inakatisha tamaa na hata zile hospitali za wilayani zinashindwa kukusanya mapato stahiki kwa sababu wale madaktari wao kama bingwa wanachukuliwa kama daktari wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuuliza swali hili humu Bungeni, kwa hiyo ninaomba lifanyiwe kazi mapema ili hospitali zote za wilaya ambazo zina uwezo wa kupata madaktari bingwa zipate madaktari bingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto kubwa imebakia kwenye uzazi. Kwa sasa hivi tumeshapunguza sana vifo vya mama na mtoto na sasa tunataka kupata maisha bora zaidi. Kwa hiyo, tunataka hao *Gynaecologists* waende huko kwenye wilaya sasa. Mabingwa waende kwenye wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu usafiri wa pikipiki ambao upo kwenye kila eneo na tunautumia sana, lakini hivyo hivyo watu wanavunjika miguu, mikono, meno. Sasa unakuta kwenye maeneo ya wilaya kwanza wataalam wa *X-Ray* wapo wachache, kuna maeneo hawapo kwa mfano kwenye vituo vya afya hawapo, lakini vilevile, hao wa meno hawapo wa kutosha. Kwa hiyo, tunachoomba tuwekeze kwenye kupata hawa wataalam. Washuke sasa huku chini ili tuendelee kufaidi kazi nzuri aliyoifanya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kuhakikisha kwaba wananchi wake wa Tanzania wanakuwa na afya bora, wanakuwa na maisha bora. Kwa kweli saa hizi hata ukimwona mtu wa kijijini hana tofauti na mtu wa mjini. Hakuna tofauti kabisa, kwa sababu wote wanafurahia maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niseme tu kwamba ninazidi kuomba. Ningetamani katika upangaji wa bajeti zinazoendelea, pale Tingi ambapo ni makao makuu ya Tarafa ya Mpepo wapate kituo cha afya ambacho kitakaribiana na hadhi ya hospitali kwa sababu idadi ya watu katika ukanda ule ni kubwa. Kwa hiyo, ni mambo ya kumalizia tu katika kazi nzuri ambazo zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizidi kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa Wilaya ya Nyasa. Kwanza kwa heshima kubwa ambayo wamenipa mimi kuwa Mbunge wao kwa vipindi viwili. Mbunge mwanamke, ninaamini sijawaangusha na ninaamini wao wananipenda na ninaamini hawatatishwa na kitu chochote kile (kiwe pesa, au maneno) bado wataendelea kumuenzi Mbunge wao mpendwa *aka* Kagauni *Engineer* Stella Manyanya, kwa sababu tumefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pia niseme tu kwamba maisha yetu yanahitaji utulivu. Maisha yetu yanahitaji upendo, maisha yetu yanahitaji kusaidiana. Kwa misingi hiyo, sisi Wabunge ambao tunamaliza muda wetu tulijitahidi kwa uwezo wetu wote kuhakikisha tunatimiza wajibu wetu. Saa hizi wao na wenyewe watapimwa kwa kutimiza wajibu wao kuwatendea haki waliofanya vizuri kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itakuwa ni motisha hata kwa Wabunge wengine wanaokuja, kwamba, kumbe nikifanya vizuri nitachaguliwa tena. Kumbe nikazane nifanye inavyotakiwa ili nichaguliwe tena, lakini kama watathamini visenti vinavyomwagwamwagwa kama upupu huko wakasahau yote mazuri yaliyofanyika, hakika watakuwa wanatunziwa vifedha kwenye bahasha halafu hakuna watakachokiona kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana wananchi wangu wamenizoea nikisema hayo kila wakati, lakini nimeona iwe kwa faida ya Watanzania wote. Hali kadhalika, hicho ndicho kitakachompa sana Mheshimiwa Rais wetu kura za kutosha kwa kazi kubwa aliyoifanya. Tunawashukuru sana wote, tunamshukuru Makamu wa Rais kwa kumsaidia sana Mheshimiwa Rais, tunamshukuru Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri wote na kwa kweli kila mmoja kwa nafasi yake bila kuwasahau wataalam wa afya. Wamekaa huko saa hizi wananisikiliza, tunawashukuru sana kwa wema weo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kumsahau *DMO* wangu, ananisaidia sana katika Jimbo langu la Nyasa. Ninasema ahsanteni sana, Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *E*ngineer Stella Manyanya kwa wosia mzito. Nimwite mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Francis Mtinga.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu sana ya mwisho ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ambayo inaangalia afya za Watanzania na Taifa lenye afya ndiyo linaendelea kuwa Taifa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze watendaji wa Wizara hususan Naibu, kwa sababu amekuwa hapo muda mrefu na kwa kweli ukimwangalia hata wakati anajibu tu maswali unajua kwamba pale Serikali imeweka chombo cha maana na ni msikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana wananchi wa Mkalama wajue tunapongea vituo vya afya ni kwenye TAMISEMI na zahanati zao ni kwenye TAMISEMI. Kwa hiyo, tunapoongelea kwenye Wizara hii tukiongelea mambo ya Kitaifa wasiseme Mheshimiwa Mbunge wetu anasimama anaongelea mambo ya Kitaifa wakati bado hatuna zahanati, hatuna vituo vya afya, huko ni TAMISEMI. Hata tunaongelea suala zima la nchi kwa maana ya afya ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanahitaji matibabu. Watanzania wa hali ya chini ambao ndio wengi wanahitaji afya, na afya ni lazima wapate matibabu na matibabu ni ghali. Popote duniani matibabu ni ghali kwa sababu ya vifaa vyenyewe na kwa sababu ya dawa zinatengenezwa kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, ndiyo maana tunakuja na suala zima la bima ili watu wazima wengi wachange fedha wawachangie wagonjwa wachache ili na wao waweze kuwa na afya bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Watanzania wajue kwamba tunapoongelea bima hatuongelei wagonjwa kuchangiana, tunaongelea Watanzania wenye afya njema wengi wachange fedha ili wagonjwa wachache katika nchi yetu waweze kutibiwa. Ndiyo maana chanzo cha fedha kinakuwa ni kitu muhimu sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wetu Watanzania si laana. Wingi wetu ni baraka na wingi wetu ni mtaji wetu, kwa sababu siku zote mtaji wa watu, watu wakiwa wengi umoja wao ndiyo mtaji wao. Kwa hiyo, ninataka niwaambie Watanzania wanielewe vizuri, Serikali na Bunge hili linielewe kwamba tunapaswa kutumia wingi wetu ili tuweze kupata afya bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo ni vingi vimetumika**,** mafuta sijui nini na nini, lakini chanzo cha wingi wetu bado hatujakitumia vizuri. Nitakwenda kwenye wingi wetu kwenye suala zima la matumizi ya simu za mkononi. Ni jambo jema sana kwamba Watanzania wamechukua vizuri teknolojia ya simu za mkononi, mpaka wazee

vikongwe wana simu, mpaka watoto wa shule wana simu na wanazitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za *TCRA* za mwezi Machi, *line* za simu zilizo hai, siyo mfu hai ni milioni 90.4; katika *line* hizi hai watumiaji wa *internet* ni milioni 49. Maana yake hawa wanatumia *MB* kweli kweli. Wanaotumia dakika tu viswaswadu vile na nini bila *internet* kwa ujumla wao, dakika zinazotumika ni takribani bilioni 40.6, dakika bilioni. Katika hizi, kutoka nje ya nchi zinakuja karibu dakika milioni 36. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Ninapenda tukitumie chanzo hiki Watanzania wanielewe. Hii wasije wakachanganya, wasije wakachanganyana yaliyotokea huko nyuma kwenye suala la kutuma fedha unakatwa na yule anayepokea sijui na nini, hapana! Hapa tunataka tuongelee mchango wa Mtanzania kidogo ambaye ni mzima amchangie Mtanzania mwenzake ili Watanzania wote wapate bima ya Taifa, bima kwa ajili ya matibabu kwa Watanzania wote, tena bima isiyo na ngazi, bima ambayo ni *flat rate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idadi hii ya Watanzania, ya *line* zilizo hai milioni 90.4, ninataka niende na hesabu ndogo sana. Tuchukulie kila Mtanzania anaponunua *voucher*, awe anaitumia kwa *MB* kwa ajili ya *internet*, awe anaitumia kwa dakika, ili mradi lazima atoe hela kidogo apate uwezo wa kuitumia simu yake. Ninataka nimwombe Mtanzania anielewe sana. Mtanzania maskini wa hali ya sana mwenye uwezo wa kununua *voucher* ya shilingi 1,000 kwa siku, nimwombe Mtanzania huyu anayenunua *voucher* ya 1,000 kwa siku atuchangie 10% ya shilingi 1,000 ambayo ni shilingi 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 100 hii ukizidisha kwa *line* zilizo hai milioni 90.4 nitapata kwa siku bilioni 9.4 *per day*, lakini hela hii nikiipeleka kwa mwezi kwa siku 30, nikachukua bilioni tisa hizi nikazizidisha mara 30 nitapata bilioni 271.2. Bilioni! Lakini nikizipeleka kwa mwaka kwa sababu bajeti zetu zinakwenda kwa mwaka, nikazidisha hizi fedha bilioni 271.2 mara 12 nitapata trilioni 3.2. Sasa,

kwa sababu hizi ni hesabu za karatasi, basi nifanye tu kwamba nimekosea sana niende *half way* ya hizi hesabu, nusu yake. Maana yake tutapata trilioni 1.5 ambayo itaingia kwenye Mfuko wa Bima kwa ajili ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania ambaye amechangia shilingi 100 kwenye 1,000 yake anaponunua *vouche*, na kampuni za simu kazi yao ni kutukusanyia tu hawatakiwi kuweka *charge* nyingine yoyote. Kwa hiyo, ninaomba Watanzania, ukitoa hiyo ambayo hutaona maumivu yake, kwa sababu wewe ukitoa 1,000 unawekewa *MB* za shilingi 900. Wala hu-*feel* lakini ujue kabisa umemsaidia Mtanzania akatibiwa kwenye *MRI*, anaweza akatibiwa kwenye *cancer* vipimo mbalimbali, kwa hiyo shilingi 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mifano hai kwenye Kodi ya Pango. Watanzania walikuwa wanalalamika sana kwenye Kodi ya Pango, lakini tulipoipeleka kwenye LUKU wala hawa-*feel*. Wananunua umeme wao wameshalipa pango, wa kijijini analipa. Tumeona kwenye ile kodi ya barabarani ile ya magari ambayo ilikuwa inasumbua sana tunakamatwa na trafiki njiani, lakini tulipoipeleka kwenye mafuta hata Mtanzania anayemwagilia nyanya tu shambani akiwasha ile *pump* yake ya petroli ameshachangia ile *levy* ya barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mtindo huu niombe sana hizi *data* zichukuliwe na kama kwa kufanya uchunguzi zaidi wakaunda hata tume wakafuatilia vizuri, hii ni pesa nyingi ambayo Mtanzania wala ha-*feel*. Wako watoto wadogo tu, wanasema baba niwekee *MB* anacheza *game* tu, baba niwekee *MB* anaangalia tu picha, lakini ukishamwekea zile *MB* za 1,000 tayari yule mtoto ameshachangia shilingi 100 kwa ajili ya matibabu ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni chanzo cha uhakika ambacho hakina maumivu, hakina kelele, lakini kinaleta trilioni tatu kwa mwaka katika bajeti ya Bima ya Afya. *(Makofi)*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Serikali ...

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Gekul.

TAARIFA

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Francis kwa mchango mzuri. Nimpe tu taarifa, kwenye Kodi ya Majengo wanaolipa siyo wale wenye LUKU tu saa hizi. Majengo yote yaliyojengwa kwa tofali pia wanalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye 1,800 kwa mwaka ikatumika tu shilingi 50 itasaidia wale wananchi ambao wanahangaika na moyo, *cancer*, *dialysis*, itatusaidia sana. Serikali ichukue mawazo mazuri ya Mheshimiwa Francis. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Francis unapokea mchango wa Mheshimiwa Gekul?

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea kwa mikono miwili. Niiombe Serikali, hivi ni vyanzo vya uhakika ambavyo Watanzania wote watatibiwa tena bima iliyo sawa, hamna acha kusema hii kubwa hii Serengeti hii sijui hii Ngorongoro. Itakuwa ni bima ambayo inaenda popote kwa sababu watakuwa wamechangia fedha za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ikianza tu leo kesho unasikia mabilioni yameingia Mheshimiwa Waziri. Yaani ikianza kesho, kesho unasikia matrilioni, haina ujanja, sisi wenyewe ndiyo tunanunua. Nina *line* nne, zote ziko hai na kila siku lazima niziwekee *voucher*. Kwa hiyo, kila nikiweka tu *line* ujue tayari nimechangia. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ichukue jambo hili, ni la muhimu ambalo litasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nimalizie kwa kusema mchango ambao ulisemwa pia na mwenzangu pale muda mfupi.

Suala zima la madaktari kufanya *consultation* kwa wagonjwa; niombe, badala ya kuangalia kituo sasa tuangalie taaluma ya yule anayetoa *consultation*. Awe ameitoa kwenye kituo cha afya, awe ameitoa kwenye zahanati, kwa sababu daktari anaweza kuwa ni *specialist* yulo kijijini kwao likizo. Ameenda kusaidia wananchi kwenye kizahanati cha pale kijijini, akatoa huduma pale akasikiliza wagonjwa; lakini sasa eti yule atachajiwa kwa sababu ya kile kituo ni kizahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini asichajiwe ile hela yake kwenye bima kwa sababu yule ni *specialist* na atakuwa amesaidia jamii pale? Hii itasababisha hata madaktari wengi ambao hawana ajira watakwenda kujitolea kwenye hizi zahanati zetu, kwa sababu anajua akitoa huduma atachajiwa kwa sababu atalipwa na bima, kwa sababu ya elimu yake, siyo kwa sababu ya kituo alikotolea huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia. Kama kuna kuogopa kwamba itatumika vibaya, Chama cha Madaktari chenyewe ndicho kidhibiti leseni zao. Kwamba kuna daktari fulani alikuwa kijijini kule Mkalama akatoa *consultation*, akaandika dawa ame-*over*. Pengine ameandika hovyo labda kwa rushwa, Chama cha Madaktari ndicho kitadhibiti kimnyang'anye leseni. Kwa hiyo, niombe huduma za *consultation* ya madaktari bingwa zitolewe na hao madaktari kwa elimu zao, siyo kwa kituo anakotolea huduma ili Watanzania watumie hii huduma ya madaktari wengi walioko mtaani ili waweze kupata afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, ninaomba mchango wangu uchukuliwe kwa uzito mkubwa sana. Ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ulistahili kuwa mchangiaji wa mwisho kwa leo.

Waheshimiwa Wabunge tumemamiza michango ya waliokuwa wamejiandikisha kwa siku ya leo na hivyo tumekamilisha Shughuli za

Bunge ambazo zilipangwa siku ya leo tarehe 2 Juni, 2025. Kwa hiyo, sasa ninaahirisha Kikao hiki cha 37 hadi kesho Jumanne, tarehe 3 Juni, 2025 saa tatu asubuhi.

(Saa 1.34 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 3 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)